# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA NANE

**Kikao cha Nane – Tarehe 6 Februari, 2025**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa tuketi. Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA, KILIMO NA MIFUGO:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2024.

**MHE. VINCENT P. MBOGO K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2024.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbogo, ahsante sana. Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

**MASWALI KWA WAZIRI MKUU**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali kwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Kasalali Emmanuel Mageni, Mbunge wa Sumve, sasa aulize swali lake.

**MHE. KASALALI E. MAGENI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa mujibu wa Sera ya Kilimo ya nchi hii mazao ya choroko na dengu yamewekwa kwenye Mfumo wa Stakabadhi Ghalani. Hata hivyo, mazao haya ni chanzo cha chakula kama yalivyo maharage na mazao mengine. Sasa mazao haya yamekuwa chanzo cha akiba kwa wananchi wa maeneo ambayo mazao haya yanalimwa kwa wingi. Hata hivyo, kuyaweka kwenye Stakabadhi Ghalani kumesabaisha taharuki kubwa na usumbufu kwa wakulima. Ni nini kauli ya Serikali kuhusu jambo hili?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Kasalali, Mbunge wa Sumve, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza ninajua kwenye Sekta ya Kilimo tuna mazao ya biashara na mazao ya chakula, lakini yapo mazao ya chakula yanayotumika pia kwa biashara. Muhimu hapa ni kwamba, Serikali yetu imeendelea kuimarisha masoko ya mazao mbalimbali hapa nchini na tunatumia mifumo mbalimbali kufanya biashara za mazao hayo. Choroko ni miongoni mwa mazao ambayo Wizara ya Kilimo imekuwa ikiratibu biashara yake pale ambapo mwananchi ameamua kuyatumia kama zao la biashara.

Mheshimiwa Spika, tuna mifumo hiyo ya mauzo, kama vile Mkulima kuuza moja kwa moja ndani ya nchi hata nje ya nchi kama anapata oda; pili, tuna mifumo ya kilimo cha mkataba, mnunuzi anafanya majadiliano na mkulima, wanakubaliana kwa maandishi kabisa kwamba zao hilo litakapoiva anaweza kulinunua; na tatu, tuna huu mfumo ambao sasa tunautumia kwa mazao mengi ya kibiashara wa minada. Minada hii ili iende vizuri tuliona tutumie Stakabadhi Ghalani ambayo Mheshimiwa umeisema.

Mheshimiwa Spika, Stakabadhi Ghalani ni mfumo ambao unawezesha wakulima kupata faida kubwa. Kwa sababu, wanunuzi wanakutana pamoja, wanaambiwa kwenye ghala letu tuna tani kadhaa za zao hili na anayetaka atuambie atanunua shilingi ngapi kwa kilo. Kwa hiyo, ule ushindani ulioko kwenye uwanda kwa njia ya mnada ndio unasababisha kupata bei kubwa.

Mheshimiwa Spika, lakini ninatambua, yako maeneo kadhaa yana migogoro ambayo inawafanya wakulima washindwe kuuamini mfumo huo, kwa sababu mfumo ule unamtaka mkulima kila alichokivuna akipeleke ghalani na wahusika wa ghala wanakusanya wakifikia kiwango cha kutosha wanatangaza mnada. Sasa kile kipindi cha kusubiri, kutoka siku unapoleta mzigo mpaka unafanya mnada wengi huwa hawawezi kuvumilia. Kwa maana hiyo Wizara ya Kilimo ilishaagiza kwa Warajisi Wasaidizi na Maafisa Kilimo kule kwenye halmashauri zetu na wilaya.

Mheshimiwa Spika, mfumo huu unahitaji elimu kwa wananchi, waelewe, waridhie kile kipindi cha kuchelewa ili pale watakapohusisha mazao yao, kila mkulima ajue kwamba atakapopeleka hilo zao lake lenye kilo mbili, kilo tano, kilo kumi au zaidi, atakaa kwa kipindi ambacho wakulima wengine wataleta mazao hayo, yatangazwe mnada, yauzwe na kulipwa. Hivyo kutakuwa na kama siku mbili, tatu, nne za kusubiri malipo. Hapo ndipo panapokuwa na mgogoro.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naagiza Wizara ya Kilimo, iendelee kutoa elimu kwenye maeneo yote yanayotaka zao hilo liuzwe kwa Mfumo Stakabadhi Ghalani, ili kuondoa migogoro ambayo siyo muhimu, kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge ameeleza.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, baada ya kuwa tulishaanza Stakabadhi Ghalani kwenye maeneo mengi, tumegundua kwamba, faida kubwa inapatikana. Kwa hiyo, muhimu ni wakulima kujua kwamba, mfumo huu unaweza kuwa na siku kadhaa za kusubiri. Hata hivyo, jitihada zetu pale ni kuhakikisha tu, tunapunguza zile siku na malipo yanapatikana kwa wakati ili wakulima waweze kupata stahiki yao. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa George Ranwell Mwenisongole, Mbunge wa Mbozi, sasa aulize swali lake.

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali kwa Waziri Mkuu. Mheshimiwa Waziri Mkuu, Serikali inajipanga vipi na mabadiliko ya Sera za Nje ya Nchi ya Marekani, ambapo tangu Rais Donald Trump aingie madarakani, amefanya mabadiliko makubwa kuhusu Sera ya Nje ya Nchi yake, ambayo inakwenda kuathiri utekelezaji wa Sera zetu kwenye Elimu, Afya na Kiuchumi *especially* miradi inayofadhiliwa na *USAID*, *EP4R* na programu ya kupunguza makali ya VVU? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa George Mwenisongole, Mbunge wa Mbozi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Serikali yetu, nchi yetu inaheshimu Sera za Mambo ya Nje na tunatekeleza mikataba kwa mujibu wa sera hizo kama ambavyo tumekubaliana na nchi husika, kwenye maeneo mbalimbali. Tumeanza kuona nchi zenye uwezo mkubwa ikiwemo Marekani kubadilisha sera zao na

mabadiliko yake yanaathiri baadhi ya nchi. Pia hata nchi yetu inaweza kupata athari, lakini kwetu sisi ni muhimu kuzingatia sera za nje kama ambavyo tumekubaliana.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwamba ameendelea kuifanya nchi hii kuwa na mahusiano na nchi nyingi sana duniani, Marekani ni moja kati ya nchi hizo. Kwetu sisi, muhimu pamoja na upana huu wa mahusiano ambao tumeuweka ni kuhakikisha kwamba tunajiimarisha, tunakuwa na uwezo wa ndani wa kuhakikisha kwamba hatuendelei kuwa wategemezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni lazima tujiimarishe kwenye mipango yetu, bajeti zetu ziweze kumudu kutekeleza maeneo yote muhimu ikiwemo na hiyo Sekta ya Afya, Elimu, Maji na maeneo mengine kadiri tulivyokubalina na nchi husika.

Mheshimiwa Spika, tuna uwezo, tuna maliasili na tuna rasilimali, kazi ambayo tunayo sasa Watanzania ni kushirikiana kuhakikisha kwamba, tunatumia maliasili na rasilimali tulizonazo kujenga uchumi wa ndani, kuwezesha mipango na bajeti yetu iweze kutekeleza haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niseme tu kwamba, Marekani wameshatangaza na inawezekana pia nchi nyingine nayo ikatangaza kukawa na mabadiliko. Sisi tunaendelea kujiimarisha kuhakikisha tunakuza uchumi wetu kupitia vyanzo vya fedha na mapato, ambavyo tunaviweka pamoja na kuyaingiza hapa Bungeni ili yapangiwe mpango kazi na maeneo yaliyopungua pungua tuweze kujaziliza.

Mheshimiwa Spika, huo ndio mkakati ambao sasa tunatakiwa kuwa nao, na ndivyo ambavyo tunaweza kujipanga kutokana na mabadiliko ambayo sasa yanaendelea kwenye nchi zilizoendelea dhidi ya nchi ambazo zinaendelea kama Tanzania.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Asia Abdukarimu Halamga, Mbunge wa Viti Maalum.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali. Mheshimiwa Waziri Mkuu, kumekuwa na ongezeko kubwa sana la vijana nchini wenye uwezo wa kuleta mageuzi makubwa ya kiuchumi kupitia fani mbalimbali katika halmashauri zetu, kutokana na uimara wa sera. Je, ni upi mpango wa Serikali kutambua vijana hawa katika halmashauri zote nchini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Asia Halamga, Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli vijana wetu sasa ndio nguvu kazi yetu. Wako vijana wabunifu na wana ujuzi, lakini wapo ambao bado hawajapata ujuzi. Serikali yetu imeandaa mkakati wa kuwawezesha vijana kitaaluma. Kupitia mpango huu, Serikali kupitia Sera yetu ya Vijana na Uwezeshaji imesisitiza na kuhamasisha vijana kushiriki katika shughuli ambazo zinaweza kuleta ujuzi, pia tumehamasisha ubunifu kwenye maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ina mpango ambao sasa unatekelezwa mpaka kwenye halmashauri zetu, kuhakikisha kwamba vijana wenye ujuzi, lakini ambao hawana ujuzi kupata ujuzi. Serikali tumeendelea kujenga Vyuo vya Ufundi, ambavyo vitakuwa vinafundisha masomo mengi ili kuwapa ujuzi vijana wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wako ambao hawajasoma, lakini ni wabunifu wameweza kubuni kazi zao. Wizara ya Elimu imebuni mfumo wa kuitisha pamoja wabunifu na kuandaa maonesho ya ubunifu, ambapo vijana na Mtanzania yoyote atapata nafasi ya kwenda kuonesha kazi yake. Hawa vijana wote wanatoka kwenye halmashauri na katika halmashauri ndiko ambako

tumejenga *VETA* zetu ili kutoa nafasi ya karibu kwa vijana hawa kwenda kujifunza na kupata ujuzi.

Mheshimiwa Spika, ambacho kinafanywa sasa kama ambavyo Mheshimiwa Asia ametaka ni kwamba, halmashauri baada ya kuwa wamepata wabunifu inawabeba kuwapeleka kuonesha ubunifu kwenye maonesho mbalimbali. Baada ya maonesho yale, hawa wabunifu wanatambuliwa, wanawezeshwa aina ya utambuzi wao ili waweze kuendeleza ubunifu wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tutaendelea kuziagiza halmashauri, kuendelea kusimamia ufundishaji wa taaluma zenye ujuzi ili kupata vijana wengi ambao watapata taaluma za ujuzi, pamoja na wale wabunifu ambao mtu mmoja mmoja anaweza kubuni kazi yake waziendeleze, halafu waratibiwe na kutambulika. Tutajua huyu mjuzi yuko wapi, amefanya kazi gani, aina gani na kumtafutia hata uwezekano wa kuwa na masoko pindi ubunifu huo au ujuzi huo unaweza kumuingiza kwenye masoko na maeneo mengine ya ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, halmashauri zetu ziendelee kuratibu vijana hawa kupitia Idara ya Maendeleo ya Jamiii ambayo tunayo katika kila halmashauri, tuweze kuwatambua. Wale ambao wanafanya kazi ya aina moja waundiwe vikundi ili wawezeshwe kupata hata mitaji kupitia mikopo ya halmashauri au mifuko yote au Taasisi za Fedha, waweze kuendeleza ujuzi huu.

Mheshimiwa Spika, mpango wa Serikali ni kuhakikisha kwamba, vijana hawa tunawaweka pamoja kwenye maeneo hayo. Nawaagiza sasa wahakikishe kwamba, kila halmashauri inakuwa na kanzidata ya kuwatambua hawa vijana ili kuwawezesha kushiriki kwenye maonesho makubwa na kuboresha kazi zao na kuwapa mitaji ya kuendeleza kazi hiyo. Hayo ndio maelezo ya swali hili.  Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Sophia Hebron Mwakagenda, Mbunge wa Viti Maalum, swali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kumuuliza swali Waziri Mkuu. Mheshimiwa Waziri Mkuu, kuwekuwa na baadhi ya mazao yanayopata bei nzuri, na yanasaidia wakulima kupata mahitaji wanayoyataka. Hata hivyo, kumekuwa na mwenendo mbaya sana wa baadhi ya mazao ambayo wawekezaji pamoja na wanunuzi, hawafanyi vizuri kwa wakulima, hasa yale mazao yanayoharibikia shambani.

Mheshimiwa Spika, ni nini mkakati wa Serikali, kusema na kutoa agizo kwa wawekezaji hao na wanunuzi hao kuhakikisha wananunua mazao hayo kwa wakati, ikiwa zao la parachichi na zao la chai? Kwa kuwa mazao hayo, ni mazao yanayokaribika na wao wanachelewa kuyanunua kwa makusudi ili bei iweze kushushwa na wakulima kuona sasa wana karibia kupata hasara? Ninaomba tamko la Serikali kutoka kwako. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo nimeeleza katika swali la awali linalohusu mazao, kwamba Serikali imejikita katika kusimamia kilimo nchini. Kilimo ambacho kinatoa mazao ya biashara na chakula, nadhani tumeona manufaa tunayoyapata hapa nchini. Kupitia usimamizi huu wa mazao ya kibiashara, tunatambua ziko changamoto kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge ameeleza, kwamba mazao mengine ni ya haraka sana kuharibika, hivyo, yanasababisha kuuzwa kwa bei ya chini.

Mheshimiwa Spika, mkakati wa Serikali kwenye eneo hili ni kuhakikisha tu kwamba, mazao haya tunayawekea utaratibu ambao ndani ya Serikali tumeamua kuweka mamlaka au bodi: kuna Bodi ya Korosho, kuna Bodi ya Kahawa na kuna Bodi ya Chai. Hata hivyo, parachichi ipo kwenye Mamlaka ya Mazao ya Bustani, *TAHA (Tanzania Horticultural Association)*, hawa wanafanya kazi ya uratibu kuanzia kilimo chake mpaka masoko yake.

Mheshimiwa Spika, sasa Serikali ili kuokoa mazao haya yasipate hasara, kwanza tumehamasisha uwekezaji kwenye viwanda, ili tuweze kuchakata mazao haya na yasifikie hatua ya kuharibika. Kwa kuchakata tunapata bei nzuri kwa sababu unapata mazao mengi, mbali ya kula lakini tunaweza kupata mafuta na vitu vingine.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, utaratibu ambao sasa tunauweka ni wa kuhamasisha uwekezaji kwenye Sekta ya Kilimo kwa mazao mbalimbali, ikiwa ni pamoja na maparachichi. Kwa bahati nzuri nami nimepata nafasi ya kutembelea wilayani kwako Tukuyu, pia nimeenda Busokelo.

Mheshimiwa Spika, nimetembelea kwenye kiwanda kimoja kikubwa ambacho wenyewe wamelima shamba na wanachakata mazao yao na pia wametoa nafasi kwa wananchi wa eneo lile kuuza mazao yao pale. Kwa hiyo, kwa kuwekeza kiwanda tumeona na mimi nimeshuhudia kwamba hakuna parachichi inaoza, hakuna parachichi inakosa soko kwa sababu yeye anakuwa mnunuzi nambari moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa hivi tumeongeza viwanda, tumeruhusu uwekezaji. Tuna kiwanda Njombe, tuna kiwanda Mufindi na huenda kikajengwa kingine kule Kilolo, Iringa. Hizi ni jitihada za kuhakikisha kwamba tunayalinda haya mazao yasiwaharibikie wakulima pindi wanapovuna yaende viwandani.

Mheshimiwa Spika, ninajua juzi nilikuwa na Mbunge wa Njombe Kusini akilalamikia uwekezaji kwenye zao la chai. Ni kweli tunayo matatizo kwenye zao la chai. Nimeiagiza Wizara kumsimamia mwekezaji huyo ambaye amechukuwa viwanda karibu vyote vya chai na haviendelei ili wakulima wa zao la chai waweze kupata eneo la kuuzia na yeye kwa sababu amechukua viwanda tunataka tuone viwanda vile vikichakata zao la chai ili majani yasiweze kuharibika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tayari Wizara imechukua hiyo na Mheshimiwa Mbunge nilimwelekeza kuonana naye na

wanaendelea kusimamia zao hilo na mwekezaji ambaye amechukua viwanda vingi. Kwa hiyo, bado nisisitize kwamba mkakati wa Serikali ni kuhakikisha kwamba tunakaribisha uwekezaji mkubwa kwenye mazao haya ili mazao yaweze kwenda mahali pale kama eneo la soko lakini ukichakata na kuongeza thamani ya mazao haya, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Martha Festo Mariki, Mbunge wa Viti Maalum.

**MHE. MARTHA F. MARIKI:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipatia nafasi niweze kumwuliza swali Mheshimiwa Waziri Mkuu. Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kuwa wanawake ni kundi muhimu na kwa kuwa tunawategemea sana wanawake katika familia zetu na katika kizazi na endelevu na Taifa kwa ujumla na kwa kuwa wanawake wamekuwa wakipambana sana kujikwamua kiuchumi hasa katika maeneo yenye mfumo dume.

Mheshimiwa Spika, je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba wanawake wanaendelea kupata ajira za kutosha sawa na makundi mengine ukilinganisha na ushindani wa ajira uliopo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Martha Mariki, Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa kupigania haki za wanawake na hamu yake ya kuona fursa za akinamama zinapatikana. Wanawake ni kundi muhimu sana na Serikali imeendelea kuratibu shughuli mbalimbali zinazokuwa kuwawezesha akinamama kuweza kumudu kuboresha uchumi binafsi na kuendesha shughuli zao kama viongozi wa familia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye eneo hili Mheshimiwa Mariki, amezungumzia Uchumi, lakini akazungumzia ushindani wa ajira,

muhimu kwenye sekta ya ajira Waheshimiwa Wabunge tunajua kwamba Serikali ina ajira rasmi na ajira zisizokuwa rasmi, lakini ajira hizi zipo zile ambazo zinahitaji ujuzi maalum na hizi ndio ambazo zinazungumzwa sana kuwa na ushindani mkubwa na kundi lote linaweza likaachwa nyuma kutokana na kukosa sifa kadri ilivyotakiwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali yetu imeweka mpango mkakati wa kumwendeleza mwanamke. Moja, hata mabadiliko ya Sera ya Elimu ambayo sasa tunayo imetoa fursa ya wazi kwa wanawake au wasichana kupata elimu kuanzia ngazi ya awali mpaka vyuo vikuu, lakini pia umewekwa msisitizo maalum kwa ajili ya elimu, zile taaluma zenye ujuzi ili kumwezesha mwanamke kuingia kwenye shindani iwe ni wa ajira au katika kujitafutia uchumi binafsi.

Mheshimiwa Spika, kwenye eneo hili nalo tumejitahidi kuweka mifumo ambayo inamwezesha mwanamke kujiwezesha kupata uchumi. Tumefungua fursa ndani ya Serikali kupitia Mifuko mbalimbali kuwezesha kutoa mikopo na wanawake nao wanapata mikopo, lakini tumeweka pia Mfuko kwenye halmashauri zetu ambao tumetenga 10%, asilimia nne ni kwa ajili ya wanawake ambao pia wanaweza kwenda kukopa na haina ya riba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali pia imezungumza na taasisi za fedha zihakikishe kuwa taasisi hizi zinafungua dirisha linalowezesha akinamama, vijana na makundi mengine kuweza kupata mitaji ya kuendesha shughuli zao za kiuchumi ili kumwezesha mwanamke au yeyote yule kati ya wakopaji kupata nafasi ya kuweza kuboresha uchumi wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunapozungumzia kwenye ajira sasa huku Serikali nayo inawaangalia sana wanawake pale ambapo panakuwa na ushindani wa mwanamke na mwanaume, lakini mwanamke anakuwa yupo kwenye ushindani ule basi nafasi ya kwanza anapewa mwanamke ili aweze kuingia kwenye hiyo.

Mheshimiwa Spika, haya ni malengo ya Serikali ya kufikia *50/50.* Kwa hiyo, mikakati yote hii inaonesha dhamira ya wazi ya Serikali yetu chini ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kuhakikisha kwamba mwanamke naye anapata nafasi ya kushiriki katika kukuza uchumi wa Taifa hili na kuchangia uchumi wa Taifa hili vilevile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba sera tuliyonayo ndani ya Serikali inaonesha jitihada za wazi kwa ajili ya kumhudumia mwanamke na kusimamia mwenendo wa shughuli za kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, vilevile, ulinzi umeimarishwa pia na kuhakikisha kwamba anapata fursa ya kupata uwezo wa kuendesha shughuli yoyote ya kiuchumi wakati wowote anapoamua kufanya hivyo. Huo ndio mwelekeo wa Serikali. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Orodha imekamilika. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea.

Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD- KATIBU WA BUNGE:**

## MASWALI YA KAWAIDA

**SPIKA:** Tunaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Khadija Shaaban Taya, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 128

### Agizo la Kutenga Ofisi ya Watu Wenye Ulemavu kwenye Ofisi za *DC*

**MHE. KHADIJA S. TAYA** aliuliza:-

Je, Wakuu wa Wilaya wametekeleza kwa kiasi gani agizo la Waziri Mkuu la kutenga ofisi za watu wenye ulemavu katika ofisi zao?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Festo Dugange, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza maagizo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu aliyoyatoa wakati wa ufunguzi wa Kongamano la Watu Wenye Ulemavu, Mkoani Dar es Salaam Agosti, 2023, mikoa kwa kushirikiana na halmashauri imeendelea kuratibu upatikanaji wa Ofisi za Vyama vya Watu Wenye Ulemavu.

Mheshimiwa Spika, kufikia Januari, 2025 Mikoa 26 na Wilaya 73 zimetenga ofisi za Vyama vya Watu Wenye Ulemavu katika majengo ya Halmashauri, Ofisi za Wakuu wa Wilaya na Ofisi za Kata.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na jitihada za kuhakikisha ofisi za Vyama vya Watu Wenye Ulemavu zinapatikana katika wilaya zote nchini. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Khadija Shaaban Taya, swali la nyongeza.

**MHE. KHADIJA S. TAYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana na naomba niipongeze Serikali kwa jitihada ambayo wameifanya kwa kuweza kufikisha 60% ya kutafuta Ofisi za watu wenye ulemavu. Ninaomba nimshukuru sana Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuweza kupata hizo ofisi na jitihada ambazo zimefanyika, nilikuwa nina ombi la kwamba

tulete marekebisho ya sheria ili sasa hili lisiwe agizo peke yake la Mheshimiwa Waziri Mkuu basi iwe sheria rasmi ambayo haitoweza kuondolewa mpaka nafasi ya watu wengine itakapokuja. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Khadija Taya mara kwa mara amekuwa akifuatilia maslahi na ustawi wa watu wenye ulemavu na Serikali hii sikivu ya Awamu ya Sita inayoongozwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan imeendelea kuhakikisha kwamba watu wenye ulemavu wanapewa stahiki zao, lakini pia wanatengenezewa mazingira bora zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwanza, nimhakikishie kwamba maelekezo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu yanatekelezeka, lakini pia wazo lake la kuwa na sheria au sera maalum kwa ajili ya hilo tumelipokea tutalifanyia kazi na kuona uwezekano wa kuendelea na utaratibu huo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Subira Khamis Mgalu, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 129

**Hatua kwa Maafisa Masuuli na Wahazini Wabadhirifu**

**MHE. SUBIRA K. MGALU** aliuliza:-

Je, Serikali inachukua hatua gani kwa Maafisa Masuuli na Wahazini wa Serikali za Mitaa kutokana na ongezeko la hoja za ukaguzi za Ripoti za CAG?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Taarifa za CAG zinaonesha kuwa, mwenendo wa hati za ukaguzi kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa umeendelea kuimarika mwaka hadi mwaka. Katika kipindi cha miaka minne (2019/2020 hadi 2022/2023), Hati Safi zimeongezeka kutoka 124 sawa na 67% mwaka 2019/2020 hadi Hati 181 sawa na 98.4% mwaka 2022/2023. Aidha, hati zenye shaka na hati mbaya zimepungua kutoka 61 sawa na 33% mwaka 2019/2020 hadi Hati tatu sawa na 1.6% mwaka 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, mwenendo huu mzuri wa Hati za Ukaguzi na utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi umechangiwa na uchukuaji wa hatua za kisheria na kinidhamu kwa watumishi wanaosababisha hoja za ukaguzi au hasara kutokana na kutotekeleza wajibu wao kikamilifu au kujihusisha na vitendo vya ubadhirifu.

Mheshimiwa Spika, mathalani, kufuatia Taarifa ya CAG ya ukaguzi wa Mwaka wa Fedha 2022/2023, jumla ya watumishi 294, wakiwemo Wakurugenzi na Waweka Hazina, wamechukuliwa hatua mbalimbali zikiwemo kufukuzwa kazi (20), kifungo jela (watano), kufikishwa Mahakamani (30), kushushwa cheo (mmoja), kupewa onyo (100), kukatwa mshahara (14) na kufikishwa Polisi na TAKUKURU kwa uchunguzi (114).

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kuboresha mifumo ya udhibiti ili kuimarisha usimamizi wa rasilimali za umma na kupunguza hoja za ukaguzi na itaendelea kuchukua hatua za kisheria kwa watakaokiuka taratibu zilizopo, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mheshimiwa Subira Mgalu, swali la nyongeza.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwanza, niipongeze sana Serikali yetu ya Awamu ya Sita kwa

maboresho mbalimbali yaliyofanyika ambapo inaoneka kupitia Taarifa za *CAG* kuna mabadiliko makubwa katika usimamizi wa fedha za umma kutokana na kupungua kwa hati mbaya na hati za mashaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza. Kwa kuwa majibu yalitolewa na Serikali inaonesha hali ni nzuri na imezidi kuimarika hatua za kisheria zimechukuliwa, lakini kwa wananchi na umma bado dhana na tafsiri kwamba hali ya ubadhirifu na matumizi mabaya ya Serikali yameongezeka. Je, Serikali ipo tayari kuunda pengine kitengo kwa kushirikiana na Ofisi ya *CAG* na Ofisi pia ya Bunge kwenye Kamati zake ili kuelimisha umma wajue tafsiri sahihi na hatua zilizochukuliwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Kwa kuwa ukaguzi wa hesabu siyo suala la kuviziana, mkaguzi anapofika anafanya vikao, anapoondoka anafanya kikao, anaacha hoja na anatoa nafasi za siku 21 kujibiwa, lakini inatokea kwamba nafasi hiyo haitumiki vizuri na wakaguliwa (Maafisa Masuuli), kiasi kwamba hoja zote zinajitokeza kwenye Ofisi ya *CAG* kwenye ripoti yake, lakini baada ya kutoka ripoti hao hao wanatafuta majibu…

**SPIKA:** Mheshimiwa Subira, uliza swali, tafadhali.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Spika, je, Serikali ipo tayari kufanya utafiti wa kujua tatizo ni nini ili iweze kuchukua hatua stahiki? Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Ni kweli, kama ambavyo jibu langu la msingi limesema hali ya ukaguzi kwa maana ya mwenendo wa hati katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa imeendelea kuimarika siku hadi siku kwa sababu ya hatua madhubuti ambazo zimechukuliwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba bado kuna baadhi ya maeneo ambayo kuna matumizi yasiyostahili ya fedha za umma. Kwa hivyo, Serikali kama ambavyo nimetangulia kusema itaendelea kuchukua hatua na kuboresha mifumo ili kudhibiti matumizi mabaya ya fedha ya umma.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la Mheshimiwa Mbunge kwamba kianzishwe kitengo maalum kwa ajili ya kutoa elimu kwa umma. Tunapokea mawazo hayo ni mazuri, lakini halmashauri zetu zinaendelea kuelimisha wananchi kwamba Serikali inachukua hatua katika eneo hili.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na suala la hati za ukaguzi kwamba kuna utaratibu wa mkaguzi kufanya *exit meetings,* lakini bado kunakuwa na hoja. Suala hili tumeendelea kulifanyia kazi kumekuwa na changamoto ya utunzaji wa *document* katika halmashauri zetu ambazo mara nyingine wakati wa ukaguzi hazipatikani mara moja lakini zinapatikana baada ya muda fulani.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tumeelekeza sasa halmashauri zetu zote wahakikishe *document* zote zinapatikana kwa wakati, wakati wakaguzi wa *CAG* wapo ili hoja zote zifungwe haraka iwezekanavyo badala ya kusubiri muda mrefu, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Samweli Xaday Hhayuma, Mbunge wa Hanang, sasa aulize swali lake.

Na. 130

**Kuboresha Zahanati za Zamani Zilizopo Makao Makuu ya Kata – Hanang'**

**MHE. SAMWELI X. HHAYUMA** aliuliza:-

Je, nini mkakati wa Serikali wa kuboresha zahanati za zamani zilizopo Makao Makuu ya Kata za Hanang'?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua uwepo wa vituo vya huduma ambavyo ni vikongwe na chakavu vinavyohitaji ukarabati. Ili kutekeleza jukumu hilo, Serikali ilifanya tathmini ya vituo chakavu, ambapo mpaka Disemba, 2024 kuna jumla ya vituo vya afya 204 na zahanati 1,226 zinazohitaji ukarabati kote nchini zikiwemo Zahanati za Sirop, Getanuwas na Dirma katika Wilaya ya Hanang'

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na ukarabati wa vituo chakavu kwa awamu na mpango wa Serikali ni kuongeza kasi ya ukarabati wa vituo vya afya na zahanati mara baada ya kukamilisha ukarabati wa hospitali kongwe 77 ambapo tayari hospitali 14 zimekwisha karabatiwa na hospitali 34 ukarabati unaendelea ambapo jumla ya shilingi shilingi bilioni 44.5. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Samweli Hhayuma, swali la nyongeza.

**MHE. SAMWELI X. HHAYUMA:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa majibu ya Serikali hospitali kongwe ambazo zimekwisha kukarabatiwa ni 18% tu. Kata ambazo Mheshimiwa Waziri amezitaja zina idadi kubwa ya watu na kweli ukiboresha huduma za afya za msingi maana yake hospitali zitapunguza kupokea watu na itakuwa rahisi watu kufikia huduma za afya.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza. Je, Serikali sasa haioni sasa kuna dharura ya kukarabati na kujenga nyumba za watumishi pamoja na huduma ya mama na mtoto kwenye Zahanati ya Dirma, Sirop, Ishponga na Getanuwas?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Kituo cha Afya Hirbadaw kina upungufu mkubwa wa vifaatiba hasa jokofu la kuhifadhia maiti. Je, Serikali ina mkakati gani wa kupeleka vifaa vya kutosheleza kwenye Kituo cha Afya cha Hirbadaw?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kuna baadhi ya vituo vya afya ambavyo ni chakavu na vina upungufu wa baadhi ya majengo yakiwemo majengo ya huduma ya afya ya mama, baba na mtoto.

Mheshimiwa Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba maeneo yote ambayo ya zahanati au vituo vya afya ambavyo havina majengo hayo Serikali imekuwa ikiweka kipaumbele kuhakikisha kwamba majengo hayo yanajengwa ili yaweze kutoa huduma hiyo muhimu kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, katika vituo vyake ambavyo Mheshimiwa Mbunge amevitaja katika Jimbo la Hanang tutahakikisha tunavifuatilia na kutafuta fedha aidha kupitia mapato ya ndani au Serikali Kuu ili majengo hayo ya huduma ya mama, baba na mtoto yaweze kujengwa na wananchi wapate huduma hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, kuhusiana na kituo cha afya ambacho Mheshimiwa Mbunge amekitaja ambacho hakina vifaatiba, ninaomba tu nimhakikishie kwamba Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan katika kipindi hiki cha mwaka wa fedha huu ameshapeleka katika halmashauri zote 184 kati ya shilingi milioni 800 mpaka shilingi bilioni tatu kwa kila halmashauri kwa ajili ya ununuzi wa vifaatiba.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, natumia nafasi hii kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, TAMISEMI kumwelekeza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Hanang kuweka kipaumbele cha vifaatiba kwenye kituo hicho cha afya ambacho hakina vifaatiba, lakini Serikali imekwishapeleka fedha

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Robert Maboto, swali la nyongeza.

**MHE. ROBERT C. MABOTO:** Mheshimiwa Spika, je, Serikali itajenga lini Kituo cha Afya katika Kata ya Sazira na Kata ya Guta katika Halmashauri ya Mji wa Bunda? Ninakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, Serikali imeweka mpango mkakati wa ujenzi wa vituo vya afya kwenye kata za kimkakati ambazo zinakidhi vigezo vya idadi ya wananchi wasiopungua 15,000, lakini umbali kutoka kituo cha jirani zaidi lakini na hali za kijiografia.

Mheshimiwa Spika, nimwelekeze Mheshimiwa Mbunge ashirikiane na Mkurugenzi na ninafahamu anashirikiana vizuri na alishaleta taarifa hiyo. Watuletee rasmi andiko la maombi ya vituo hivyo vya afya katika kata hizo ili Serikali iweke kwenye mpango kazi wa ujenzi wa vituo hivyo kwa kushirikiana na mapato ya ndani ya halmashauri. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Condester Sichalwe, swali la nyongeza.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa nafasi. Mheshimiwa Naibu Waziri, unaonaje baada ya kumaliza Bunge hili uongozane nami kwenda Jimbo la Momba? Tupitie Kijiji cha Makamba, Kijiji cha Sanja, Siliwiti na Itumba ili uone changamoto ambayo wananchi wanapitia baada ya kukosa zahanati?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, nipo tayari kuambatana na Mheshimiwa Mbunge kwenda katika Jimbo lake la Momba na katika vijiji ambavyo amevitaja ili tuweze kushirikiana kuona namna nzuri ya kujenga zahanati katika maeneo hayo. Wakati huo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, sauti yake inasikika ipasavyo na tayari ameleta majina ya vijiji

hivyo. Serikali iko kwenye utaratibu wa kutafuta fedha, kwa ajili ya ujenzi wa zahanati hizo. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zaytun Swai, swali la nyongeza.

**MHE. ZAYTUN S. SWAI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kituo cha Afya cha Moshono, Wilaya ya Arusha Mjini, kina nyufa nyingi na hasa kwenye jengo la mama na mtoto na hivyo kuhatarisha maisha ya wananchi. Je, ni upi mkakati wa Serikali kukarabati kituo hiki?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ninaomba kutumia nafasi hii kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, kumwelekeza Mkurugenzi wa Jiji la Arusha atume wataalam wake, wahandisi wa ujenzi, waende wakafanye tathmini ya jengo hilo lenye nyufa. Ikiwa ni hatarishi, basi hatua stahiki zichukuliwe mapema na Serikali iweke utaratibu wa kukarabati au kujenga jengo lingine, ili kuhakikisha kwamba, wananchi wanakuwa salama na wanapata huduma bora. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Deo Sanga, swali la nyongeza.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Spika, nini mpango wa Serikali kuunga mkono jitihada za wananchi wa Mkolango, ambao wamejenga? Wanaomba hela, Serikali imalizie nguvu zao. Nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA – (MHE. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga amefuatilia kwa karibu sana suala la Zahanati ya Mkolango na ninafahamu wananchi walitoa nguvu zao, zaidi ya miaka saba wanasubiri Serikali kukamilisha.

Ninaomba kumhakikishia, kama ambavyo tumekubaliana, tumeshaingiza kwenye vipaumbele vya mwaka huu wa fedha kupata fedha hiyo, kwa ajili ya kukamilisha Zahanati ya Mkolango. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Nicodemas Maganga, swali la nyongeza.

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Spika, vijiji vingi vya Mbogwe vilishajenga maboma ya zahanati. Mpango wa Serikali ukoje kutoa pesa, ili zahanati hizi ziweze kukamilika wananchi waendelee kupata huduma? Ninakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, Serikali hii ya Awamu ya Sita, chini ya uongozi mahiri wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tangu mwaka 2021 mpaka sasa zaidi ya shilingi 15,000,000,000 hadi shilingi 30,000,000,000 zinatolewa kila mwaka, kwa ajili ya ukamilishaji wa maboma ya zahanati na vituo vya afya katika halmashauri zote, kote nchini, ikiwemo Halmashauri ya Mbogwe.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge, nafahamu kwamba, kuna zahanati zimekamilishwa kwa fedha ya Serikali Kuu, lakini nafahamu bado kuna maboma, tuwapongeze wananchi kwa kazi hiyo nzuri. Nakuhakikishia kwamba, Serikali itaendelea kutenga fedha, kwa ajili ya kukamilisha maboma hayo katika Wilaya ya Mbogwe. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Minza Mjika, swali la nyongeza.

**MHE. MINZA S. MJIKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Kituo cha Afya Iramba Ndogo kina jengo moja tu lililokamilika la *OPD*, hakuna jengo la wazazi, maabara na

kichomea taka. Je, ni lini Serikali itapeleka fedha kwa ajili ya kujenga majengo hayo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ujenzi wa vituo vya afya unafanyika kwa awamu, tulianza na awamu ya kwanza ya majengo ya *OPD*, maabara na majengo mengine. Namhakikishia tu Mheshimiwa Mbunge, tunafahamu kwamba, Kituo cha Afya cha Iramba Ndogo kina jengo moja na majengo mengine muhimu bado hayajajengwa.

Mheshimiwa Spika, kwa bahati nzuri tumekwishakiweka kwenye mpango wa ujenzi wa majengo yaliyobaki. Kwa hiyo, ninaomba kukuhakikishia Mheshimiwa Mbunge, Serikali inalifanyia kazi suala hilo. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Suma Ikenda Fyandomo, swali la nyongeza.

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa swali dogo la nyongeza. Hospitali ya Wilaya ya Kyela majengo yake yamechakaa sana, hata unapokwenda kuona wagonjwa unahisi huruma sana. Sasa je, ni lini Serikali itapeleka fedha za kujenga hospitali ile, angalau hata kwa kukarabati? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ni kweli Hospitali ya Wilaya ya Kyela ni hospitali kongwe, kwa bahati njema nimefanya pale kama miaka tisa, naifahamu vizuri sana. Serikali hii sikivu imeweka mpango madhubuti, ilishapeleka fedha, kwa ajili ya ujenzi wa jengo la ghorofa, najua limeanza ujenzi na tumeweka mpango wa kujenga majengo yote ya wodi na *OPD* yawe bora zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge naomba kukuhakikishia kwamba, Serikali imeshaiingiza kwenye mpango na tutaendelea kujenga kwa awamu, ili kuibadilisha kabisa Hospitali ya Wilaya ya Kyela.

**SPIKA:** Mheshimiwa Grace Tendega, swali la nyongeza.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Spika, Zahanati ya Welu ambayo ipo katika Kata ya Ulanda, Jimbo la Kalenga, ambayo inahudumia vijiji vinne, imejengwa na imekarabatiwa vizuri, lakini ina changamoto ya daktari. Nini mkakati wa Serikali kupeleka daktari? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ninaomba kutumia nafasi hii kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais TAMISEMI, kumsisitiza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Iringa kuhakikisha kwamba, wanafanya msawazo wa ndani kutoa mganga kutoka zahanati ambayo ina waganga zaidi ya wawili au watatu, ili wapelekwe pale, kwa ajili ya kuongeza huduma za afya kwenye Zahanati ya Welu.

Mheshimiwa Spika, wakati huo huo, ninamhakikishia tu Mheshimiwa Mbunge, Serikali imeendelea kutoa vibali vya ajira na mwaka huu wa fedha wataalam zaidi ya 10,183 wamekwishaajiriwa na Wilaya ya Iringa itapata wataalam hao. Kwa hiyo, tutaendelea kuboresha ikama ya watumishi na ninamhakikishia tu kwamba, hicho ni kipaumbele cha Serikali. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Iddi Kassim iddi, swali la nyongeza.

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Spika, Zahanati ya Kijiji cha Kabondo, Kata ya Mwanase, ni muda sasa haijakamilika. Nataka kufahamu Kauli ya Serikali, ni lini sasa zahanati hii itakamilika na

kuanza kutoa huduma, ili wananchi wa Kabondo waweze kupata huduma ya zahanati?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, katika ukarabati na ukamilishaji wa zahanati, ziko zahanati ambazo zilianza ujenzi kwa nguvu za wananchi, lakini Serikali ikapeleka shilingi 50,000,000 kwa ajili ya ukamilishaji. Kwa hiyo, kwa zahanati ambazo zilipokea shilingi 50,000,000 kwa ajili ya ukamilishaji zikiwa hatua ya lenta, tunatarajia ziwe zimekamilika na zimeanza kutoa huduma kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba kuchukua nafasi hii kumuhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, zahanati hiyo ya Kabondo tutaifuatilia, kama ilipokea shilingi 50,000,000 basi inatakiwa iwe imekamilika na tutachukua hatua stahiki kuhakikisha kwamba, inakamilika kwa wakati, lakini kama haijapokea tutaiingiza kwenye kipaumbele cha zahanati ambazo zitaletewa fedha hiyo ili iweze kukamilika. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zuberi Kuchauka, swali la nyongeza.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa nafasi. Vijiji vya Makinda, Mitawa B, Nyera na Tepetepe vina uhitaji mkubwa sana wa ujenzi wa zahanati na wananchi wameshaanza. Je, Serikali iko tayari kuwa-*support* wananchi hawa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA – (MHE. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, vijiji vyote ambavyo vina mpango wa ujenzi wa zahanati na ambavyo wataalam wamejiridhisha kwamba, vinakidhi vigezo vya ujenzi wa zahanati tunawapongeza wananchi ambao wameanza kutoa nguvu zao, kwa ajili ya ujenzi huo.

Mheshimiwa Spika, nawahakikishia tu kwamba, Serikali kwa awamu itaendelea kutenga bajeti, kwa ajili ya kuchangia nguvu za wananchi na kukamilisha zahanati hizo katika Jimbo la Liwale, lakini pia, katika majimbo mengine katika nchi yetu kwa ujumla.

**SPIKA:** Mheshimiwa Vita Kawawa, swali la nyongeza.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, je, Serikali imefikia wapi mpango wa kuvikarabati Vituo vya Afya vya Lusewa, Mkongo Gulioni na Mputa, Wilayani Namtumbo, ambavyo vilijengwa miaka ya 70? Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Vita Kawawa amewasilisha mara kadhaa hoja hiyo ya ukarabati wa Vituo hivyo vya Afya vya Mkongo na vingine. Ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, katika vile vituo vya afya 204 ambavyo vimefanyiwa tathmini na kwamba, ni vikongwe na vichakavu katika Jimbo la Namtumbo, vimo kwenye orodha hiyo. Kwa hiyo, naomba kumhakikishia tu kwamba, baada ya ukamilishaji wa ukarabati wa hospitali za wilaya tutahakikisha tunatoa kipaumbele kuanza ukarabati wa vituo hivyo vya afya, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Salma Rashid Kikwete, swali la nyongeza.

**MHE. SALMA R. KIKWETE:** Mheshimiwa Spika, je, ni lini Serikali itatupelekea pesa katika Zahanati yetu ya Mputwa na hasa, kwenye nyumba ya watumishi? Kwa sababu, nyumba ile ya watumishi imejengwa kidogo, upande huu kuna *sitting room* na chumba kimoja; sasa *sitting room* anakaa mtumishi mmoja na watoto wake halafu kwenye chumba anakaa mtumishi wa kiume.

Mheshimiwa Spika, ina maana kwamba, wanakaa sehemu moja, hata wakitaka kwenda kujisaidia ni shida, inabidi huyu apite

hapa kwa kina mama halafu aende kule. Sasa, je, lini mtatupatia pesa kumalizia ile nyumba ya watumishi? Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa, mama yangu, Salma Kikwete amelisema hili suala, ni suala nyeti na amekuwa akifuatilia sana ustawi wa wananchi wa Jimbo la Mchinga. Ninaomba kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, kwanza dhamira ya Serikali ni kuhakikisha watumishi wetu katika sekta ya afya wanakaa katika mazingira bora ili waweze kutoa huduma bora kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, kuna Mpango wa Serikali ambao unatekelezwa sasa, wa ujenzi wa nyumba za *two in one* na *three in one* na zoezi hili ni endelevu. Ninaomba kupokea hoja ya Mheshimiwa Mbunge, twende tukaifanyie kazi kwa haraka kupata fedha, kwa ajili ya ujenzi wa nyumba ya watumishi katika zahanati ambayo ameitaja.

**SPIKA:** Mheshimiwa Seif Gulamali, swali la nyongeza.

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kumuuliza swali Mheshimiwa Naibu Waziri juu ya fedha za Kituo cha Afya cha Chomachankola pamoja na Uswai. Je, ni lini fedha hizo mtatupatia? Ninakushukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, Kituo cha Afya cha Chomachankola kimeingizwa kwenye mpango wa Benki ya Dunia *(Team Chip)* na tuko hatua za mwisho. Jana kulikuwa na kikao cha Ofisi ya Rais, TAMISEMI na watu wa *World Bank* kuweka mpango wa ku-*release* zile fedha, kwa ajili ya ujenzi wa vituo hivyo. Kwa hiyo, ninaomba kumhakikishia Mheshimiwa

Gulamali kwamba, tuko hatua za mwisho kutoa fedha hiyo, kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya cha Chomachankola. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jesca Msambatavangu, swali la nyongeza.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, Kituo cha Afya, Ipogolo na Kituo cha Afya Ngome, ni vituo vikongwe sana vya miaka zaidi ya 30. Ni lini Serikali itatuletea, hasa, wodi za kisasa za kujifungulia wanawake?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, katika vituo vyetu vya afya, vipo vituo ambavyo ni vikongwe, lakini vina miundombinu yote na pia, vipo vituo vya afya ambavyo vina miundombinu pungufu na hususan wodi za wanawake, wanaume na watoto.

Mheshimiwa Spika, nafahamu vituo vya afya vikongwe na vingine ambavyo amevitaja Mheshimiwa Mbunge vina upungufu wa majengo hayo na tumeshaweka mpango wa awamu ya pili ya upanuzi na ukarabati.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nakuhakikishia Mheshimiwa Msambatavangu kwamba, Serikali itahakikisha inatenga fedha, inaweka kipaumbele, inakwenda kukarabati na kufanya upanuzi wa vituo hivyo vya afya. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Felista Deogratius Njau, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 131

**Hitaji la Shule Mpya ya Sekondari Kata ya Mabogini, Moshi Vijijini**

**MHE. FELISTA D. NJAU** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga shule mpya ya sekondari katika Kata ya Mabogini, Moshi Vijijini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA – (MHE. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Kata ya Mabogini ina jumla ya shule za sekondari tatu ambazo ni Mpirani yenye jumla ya wanafunzi 1,158, Mabogini wanafunzi 711 na Mtakuja B wanafunzi 234. Aidha, Mwaka wa Fedha 2022/2023 Serikali ilipeleka shilingi milioni 584.2, kwa ajili ya ujenzi wa shule ya kutwa katika Kata ya Mabogini. Ujenzi wa shule hii umekamilika na kusajiliwa kwa jina la Mtakuja B Sekondari.

Mheshimiwa Spika, mpango wa Serikali kwa sasa ni kujenga shule za kutwa kwa kuzingatia vigezo vitatu ambavyo ni, kila kata kuwa na shule ya sekondari walau moja katika maeneo ya msongamono mkubwa wa wanafunzi na sehemu ambazo watoto wanatembea zaidi ya kilometa 5. Kwa kuzingatia kuwa, Kata ya Mabogini tayari ina shule tatu za sekondari, haijaingizwa kwenye mpango wa kujengewa shule nyingine ya sekondari. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Felista Njau, swali la nyongeza.

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu ya Serikali, lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza. Kutoka Kijiji cha Mvuleni, Mji Mpya, mpaka kufika kwenye hiyo shule ya sekondari inayojengwa ni zaidi ya kilometa tano. Vigezo vinaonesha, zikishazidi kilometa tano ni lazima kuwe na shule na *population* katika kata ile ni zaidi ya watu 50,000. Je, Serikali haioni umuhimu wa kujenga shule nyingine, ili kuweza kuwapunguzia wanafunzi wetu makali?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Kuna maeneo mengi nchini yenye urefu wa namna hiyo na watoto wetu wa kike wanaathirika kwa kupata mimba za utotoni. Je, Serikali haioni ni wakati sasa wa kufanya utafiti na kujenga shule ambazo ziko mbali zaidi ya kilometa tano ili kusaidia wanafunzi wetu? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, ziko kata ambazo zina idadi kubwa ya wananchi, lakini kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge ametaja, Kata hiyo ya Mvuleni na Mji Mpya kwamba, zina umbali wa zaidi ya kilometa tano na wananchi zaidi ya 50,000.

Mheshimiwa Spika, naomba tulichukue suala hilo, ni suala muhimu, twende tukaone uwezekano wa kufanya tathmini na pia, uwezekano wa kupata fedha, kwa ajili ya kuboresha huduma za elimu katika eneo hilo na kupunguza umbali kwa wanafunzi. Kwa hiyo, Serikali hii sikivu tutahakikisha tunalifanyia kazi ili tuweze kutoa maamuzi bora zaidi.

Mheshimiwa Spika, pili, ni kweli kwamba, katika nchi yetu zipo baadhi ya kata ziko mbali zaidi, lakini sera ni ndani ya kilometa tano tunakuwa na shule ya sekondari ndani ya kata. Kwa hivyo, zile kata ambazo zina umbali mkubwa zaidi tunaendelea kufanya tathmini na kupeleka fedha, kwa ajili ya ujenzi wa shule za sekondari, ikiwa vigezo vyote vitakuwa vimetimia. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Michael Mwakamo, swali la nyongeza.

**MHE. MICHAEL C. MWAKAMO:** Mheshimiwa Spika, ninafahamu kwamba, Serikali ina mpango wa kujenga shule za sekondari za kata nchi nzima katika kata ambazo hazipo. Je, Serikali ina mpango gani wa kutupatia pesa kujenga shule za Kata ya Janga na Mtambani, pale katika Mji Mdogo wa Mamlaka, Mlandizi? Ninakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA – (MHE. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, kupitia Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari *(SEQUIP),* Serikali imeendelea kutoa fedha, kwa ajili ya ujenzi wa shule za sekondari za kata. Ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, tuna orodha ya kata zote zenye vigezo ambazo hazijapata shule za sekondari na kazi inayoendelea sasa ni kupata fedha, kwa ajili ya kwenda kujenga shule hizo. Kwa hiyo, namhakikishia Mheshimiwa Mwakamo kwamba, kata zake hizo mbili zitapelekewa fedha, kwa ajili ya ujenzi wa shule za sekondari. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa John Pallangyo, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa hii nafasi. Kata ya Akheri imetenga eneo katika Kitongoji cha Maksoru, Kijiji cha Nguruma, kwa ajili ya ujenzi wa sekondari mpya na wananchi wameshaanza kujitolea, kwa ajili ya ujenzi huo. Je, Serikali ina mkakati gani wa kutenga fedha, kwa ajili ya kujenga hiyo sekondari? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ni kweli Mheshimiwa Dkt. Pallangyo alikwishawasilisha hoja hiyo Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Natumia nafasi hii kuwapongeza wananchi wa Kata hiyo ya Akheri pamoja na kijiji hicho kwa kutenga eneo na kuanza kutumia nguvu zao katika ujenzi wa sekondari.

Mheshimiwa Spika, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge na Wananchi wa Jimbo la Arumeru kwamba, Serikali hii sikivu itapeleka fedha, ili kuhakikisha shule hiyo inakamilika na wananchi na watoto wetu wanapata maeneo jirani na bora zaidi, kwa ajili ya kupata elimu.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, miundombinu ya Shule Kongwe ya Kata ya Mogabiri ambayo imepandishwa hadhi na kuwa ya Kidato cha Tano na Sita ni chakavu sana. Nini mkakati wa Serikali wa kuhakikisha kwamba, inakarabati miundombinu ile, ili iweze kuendana na majengo ya kisasa ambayo mnajenga na kuweka mazingira safi kwa wanafunzi kujifunza? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, mpango wa Serikali ulianza na ukarabati wa shule za sekondari za kitaifa ambazo zote zimekarabatiwa, lakini tunaendelea na ukarabati wa shule zote chakavu ili kuwezesha mazingira ya wanafunzi wetu kusoma katika mazingira bora zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba kumhakikishia Mheshimiwa Esther Matiko kwamba, shule hiyo ya sekondari itapewa kipaumbele, ili fedha iweze kupatikana, kwa ajili ya ukarabati na kuboresha miundombinu chakavu ili wanafunzi waweze kusoma katika mazingira bora zaidi. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Charles Kajege, swali la nyongeza.

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Spika, wananchi wa Kisiwa cha Nafubo wameanza kuchangia, kwa ajili ya ujenzi wa sekondari yao. Je, ni lini Serikali itawashika mkono ili kukamilisha zoezi hilo? Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, moja ya vipaumbele vya juu kabisa ni kujenga miundombinu ya huduma

za jamii, ikiwemo shule katika maeneo magumu kufikika kijiografia na hususan maeneo ya visiwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge, kwanza tunawapongeza wananchi hao kwa kuanza na tunawatia moyo waendelee kuchangia nguvu zao katika ujenzi wa shule hiyo ya sekondari. Serikali hii sikivu itawashika mkono kwa kupeleka fedha ili kukamilisha ujenzi wa shule hiyo ya sekondari.

**SPIKA:** Mheshimiwa Boniphace Butondo, swali la nyongeza.

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO:** Mheshimiwa Spika, Kata ya Mwasubi ni moja kati ya kata ambazo hazina shule za sekondari na wanafunzi wamekuwa wakisafiri kwenda Sekondari ya Bunambiu. Nguvu za wananchi zimeshaanza kuchangiwa na sasa ujenzi wa madarasa mawili upo katika hatua ya lenta, unakwenda vizuri. Je, Serikali ina mpango gani kuhakikisha kwamba, inaweka nguvu za kutosha kukamilisha ujenzi huo?

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA – (MHE. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, namhakikishia tu Mheshimiwa Butondo kwamba, Mpango wa Serikali ni kujenga shule za sekondari za kata kila kata. Nawapongeza wananchi wa kata hiyo kwa kuanza kwa nguvu zao na waendelee kufanya hivyo, wakati Serikali inatafuta fedha, kwa ajili ya kwenda kukamilisha shule hiyo ya sekondari. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Dkt. Jasson Samson Rweikiza, Mbunge wa Bukoba Vijijini, sasa aulize swali lake.

Na. 132

**Tanzania Kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa Kujikinga na Bidhaa za Nyuklia**

**MHE. DKT. JASSON S. RWEIKIZA** aliuliza:-

Je ni lini Tanzania itaridhia Mkataba wa Kimataifa wa Kujikinga na Bidhaa za Nyuklia?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, kwa niaba ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Patrobass Katambi, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU K.n.y. WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Elimu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Jasson Samson Rweikiza, Mbunge wa Bukoba Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatarajia kukamilisha mchakato wa kuridhiwa kwa Mkataba wa Kimataifa wa Kujikinga na Bidhaa za Nyuklia kabla au ifikapo tarehe 30 Juni, 2025. Aidha, mkataba huo umeshawasilishwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kufanyiwa uridhiwaji. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Jasson Rweikiza, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. JASSON S. RWEIKIZA:** Mheshimiwa Spika, nina maswali mawili ya nyongeza pamoja na shukrani kwa jibu zuri. Swali la kwanza; swali langu lilihusu Mkataba wa Kimataifa wa Kuzuia Vitendo vya Kigaidi kwa kutumia Nyuklia *(International Convention for the Suppression of Acts of Nuclear Terrorism)*. Sasa jibu limehusu Mkataba wa Kimataifa wa Kujikinga na Bidhaa za Nyuklia. Je, wana maana hiyo hiyo au ni mkataba mwingine tofauti?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kama jibu ni ndiyo, je, mnafahamu kwamba tukijiunga na mkataba huo wa kuzuia vitendo vya kigaidi kwa kutumia nyuklia *(ICSANT)*, hakuna malipo yoyote ya mwanzo wala ya kila mwaka...

**SPIKA:** Mheshimiwa Sanga, keti kwanza. Malizia swali lako la pili.

**MHE. DKT. JASSON S. RWEIKIZA:** Mheshimiwa Spika, swali la pili; kama jibu la swali la kwanza ni ndiyo, je, Serikali inafahamu kwamba tukijiunga na huu mkataba wa Kimataifa wa kuzuia vitendo vya kigaidi kwa kutumia nyuklia, hakuna malipo yoyote ya mwanzo au ya kuendelea na kila mwaka *(initially)*. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Rweikiza, Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza ameuliza kuhusiana na swali lake na jinsi ambavyo tumelijibu kama ni sahihi. Kujikinga na kutokomeza, yote ni katika tafsiri na mikataba hii ya kimataifa iko katika maeneo matatu. Moja, upo mkataba wa kimataifa unaozuia kugandamiza vitendo vya kigaidi, huo ni wa mwaka 2005, lakini pia tunao mkataba wa kimataifa unaohusiana na masuala ya kutokomeza silaha za kinyuklia wa mwaka 2021. Yote hii inalenga katika kuhakikisha kwamba kunakuwa na matumizi sahihi ya nyuklia pamoja na matumizi salama ya nyuklia duniani.

Mheshimiwa Spika, katika ile mikataba ni *crosscutting* kwa maana kwamba inahusianisha pia Wizara nyingi, Wizara ya Ulinzi na Wizara ya Elimu, kwa maana kwamba sisi tuna tume maalum ambayo ni Tume ya Nguvu za Atomu. Ambapo kwa pamoja waliweza kufanya kazi kupitia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na Wakala wa Kimataifa wa Nguvu za Atomu,

kuweza kuhakikisha kwamba tunaingia kwenye mkataba huo tukiwa tunatambua kwamba utakuwa salama na utaleta matumizi sahihi ya kinyuklia.

Mheshimiwa Spika, tunatambua sisi tunayo *uranium* hapa nchini, hatua ambazo tumekwisha kuzifikia katika kuipembua mikataba yote hiyo ile ambayo inatengeneza bidhaa za madawa, silaha au kemikali zinazoweza kuleta athari, yote hii tunaipitisha katika chujio la kuanza kwanza na hatua ya kupitiwa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, hatua ya pili ni kuwa na maoni ya wadau mbalimbali juu ya matumizi sahihi ya hizo nyuklia na hatua ya tatu ni kupeleka katika Kamati ya Baraza la Mawaziri kwa ajili ya ushauri na baadaye mapendekezo hayo yataletwa Bungeni na kama itapendeza basi Bunge hili litaweza kusaini na kuridhia mikataba hiyo ya kimataifa.

Mheshimiwa Spika, kwenye eneo la pili aliuliza kuhusiana na kwamba, Serikali inatambua kuwa ni bure. Ni kweli mikataba mingi ambayo inahusianisha *United Nations Council* hasa *Security Council,* inayoleta matumizi ya kemikali hasa zile ambazo zinaweza zikaathiri aidha usalama au uhai wa wanadamu, kwa mara nyingi imekuwa ni jitihada ya Umoja wa Mataifa pamoja na nchi wanachama kuweza kuhakikisha kwamba wanachama hawaingii kwenye gharama au tozo ili kuweza kuhakikisha kwamba dunia inakuwa sehemu salama.

Mheshimiwa Spika, ninatambua kwamba Mheshimiwa Rweikiza ni *Member* wa *Parliamentary for Global Action*, nafahamu kwenye vikao vyao wanayajadili haya. Kwa hiyo, tunatambua hilo na ndiyo maana tunapitisha mchakato sahihi wa Serikali ili tukiridhia tuweze kuwa na faida na tija kwa ajili ya Taifa letu. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Rweikiza, huu Mkataba wa *International Convention for the Suppression of Acts of Nuclear Terrorism*, ni wa mwaka gani?

**MHE. DKT. JASSON S. RWEIKIZA:** Mheshimiwa Spika, mkataba huu ni wa mwaka 1971.

**SPIKA:** 1931!

**MHE. DKT. JASSON S. RWEIKIZA:** Mheshimiwa Spika, 1971.

**SPIKA:** 1971?

**MHE. DKT. JASSON S. RWEIKIZA:** Mheshimiwa Spika, ndiyo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, najua haya majibu yametayarishwa na Wizara ya Elimu, sasa wao wametaja mkataba tofauti na ule ambao Mheshimiwa Mbunge ameuliza. Kwa sababu yeye ameuliza *International Convention for the Suppression of Acts of Nuclear Terrorism* wa 1971. Humu kwenye majibu kunaonekana mkataba uliotajwa ni mwingine.

Kwa hiyo, ndiyo maana Mheshimiwa Mbunge alikuwa anauliza ni wenyewe au siyo wenyewe. Kwa hiyo, kwa bei ya jina, mkataba ni tofauti na kama yote inalenga kitu kimoja, sidhani kama ingetengenezwa miwili halafu yote inatoka sehemu moja, labda kama huu mwingine umekuja kwa ajili ya kujazia ule mwingine, lakini Mheshimiwa Mbunge alipaswa ajibiwe kwa mkataba ule ambao yeye ameuulizia.

Kwa hiyo, kwa sababu hili jibu limetayarishwa na Wizara nyingine, ninashindwa kukuuliza wewe maswali mengine. Ninaona unataka kusema jambo?

Nataka niwarejeshee ili wamjibu Mheshimiwa Mbunge swali ambalo yeye ameuliza. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Spika, kimsingi kilichojibiwa hapa na Wizara kwa kutumia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa ushirikiano na Tume ya Nguvu Kazi za Atomu, ambayo ilifanya kwa pamoja kwa ushirikiano na Wakala wa

Kimataifa wa Nguvu za Kiatomu, majibu yaliyotolewa hapa ni yale ya ujumla ya mikataba yote inayohusiana na masuala ya kinyuklia, ambayo...

**SPIKA:** Yeye ameuliza wa kwake maalum, ndiyo maana alikuwa anauliza lile swali la kwanza. Kwa sababu yeye ameulizia mkataba fulani; yeye hataki yale ya jumla, nyuklia na nini, yeye anataka wa kwake ujibiwe. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Spika, itakuwa ni *context* ya swali, lakini bado haidhuru pia, tuko tayari kulijibu kwa jinsi ambavyo utaona inapendeza. Ahsante.

**SPIKA:** Aaah, kwa hiyo, uko tayari kumjibu hapa au niwarejeshee ili wakalete majibu ya Mbunge?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Spika, ninadhani swali liwe *customized* ili tuweze kujua *specific* ili kuwa na majibu sahihi ambayo yanaendana na hilo. Kwa hiyo, tuko tayari kulipokea kwa ajili ya marekebisho.

**SPIKA:** Sawa Mheshimiwa, ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, swali la Mheshimiwa Dkt. Jasson Samson Rweikiza litajibiwa upya na Serikali ili liweze kujibu kile ambacho Mheshimiwa Mbunge alikuwa ameuliza. Pia, kwa sababu hii ndiyo Wizara ya Elimu, kwa kweli tunapaswa kujielimisha na kwenye mambo mengine.

Hiki Kiswahili cha "Mkataba huo umeshawasilishwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kufanyiwa Uridhiwaji", Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali hairidhii mikataba. Kwa hiyo, ukileta jibu kama hili na hii ndiyo Wizara ya Elimu, kidogo inaleta mtihani.

Haya maneno hapa mwisho ya kufanyiwa uridhiwaji, kwanza hicho Kiswahili sijakielewa, sijui kitenzi ni kipi, sijui kipi ni kipi? Tunaelekea kwenye Kiswahili fasaha jamani. Kufanyiwa uridhiwaji, aah Hapana! Siyo Kiswahili sanifu. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge kwenye swali lako 132, majibu yataletwa mapya. Watakapokuwa tayari watatuletea na tutalipanga kama utaratibu ulivyo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Wizara ya Maji, Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 133

**Upungufu wa Maji Mji Mdogo wa Karatu**

**MHE. CECILIA D. PARESSO** aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuondoa tatizo la upungufu wa maji katika Mji Mdogo wa Karatu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, Mhandishi Kundo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, hali ya upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama katika Mji Mdogo wa Karatu ni wastani wa 75%. Mahitaji ya maji katika Mji huo ni wastani wa lita 8,750,000 kwa siku wakati uzalishaji ukiwa ni wastani wa lita 5,919,000 kwa siku.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha huduma ya maji inakuwa toshelevu kwenye Mji huo, Serikali inaendelea na utekelezaji wa Mradi wa Maji wa Bwawani Na. 3 kwa ajili kunufaisha kata tatu za Karatu, Ganako na Qurus. Mradi huo umefikia wastani wa 77% za utekelezaji na unatarajiwa kukamilika mwezi Oktoba, 2025.

Mheshimiwa Spika, vilevile, katika bajeti ya Mwaka wa Fedha 2024/2025, Serikali itatekeleza mradi wa kuongeza uzalishaji wa maji katika Mji huo kwa kuchimba kisima kimoja pamoja na kuendeleza visima viwili vilivyopo katika eneo la Qorong'aida.

Mheshimiwa Spika, aidha, kazi zingine zitakazotekelezwa kupitia mradi huo ni pamoja na ujenzi wa tanki la lita 50,000, ukarabati wa matanki manne yenye jumla ya ujazo wa lita 625,000 na ununuzi na ufungaji wa dira za maji 2,000. Mradi huo utatekelezwa kwa muda wa miezi 18 ambapo unatarajiwa kukamilika mwezi Mei, 2025. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso, swali la nyongeza.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwanza, naishukuru na kuipongeza Serikali kwa majibu na kwa jitihada ambazo zinaendelea ili kuhakikisha kwamba upungufu wa maji unakwisha kabisa. Swali la kwanza, Je, Serikali sasa inawahakikishiaje wananchi kwamba, miradi hii ikikamilika upungufu huu wa maji katika Mji wa Karatu unakwisha kabisa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Je, Serikali haioni ni wakati sasa wa kuipatia ruzuku miradi ya maji iliyoko pembezoni mwa Mji wa Karatu ambayo inaendeshwa na Bodi ya Wananchi ikiwemo Endawasu, Gewasu na Mowasu ili wananchi waweze kupata maji kwa uhakika? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu swali la nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, Serikali inatambua changamoto kubwa iliyopo, lakini mradi huu utakapokamilika siyo kwamba changamoto itaisha kwa 100%, isipokuwa huduma ya

upatikanaji wa maji katika mji huo itaongezeka kutoka 75% mpaka kufikia 82%. Kwa hiyo, tutaendelea kuhakikisha kwamba tunasanifu miradi ambayo itaenda kupanua wigo wa upatikanaji wa maji mpaka kufikia katika hatua ambayo itaridhisha kwa wananchi wote kupata hiyo huduma ya maji safi na salama.

Mheshimiwa Spika, vile vile, katika kipengele cha pili, ninaendelea kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kazi kubwa ambayo anaendelea kuifanya nasi tunatambua Bodi za Maji za Gewasu, Endawasu pamoja na Mowasu ni bodi ambazo bado zinasimamiwa na Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini *(RUWASA)*.

Mheshimiwa Spika, maana yake ni kwamba, hata ujenzi wa miradi yenyewe inajengwa na *RUWASA*, pia tumeshapata mtaalam mshauri ili kwenda kuangalia namna bora ya kuendelea kupata vyanzo vingine vya maji ili tujenge mtandao ambao utakaowafikia wananchi wote ili waweze kupata huduma ya maji safi na salama.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge, Serikali kupitia Wizara ya Maji tunaendelea kuifanya kazi hiyo vizuri sana. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Martha Nehemia Gwau, swali la nyongeza.

**MHE. MARTHA N. GWAU:** Mheshimiwa Spika, suala la upungufu wa maji bado linakabili Wilaya za Manyoni, Iramba na Singida Mjini. Ni lini mradi wa Miji 28 utakamilika ili kutatua changamoto hiyo iliyopo kwa sasa? Ninashukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Mbunge, lakini na Waheshimiwa Wabunge wote ambao wanaendelea kuupambania Mradi huu wa Miji 28. Bahati nzuri wiki moja iliyopita nilikuwepo Manyoni kukagua utekelezaji wa mradi huo na namna ambavyo unaenda kukamilika. Ifikapo Oktoba mwaka huu mradi huu utakuwa umekamilika na wananchi watapata huduma ya maji safi na salama. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Aysharose Mattembe, swali la nyongeza.

**MHE. AYSHAROSE N. MATTEMBE:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa nafasi. Ninapenda kufahamu ni lini sasa Serikali itakamilisha miradi yote ya maji katika Mkoa wa Singida? Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu swali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni dhamira ya Serikali inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na kwa maelekezo mahsusi ni kwamba, kuna miradi zaidi ya 1,000 inayoendelea kutekelezwa nchi nzima na kuna miradi ambayo inaendelea kutekelezwa ndani ya Mkoa wa Singida.

Mheshimiwa Spika, miradi hii iko katika hatua mbalimbali za utekelezaji, kwa hiyo, ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwa kadri watakavyokuwa wanaomba pesa za kulipa kulingana na madai ya wakandarasi, basi miradi hiyo itaendelea kukamilika kulingana na mkataba ambao tutakuwa tumeingia na wakandarasi. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dorothy Kilave, swali la nyongeza.

**MHE. DOROTHY G. KILAVE:** Mheshimiwa Spika, je, Serikali mna mkakati gani wa kumaliza mgao wa maji ndani ya Kata za Buza,

Kilakala, Makangarawe na nyinginezo ndani ya Jimbo la Temeke? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, Temeke na kwa Mkoa wa Dar es Salaam chanzo chake cha maji ni kutoka Mkoa wa Pwani. Tuko katika upanuzi wa vyanzo vya maji kwa kuanzisha miradi mbalimbali ili lengo tuwe na maji ya kutosha.

Mheshimiwa Spika, tukiwa na maji ya kutosha, maana yake ni kwamba tutakiwa na uwezo wa kuwafikishia wananchi wote maji kwa wakati wote bila kuwa na mgao. Kwa sasa ni lazima tukiri kwamba, mgao bado upo, lakini tunahakikisha mgao huu unakuwa *predictable*. Maana yake tukishasema Jumatatu au Jumatano, basi watu wa maeneo husika waweze kuwa na uhakika wa kupata maji katika siku hizo ambazo tumewapangia mgao huo.

Mheshimiwa Spika, juhudi za Serikali zinaendelea; tunaendelea kujenga mabwawa mbalimbali, lengo ni kuhakikisha kwamba tunapata zao la maji la kutosha ili wananchi wa Kinondoni, Kibamba, Temeke na wa Kigamboni, wote wapate huduma ya maji safi na salama na yawe toshelevu na yenye gharama ambayo inakubalika. Ahsante sana.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ninawaona mmesimama. Ulizeni maswali mafupi, nenda moja kwa moja kwenye swali, Mheshimiwa Naibu Waziri naye atawapa majibu mafupi. Mheshimiwa Mwita Waitara, swali la nyongeza.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Spika, Mradi wa Maji kutoka Ziwa Victoria kwenda Sirari, Nyamwaga na Nyamongo, umesimama kabisa na Tarime kwa ujumla wake kuna shida ya maji. Je, nini kauli ya Serikali ili mradi uweze kuendelea ili watu wa Tarime wapate maji? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge, lakini hapa Katikati tulikuwa na changamoto, tunawashukuru sana Wizara ya Fedha na tunamshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa maelekezo ya kutoa fedha kwa wakandarasi wanaotekeleza miradi mikubwa na ya kimkakati ili wakandarasi warudi *site* na waendelee na utekelezaji ili miradi hiyo ikamilike.

Mheshimiwa Spika, kati ya miradi ya kimkakati ni pamoja na mradi ambao Mheshimiwa Mbunge ameutaja. Ninakuhakikishia kuwa tutaendelea kuhakikisha kwamba, miradi yote ambayo inaenda kuleta mabadiliko na kuongeza upatikanaji wa huduma ya maji, tutaisimamia kikamilifu ili iweze kukamilika kwa wakati. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, swali la nyongeza.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Spika, je, ni lini maji kutoka *Lake Victoria* yatafika Urambo ili tumalize tatizo kubwa la maji tulilonalo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, mradi wa kufikisha maji kwenda Urambo unatokana na mradi mkubwa ulioanza wa shilingi bilioni 680, ambapo *extension* yake ni Urambo pamoja na Kaliua. Tayari shilingi bilioni 143 imetengwa kwa ajili ya mradi huo na sasa mabomba yameshafika *site* na mradi huu uko katika 65%. Tunatarajia muda siyo mrefu ninaamini kwamba kabla ya mradi wenyewe kukamilika kuna maeneo mengine yataanza kupata huduma ya maji wakati utekelezaji ukiwa unaendelea katika kukamilisha. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ritta Kabati, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, je, ni lini Mradi wa Maji wa Kata ya Ng'ang'ange utaanza kufanya kazi kwa

sababu toka mwaka jana ulikuwa umesainiwa na Serikali? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ninaukumbuka mradi huu kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge ameuongelea, uko katika Jimbo la Kilolo. Bahati nzuri katika utiaji wa Saini nilikuwepo mimi mwenyewe, ilikuwa mwaka jana mwezi Mei. Mkataba huu ni wa miezi 12 ambao gharama yake ni zaidi ya shilingi milioni 987 na mkandarasi mpaka sasa ameshalipwa shilingi milioni 148 na kazi hii inatekelezwa na Mkandarasi *anaitwa Afrocentric Company Limited*.

Mheshimiwa Spika, tunaamini kabisa kwamba kwa kazi ambayo tayari ameshaianza, ameshajenga *foundation* ya tenki na ameshaleta mabomba, kwa hiyo tunaamini kwamba, kwa kasi anayoenda nayo tunaamini kwamba atakamilisha ndani ya muda wa mkataba ambao tulikubaliana naye. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Ally Mchungahela, swali la nyongeza.

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Mheshimiwa Spika, Mradi wa Mbangala umekuwa ukitengewa bajeti takribani kwa miaka mitatu sasa. Ni lini mradi huu utaanza kujengwa? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ninamshukuru sana Mheshimiwa Mbunge na labda nikiri kwamba nimeshafanya ziara kwenye Jimbo lake na tulikuwepo wote, huu ni mradi wa kimkakati katika eneo la Mheshimiwa Mchungahela.

Mheshimiwa Spika, Serikali tukipata fedha mradi huu utaanza mara moja ili wananchi wa eneo hilo wapate huduma ya maji safi na salama. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia swali la nyongeza. Je, kuna mkakati gani wa kupunguza tatizo la maji katika Kata ya Mikese na hasa Tarafa ya Mtego wa Simba?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, mkakati wa Serikali kwanza kabisa ni kuendelea kubainisha vyanzo vya maji ambavyo vitatuongezea maji katika mtandao wetu, lakini vile vile ni kuhakikisha kwamba tunaendelea kulinda vyanzo vya maji pamoja na kujenga mtandao ili uendelee kuwafikia wananchi.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutatuma timu yetu ikafanye utafiti ili tujiridhishe fedha kiasi gani zinahitajika, ili tufahamu kwamba kama tutahitaji kujenga mradi mpya tujenge mradi mpya kama itahitaji kufanya *extension* ya mradi uliopo basi tutafanya hivyo ili wananchi wa kata hiyo waweze kupata huduma ya maji safi na salama.

**SPIKA:** Mheshimiwa Genzabuke swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Maji yanayotoka katika Mji wa Kasuru hayafai kwa matumizi ya binadamu, ni machafu sana. Je, ni lini Serikali itamaliza tatizo hilo la maji katika Mji wa Kasuru?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Kasuru, kwanza kabisa tuna mradi wa zamani ambao ulikuwepo. kwa bahati nzuri nilifanya ziara Mkoa wa Kigoma na hususani eneo la Kasuru; lakini pia tuna Mradi wa Miji 28 unaoendelea kutekelezwa pale, ambapo zaidi ya kata 19 zitapitiwa na mradi ule. Vilevile katika mradi wa zamani ambao ulikuwa unatumia maji kutoka kwenye kile chanzo kingine hatukuwa na chujio ambalo ndiyo ilikuwa changamoto ya watu kupata maji ambayo hayakuwa safi.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan ilitoa fedha kwa ajili ya kuanza kujenga chujio ili liweze kuyachuja maji na kuhakikisha kwamba tunapata maji safi, lakini pia tunayatibu ili tupate maji salama na pia tuwe na maji ya uhakika ambayo yatapatikana muda wote. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba chujio hilo litakapokamilika wananchi wa Kasulu watapata huduma ya maji ambayo yapo safi. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, kule nyuma ni Mheshimiwa Rehema Migilla umehama kiti ama? Ni Mheshimiwa Rehema Migilla?

**MHE. REHEMA J. MIGILLA:** Mheshimiwa Spika, ndiyo.

**SPIKA:** Umehama kiti, haya Mheshimiwa Rehema Migilla swali la nyongeza.

**MHE. REHEMA J. MIGILLA:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa nafasi. Ninapenda kuuliza swali dogo la nyongeza. Bwawa la Ichemba lilitengewa fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi lakini fedha zile zilirudishwa makao makuu hatujui sababu hatujui sababu za kurudishwa. Je, ni lini fedha zile zitarudishwa ili mradi uanze kufanya kazi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, naomba kwa heshima na unyeyekevu na kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri nipokee hii changamoto niende nikaone changamoto iliyojitokeza mpaka fedha zikarudishwa Wizarani wakati fedha hizi tunatakiwa kuzipeleka kule kwa ajili ya kwenda kutatua changamoto ya ujenzi wa miradi ya maji. Ninaomba nilipokee kwa ajili ya utekelezaji. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Maliasili

na Utalii, Mheshimiwa Profesa Patrick Alois Ndakidemi, Mbunge wa Moshi Vijijini, sasa aulize swali lake.

Na. 134

**Uzalishaji wa Asali Moshi Vijijini**

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani kuwasaidia wananchi wa Jimbo la Moshi Vijijini kuzalisha asali kwa kuwa kuna idadi kubwa ya miti inayoweza kutundikwa mizinga?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Dunstan Kitandula, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu wa ufugaji nyuki kwenye kuimarisha uhifadhi na kuongeza kipato cha wananchi wa Wilaya ya Moshi Vijijini Serikali kupitia Mfuko wa Misitu Tanzania imewezesha miradi minne ya ufugaji nyuki yenye thamani ya shilingi 32,270,000 kwa Shule ya Sekondari Komakya, Kikundi cha Jikomboe cha Kijiji cha Komela, Mradi wa Uanzishwaji wa Kitalu cha Miti na Upandaji Miti katika Shule ya Sekondari ya Weruweru na Mradi wa Uanzishwaji wa Vitalu vya Miti na Kuhamasisha Upandaji Miti katika Kata ya Mwika Kusini.

Mheshimiwa Spika, kwa upande mwingine, Serikali kupitia Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania inaendelea kuwajengea uwezo wafugaji nyuki wa Wilaya ya Moshi Vijijini, ambapo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 imepanga kuwezesha mizinga 40 na vifaa vingine vya ufugaji nyuki. Katika kuongeza wigo wa wanufaika wa miradi ya ufugaji nyuki, Wizara kupitia Mfuko wa Misitu Tanzania itaendelea kutoa elimu na kuhamasisha wananchi katika Wilaya ya Moshi Vijijini kuhusu namna ya kuandaa na kuwasilisha maandiko ya kuomba ruzuku kwenye mfuko wa misitu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Profesa Ndakidemi, swali la nyongeza.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali y a nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza. Wafugaji wengi wa nyuki katika Halmashauri ya Moshi na maeneo mengine ya vijijini Tanzania wanakosa elimu ya mbinu bora ya ufugaji wa nyuki. Je, Serikali ina mpango gani wa kuanzisha *program* za mafunzo haya kwa wananchi wetu hawa kupitia kwa Maafisa Ugani wa Nyuki hapa nchini?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Moja ya changamoto kubwa inayowakabili wafugaji nyuki wetu hapa nchini na hasa wale wa Jimbo la Moshi Vijijini na maeneo mengine ni ukosefu wa vifaa bora vya kufugia nyiki kama mizinga ya kisasa. Je, Serikali ina mikakati gani au mipango gani ya kutoa ruzuku kwa wafugaji hawa wa nyuki ili wapate hizi dhana waweze kufuga nyuki kwa uhakika?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuelewa kwamba sekta hii ili ikue suala la elimu ni muhimu. Serikali inaendelea kutoa mafunzo ya ufugaji nyuki katika chuo chetu cha ufugaji nyuki Tabora, lakini vile vile inatoa mafunzo kupitia Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine pamoja na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, wataalam hawa wanaopata mafunzo kwenye eneo hili wanatumika kwa kuajiriwa kwenye halmashauri zetu lakini vile vile wanaajiriwa na taasisi yetu ya *TFS*. Kupitia taasisi hizi na halmashauri zetu Serikali iliandaa mpango maalum wa mafunzo ambao unatumika na wataalam hawa kutoa mafunzo kwa wananchi kwenye maeneo yetu.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na swali lake la pili kuhusu ruzuku ya vifaa. Serikali kupitia Mfuko wa Misitu Tanzania ina mpango wa kutoa ruzuku kwa halmashauri zetu, lakini vile vile kwa wananchi wanaojiingiza kwenye Sekta hii ya Ufugaji wa Nyuki.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwafahamisha wananchi kwa ujumla kwamba tayari dirisha la kuomba ruzuku kupitia Mfuko wa Misitu limekwishafunguliwa. Dirisha hili litakuwa wazi mpaka mwezi Machi. Hivi nitoe rai kwa halmashauri zetu na wananchi wote kuitumia fursa hii ili kuweza kupata ruzuku ya ufugaji nyuki pamoja na vifaa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hassan Zidadu Kungu, Mbunge wa Tunduru Kaskazini, sasa aulize swali lake.

Na. 135

**Kupeleka Askari wa Kutosha wa Jeshi la Uhifadhi Tunduru**

**MHE. HASSAN Z. KUNGU** aliuliza:-

Je, lini Serikali itapeleka askari wa kutosha wa Jeshi la Uhifadhi Tunduru Kaskazini ili kumaliza athari zinazosababishwa na wanyama pori?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Wizara imepewa kibali cha kuajiri jumla ya askari 578 kupitia taasisi zake za uhifadhi. Askari hawa pamoja na majukumu mengine watatumika katika kushughulikia changamoto ya wanyamapori wakali na waharibifu kwenye maeneo ya wananchi ikiwemo Tunduru Kaskazini.

Mheshimiwa Spika, Wizara inatambua changamoto ya uchache wa askari katika Wilaya ya Tunduru kwani kwa sasa

jumla ya Askari wa Jeshi la Uhifadhi 18 na askari wahifadhi wa vijiji 60 wapo katika Wilaya ya Tunduru. Katika juhudi za kupambana na changamoto hiyo ya uchache wa askari, Serikali ina mpango wa kuongeza askari wa Jeshi la Uhifadhi kutoka askari waliopo sasa 18 hadi kufikia Askari wa Jeshi la Uhifadhi 25 na Askari Wahifadhi wa Vijiji kutoka 60 hadi 80.

Mheshimiwa Spika, sambamba na askari hao, Serikali imepanga kuongeza vitendea kazi kwa ajili ya taasisi za Jeshi la Uhifadhi Kanda ya Kusini ikiwemo magari tisa, pikipiki 10 na ndege nyuki tano kwa ajili ya kuwawezesha kuongeza ufanisi wa kukabiliana na wanyamapori wakali katika Wilaya ya Tunduru na eneo lote la Kusini.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hassan Zidadu Kungu, swali la nyongeza.

**MHE. HASSAN Z. KUNGU:** Mheshimiwa Spika, ninaishukuru Serikali kwa majibu mazuri yenye kuleta tija; lakini pamoja na majibu hayo mazuri naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza; naishukuru na kuipongeza Serikali kwa kutupatia ndege nyuki moja ambayo inafanya kazi kwa ufanisi mkubwa sana. Kwa kuwa tuna uhitaji mkubwa sana wa ndege nyuki, ndege nyuki ile inazidiwa. Je, ni lini hasa Serikali itatupatia ndege nyuki hizo tano ili zije kutatua kabisa changamoto?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; Wilaya ya Tunduru ina hekta za mraba 18,778 na tunayo magari mawili ya askari wa wanyamapori. Kati ya magari mawili hayo moja ndilo linalofanya kazi vizuri lakini moja lina changamoto, halifanyi kazi. Ninataka kufahamu. Je, ni lini hasa magari hayo tisa yaliyozungumzwa yataletwa Wilayani Tunduru ili kuweza kutatua changamoto hiyo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba eneo la Mheshimiwa Mbunge ni maeneo ambayo

yana changamoto kubwa ya wanyama wakali na waharibifu. Kwa kulitambua hili tayari Serikali kupitia wadau wa maendeleo na sisi wenyewe tumekwishanunua hizi ndege nyuki tano.

Mheshimiwa Spika, kinachofanyika sasa ni kuendesha mafunzo kwa askari wa vijiji 20 watakaotumika kuendesha ndege nyuki hizi. Mafunzo haya yanaendelea kwenye Chuo chetu cha Mafunzo ya Maliasili kwa Jamii Likuyu Sekamaganga. Tunategemea mafunzo haya yatakwisha kwenye tarehe 15 hii mwezi Februari. Baada ya kukamilika mafunzo haya tutaelekeza nguvu kwenye eneo hili.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na swali lake la pili la vifaa; mpango wetu kupitia taasisi zetu za uhifadhi ni kwamba tutaongeza magari tisa. Matarajio yetu ni kwamba ikifika mwishoni mwa mwezi Februari au mwanzoni mwa mwezi wa tatu magari haya yatakuwa yamekwishapatikana kulingana na zoezi la manunuzi na mara baada ya kupatikana tutayaelekeza kwenye maeneo haya.

**SPIKA:** Mheshimiwa Oliver Semuguruka, swali la nyongeza.

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona. Katika Wilaya ya Ngara Kata ya Kasuru tembo wamevamia mashamba ya wananchi, wamekula mahindi, wamekula maharage mapaka migomba. Ningependa kujua, je, Serikali inatusaidiaje kuhusiana na kupeleka askari wa wanyamapori katika eneo hilo ili kutatua changamoto hiyo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ni kweli tunazo taarifa kwamba tembo wametoka kwenye Pori la Kimisi kwenda kwenye eneo ambalo Mheshimiwa Mbunge amelisema.

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Mbunge kwa sababu jana alipopata taarifa hii mara moja alitupa taarifa

na sisi tulipowasiliana na askari wa uhifadhi kwenye eneo lile walisema ni kweli. Kuna timu ya utangulizi ya kundi la askari ilitumwa, lakini ilionekana kwamba kadhia iliyopo ni kubwa, kwa hiyo tumetoa maelekezo kwamba askari waongezwe zaidi ili kwenda kushughulikia tatizo hili. Tunalishughulikia, ninaomba Mheshimiwa Mbunge na wananchi wawe na subira wakati jambo hili linashughulikiwa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Abubakari Asenga, swali la nyongeza.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Tarafa ya Mang'ula na Kidatu bado zinasumbuliwa na tembo. Je, ni lini Wizara itatuongezea askari wa uhifadhi pamoja na vifaa ili kudhibiti hali hiyo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kwenye eneo hili kuna changamoto kubwa ya tembo na Serikali imefanya kazi kubwa. Eneo hili linalounganisha Hifadhi ya Udzungwa na Hifadhi ya Nyerere kuna ushoroba pale ambao ulikuwa umevamiwa. Serikali imefanya kazi kubwa sana ya kuongoa ushoroba ule kwa kujenga daraja la chini linalowezesha wanyama kupita. Hatua inayofuata sasa ni kuongeza askari katika eneo lile ili kuweza kukabiliana na changamoto hii ya wanyama wakali na waharibifu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge amekuwa akija mara kwa mara. Kama nilivyomweleza tulipokutana, kwamba tayari tumepata kibali cha askari 575. Ni imani yangu ni kwamba baada ya kupatikana kwa kibali hiki na askari hawa kuajiriwa tutaelekeza nguvu ya kuongeza askari kwenye eneo lake. Ninaomba awe na subira.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mhata, swali la nyongeza.

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mheshimiwa Spika, utumiaji wa ndegenyuki kwa ajili kukabiliana na wanyama haribifu, hasa

tembo, imeleta ufanisi mkubwa katika Wilaya ya Tunduru. Kwa kuwa Wilaya ya Tunduru inapakana na Wilaya yangu ya Nanyumbu. Je, Serikali haioni haja na sisi Wilaya ya Nanyumbu tukapatiwa ndegenyuki moja ili kukabiliana na wanyama hawa waharibifu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema, kwamba tayari tumekwishanunua ndegenyuki tano kwa ajili ya kuhudumia ukanda huu wa kusini. Mheshimiwa Mbunge awe na amani, ombi lake litakuwa ni sehemu ya maeneo ambayo yatapatiwa ndegenyuki hizi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Afya, Mheshimiwa Askofu Josephat Mathias Gwajima Mbunge wa Kawe sasa aulize swali lake.

Na. 136

**Matibabu ya Ugonjwa wa Seli Mundu**

**MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaanza Matibabu ya Wagonjwa Wenye Seli Mundu kwa kutumia *Crispr Gene Editing Technology*?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya Godwin Mollel, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali wakati wote inafuatilia tiba zote bora kabisa duniani na zinazotumia teknolojia bora na mpya, ikiwemo tiba ya *CRISPR Cas 9 Technology (Gene Editing)*.

Mheshimiwa Spika, *CRISPR Cas 9 Technology (Gene Editing)* ni tekinolojia ambayo toka imeanza kutumika kwa binadamu ni chini ya miaka miwili sasa. Aidha, wakati wa ziara ya Mheshimiwsa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan Nchini Marekani mwaka 2022 alifuatilia tiba hii. Mwaka 2024 wakati wa Mkutano wa Umoja wa Mataifa Mheshimiwa Rais aliwakilishwa na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; na suala hili lilikuwa moja ya ajenda iliyojadiliwa kwenye mikutano ya Waziri Mkuu na taasisi za tiba na teknolojia za Kimarekani, pia wagonjwa waliotibiwa na teknolojia hiyo walishiriki katika vikao hivyo.

Mheshimiwa Spika, mara tu teknolojia hii ya *CRISPR Cas 9 Technology (Gene Editing)* itakapoanza kutumika rasmi duniani kote kama tiba, sisi tutakuwa miongoni mwa nchi za kwanza kupokea kwani toka mwaka 2022 tumeanza kufanya matayarisho ya wataalam na tekinolojia. Kwa sasa nchini kwetu tiba hii tunatoa kwa kufanya upandikizaji wa uloto, huduma ambayo inafanyika katika Hospitali ya Benjamin Mkapa.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Askofu Josephat Gwajima, swali la nyongeza.

**MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ninaomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa *Gene Editing by CRISPR Cas Technology* ni matibabu ambayo yanahusu ku-*edit gene* ya mtu; kwa maana kwamba mtu anaingia kutibiwa halafu wanai-*edit gene* ya mtu kuingia kwenye *DNA*.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza. Je, pamoja na kwamba wameanza matayarisho Waziri anatuhakikishiaje kwamba mtu haingii kwenye matibabu halafu akafanyiwa *editing,* vitu vingine ambavyo ni utu wa mtu matokeo yake, *procedure* ikatoka na mtu wa pili badala ya mtu aliyeingia?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Je, Serikali inajiandaaje kuhusiana na kuleta Muswada Bungeni ili kuwe na sheria maalum zinazoongoza watu wanaoingia kwenye kufanyiwa *gene editing* ili kuzuia mtu asifanyiwe *editing* rangi ya macho, rangi ya ywele, rangi ya ngozi na *IQ* ya mtu na utu wa mtu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Baba Askofu Gwajima kwa sababu wakati wote yanapotokea mambo mapya na magumu duniani na ya tiba amekuwa akiwa anapaza sauti kutufikirisha zaidi. Nimhakikishie hata kipindi cha *Corona* alitoa mawazo mazuri sana yaliyotufikirisha, lakini niwaambie kwamba tunaye Jemedari Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye anaipenda Tanzania na ndiyo maana unaona hata wakati wa *Corona* alikuja akakubali chanjo wakati muafaka na sasa Watanzania wako salama baada ya hiyo chanjo kufanyika.

Mheshimiwa Spika, juzi mmeona dunia imekuja Tanzania na amepewa nishani ya namna ambayo ni ya kwanza kwa Rais wa Afrika kupewa. Alipewa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na haijatokea kwa bahati mbaya, imetokea kwa sababu ya uwezo wake wa kutafakari masuala ya afya na kuweka kanuni ambayo imeleta *solution* ambayo nchi nyingi za Afrika zimeshindwa na ndiyo maana dunia ilikuja Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Gwajima kuwa Jemedari tuliye naye nina hakika tuko salama. Ndiyo maana toka mwaka 2022 yeye mwenyewe amekutana na hao wanaofanya tiba hii na kujadiliana na kuanza kuiweka Tanzania kwenye *roll* kwa ajili ya usalama na mambo mengine.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, ni kweli kwamba kuna mambo yanaweza yakatokea. Kwa mfano, wakati wanaanza kufanya *experiment* za hili suala katika nchi nne kubwa duniani, mtaalam mmoja wa nchi hizo alitoka Marekani kwenye maabara zinazofanya hii akaenda akakutana na wazazi wenye *HIV*.

Mheshimiwa Spika, wale wazazi walipokutana, mbegu ya baba na mama ilipokutanishwa basi akaingia kwenye kizazi cha mama akachukua ile mbegu ya mama iliyorutubishwa na mbegu ya baba akaenda maabara halafu aka-*edit,* akatoa lile eneo la *gene* linalotoa kile kisehemu kinachosababisha mtu aweze kushika UKIMWI alivyotoa akarudisha kwenye tumbo la mama. Mwisho wa siku wakazaliwa watoto wawili ambao hawawezi kupata UKIMWI hata ukiwawekea ndoo nzima ya damu yenye UKIMWI hawawezi kupata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, mwanasayansi huyo kwenye nchi yake alikamatwa. Inawezekana alikamatwa kwa kufungwa kweli au kwa ajili ya nchi hiyo kuendelea kujifunza hiyo teknolojia zaidi kwa ajili ya kufanya biashara baadaye, lakini nikwambie, ni kweli kwamba lazima tutunge sheria za kuhakikisha tunawalinda wahuni wasifanye chochote kwa kutumia hii teknolojia.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, imeshaonekana duniani kuna umuhimu wa kanuni na mambo mengine, lakini hii inahusu *gene editing.* Mki-*edit* maana yake unasababisha mtu anabeba mwilini kwako na ataambukiza kwa watoto wake na watoto wake watakuja kuoa watoto wako kwa hiyo hakuna atakaye kuwa salama. Kwa hiyo, yeyote atakayecheza hata na yeye atapata matatizo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nilishindwa kumkatisha kwa sababu majibu ni ya kitaalam sana. Kwa hiyo, nikaona amalize kwanza ya kitaalam vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Ghati Chomete, swali la nyongeza.

**MHE. GHATI Z. CHOMETE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa nafasi ya swali. Ninampongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuwezesha huduma hii ya uroto katika Hospitali ya Benjamini Mkapa na kuokoa maisha ya watoto wengi wa kitanzania. Je, ni lini sasa huduma hii itashuka katika Hospitali ya Mkoa wa Mara? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa sababu wakati wote amekuwa mpiganaji muhimu kwa wananchi wa Mkoa wa Mara, lakini nimwambie kwamba Rais wetu amewekeza sana kwenye eneo la teknolojia. Maana yake ili hili liweze kushuka mikoani unahitaji teknolojia na utaalam na tayari Rais wetu kwenye teknolojia ameshawekeza kwenye hospitali zetu na kwenye majengo kwa maana ya hospitali za kanda zinatoa moja.

Mheshimiwa Spika, tukikamilisha hospitali zote za kanda zikawa zinatoa huduma hii, tutaanza kushuka hospitali za mikoa na ndiyo maana unasikia *Dr. Samia Specialized Scholarship* zile za kwenda kutengeneza Madaktari Bingwa. Ni mkakati maalum wa Rais wetu wa kupeleka madaktari duniani wanakuja na ujuzi mbalimbali na sasa wakija tutakuwa na madaktari, watashuka chini kwa sababu Rais wetu ameshawekeza kwenye eneo la teknolojia. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Ujenzi, Mheshimiwa Dkt. Christina Christopher Mnzava, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 137

**Ujenzi wa Barabara ya *Old* Shinyanga hadi Solwa**

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA** aliuliza:-

Je, lini ujenzi wa Barabara ya *Old Shinyanga* hadi Solwa utaanza?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Mheshimiwa Mhandisi Godfrey Kasekenya Msongwe, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kazi ya ujenzi wa Barabara ya *Old* Shinyanga hadi Solwa yenye urefu wa kilometa 64.7 imeanza kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha. Katika eneo la Solwa, kipande chenye urefu wa mita 400 kimejengwa na kukamilika mwezi Agosti, 2024. Kwa sehemu iliyobaki, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuendelea na ujenzi, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Christina Mnzava, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kama ulivyosema kwenye jibu lako la msingi kwamba ni mita 400 tu ambazo zimejengwa kwa hiyo bado kama kilometa 64 hazijajengwa. Je, ni lini sasa Serikali itapata fedha ili barabara hii ianze kujengwa?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; Barabara ya kutoka *Old* Shinyanga kwenda Solwa inaunganisha Manispaa ya Shinyanga kwa maana ya Mkoa kwenda kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, lakini kipindi cha mvua haipitiki na tumeona juhudi kubwa zilizofanywa na Serikali kwa kujenga lami katika Halmashauri ya Msalala, Bulige, Segese na sehemu nyingine na kuweka taa.

Mheshimiwa Spika, je, kwa sababu Halmashauri ya Shinyanga ndiyo makao makuu na hakuna hata kilometa moja, ni lini Serikali itaweza kutujengea angalau mita chache katika Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Ninaomba kujibu maswali ya Mheshimiwa Mbunge kwa pamoja.

Mheshimiwa Spika, tunatambua kwamba barabara hii pia ndiyo inayopita katika Makao Makuu ya Halmashauri na tulishapokea maombi rasmi ya mkoa kwa maana kwamba tufikishe barabara hii mpaka makao makuu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kujenga kipande cha lami walau kifupi katika eneo la halmashauri, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutalifanyia kazi, kwa sababu mpango ni kwamba katika maeneo yote ya Makao Makuu ya Wilaya au Halmashauri, basi eneo linalohusu huo mji liweze kuwa na lami.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutalichukua na kulifanyia kazi ikiwa ni pamoja na ombi la *RCC* kuunganisha Mji wa Shinyanga na Halmashauri ya Shinyanga *DC*. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Stephen Byabato swali la nyongeza.

**MHE. STEPHEN L. BYABATO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa nafasi. Wanabukoba tunamshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia kwa kufanya miradi ya kimageuzi katika mkoa wetu na Bukoba Mjini tukiwemo. Sasa ujenzi wa barabara ya njia nne katika Mji wa Bukoba Mjini unaogharimu shilingi bilioni 12.4 tayari umeshaanza, naomba kufahamu ni lini mradi huu utakamilika? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli tuna mradi wa kujenga kutoka barabara mbili kwenda barabara nne na tumegawanya katika vipande viwili. Kipande cha kwanza kiko karibu 44%. Kwa mujibu wa mkataba tunategemea kufikia mwishoni mwa mwezi Mei iwe imekamilika. Kipande cha pili kikihusisha na Mto wa Kanoni ambao tumetumia hela za *emergency* kwa sababu kunakuwa na mafuriko; kwa mujibu wa mkataba tunategemea ikamilike mwezi Desemba mwaka huu. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, wote mliosimama nimewaona, tatizo mnauliza maswali kwa kirefu, kila mtu anataka atoe na historia kwenye kipindi cha maswali; hiyo, ndiyo changamoto. Kwa hiyo, hamwezi kupata wote kwa sababu ya

hiyo changamoto. Mheshimiwa Hussein Nassor Amar, swali la nyongeza.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa kuwa nikiwa nauliza kila mara kuweza kupata jibu la lini Mshauri Mwelekezi kwa ajili ya barabara yetu inayounganisha Wilaya tatu: Kahama, Nyangh'wale, Busisi-Sengerema, ni lini atapatikana maana hata juzi niliuliza Waziri akasema kwamba nimfuate, tuongee, sasa leo ninataka anijibu kwenye Bunge hili Tukufu. Ni lini sasa Mshauri huyu atapatikana? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli aliuliza swali na ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Nyangh'wale kwamba barabara hii inaunganisha Mikoa mitatu, Geita, Mwanza na Shinyanga na *junction* ni Mji wa Nyangh'wale. Ninataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, tunavyoongea sasa hivi mikataba ipo kwa Mwanasheria Mkuu kwa ajili ya kupitiwa kwa mara ya mwisho na tunategemea kwamba mwezi Machi baada ya mwezi huu wa Februari, Mhandisi Mshauri atakuwa *site* kwa ajili ya kuanza upembuzi yakinifu na usanifu wa kina. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ally Mlaghila Jumbe, swali la nyongeza.

**MHE. ALLY A. J. M. JUMBE:** Mheshimiwa Spika, ni lini Barabara ya kutoka Matema – Lyulilo - Ikombe itafikia mwisho kwa kilometa mbili zilizobaki? Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, barabara aliyoitaja Mheshimiwa Mbunge alikuja ofisini na baada ya kueleza changamoto ambazo zinawakabili wananchi, Wizara iliagiza Makao Makuu *TANROADS* wamwagize Meneja wa *TANROADS* Mkoa wa Mbeya aende akafanye tathmini ili aweze kuleta mapendekezo ya haraka nini kiweze kufanyika ili kuondoa adha

ya wananchi ambayo wanaipata katika barabara hiyo ambayo Mheshimiwa Mbunge ameisema. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hassan Mtenga, swali la nyongeza.

**MHE. HASSAN S. MTENGA:** Mheshimiwa Spika, naomba Serikali iwaeleze wananchi wa Mtwara kwenye upanuzi wa Barabara ya kutoka Mtwara - Mnivata mpaka Masasi, wale ambao waliahidiwa watalipwa fidia na wakapeleka *documents* zao zote pamoja na kufungua akaunti za kuingizia hizo fedha. Je, ni lini Serikali itawalipa fidia wananchi hao ambao walipisha ujenzi wa Barabara ya Mtwara? Ninakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Mtwara kwamba tayari tuko kwenye maandalizi ya kupata hizo fedha ili tuweze kuwalipa kwenye huo mradi ambao unaendelea. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jacqueline Msongozi, swali la nyongeza.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa Barabara ya *bypass* Songea Manispaa? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, bahati nzuri Barabara hiyo ya *Songea bypass* ndiyo inayounganisha na ukarabati mkubwa wa Barabara ya Songea kwenda Lutukira hadi Njombe. Sasa hivi tunavyoongea Mkandarasi yupo *site* na tayari tumeshaanza kuwalipa fidia wananchi ambao watapisha hiyo barabara. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tayari mkandarasi ameshapatikana na tayari yupo *site,* tumeshalipa fidia ili kazi ianze, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mussa Sima, swali la nyongeza.

**MHE. MUSSA R. SIMA:** Mheshimiwa Spika, ni lini Barabara ya *bypass* ya kilometa 46 itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami ukizingatia upembuzi yakinifu tayari? Ninashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, barabara hiyo imeshafanyiwa usanifu wa *bypass* ya Singida na Serikali tunaendelea kutafuta fedha ili tuweze kuijenga kupunguza msongamano mkubwa ambao sasa upo katika Mji wa Singida, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hawa Mchafu, swali la nyongeza.

**MHE. HAWA M. CHAKOMA:** Mheshimiwa Spika, Mradi wa Njia Nane Kibaha Maili Moja hadi Chalinze upo katika hatua ipi?
**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, Chalinze sija… labda nimwelewe vizuri…

**MHE. HAWA M. CHAKOMA:** Mheshimiwa Spika, Mradi wa Njia Nane unaoanzia Kibaha Maili Moja hadi Chalinze uko katika hatua ipi?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ni mwendelezo wa Barabara ya Kimara kwenda Kibaha. Hii barabara tunategemea tuijenge kwa Mfumo wa *PPP*.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, sasa hivi ipo kwenye hatua za usanifu na baada ya hapo nadhani wakandarasi ambao wamejitokeza tutatafuta mkandarasi ambaye anaijenga na ni mwendelezo kutoka Kibaha hadi Morogoro na Morogoro hadi Dodoma, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Innocent Kalogeris.

**MHE. INNOCENT E. KALOGERIS:** Mheshimiwa Spika, ni lini mkandarasi wa Barabara ya Bigwa – Kisaki atapata *advance payment* ili aweze kuingia kikamilifu katika kutekeleza majukumu yake na kuwaokoa wananchi katika adha ya kukwama hasa katika kipindi cha mvua? Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, Barabara aliyoitaja ya Bigwa - Kisaki kilometa 78 ilishapata mkandarasi na barabara zote ambazo zilikuwa zimekwama kwa kusubiri *advance,* nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge sasa hivi tumeshaanza kutoa fedha na barabara nyingi ikiwemo hiyo ipo kwenye mpango ambao tuna uhakika muda siyo mrefu itapata *advance* ili mkandarasi aendelee na kazi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Issa Mtemvu, swali la nyongeza.

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Spika, Barabara ya Victoria - Mbezi Shule - Mpiji Magohe imetangazwa kwa kilometa 12 zaidi ya miezi sita na mkandarasi bado hajapatikana. Je, ni lini mkandarasi atapatikana na barabara hii itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami? Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge hata Wizara tunajua umuhimu wa barabara hiyo ambayo itakuwa ni mkombozi mkubwa sana kwa foleni ambayo ipo katika Jimbo la Mheshimiwa. Taratibu zinazoendelea ni za kupata huyo mkandarasi sahihi, tulishatangaza na kwa hiyo taratibu za manunuzi zitaendelea. Tukishakamilisha mkandarasi ataingia *site* kuanza ujenzi huo muhimu wa Barabara, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka, swali la nyongeza.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Spika, Barabara inayotoka Arusha, Orkesumet - Kibaya – Kongwa ambayo ni barabara ya *EPC+ Finance* itaanza kujengwa lini kwa kiwango cha lami? Nakushukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, nimekuwa nikijibu mara kadhaa kuhusu hiyo barabara ambayo ilikuwa ni moja ya zile barabara saba ambazo zilikuwa kwenye utaratibu wa *EPC + F.* Mara kadhaa nimekuwa nikieleza Bunge hili kwamba tumebadilisha utaratibu; Kamati imeundwa na kutafuta utaratibu.

Mheshimiwa Spika, tutawatumia walewale wakandarasi, lakini tutajenga kwa utaratibu tofauti. Hii imeundwa kuona kwamba wakandarasi ambao tulikuwa tumewapata ikiwezekana ndiyo waweze kufanya hiyo kazi, ikiwepo na hiyo barabara ambayo Mheshimiwa Ole-Sendeka ameitaja, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Josephat Kandege, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona, Barabara ya kutoka Matai kwenda *Kasesha Border* ni barabara muhimu sana na sasa hivi mkandarasi hayupo. Je, ni lini atalipwa fedha ili ujenzi uendelee?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli barabara ilishaanza na mkandarasi ailikuwa *site,* lakini tunachofanya sasa hivi ni kutafuta fedha ili mkandarasi huyo aendelee na kazi kwa kuendelea kulipa *IPC* ambazo amezileta Wizarani. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba muda siyo mrefu mkandarasi huyo ataanza kuendelea na hiyo kazi ambayo alikuwa anaifanya. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa maswali kutoka kwenu na majibu kutoka upande wa Serikali. Sasa nilete matangazo niliyonayo hapa mbele. Tangazo la kwanza linahusu wageni waliopo Bungeni.

Waheshimiwa Wabunge, tutaanza na wageni waliopo Jukwaa la Spika na tutaanza na wageni wa Spika. Kwanza tunao watendaji 36 kutoka Kata za Mbeya Mjini. Karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Watendaji hawa wameongozana na Katibu wa Mbunge anayeitwa Stephen Chambanenge. Karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Pia, yupo Mheshimiwa Diwani wa Viti Maalum kutoka Mbeya Mjini Mheshimiwa Atupele Msai. Pia yupo Katibu wa Umoja wa Wanawake Tanzania wa Mkoa wa Mbeya, huyu anaitwa Lucia Sulle. Karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni wa Mheshimiwa Waziri Mkuu ambao ni wachezaji 25 na viongozi saba wa Timu ya Mpira wa Miguu kutoka Ruangwa, Mkoa wa Lindi. Karibuni sana. *(Makofi)*

Sasa katika hao wageni ambao wamesimama hapo yupo *Coach* Zahera ambaye ni Mkurugenzi wa Ufundi kwa programu ya vijana Ruangwa. Karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni wengine ambao wapo Jukwaa la Spika na wengine huenda wamekaa sehemu nyingine.

Tunao wageni saba wa Mheshimiwa Naibu Spika, Mbunge wa Jimbo la Ilala, ni viongozi wa Jumuiya ya Wafanyabiashara na wajumbe wa Halmashauri Kuu ya Soko la Kariakoo, Jijini Dar es Salaam. Karibuni sana viongozi wetu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa upekee yuko hapa Makamu Mwenyekiti, Mfaume Mfaume, Ndugu Donald Kibwana ambaye ni Naibu Katibu. Pia, ni wajumbe wa Kamati inayoongoza Jumuiya ya Wafanyabiashara. Karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Tunao wageni mbalimbali ambao ni wageni wenu. Kwanza, tunao Wageni 16 wa Mheshimiwa Dkt. Selemani Jafo, Waziri wa Viwanda na Biashara, hawa ni Viongozi wa Jumuiya ya Wafanyabiashara wa Soko la Kariakoo kutoka Jijini Dar es Salaam. Karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Tunao Wageni wawili wa Mheshimiwa Cosato David Chumi, Naibu Waziri wa Mambo ya Nje, hawa ni ndugu zake kutoka Jijini Dar es Salaam. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 38 wa Mheshimiwa Hussein Nassor Amar, ambao ni Viongozi wa Chama Cha Mapinduzi kutoka Jimbo la Nyang'hwale Mkoa wa Geita. Karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Tunao wageni 32 wa Mheshimiwa Ghati Zephania Chomete, ambao Wenyeviti wa Umoja wa Wanawake Tanzania kutoka Wilaya za Mkoa ya Mara, wapo pia Makatibu wa Umoja wa Wanawake Tanzania wa Mkoa wa Mara, Waheshimiwa Madiwani Kata, Madiwani wa Viti Maalum, wote hawa wanatoka Mkoa wa Mara. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni watano wa Mheshimiwa Zuberi Mohamedi Kuchauka, ambao ni Wawakilishi wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi kutoka Jimbo la Liwale, Mkoa wa Lindi. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni 17 wa Mheshimiwa Anna Richard Lupembe, ambao ni Viongozi wa Umoja wa Vijana Tanzania wa Chama Cha Mapinduzi kutoka Jimbo la Nsimbo, Mkoa wa Katavi. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 21 wa Mheshimiwa Seif Khamis Gulamali, Wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma wanaotokea Jimbo la Manonga, Mkoani wa Tabora. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni 16 wa Mheshimiwa Boniventura Destery Kiswaga, Viongozi wa Umoja wa Wanawake Tanzania na Madiwani wa Viti Maalum kutoka Mkoa wa Iringa. Hili tangazo liko sawasawa? Mheshimiwa Kiswaga, ni wageni wako? *(Makofi)*

**MHE. BONIVENTURA D. KISWAGA:** Mheshimiwa Spika, ndiyo.

**SPIKA:** Haya ahsante sana. Nilifikiri labda tangazo limechanganya, maana kuna Kiswaga wa Iringa humu ndani. Sawa, sasa ngonja niwataje vizuri.

Wageni 16 wa Mheshimiwa Boniventura Destery Kiswaga, Viongozi wa Umoja wa Wanawake Tanzania na Madiwani wa Viti Maalum kutoka Mkoa wa Iringa. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni 36 wa Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi….

**MHE. BONIVENTURA D. KISWAGA:** Mheshimiwa Spika, umechanganya tena, umesema Iringa. Ni Mkoa wa Mwanza, Jimbo la Magu.

**SPIKA:** Kwa hiyo, kilichokosewa ni kutaja Iringa? Ndiyo, maana nikasema hawa ni wageni wako au wa kule? Maana ulivyosema wa kwako nikaendelea kusoma na Iringa kama nilivyosoma mwanzo. Kwa hiyo, hawa wanatoka Mwanza na siyo Iringa na wanatoka jimboni kwako?

**MHE. BONIVENTURA D. KISWAGA:** Mheshimiwa Spika, ndiyo.

**SPIKA:** Sawa. Wageni 16 wa Mheshimiwa Boniventura Destery Kiswaga, Viongozi wa Umoja wa Wanawake Tanzania na Madiwani wa Viti Maalum kutoka Mkoa wa Mwanza, Jimbo la Maswa. Haya ahsante. Mheshimiwa Kiswaga, jimbo gani tena? *(Makofi)*

Jimbo gani tena Mheshimiwa Kiswaga?

**WABUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, Jimbo la Magu.

**SPIKA:** Jamani, Jimbo la Magu. Huyu ni Mbunge wa Jimbo la Magu. *(Makofi)*

Tunao wageni 36 wa Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi, ambao ni Viongozi wa Jumuiya ya Wazazi wa Chama Cha Mapinduzi kutoka Jimbo la Msalala Mkoa wa Shinyanga. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni saba wa Mheshimiwa Festo Sanga, Viongozi wa Umoja wa Wanawake Tanzania na Familia yake kutoka Makete, Mkoa wa Iringa. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni 60 wa Mheshimiwa Aysharose Mattembe, Viongozi wa Umoja wa Wanawake Tanzania na Waheshimiwa Madiwani kutoka Mkoa wa Singida. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni nane wa Mheshimiwa Angelina Mabula, Shirikisho la Vyama vya Watu Wenye Ulemavu Tanzania (SHIVYAWATA). Naona ana makundi mawili ya wageni, kwa hiyo, tuanze na hawa wa SHIVYAWATA. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wengine wa Mheshimiwa Angelina Mabula, ni wafanyakazi wastaafu wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni 15 wa Mheshimiwa Ally Mlaghila Jumbe, Madiwani wa Viti Maalum wakiongozwa na Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake Tanzania kutoka Jimbo la Kyela, Mkoa wa Mbeya. Karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, katika wageni hawa yupo pia mgeni wa Mheshimiwa Lucy Mayenga, huyu ni mfanyabiashara wa Kariakoo ni kaka yake anaitwa Deo Mayenga. Karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ninalo tangazo lingine kutoka kwa Katibu wa Bunge, anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote kuwa leo tarehe 6 Februari, 2025 kutafanyika Muhadhara kuhusu

*Artificial Intelligence*. Humu wataalam wa Kiswahili sasa hivi wameshakuwa wengi. Akili Mnemba, lile jina lingine ni kama limenishinda hivi. Unde? Haya muhadhara kuhusu akili unde, muhadhara huo utatolewa na Profesa Ragu Nathan kutoka *Institute of Technology Madras India*. Mara baada ya kusitisha shughuli za Bunge saa saba mchana katika ukumbi wa Msekwa.

Waheshimiwa Wabunge, wote tunafahamu mwaka huu ni mwaka wa uchaguzi na hii akili unde ina changamoto nyingi sana. Kwa hivyo, ni muhimu sana sote kuhudhuria muhadhara huu ili tupate uelewa juu ya jambo hili na sisi tujiandae watakapotumia wengine na sisi tujue nini cha kufanya. Kwa hiyo, itatusaidia sana, ndiyo maana tumemwomba huyu profesa aje kuzungumza nanyi.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, itakuwa ni jambo la kheri kama wote tukiweka umuhimu kwenye jambo hili kuhudhuria mafunzo hayo ili huko tunakoelekea tupunguze zile athari za hii akili unde *(Artificial Intelligence)* kwenye masuala yetu ya demokrasia, utawala bora, haki za binadamu kwa sababu kuna athari chanya na athari hasi pia.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, tunaendelea na ratiba zetu.

Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

## HOJA ZA KAMATI

### Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo, kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2024

**Na**

### Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu shughuli za Kamati kwa Mwaka 2024

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sasa nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo, Mheshimiwa Deodatus Mwanyika.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA, KILIMO NA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, kutokana na ufinyu wa muda, naomba Taarifa yote ya Kamati iingie kwenye Kumbukumbu za Bunge kama ilivyowasilishwa Mezani.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 136(15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 na kwa niaba ya Kamati, naomba kuwasilisha Taarifa ya Mwaka ya Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo kwa kipindi cha kuanzia Februari, 2024 hadi Januari, 2025.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, subiri kidogo. Waheshimiwa Wabunge najua tunajadiliana mambo ya msingi kabisa, lakini tupunguze sauti kidogo ili Mwenyekiti aweze kusikika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, endelea.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA, KILIMO NA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, madhumuni ya taarifa hii ni kulijulisha Bunge kuhusu hali ya utekelezaji wa shughuli za umma katika Sekta zinasimamiwa na Kamati ambazo ni Viwanda, Biashara, Kilimo, Mifugo pamoja na Uvuvi. Lengo ni kulipa Bunge fursa ya kuisimamia na kuishauri Serikali kwa mujibu wa Ibara ya 63(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977.

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya Kamati ina muundo ufuatao:-

(i) Utangulizi na Orodha ya shughuli zilizotekelezwa;

(ii) Uchambuzi, mafanikio na changamoto;

(iii) Maoni ya ujumla, mapendekezo; na

(iv) Hitimisho na kutoa hoja.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Februari, 2024 hadi Januari, 2025, Kamati ilitekeleza shughuli zifuatazo:-

(i) Kupokea na kujadili Taarifa za Utekelezaji wa Wizara;

(ii) Kutembelea na kukagua miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025;

(iii) Kuchambua taarifa na Utekelezaji bajeti ya mwaka 2023/2024; na

(iv) Makadirio ya Bajeti ya Mwaka 2024/2025.

Mheshimiwa Spika, ufuatiliaji wa maazimio ya Bunge katika Taarifa ya Mwaka 2022. Sekta ya Viwanda na Biashara. Mapendekezo yaliyotolewa na Bunge yanaendelea na utekelezaji katika hatua mbalimbali. Kwa mfano, azimio kuhusu Vituo vya Pamoja vya Mipakani *(OSBP)* kukosa mashine za ukaguzi limeanza kutekelezwa kwa kufunga mashine katika Mpaka wa Tunduma/Nakonde.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hatua hizi, Kamati inaitaka Serikali kuchukua hatua za haraka na za makusudi ili kuhakikisha inajenga mifumo imara ya udhibiti wa uingizaji wa bidhaa nchini katika maeneo yote ya mipakani ikiwa ni pamoja na kufunga mashine za ukaguzi *(scanners)*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande mwingine, uliipatia Kamati jukumu la kufuatilia Utekelezaji wa Serikali kuhusu utatuzi wa changamoto za mikopo ya matrekta ya kampuni ya *URSUS* na kuripoti kwenye taarifa ya mwaka pamoja taarifa za bajeti. Maelekezo hayo yalitokana na Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, biashara, Kilimo na Mifugo, kuhusu maoni na ushauri wa namna ya kutatua changamoto zinazowakabili

wakulima waliokopa matrekta ya kampuni ya *URSUS* iliyowasilishwa Bungeni tarehe 4 Septemba,2023.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipokea taarifa za Serikali kuhusu utekelezaji wa maazimio hayo. Kamati ilichambua taarifa hiyo na kubaini yafuatayo:-

(i) Timu ya wataalam ya kufanya tathmini ya mikopo ya matrekta hayo iliundwa na kukamilisha kazi yake. Taarifa pia inaeleza kuwa kwa sasa Serikali inaendelea kuchakata taarifa hiyo kwa hatua mbalimbali; na

(ii) Maandalizi ya ndani ya kufanya majadiliano ya kidiplomasia kati ya Serikali ya Tanzania na Serikali ya Poland yanaendelea.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hatua hizo ambazo zimechukuliwa na Serikali, Kamati pia ilifahamishwa kuwa, Serikali imesimamisha zoezi la kukusanya madeni yanayotokana na mikopo hiyo ya matrekta na hivyo kupunguza kero kwa wananchi wakulima waliokopa makrekta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati inapongeza hatua hizo ambazo zimeanza kuchukuliwa na Serikali. Aidha, Kamati inaitaka Serikali kukamilisha hatua zilizobaki ili kumaliza changamoto zilizoambatana na mikopo hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Kilimo, utekelezaji wa mapendekezo ya sekta hii kwa kiasi kikubwa unaendelea. Kwa mfano, Azimio lililohusu changamoto za kiuendeshaji za Kampuni ya Mbolea *(TFC)* zinazotokana na mfumo wa ununuzi katika Sekta za Umma. Taarifa ya utekelezaji ilieleza kuwa, Serikali kupitia Msajili wa Hazina na Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma *(PPRA)* imeridhia *TFC* kuandaa utaratibu wa kununua mbolea na pembejeo nyingine moja kwa moja kutoka kwa wazalishaji.

Mheshimiwa Spika, vilevile, Azimio kuhusu upungufu wa viuatilifu nchini limeanza kutekelezwa, ambapo Serikali kwa

kushirikiana na sekta binafsi imewezesha ujenzi wa Kiwanda cha *Plant Biodefenders Limited* kilichopo Mkoa wa Kilimanjaro, chenye uwezo wa kuzalisha lita 20,000 kwa mwezi, sawa na *acre pack* 160,000. Maana yake inaweza kugharamia ekari 160,000.

Mheshimiwa Spika, Azimio lililohusu upungufu wa sukari nchini, Kamati ilijulishwa kwamba, hatua mbalimbali zilichukuliwa katika kuhakikisha sukari inapatikana nchi nzima na kwa bei inayohimilika. Kamati inaipongza Serikali kwa juhudi hizo za kukabiliana na uhaba wa sukari uliokuwa umejitokeza. Aidha, Kamati inaitaka Serikali kuendelea kuboresha mazingira ya kuzalisha sukari ya kutosha nchini ili na kuzalisha sukari nje ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Mifugo; kwa upande wa Sekta ya Mifugo na Uvuvi, kuna jumla ya masuala manne (4) yaliyoguswa na maazimio ya Bunge. Uchambuzi wa Kamati unaonesha kuwa, maazimio yote manne (4) yapo kwenye hatua tofauti za utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, Azimio linalohusu malalamiko ya wananchi hasa wavuvi kulazimishwa kutumia vizimba ilihali wao hawaoni umuhimu huo kutokana na kukosa uelewa wa jambo hilo. Kamati ilifahamishwa kuwa, Wizara imetoa elimu kwa wadau 1,497 kati ya 6,493 waliokusudiwa. Suala hili ni endelevu hivyo Kamati inaihimiza Serikali kuendelea kuwafikia wadau wengi zaidi ili kuondoa changamoto zinazotokana na uelewa mdogo.

Mheshimiwa Spika, kwa upande mwingine, Kamati haijaridhishwa na mchakato wa uanzishwaji wa Mamlaka za Usimamizi wa Shughuli za Maendeleo za Sekta ya Mifugo pamoja na Sekta ya Uvuvi ambapo taarifa zinaonesha suala hili bado lipo kwenye mchakato.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaitaka Serikali kuona umuhimu wa kukamilisha sehemu iliyobaki ili mamlaka hizi zianzishwe na kuanza kutekeleza majukumu yake na kupata tija iliyokusudiwa kwenye Sekta husika.

Mheshimiwa Spika, ziara za ufuatiliaji miradi ya maendeleo. Tarehe 11 hadi 19 Machi, 2024 Kamati ilitembelea mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Tanga, Pwani na Dar es Salaam kukagua miradi katika sekta ya viwanda, biashara, kilimo na mifugo. Katika ziara hiyo, Kamati ilibaini mafanikio na changamoto zilizowasilishwa Bungeni kupitia Taarifa kwenye Bunge la Bajeti.

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi wa Muswada na Maazimio; Kamati ilipata fursa ya kuwasilisha taarifa yake Bungeni kuhusu Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Ushindani ya Mwaka 2024 *(The Fair Competition Amendment Bill 2024)*.

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi na matokeo (mafanikio na changamoto). Naomba kulijulisha Bunge matokeo ya mafaniko na changamoto kwa kila sekta kama ifuatavyo: -

(a) Sekta ya Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini mafanikio katika sekta hii kama ilivyoelezwa katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya 2020/2025 Ibara ya 46. Kamati ilibaini changamoto mbalimbali kutoka sekta ya viwanda na biashara. Mfano;

(i) Ukosefu wa soko la uhakika la bidhaa zinazozalishwa nchini na taasisi kama vile *TEMDO, CAMARTEC* na *KMTC*; na

(ii) Upungufu wa Mtaji na bajeti ya maendeleo kwa taasisi na mashirika yaliyochini ya Wizara ya Viwanda na Biashara pamoja na sera, Sheria na baadhi ya kanuni kupitwa na wakati na hivyo, kuwaathiri wafanyabiashara wakubwa na wadogo Pamoja na pato la Taifa kwa ujumla.

(b) Sekta ya Kilimo

Mheshimiwa Spika, kamati ilibaini mafanikio katika sekta hii kama ilivyoelezwa katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya 2020/2025 Ibara ya 37. Katika hatua hii Kamati inaipongeza Serikali kwa kupunguza kwa kiasi kikubwa upungufu

wa sukari nchini na kuhakikisha kuwa inapatikana kwa bei himilivu nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hizi Kamati ilibaini changamoto katika Sekta ya Kilimo. Mfano, ufinyu wa mtaji na bajeti za maendeleo katika taasisi za kilimo; mikopo chechefu inayoikabili Mfuko wa pembejeo za kilimo pamoja na mtiririko usioridhisha wa fedha za miradi ya umwagiliaji, ambapo miradi mingine inachelewa kukamilika.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Mifugo na Uvuvi, Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya Uchaguzi Mkuu 2020/2025 Ibara ya 40(a) mpaka (e), pamoja na Ibara ya 41 imejikita kuleta mabadiliko makubwa na ya kisayansi kwa kuhimiza ufugaji wa kisasa wenye kuzingatia kinga, tiba na utafiti wa mifugo ili kuzalisha ajira nyingi hasa kwa vijana na kuinua mchango wa sekta katika pato la Taifa na kuleta ustawi wa wananchi.

Mheshimiwa Spika, vilevile, kuhakikisha shughuli za uvuvi nchini zinaboreshwa, vitendo vya uvuvi haramu vinadhibitiwa ili kuwezesha upatikanaji wa samaki wenye ukubwa unaokubalika na kuongeza kwa viwanda vya kuchakata samaki na hivyo kuongeza mauzo ya bidhaa za samaki nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuwa kuna changamoto ambazo zinahitaji kupatiwa ufumbuzi. Mfano, kutokuwepo na mfumo endelevu unaofahamika wa chanjo za mifugo, hali inayosababisha kukosa soko la nyama nje ya nchi pamoja na uhaba wa meli za uvuvi na doria.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla sekta ya viwanda, biashara, kilimo na mifugo zinakabiliwa na ufinyu wa bajeti, vitendea kazi pamoja na rasilimali watu katika taasisi zake za utafiti. Hali hii inapunguza ufanisi katika sekta hizo. Hakuna taasisi au sekta inayoweza kuendelea bila tafiti za kutosha. Kamati inaitaka Serikali kutenga na kupeleka fedha kwenye taasisi zake za utafiti ili ziweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, maoni na mapendekezo; **k**utokana na Shughuli zilizotekelezwa na Kamati kwa mwaka 2024, Kamati ilibaini mambo mbalimbali kama yalivyoelezwa katika sehemu ya pili ya Taarifa hii. Kutokana na matokeo hayo Kamati ina mtazamo na maoni yafuatayo:-

(i) Upungufu wa mitaji na ufinyu wa bajeti katika miradi ya maendeleo unazorotesha utekelezaji wa miradi ya taasisi za umma kama vile *TEMDO, KMTC, SIDO, WRRB, CAMARTEC* na *FTC*;

(ii) Mkataba wa Kuuza na Kununua Viuadudu vinavyozalishwa na *NDC* kupitia Kiwanda cha *Biotech Products Limited* – Kibaha unasuasua kutokana na TAMISEMI kutotekeleza matakwa ya Mkataba huo;

(iii) Ukosefu wa masoko ya uhakika ya vifaa na mitambo inayozalishwa nchini kutoka *KMTC, TEMDO* na *CAMARTEC* unaathiri mapato ya taasisi husika pamoja na Serikali kwa ujumla;

(iv) Suala la elimu ya wananchi na wafugaji kuhusu ufugaji wa samaki wa vizimba ni muhimu likatekelezwa ili kuongeza ari, kipato cha mtu mmoja mmoja na pato la Taifa kwa ujumla;

(v) Uwezo mdogo wa kununua wa wadau wa teknolojia za *CAMARTEC* ambao ni wakulima waishio vijijini unaweza kutatuliwa kwa kuipatia *CAMARTEC* ruzuku ili kutimiza malengo hayo ya kupeleka zana na teknolojia rahisi vijijini;

(vi) Upungufu wa wafanyakazi pamoja na vitendea kazi unaozikabili taasisi mbalimbali za umma unachangia taasisi hizo kutotekeleza majukumu yake ipasavyo;

(vii) Kutokuwepo kwa mashine za kukagulia mizigo katika vituo vya mipakani kunaweza kuikosesha Serikali mapato lakini pia kuhatarisha uingizwaji wa bidhaa zisizohitajika nchini;

(viii) Kuanguka kwa bei ya mafuta ya alizeti kumesababisha wakulima wengi kuacha kulima zao hili. Hali hii inapaswa kupatiwa uvumbuzi ili kunusuru zao hili;

(ix) Tija ndogo ya Sekta ya umwagiliaji inayotokana na fedha za miradi ya umwagiliaji kutotolewa kwa wakati na kwa kiasi sahihi;

(x) Tasnia ya chai nchini imedorora kutokana na wawekezaji waliochukua mashamba na viwanda vya chai kushindwa kuyaendesha kwa mujibu wa Mkataba;

(xi) Kutokuwepo na mfumo endelevu na unaoeleweka wa chanjo ya mifugo kumesababisha wafugaji kukosa soko la nyama nje ya nchi;

(xii) Upungufu wa majosho na malisho ya uhakika umesababisha mifugo kudorora na wakati mwingine kufa kwa kukosa huduma;

(xiii) Ushiriki mdogo wa sekta binafsi katika udhibiti wa uvuvi haramu kumechangia kupunguza ufanisi wake;

(xiv) Mfuko wa Pembejeo unakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwemo ufinyu wa bajeti, mikopo chechefu, kutomudu gharama za ukaguzi na ufuatiliaji wa wakopaji; na

(xv) Sera, Sheria na Kanuni zinazotumika katika Sekta za Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo, zisipofanyiwa mapitio zitaendelea kuweka misimamo iliyopitwa na wakati, kuweka masharti yasiyoendana na hali halisi na kuweka taratibu zisizokidhi mahitaji.

Mheshimiwa Spika, aidha, Sera, Sheria na Kanuni hizo za kila sekta zisipofungamanishwa na miongozo, masharti na taratibu za sekta nyingine kati ya hizo zitakosesha manufaa ya kiuchumi ya Sekta za Viwanda, Biashara, Kilimo na Uvuvi.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo; upungufu wa mitaji na bajeti ya maendeleo kwa taasisi na mashirika ya umma:

KWA KUWA, Taasisi kama *TEMDO, WRRB, CAMARTEC, KMTC, SIDO* na *FTC* zinakabiliwa na upungufu wa fedha za uendeshaji pamoja na za Miradi ya Maendeleo;

NA KWA KUWA, upungufu huo unapelekea taasisi hizo kushindwa kutekeleza majukumu yake kikamilifu na hivyo kutofikia malengo ya kuhudumia na kuleta ustawi wa wananchi kama ilivyokusudiwa pamoja na kuikosesha Serikali mapato kwa ujumla;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Serikali ifanye tathmini ya kina na kuzipatia taasisi zake bajeti ya kutosha ya uendeshaji na ya maendeleo ili ziweze kutoa huduma kwa ufanisi na kuongeza mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ukosefu wa soko la uhakika la bidhaa zinazozalishwa nchini:

KWA KUWA, hali ya jumla ya upatikanaji wa masoko ya uhakika hasa kwa bidhaa zinazozalishwa na taasisi kama vile T*EMDO* na *CAMARTEC* hairidhishi kutokana na:-

(i) Taasisi za Serikali kutokuwa na utayari wa kununua bidhaa husika hata kama zina ubora unaokubalika kutokana na taratibu za manunuzi; na

(ii) Bidhaa zinazozalishwa kuwa ghali hivyo wanunuzi kutokuwa na uwezo wao wa kununua. Mfano mdogo ni CAMARTEC ambapo wanunuzi wa bidhaa ni wakulima wa vijijini ambao uwezo wao kununua uko chini;

NA KWA KUWA, ukosefu huo wa masoko unapelekea:-

(i) Taasisi kushindwa kuuza bidhaa na hivyo kujiendesha kwa hasara pamoja na kuikosesha Serikali mapato; na

(ii) Serikali kutumia fedha nyingi za kigeni kununua bidhaa nje ya nchi ambazo zinapatikana nchini.

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia yafuatayo:-

(i) Serikali iweke utaratibu mahsusi wa manunuzi utakaowezesha bidhaa zinazopatikana ndani ya nchi zitumike ili kuinua na kukuza wazalishaji wa ndani na kuokoa fedha za kigeni;

(ii) Serikali izipatie ruzuku taasisi hasa zinazopeleka huduma kwa wananchi moja kwa moja kama vile *CAMARTEC* na *SIDO* ili kuwapatia unafuu wananchi wanaonunua bidhaa hasa zana za kilimo.

Mheshimiwa Spika, Mfumo wa Stakabadhi Ghalani:-

KWA KUWA, changamoto ya uchache wa maghala na baadhi kuwa mbali na maeneo ya mashamba hulazimisha wakulima kusafiri umbali mrefu kupeleka mazao;

NA KWA KUWA, hali hiyo imesababisha mambo yafuatayo:-

(i) Wakulima kuingia gharama kubwa kusafirisha mazao yao umbali mrefu; na

(ii) Madalali hutumia fursa hiyo kununua mazao kutoka kwa wakulima kwa bei ndogo na hivyo kukwamisha utekelezaji wa Mfumo wa Stakabadhi Ghalani.

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba:-

(i) Serikali iongeze kasi ya kushirikiana na Sekta Binafsi kujenga maghala ya kutosha katika maeneo ya wakulima;

(ii) Serikali ijumuishe mazao ambayo bado hayajaingizwa kwenye Mfumo wa Stakabadhi Ghalani ikiwemo kahawa ili kunufaisha wakulima wengi zaidi;

(iii) Serikali iweke mfumo mzuri wa uendeshaji na usimamizi wa maghala ili kudhibiti tabia za wamiliki wa maghala kuwalipisha wakulima gharama zisizowahusu; na

(iv) Serikali itoe elimu kwa wakulima kuhusu umuhimu wa kuuza mazao yao kwa kutumia Mfumo wa Stakabadhi Ghalani.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hali ya mafuta ya kula nchini:-

KWA KUWA, bado tunakabiliwa na upungufu wa mafuta ya kula unaosababishwa na wakulima wengi kusitisha kilimo cha alizeti kutokana na kukosa soko la uhakika;

NA KWA KUWA, upungufu huo wa mafuta unasababisha wafanyabiashara kuingiza shehena kutoka nje ambayo huuzwa kwa bei ya juu;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba: -

(i) Serikali iendelee kuhamasisha, kuendeleza na kujenga viwanda vya kutosha vya kuzalisha mafuta ya kula nchini ili kupunguza utegemezi wa uingizaji wa mafuta ya kula na kujihakikishia usalama wa chakula nchini;

(ii) Serikali iendelee kupitia upya vivutio ilivyotoa kwa wazalishaji wa ndani wa mafuta ili kuondoa athari zilizojitokeza kwa wakulima wa alizeti; na

(iii) Alizeti kama ilivyo kwa mazao mengine, iwekewe bei ambayo zitawavutia wakulima ili wahamasike kulima kwa wingi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu upatikanaji wa sukari nchini:-

KWA KUWA, upatikanaji wa sukari inayozalishwa nchini bado haujitoshelezi, jambo linalosababisha kuagiza kutoka nje ya nchi ili kuziba nakisi;

NA KWA KUWA, kutopatikana kwa sukari ya kutosha kunaweza kusababisha: -

(i) Upungufu wa sukari;

(ii) Kutowafikia walaji kwa wakati; na

(iii) Bei kuwa juu.

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Serikali iendelee kuhamasisha uwekezaji wa viwanda vya sukari ili kuongeza uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, kuhusu upungufu wa *scanners* katika mipaka nchini:-

KWA KUWA, baadhi ya vituo vya mipakani vinakabiliwa na ukosefu wa *scanners;*

NA KWA KUWA, ukosefu huo unaweza kusababisha yafuatayo: -

(i) Kuikosesha Serikali mapato kutokana na wafanyabiashara wasio waaminifu kutumia mwanya huo kukwepa kodi;

(ii) Mizigo kukaa mipakani kwa muda mrefu na baadhi yake kuharibika; na

(iii) Uingizwaji wa bidhaa zisizohitajika nchini.

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Serikali ichukue hatua za haraka na za makusudi ili kuhakikisha inaweka mifumo

imara ya udhibiti wa uingizaji wa bidhaa nchini katika maeneo yote ya mipakani ikiwa ni pamoja na kufunga *scanners.*

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Biashara Nchini:-

KWA KUWA, Sekta ya Biashara ina mchango mkubwa katika ujenzi wa uchumi, uongezaji wa Pato la Taifa na kodi zinazotokana na wafanyabiashara;

NA KWA KUWA, sekta hii inakabiliwa na changamoto nyingi ikiwa ni pamoja na Sera, Sheria na baadhi ya Kanuni kupitwa na wakati na hivyo kuathiri wafanyabiashara wakubwa na wadogo pamoja na Pato la Taifa;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Serikali iendelee kuchukua hatua madhubuti kuhakikisha vikwazo na changamoto hizo zinaondolewa ikiwa ni pamoja na kufanyia mapitio Sera na Sheria zinazohusika ili kuimarisha sekta ya biashara nchini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ujenzi wa viwanda nchini:-

KWA KUWA, nchi inakabiliwa na upungufu wa viwanda vya kuzalisha bidhaa mbalimbali pamoja na hatua zinazochukuliwa;

NA KWA KUWA, ukosefu wa viwanda hivyo unasababisha: -

(i) Uingizwaji wa bidhaa kutoka nje kwa kutumia fedha za kigeni;

(ii) Ukosefu wa ajira kwa vijana; na

(iii) Kukosekana kwa soko la malighafi inayozalishwa hapa nchini.

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Serikali iendelee kuhamasisha na kuweka mazingira ya kuvutia uwekezaji wa viwanda ili kupunguza changamoto ya ajira inayoendelea kukua siku hadi siku; kuagiza bidhaa kutoka nje na kuongeza soko la

malighafi ambalo litaongeza Pato ya Taifa na mwananchi mmoja mmoja.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Vituo vya Rasilimali za Kilimo vya Kata *(Ward Agricultural Resources Centres)*:

KWA KUWA, Vituo vya Rasilimali za Kilimo vya Kata katika maeneo mbalimbali nchini vilivyokabidhiwa Halmashauri za Wilaya kwa lengo la kuwafikishia wakulima huduma mbalimbali ikiwemo elimu na huduma za ugani havitekelezi azma hiyo kutokana na baadhi kubadilishiwa matumizi kinyume na utaratibu;

NA KWA KUWA, kubadilishwa matumizi kumepelekea kutofikiwa kwa malengo ya kupeleka huduma za kuridhisha za ugani pamoja elimu katika ngazi hiyo;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Serikali:-

(i) Iviondoe vituo hivyo kwenye usimamizi wa Halmashauri na vikabidhiwe Wizara ya Kilimo ili viwe *mechanization centers* vitakavyosimamiwa na Wakala wa Wagani itakayoanzishwa baadaye;

(ii) Uanzishwaji wa Wakala wa Wagani ambao uko katika hatua za mwanzo uharakishwe ili vituo hivyo vilete tija iliyokusudiwa;

(iii) Serikali itenge fedha za kutosha kununua matrekta angalau mia moja kwa kuanzia ili vituo hivyo viweze kufanya kazi kwa ufanisi katika bajeti inayokuja;

(iv) Miundombinu ya vituo kama maji, umeme na barabara viboreshwe ili vituo vifikike kwa urahisi; na

(v) Vituo vyote vipatiwe hatimiliki na kuwekewa uzio ili kuondoa migogoro isiyo ya lazima.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mchango wa tasnia ya umwagiliaji katika Sekta ya Kilimo:

KWA KUWA, Tasnia ya Umwagiliaji imebainika kuwa na mchango mdogo katika Sekta ya Kilimo kutokana na: -

(i) Ucheleweshaji wa fedha toka Hazina kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji;

(ii) Idadi ndogo ya Wataalamu mbalimbali wa Umwagiliaji katika ngazi ya Wilaya; na

(iii) Mwamko mdogo wa wakulima katika kulipia ada za huduma za umwagiliaji.

NA KWA KUWA, changamoto hizo zinakwamisha tija iliyokusudiwa na kusababisha uzalishaji mdogo wa Sekta ya Kilimo;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba:-

(i) Serikali ifanye uchambuzi wa kina kubaini miradi yote inayohusiana na ujenzi wa mabwawa na kilimo cha umwagiliaji ili utekelezaji wake uwe na tija kwa sekta hii muhimu ya kilimo. Aidha, kutokana na wingi wa Miradi na kwa kuzingatia ufinyu wa bajeti, Serikali iainishe vipaumbele vya miradi ya kutekelezwa na itengewe bajeti kwa ajili ya utekelezaji;

(ii) Serikali iendelee kuongeza na kutoa kwa wakati fedha za ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji ili kuongeza uzalishaji; na

(iii) Serikali iweke mifumo mizuri itakayowawezesha wakulima kulipa ada za huduma kwa wakati. Aidha, mifumo ya ufuatiliaji wa madeni yatokanayo na ada hizo iimarishwe.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Tasnia ya Chai Nchini:

KWA KUWA, wawekezaji waliochukua mashamba na viwanda vya chai wameshindwa kuyaendesha kwa mujibu wa mikataba yao;

NA KWA KUWA, kutokuendelezwa huko kumepelekea yafuatayo:-

(i) Tasnia ya chai kudorora;

(ii) Uingizwaji wa chai toka nje ya nchi; na

(iii) Wakulima wadogowadogo wa chai kuendelea kuwa na hali duni ya maisha kutokana na kutolipwa fedha za mauzo ya chai yao.

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Serikali ikamilishe haraka majadiliano na Wawekezaji wa viwanda ambao wameshindwa kuendesha mashamba na viwanda kwa lengo la kuwapa wawekezaji wengine wenye uwezo. Aidha, Serikali ipitie upya mfumo wa uendeshaji wa mashamba na viwanda kwa nia ya kuwahusisha wakulima wadogo na wa kati kwenye uendeshaji na umiliki wa mashamba ya chai.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (*NFRA*):-

KWA KUWA, Wakala unakabiliwa na changamoto zifuatazo: ufinyu wa bajeti; na Bajeti inayoidhinishwa na Bunge haitoki kwa wakati;

NA KWA KUWA, changamoto hizo zinasababisha Wakala kushindwa kununua mazao kwa wakati kutoka kwa wakulima;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Serikali iiongezee Wakala bajeti ya kutosha na kuhakikisha kuwa fedha zote zinazoidhinishwa zinatoka kwa wakati. Vilevile, iwezeshwe kununua, kutunza na kusambaza sukari uhaba unapotokea.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mfuko wa Pembejeo za Kilimo:-

KWA KUWA, Mfuko wa Pembejeo unakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwemo ufinyu wa bajeti, mikopo chechefu, kutomudu gharama za ukaguzi na ufuatiliaji wa wakopaji;

NA KWA KUWA, changamoto hizo zinachangia kutopatikana kwa pembejeo kwa wakati;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba:-

(i) Serikali iweke mikakati ya kuhakikisha watu wote wanaodaiwa na *AGITF* wanalipa madeni yao. Aidha, Serikali ifute mikopo isiyolipika kwa mujibu wa Sheria za Fedha;

(ii) Serikali ianzishe Ofisi za Kanda ili kurahisisha usimamizi, ufuatiliaji na kusaidia utoaji na urejeshaji wa mikopo kwa wakati; na

(iii) Serikali ihakikishe *AGITF* inaweka mfumo wa mikopo yenye riba nafuu ambayo wakulima wanaweza kumudu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko (*CPB*):

KWA KUWA, *CPB* inakabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwemo: mtaji usiotosheleza; Sheria ya uendeshaji ambayo haiipi Bodi uwezo na urahisi wa kushindana kibiashara; na ajira zenye ukomo wa miaka miwili miwili;

NA KWA KUWA, changamoto hizo zinapelekea Bodi kutotekeleza majukumu yake kwa ufanisi na kupoteza wafanyakazi wengi;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Serikali iendelee kuchukua hatua madhubuti kuiongezea nguvu *CPB* ili iweze

kutengeneza soko la uhakika kwa wakulima. Aidha, Serikali iharakishe hatua zinazoendelea za kuifanya taasisi hii kuwa kampuni ili iweze kufanya kazi zake kibiashara na kurahisisha utekelezaji wa majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, kuhusu chanjo ya mifugo:

KWA KUWA, mfumo wa chanjo za mifugo haujapata msukumo unaostahili ikiwa ni pamoja na kutokuwepo mifumo endelevu katika ngazi zote inayoeleweka vizuri kwa wafugaji;

NA KWA KUWA, kukosekana huko kwa mfumo kunaikosesha Serikali fedha za kigeni na wafugaji kutonufaika na mifugo yao;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba:-

(i) Serikali ikamilishe mchakato wa kutoa chanjo kwa mifugo yote nchini;

(ii) Serikali itoe elimu kwa wananchi ili watambue umuhimu wa chanjo kwa mifugo yao;

(iii) Maafisa Ugani wapewe elimu ya namna ya kuchanja ili kutosababisha madhara kwenye mifugo; na

(iv) Serikali itoe bei elekezi ya chanjo kwa kila aina ya mifugo ili kudhibiti upandishwaji holela wa gharama za chanjo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu majosho na malisho ya mifugo:-

KWA KUWA, kuna upungufu mkubwa wa majosho, mabwawa na malisho ya mifugo;

NA KWA KUWA, upungufu huo unasababisha kupata mazao duni ya mifugo ikiwa ni pamoja na kuugua na hata kufa;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba:-

(i) Serikali ihakikishe inaongeza bajeti ya kujenga majosho, mabwawa na malisho ya kutosha na yanayofaa kwa matumizi ya mifugo;

(ii) Serikali iharakishe ukamilishaji wa uanzishwaji wa Mamalaka ya Mifugo itakayosimamia masuala ya uendelezaji wa mifugo nchini; na

(iii) Serikali iendelee kutoa elimu kwa wafugaji ili waone umuhimu wa kupeleka mifugo yao kwenye majosho.

Mheshimiwa Spika, kuhusu udhibiti wa uvuvi haramu;

KWA KUWA, uvuvi haramu umechangia kwa kiasi kikubwa kuharibu mazalia ya samaki na kuchangia utoroshwaji wa samaki nje ya nchi;

NA KWA KUWA, hali hiyo imeathiri upatikanaji wa samaki hasa katika maeneo yote ya maziwa na bahari;

KWA HIYO BASI, Serikali iendelee kuimarisha mifumo ya udhibiti wa uvuvi haramu ili rasilimali za uvuvi ziweze kuwa na tija kwa Taifa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Taasisi za Utafiti:-

KWA KUWA. Taasisi za Utafiti zinazosimamiwa na Sekta za Uvuvi (*TIRDO*, *TEMDO, TARI*, *TALIRI, TVLA* na *TAFIRI*) zinakabiliwa na ufinyu wa bajeti;

NA KWA KUWA. upungufu huo wa bajeti unasababisha yafuatayo: -

(i) Matokeo ya tafiti kuchukua muda mrefu;

(ii) Uchakavu wa miundombinu unaopunguza tija;

(iii) Kukosekana vifaa vya kutosha vya utafiti;

(iv) Upungufu wa rasiliamali watu; na

(v) Uzalishaji kutofikia lengo.

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Serikali iweke mikakati ya kuhakikisha Taasisi hizi muhimu zinatengewa bajeti ya kutosha na kuipeleka kwa wakati ili zitekeleze majukumu yake kwa ufanisi ikiwemo kufanya tafiti zenye manufaa katika sekta husika.

Mheshimiwa Spika, hitimisho na kufunga hoja; kwa namna ya kipekee ninapenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha Taarifa hii mbele ya Bunge lako. Mafanikio ya Kamati ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo katika kutekeleza Shughuli zake kwa kipindi cha Februari, 2024 hadi Januari, 2025 yametokana na juhudi, weledi pamoja na umahiri mkubwa wa Wajumbe katika kushiriki na kutoa maoni yenye tija wakati wote ambapo Kamati imekuwa ikiisimamia Serikali.

Mheshimiwa Spika, ni wazi kwamba, ufanisi wa utendaji wa Kamati hii, unatokana zaidi na Ofisi yako kuwajengea uwezo Wabunge na kuwapa msaada stahiki wa kitaalamu na kiushauri wakati wote. Kwa heshima kubwa ningependa kuwataja majina yao.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, kutokana na ufinyu wa muda naomba majina yao yaingizwe kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge (*Hansard)*.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru; Waziri wa Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Dkt. Selemani Said Jafo; Naibu wake, Mheshimiwa Exaud Silaoneka Kigahe; Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe; Naibu wake, Mheshimiwa David Ernest Silinde; Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji, na Naibu Waziri wake, Mheshimiwa Alexander Pastory Mnyeti; Makatibu Wakuu; Naibu Makatibu Wakuu; pamoja na watendaji wote wa Wizara hizo kwa

ushirikiano waliouonesha katika kipindi chote ambacho Kamati imekuwa ikitekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, mwisho lakini siyo kwa umuhimu, ninapenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Ndugu Baraka Leonard, kwa kuwaongoza vyema Watumishi wa Ofisi ya Bunge katika uratibu na usimamizi wa shughuli za Kamati na Bunge kwa ujumla hadi kukamilika kwa taarifa hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kueleza shughuli zilizotekelezwa na Kamati, uchambuzi wa matokeo ya utekelezaji shughuli hizo na pia maoni na mapendekezo ya Kamati, sasa ninaomba kutoa hoja kwamba, Bunge sasa lipokee, kujadili na hatimaye kuikubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo pamoja na maoni na mapendekezo yaliyomo katika taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. FREDY A. MWAKIBETE:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mwenyekiti wetu. Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, Mheshimiwa Vita Kawawa. *(Makofi)*

**MHE. VITA R. KAWAWA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA:** Mheshimiwa Spika, naomba Taarifa hii yote iingizwe kwenye Taarifa Rasmi za Bunge, kama ilivyowasilishwa Mezani leo asubuhi na Makamu Mwenyekiti wa Kamati.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naomba kuwasilisha Taarifa ya Mwaka 2024 ya Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama, Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuendelea kuviboresha, kuvisimamia na kuviimarisha vyombo vyote vya ulinzi na usalama.

Mheshimiwa Spika, aidha, kwa namna ya pekee nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kuimarisha hali ya mahusiano ya kimataifa kwa kutembelea nchi mbalimbali kwa lengo la kukuza uhusiano na diplomasia ya uchumi. Halikadhalika, Kamati inampongeza Mheshimiwa Rais kwa juhudi zake za kuleta maridhiano, ili kuhakikisha Ukanda wa *SADC* na *East Africa* kunakuwa na amani na utulivu.

Mheshimiwa Spika, vilevile Kamati inampongeza Mheshimiwa Rais kwa kupewa tuzo ya *Goalkeepers Award* kufuatia mafanikio makubwa yaliyofikiwa chini ya uongozi wake katika Sekta ya Afya, hususani afya ya uzazi, mama na mtoto.

Mheshimiwa Spika, aidha, nitumie fursa hii kuwashukuru Wajumbe wa Kamati kwa namna walivyojitokeza kikamilifu na kutekeleza majukumu yao kwa moyo, uzalendo, ari na weledi hivyo, kuiwezesha kamati kukamilisha majukumu yake kwa ukamilifu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Shughuli Zilizotekelezwa; Madhumuni ya taarifa hii ni kuliwezesha Bunge kupata taswira ya jumla ya matokeo ya kazi za Kamati inayosimamia sekta tatu, ambazo ni Sekta ya Ulinzi wa Mipaka, Sekta ya Usalama wa Raia na Mali zao na Sekta ya Ushirikiano wa Kimataifa, Uhusiano na Mtangamano wa Kikanda, kwa msingi huo naomba kulijulisha Bunge kuwa, Kamati ilitekeleza shughuli zifuatazo: -

(i) Kupata mafunzo na semina mbalimbali;

(ii) Kupokea na kujadili taarifa za utekelezaji za Wizara;

(iii) Kutembelea na kukagua utekelezaji wa miradi ya maendeleo;

(iv) Kutembelea na kukagua utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Wizara;

(v) Kupokea na kujadili Taarifa za Wizara kuhusu utekelezaji wa Bajeti, makadirio, mapato na matumizi;

(vi) Kushughulikia Taarifa za wawakilishi katika vyama mbalimbali vya Kibunge na Mabunge ya Kikanda;

(vii) Kushughulikia Taarifa kuhusu ushirikiano wa Bunge na Mabunge mengine; na

(viii) Kufuatilia mwenendo na hali ya mtangamano na kupokea Taarifa ya utekelezaji wa maazimio ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, taarifa hii imegawanyika katika sehemu zifuatazo:-

(i) Sehemu ya Kwanza, inatoa maelezo ya jumla kuhusu taarifa iliyowasilishwa;

(ii) Sehemu ya Pili, inafafanua uchambuzi wa matokeo ya uchambuzi; na

(iii) Sehemu ya Tatu, inabainisha maoni na mapendekezo kutokana na uchambuzi.

Mheshimiwa Spika, lengo ni kuliwezesha Bunge kufanya uamuzi ambao ni bayana na kutokana na Masuala Yanayotolewa Taarifa Kuhusu Sekta zilizo chini ya Kamati hii.

Mheshimiwa Spika, Kuhusu Ufafanuzi na Uchambuzi wa Matokeo ya Shughuli za Kamati. Ulinzi na Usalama wa Raia na Mali Zao. Taarifa zilizowasilishwa kwenye kamati zilionesha kuwa, hali ya usalama wa raia na mali zao kwa ujumla ni shwari na

kwamba, kuna utulivu, amani na usalama. Matokeo hayo yanaonesha kuwepo kwa juhudi za pamoja kati ya vyombo vya ulinzi na usalama, jamii na Serikali.

Mheshimiwa Spika, changamoto ni moja, ya kawaida, katika uendeshaji wa shughuli za umma Duniani; muhimu ni kuzibaini na kuzishughulikia ipasavyo. Kwa msingi huo kamati imebaini changamoto katika ulinzi na usalama wa raia na mali zao kama ifuatavyo:-

(i) Upungufu wa vifaa na vitendea kazi vya kisasa katika eneo la upelelezi na uchuguzi wa kisayansi;

(ii) Upungufu wa vyombo vya usafiri kama vile magari, helikopta, pikipiki na boti kwa vyombo vya ulinzi na usalama. Mathalani, Jeshi la Uhamiaji lina upungufu wa magari 348, pikipiki 390 na boti 13;

(iii) Jeshi la Zimamoto na Uokoaji lina upungufu wa magari ya kuzima moto 156 na boti za uokozi 36;

(iv) Uchache wa vituo vya zimamoto na uokoaji nchini. Mathalani, nchi nzima kuna upungufu wa vituo vya zimamoto na uokoaji 157;

(v) Baadhi ya vifaa vya kitaalam vilivyopitwa na wakati ikiwemo vya maabara na sayansi ya uchunguzi;

(vi) Uwepo wa uwiano usio sawa kati ya askari na wananchi wanaohudumiwa;

(vii) Mwamko mdogo wa wananchi katika utoaji wa Taarifa fiche kuhusu uhalifu na wahalifu; na

(viii) Ongezeko la makosa mapya ya uhalifu yanayosababishwa na maendeleo ya sayansi na teknolojia, utandawazi, ukuaji wa miji, ongezeko la watu, ukosefu wa kazi na ujenzi holela wa makazi na upungufu

wa rasilimali watu kwa vyombo vya ulinzi na usalama ambapo Magereza kuna upungufu wa askari 6,000, Zimamoto 7,500 na Uhamiaji 1,200.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Huduma za Magereza na Urekebu; miongoni mwa majukumu ya Jeshi la Magereza ni kuwarekebisha wafungwa, ili wanapomaliza kutumikia adhabu zao wawe raia wema. Hata hivyo, katika kutekeleza jukumu hili jeshi hili linakabiliwa na uchakavu wa miundombinu katika magereza.

Mheshimiwa Spika, Magereza 85 kati ya magereza zaidi ya 100 nchini zimejengwa kabla ya uhuru. Kwa msingi huo, miundombinu ya magereza hayo imekuwa chakavu kwa kuwa, yalijengwa zaidi ya miaka 100 iliyopita, kwa kipindi hicho ujenzi wake haukuzingatia mahitaji ya huduma za urekebu na hifadhi salama kutokana na madhumuni ya utawala wa kikoloni uliokuwepo. Hivyo, hali hii inapunguza ufanisi wa elimu ya urekebu inayopaswa kuendana na wakati wa sasa.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi zaidi ulibaini kuwa, zaidi ya 85% ya magereza nchini hazina mifumo ya TEHAMA na hivyo, kuwa na changamoto katika eneo la kukusanya, kuchakata, kuhifadhi na kutumia taarifa kidijiti. Vilevile, jeshi hilo linashindwa kufuatilia kidijiti mienendo ya wafungwa, mahabusu, wageni mbalimbali wanaotembelea magereza na askari. Hali hii si nzuri katika kukabiliana na changamoto za kiusalama ambazo zinabadilika kimfumo, kimuundo, kiuhusiano na kiasili yake kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Usafiri wa Bodaboda; uchambuzi wa taarifa na maelezo yaliyotolewa umebainisha mambo mbalimbali yanayofaa kuripotiwa Bungeni kuhusu masuala ya bodaboda nchini. Masuala hayo ni: -

(i) Kwa sasa hakuna mfumo rasmi wa kurekodi Taarifa za waendesha bodaboda (Mfumo wa Utambuzi wa Bodaboda);

(ii) Waendesha bodaboda waliopo wanaainishwa katika *category* ya wenye leseni na wasio na leseni;

(iii) Hadi sasa hakuna utaratibu rasmi wa mafunzo kwa waendesha bodaboda kama sekta rasmi; na

(iv) Serikali haijaweka baadhi ya miundombinu ya muhimu ya bodaboda kama vile maegesho au vituo rasmi vya bodaboda.

Mheshimiwa Spika, kwa matokeo hayo ya uchambuzi, sekta ndogo ya usafiri wa bodaboda inaendelea kuwa na rekodi ya ajali na mazalia ya uhalifu, kutokana na wachache miongoni mwa madereva wa bodaboda kutokuwa raia wema, hivyo kuwa hatarishi kwa usalama barabarani na usalama wa raia na mali zao.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Udhibiti wa Ajali za Barabarani. Matokeo ya uchambuzi yameonesha kuwa, kwa ujumla Serikali inaendeleza juhudi za kupunguza ajali na udhibiti wa matukio ya ajali za barabarani. Hata hivyo, yapo maeneo yaliyobainika kuhitaji maboresho katika mkakati wa kupunguza ajali za barabarani. Maeneo hayo ni: -

(i) Matumizi ya teknolojia mpya katika kudhibiti ajali;

(ii) Kuendeleza elimu yenye tija kwa umma na kampeni mbalimbali kuhusu usalama barabarani;

(iii) Kujenga barabara pana zenye kukidhi mahitaji ya sasa na ya baadaye;

(iv) Ukaguzi wa magari kabla ya kupewa leseni;

(v) Kufanya ukaguzi endelevu na wenye tija; na

(vi) Bima za ajali kwa magari ya abiria pamoja na elimu kuhusu kazi za bima kwa abiria baada ya ajali.

Mheshimiwa Spika, baada ya Kamati kupokea taarifa kutoka Serikalini kuhusu mkakati wa kudhibiti ajali za barabarani, changamoto zifuatazo zilibainika:-

(i) Wembamba, uchakavu na ubovu wa barabara ambao unachangia kutokea kwa ajali;

(ii) Ukaguzi wa magari usio na tija; hali hii husababisha hata magari yasiyokaguliwa kuwa na stika ya usalama barabarani ambayo ni nyaraka inayoonesha kuwa gari husika limekaguliwa;

(iii) Kuongezeka kwa makosa ya kibinadamu yanayotokana na uzembe ambayo yanachangia kutokea kwa ajali; na

(iv) Adhabu ndogo na zisizoendana na mazingira ya sasa kwa makosa yanayotokana na uvunjifu wa Sheria ya Usalama Barabarani.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Udhibiti wa Biashara Haramu ya Usafirishaji wa Binadamu. Uchambuzi unaonesha kuwa, Serikali inachukua hatua kukabiliana na tatizo la usafirishaji wa binadamu. Sheria iliyotungwa na Bunge inasimamiwa ipasavyo na Sekretarieti ya kuzuia na kupambana na biashara haramu ya usafirishaji binadamu na vyombo vya ulinzi vya usalama vinashirikiana vizuri.

Mheshimiwa Spika, hili linathibitishwa kwa ukweli kuwa, katika kipindi cha Mwaka 2024 zaidi ya wahanga 1,110 wa usafirishaji wa biashara haramu wa binadamu wameokolewa, ambapo 902 ni wa ndani ya nchi na 208 waliokolewa toka nje ya nchi. Katika udhibiti wa biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu changamoto zilizobainika ni:-

(i) Elimu ndogo kwa wananchi kuhusu biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu ilivyo;

(ii) Bajeti isiyokidhi mahitaji inayotengewa Sektretarieti ya Kuzuia na Kupambana na Biashara Haramu ya Usafirishaji wa Binadamu;

(iii) Uhaba wa vifaa na vitendea kazi unaoikabili Sektretariati ya Kuzuia na Kupambana na Biashara Haramu ya Usafirishaji wa Binadamu pamoja na vyombo vingine vya ulinzi na usalama;

(iv) Ukosefu wa matumizi ya teknolojia katika kukabiliana na baishara haramu ya usafirishaji wa binadamu;

(v) Upungufu wa rasilimali watu katika Sekretarieti ya Kuzuia na Kupambana na Biashara Haramu ya Usafirishaiji wa Binadamu; na

(vi) Kukosekana kwa ushirikiano wa kimkakati baina ya Serikali, mashirika ya kidini, mashirika ya kiraia pamoja na viongozi wa kijamii katika mapambano dhidi ya biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Wakimbizi Walio Nje ya Kambi. Ufuatiliaji na uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa, mbali ya wakimbizi hao walio katika kambi na makazi maalum wapo wakimbizi ambao wanaishi nje ya kambi na makazi ya wakimbizi kinyume na utaratibu.

Mheshimiwa Spika, wakimbizi hao wanaoishi nje ya kambi kinyume na utaratibu, baadhi yao wameweza kuanzisha makazi ya kudumu na wanaendesha shughuli mbalimbali za kiuchumi, kama wananchi wengine, hasa katika Mikoa ya Tabora, Kigoma, Katavi, Rukwa, Tanga, Geita na Kagera.

Mheshimiwa Spika, hali hiyo ni kinyume na Sheria za kimataifa, Sheria za Nchi pamoja na taratibu za wakimbizi. Kamati inatambua Serikali inafanya juhudi kubwa katika kuwatambua wakimbizi walio nje ya kambi, kinyume na utaratibu. Hata hivyo zoezi hilo linakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

(i) Upungufu wa rasilimali watu na rasiliamali fedha unaoikabili Idara ya Huduma za Wakimbizi;

(ii) Wananchi kutokuwa na mwamko wa kutoa taarifa fiche kuhusu wakimbizi walio kwenye makazi yao;

(iii) Kukosekana kwa kitengo maalum katika muundo wa idara ya huduma kwa wakimbizi kinachohusika na wakimbizi walio nje ya kambi kinyume na sheria; na

(iv) Wakimbizi walio nje ya kambi kinyume na sheria wameachwa kwa muda mrefu pasipo kufuatiliwa na kuchukuliwa hatua stahiki na hivyo wameweza kujipenyeza kwenye jamii na kunufaika na huduma nyingine kama wananchi wengine na hivyo kuweka mazingira magumu kuwatambua.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hali ya mtangamano wa kikanda, Jumuiya ya Afrika Mashariki: Tanzania imeendelea kunufaika na kuwa mwanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki katika nyanja za kibiashara, sekta za uchumi pamoja na uhusiano wa Nchi Wanachama wa Jumuiya hiyo. Uanachama umeendelea kuleta manufaa mbalimbali kwa nchi katika kipindi cha mwaka 2024. Manufaa hayo ni pamoja na yafuatayo:-

(i) Kukua kwa soko la bidhaa na huduma mbalimbali ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki;

(ii) Urahisi wa Watanzania kusafiri ndani ya nchi wanachama umeongezeka;

(iii) Mchango wa Tanzania kwenye juhudi za kuleta amani na utulivu katika ukanda wa Maziwa Makuu umeiwezesha Tanzania kuwa na heshima na kuimarisha utulivu na amani ndani ya nchi; na

(iv) Manufaa ya ufanisi wa biashara katika soko la kikanda kutokana na kuongezeka kwa urahisi wa kufanya biashara ndani ya kanda.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Jumuiya ya Maendeleo Kusini Mwa Afrika *(SADC)*. Kamati ilipokea na kujadili taarifa ya Wizara kuhusu Hali ya Mtangamano wa *SADC*. Uchambuzi ulionesha kuwa, *SADC* inatekeleza hatua moja tu ya mtangamano, ambayo ni eneo huru la biashara.

Mheshimiwa Spika, Tanzania imenufaika katika kuuza bidhaa zake kwa Nchi Wanachama kwa urahisi kutokana na utaratibu wa kuondoleana ushuru. Mathalani, katika kipindi cha miaka mitano kuanzia mwaka 2019 - 2023, uraimu wa biashara umefikia wastani wa Dola za Kimarekani milioni 783.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio makubwa ya uanachama wa Tanzania katika Jumuiya ya Afrika Mashariki na *SADC,* zipo changamoto kwa Jumuiya hizo na Nchi Wanachama, Kwa upande wa Jumuiya ya Afrika Mashariki changamoto hizo ni pamoja na:-

(i) Kasi ndogo ya utekelezaji wa itifaki ya soko la pamoja kutokana na kukosekana kwa Sheria moja ya Jumuiya ya kutekeleza itifaki hiyo kama ilivyo kwa Itifaki ya Umoja wa Forodha;

(ii) Baadhi ya nchi kuendelea kuweka vikwazo vya biashara visivyo vya kodi kinyume na Itifaki ya Forodha;

(iii) Baadhi ya nchi wanachama kuwa na migogoro ya ndani ya kisiasa inayochangia kuzorota kwa hali ya usalama; na

(iv) Kasi ndogo ya nchi wanachama katika utoaji wa michango ya bajeti katika Jumuiya.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa *SADC*. Changamoto ni pamoja na:-

(i) Baadhi ya Nchi Wanachama kutowasilisha kwa wakati michango yao. Hivyo, kupunguza kasi ya utekelezaji wa program za mtangamano na baadhi ya taasisi kushindwa kutekeleza majukumu yake ipasavyo;

(ii) Sekta binafsi kutochangamkia ipasavyo fursa zilizopo na mtangamano wa kikanda na ushirikiano wa kimataifa; na

(iii) Baadhi ya nchi wanachama kuwa na migogoro ya ndani ya kisiasa inayochangia kuzorota kwa hali ya kiusalama.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Uwakilishi wa Bunge Kwenye Vyombo vya Kiuwakilishi wa Kibunge. Kutokana na uchambuzi wa taarifa zilizowasilishwa Kamati imethibitisha kuwa, ushiriki wa Wawakilishi wa Bunge kwenye Vyombo vya Kibunge umesaidia kuimarisha ushirikiano na Vyombo vya Kibunge. Matokeo ya uimara huo yanaongeza manufaa ya Tanzania kushirikiana na Nchi Wanachama wa Jumuiya za Kikanda.

Mheshimiwa Spika, aidha, utaratibu huu wa wawakilishi kuripoti kwenye Kamati umesaidia kuhakikisha kwamba, wawakilishi wanawajibika ipasavyo kusimamia maslahi ya Taifa kwa kadiri Bunge hili linavyotarajia. Uzoefu huo umeongeza Usimamizi wa Kibunge wa masuala ya kisera kuhusu ushirikiano wa kikanda na kimataifa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Ushirikiano wa Kibunge. Matokeo ya uchambuzi yanaonesha kuwa, Bunge lako Tukufu limefanikiwa kuimarisha ushirikiano kati yake na Mabunge ya Nchi za Afrika, Asia na Ulaya. Mfano wa mambo yanayojenga ushirikiano huo ni Ziara za Kibunge na Mawasiliano ya Kibunge kwa baadhi ya Nchi kama vile, Malawi, Uganda, Zimbabwe, China na Ghana katika kipindi cha mwaka 2024.

Mheshimiwa Spika, hadi sasa Bunge la Tanzania lina vyama vya urafiki wa Kibunge na Mabunge mbalimbali vipatavyo 13.

Kwa mwaka 2024, Bunge lilianza mchakato wa kuwa na vyama vya urafiki wa Kibunge kati yake na Bunge la Misri na Rwanda. Kamati inaridhishwa na maendeleo ya ushirikiano wa Kibunge kati ya Bunge la Tanzania na Mabunge ya nchi nyingine ambayo yamefanyika mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Maoni na Mapendekezo. Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, kwa kuzingatia matokeo ya ufuatiliaji wa utekelezaji wa majukumu ya Wizara hii, Kamati ina maoni katika maeneo mbalimbali. Kwanza, ni Maoni ya Kamati kuwa, kuimarisha Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa kushawishi utekelezaji wa Masharti ya Mkataba wa Uanzishaji wa Jumuiya hiyo pamoja na itifaki zake.

Mheshimiwa Spika, ni jambo muhimu kwa Tanzania kushawishi. ushawishi huo pia, uguse msukumo wa kuboresha uwiano wa tozo, ushuru na ada kwa bidhaa zinazokumbwa na vikwazo na kuhimiza juhudi za kidiplomasia, ili kutatua migogoro ya kikanda.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, kwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, ni mtazamo wa Kamati kuwa, Wizara hii itaendelea kufanikiwa kulinda maisha na mali, kuwezesha na kudhibiti utokaji na uingiaji nchini kwa raia na wageni, kuwarekebisha wafungwa na kutoa huduma kwa wakimbizi waliopo. Hata hivyo, mafanikio hayo yanahitaji ufanisi wa vyombo vya ulinzi na usalama nchini na kuwa na bajeti ya kutosha, vifaa vya kisasa na matumizi ya sayansi na teknolojia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, juhudi za kuendeleza miundombinu ya usalama, ikiwemo ujenzi wa vituo vya Zimamoto, kuboresha miundombinu ya Magereza na kuanzisha mikakati ya kudhibiti ajali barabarani kupitia matumizi ya teknolojia ya kisasa, ni mambo muhimu katika usalama wa raia na mali zao. Aidha, ushirikiano kati ya Serikali, sekta binafsi na wadau wengine unahitajika ili kuimarisha usalama na kuzuia uhalifu, hasa kupitia uwekezaji katika TEHAMA unaodhibiti usafirishaji haramu wa

binadamu na ufuatiliaji wa wakimbizi wanaohifadhiwa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, kutokana na uchambuzi, Kamati ina maoni kuwa, kuendelea kuimarisha mifumo ya ulinzi katika mageuzi madhubuti ya mifumo ya usimamizi wa madeni ambayo SUMA JKT inazidai taasisi mbalimbali na elimu kwa jamii za mipakani ni mambo yanayohitaji msukumo na mwendelezo. Kufanya hivyo, kutachangia usalama wa mipaka, ufanisi wa kifedha na uendeshaji bora wa SUMA JKT. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mapendekezo kwa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki; vikwazo vya biashara visivyo na kodi, Bunge linaazimia kwamba, Serikali ya Tanzania ifanye mambo yafuatayo: -

(i) Kuendelea kuzishawishi nchi wanachama ili zizingatie inavyostahili masharti ya Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuia ya Afrika Mashariki pamoja na Itifaki zake; na

(ii) Kuzishawishi nchi wanachama kukamilisha zoezi la uoanishaji tozo, ushuru na ada kwa bidhaa ambazo zinawekewa vikwazo zaidi visivyo vya kikodi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ufinyu wa bajeti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, Bunge linaazimia kwamba:-

(i) Serikali ya Tanzania iendelee kushawishi nchi wanachama zitekeleze ipasavyo masharti ya Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya, ikiwemo kutoa michango ya Jumuiya kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, kuhusu migogoro ya ndani kwa baadhi ya nchi wanachama wa jumuiya, Bunge linaazimia kwamba:-

(i) Serikali ya Tanzania itumie ushawishi wake kushirikiana na nchi nyingine wanachama na wadau mbalimbali ili

kutumia juhudi za kidiplomasia kwa kuzingatia mazingira yaliyopo kutafuta suluhu ya kudumu ya migogoro hiyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu sekta binafsi kushindwa kutumia ipasavyo fursa ya kiuchumi katika Jumuiya za Kikanda, Bunge linaazimia kwamba:-

(i) Serikali iandae mpango mkakati unaotekelezeka ambao utabainisha fursa za kiuchumi katika mtangamano wa kikanda na namna sekta binafsi zitakavyoweza kuzitumia fursa hizo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi:-

(i) Kuendeleza uwezo wa vyombo vya ulinzi na usalama wa raia na mali zao.

Mheshimiwa Spika, Bunge linaazimia kwamba, Serikali iendelee kuviwezesha vyombo vya ulinzi na usalama wa raia na mali zao kwa kufanya yafuatayo: -

(i) Kuvipa uwezo wa kuendana na maendeleo ya kisayansi na teknolojia duniani katika utekelezaji wa majukumu yao;

(ii) Kuvipa bajeti ya kutosha kuendelea kuimarisha ulinzi na usalama wa raia na mali zao; na

(iii) Kuendelea kuvipatia vifaa na vitendea kazi vya kutosha na vya kisasa zaidi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uchache wa vituo vya zimamoto na uokoaji, Bunge linaazimia kwamba:-

(i) Serikali iandae mpango wa ujenzi wa vituo vya zimamoto na uokoaji katika Wilaya na Mikoa yote ambayo haina vituo hivyo nchini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu miundombinu chakavu ya magereza, Bunge linaazimia kwamba:-

(i) Serikali iandae mpango mahususi wa kuboresha miundombinu ya Magereza nchini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu matumizi ya TEHAMA Magerezani, Bunge linaazimia kwamba:-

(i) Serikali kwa kuwashirikisha wadau wa maendeleo iongeze uwekezaji katika TEHEMA na mifumo ya kidijitali ili kuliwezesha Jeshi la Magereza kuwa na mifumo na nyenzo za kiteknoljia zinazowezesha huduma za kisasa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utambuzi wa waendesha bodaboda nchini, Bunge linaazimia kwamba:-

(i) Serikali ilisimamie Jeshi la Polisi ili liweze kushirikiana na *LATRA*, Halmashauri za Miji na Wilaya na taasisi nyingine za Serikali pamoja na wadau mbalimbali, kuandaa mfumo rasmi wa kisasa wa kidijitali kwa ajili ya utambuzi wa waendesha bodaboda nchini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hali ya barabara kuu nchini, Bunge linaazimia kwamba:-

(i) Serikali itumie utaratibu wa kujenga barabara za viwango vya nyota tatu kuanzia sasa; na

(ii) Kwa barabara kuu ambazo zilijengwa kipindi kilichopita, Serikali iziboreshe inavyostahili ili kufikia azma ya kuwa na barabara kuu zenye nyota tatu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu teknolojia katika udhibiti wa ajali za barabarani, Bunge linaazimia kwamba:-

(i) Jeshi la Polisi lifanye tathmini ya mpango wake wa kudhibiti na kuzuia ajali barabarani kwa lengo la

kubaini kama mpango huo una tija iliyokusudiwa katika kudhibiti na kuzuia ajali barabarani.

(ii) Serikali iweke mpango mkakati unaotekelezeka wa ununuzi wa vifaa vya kisasa kwa kuzingatia teknolojia mahususi kwa uhalisia wa barabara zetu na kuvifunga katika barabara zetu kwa kuanzia na barabara kuu ikiwa ni sehemu ya mkakati wa kupambana kudhibiti ajali za barabarani; na

(iii) Serikali iandae mpango wa kuwapatia mafunzo Askari wa Usalama Barabarani ili kuwa na uelewa na ujuzi wa kutumia na kufuatilia vifaa vya kitekonolojia vitakavyofungwa kwa ajili ya usalama barabarani.

Mheshimiwa Spika, kuhusu biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu, Bunge linaazimia kwamba, Serikali ifanye yafuatayo:-

(i) Kuendeleza kushirikiana kati yake na sekta binafsi na wadau wengine ili kujenga mazingira wezeshi ya kiuchumi kwa vijana na makundi maalumu;

(ii) Kushirikiana na mashirika ya kidini, asasi za kiraia na wadau wengine ili kuelimisha umma kuhusu mikakati inayotumiwa na wahalifu pamoja na madhara ya biashara hiyo kwa jamii na Taifa;

(iii) Serikali itenge fedha za kutosha kwa Sekretarieti ya Kuzuia na Kupambana na Biashara Haramu ya Usafirishaji Binadamu ili iweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo sambamba na kununua vifaa na vitendea kazi vya kisasa; na

(iv) Kuwezesha matumizi ya vifaa na teknolojia ya kisasa katika shughuli za udhibiti na uzuiaji wa usafirishaji.

Mheshimiwa Spika, kuhusu wakimbizi walio nje ya kambi, Idara ya Wakimbizi iwe idara inayojitegemea na kujiendesha kwa namna inayoiwezesha kusimamia masuala ya wakimbizi kwa ufanisi, iwezeshe upatikanaji wa Fungu maalumu la kibajeti *(Vote)* kwa Idara ya Wakimbizi tofauti na sasa ambapo idara hiyo inapata fedha zake kupitia Fungu 51 la Wizara.

Mheshimiwa Spika, Serikali itenge bajeti ya kutosha kwa idara ya wakimbizi ili iweze kutekeleza majukumu yake kama ilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa; kuendeleza juhudi za ulinzi wa mipaka, Bunge linaazimia kwamba:-

(i) Serikali iendeleze juhudi zake za kuimarisha ulinzi wa mipaka kwa kuwezesha ulinzi na elimu kwa jamii zinazoishi mipakani.

Mheshimiwa Spika, kuhusu madeni ya SUMA JKT na taasisi za umma, Bunge linaazimia kwamba:-

(i) Ihakikishe kuwa, taasisi zote za umma na binafsi zinazodaiwa na SUMA JKT zinalipa madeni yao haraka na kwa ukamilifu;

(ii) Ilisimamie shirika kufanya tathmini ya sera yake ya madeni kwa kuzingatia azma ya kukusanya madeni na kuzuia au kupunguza uwezekano wa ongezeko la madeni; na

(iii) Iliwezeshe shirika kuweka mfumo madhubuti na endelevu ambao hautaruhusu utoaji wa huduma unaochangia ongezeko la madeni.

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha taarifa ya mwaka ya Kamati kuhusu utekelezaji wa shughuli zake katika kipindi cha Januari,

2024 hadi Februari, 2025. Ni imani ya Kamati kuwa fursa hii inayotokana na masharti ya Kanuni ya 136 (15), ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 itasaidia kuliwezesha Bunge lako Tukufu kutekeleza wajibu wake na kuisimamia Serikali ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuchukua nafasi hii kuwashukuru Waziri wa Mambo ya Ndani, Mheshimiwa Innocent Bashungwa, Mbunge, pamoja na Naibu Waziri wake, Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, Mbunge, kwa ushirikiano walioutoa kwa Kamati.

Mheshimiwa Spika, vilevile, namshukuru Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa Mheshimiwa Dkt. Stagomena Lawrence Tax, Mbunge na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki; Mheshimiwa Mahmoud Thabit Kombo, Mbunge na Naibu Mawaziri wake Mheshimiwa Cosato David Chumi, Mbunge na Mheshimiwa Denis Lazaro Londo, Mbunge, pamoja na Watendaji wote wa Wizara hizo kwa ushirikiano waliouonesha katika kipindi chote ambacho Kamati imekuwa ikitekeleza majukumu yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho lakini siyo kwa umuhimu, nawashukuru watumishi wote wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi wa Ndugu Baraka Idelfornce Leornad, Katibu wa Bunge, kwa kuisaidia Kamati kutekeleza majukumu yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kueleza shughuli zilizotekelezwa na Kamati, uchambuzi wa matokeo ya utekelezaji wa shughuli za Kamati, maoni na mapendekezo, sasa naomba kutoa hoja kwamba Bunge liipokee, kujadili na hatimaye kuikubali taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama pamoja na maoni na mapendekezo yote ya Kamati yaliyo katika taarifa hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa Hoja. *(Makofi)*

**TAARIFA YA MWAKA 2024 YA SHUGHULI ZA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

*[Inatolewa chini ya Kanuni ya 136 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023]*

---

## SEHEMU YA KWANZA

**UTANGULIZI**

**Maelezo ya Jumla**

**Mheshimiwa Spika**, kama inavyofahamika, madhumuni ya Kanuni ya 136 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, ni kuliwezesha Bunge kutekeleza madaraka yake ya kuishauri na kuisimamia Serikali kwa mujibu wa Ibara ya 63(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kanuni hiyo inatoa fursa kwa Serikali kuzingatia tathmini ya masuala mbalimbali ya kisekta. Mahsusi, Taarifa hii inaonesha tathmini ya hali ya ushirikiano wa kimataifa na kikanda pamoja na sekta ya ulinzi na usalama sanjari na kuweka msingi wa kuishauri Serikali kuhusu maeneo ya kuzingatia wakati wa mchakato wa bajeti kwa mwaka 2025/2026.

**Madhumuni na Muundo wa Taarifa**

**Mheshimiwa Spika**, madhumuni ya Taarifa hii ni kuripoti matokeo ya kazi za Kamati kuhusu:

(i) Ufuatiliaji wa shughuli za umma katika sekta tatu chini ya usimamizi wake;

(ii) Ufuatiliaji wa hali ya ushirikiano wa kibunge na hali ya jumla ya uwakilishi wa Bunge letu katika vyama vya uwakilishi wa Kibunge; na

(iii) Utekelezaji wa majukumu ya Serikali katika Mtangamano wa Afrika Mashariki na Jmuiya ya maendeleo ya nchi za Kusini mwa Afrika ikilinganishwa na lengo la Serikali kufanikisha ustawi wa wananchi.

**Mheshimiwa Spika**, ili kukidhi madhumuni hayo, Taarifa hii imezingatia masharti ya Kanuni ya 142 ya Kanuni za Bunge kuhusu muundo wa Taarifa inayowasilishwa Bungeni. Kwa msingi huo, Taarifa hii imegawanyika katika sehemu zifuatazo:-

(i) Sehemu ya kwanza ambayo inatoa maelezo ya jumla kuhusu Taarifa inayowasilishwa. Lengo ni kuweka msingi wa maudhui;

(ii) Sehemu ya pili ambayo inafafanua hali ilivyo na matokeo ya uchambuzi. Lengo ni kubainisha maeneo yanayostahili kufanyiwa kazi kwa kuendelezwa au kuboreshwa; na

(iii) Sehemu ya Tatu ambayo inabainisha maoni na mapendekezo kutokana na uchambuzi. Lengo ni kuliwezesha Bunge kufanya uamuzi ambao ni bayana kutokana na masuala yanayotolewa taarifa kuhusu sekta zilizo chini ya Kamati hii.

**Wajumbe wa Kamati**

**Mheshimiwa Spika**, Ili kuendana na desturi na misingi ya uandishi wa taarifa za Kibunge, naomba kuwatambulisha Wajumbe wa Kamati iliyoandaa Taarifa hii kwa majina kama ifuatavyo:-

(1) Mhe. Vita Rashid Kawawa, Mb - Mwenyekiti
(2) Mhe. Vincent Paul Mbogo, Mb - M/ Mwenyekiti
(3) Mhe. Daniel Tlemai Awack, Mb - Mjumbe
(4) Mhe. Minza Simon Mjika, Mb - Mjumbe
(5) Mhe. Maulid Saleh Ali, Mb - Mjumbe
(6) Mhe. Maimuna Salum Mtanda, Mb - Mjumbe
(7) Mhe. Balozi Liberata Mulamula, Mb - Mjumbe
(8) Mhe. Grace Victor Tendega, Mb - Mjumbe
(9) Mhe. Zahor Mohammed Haji, Mb - Mjumbe

(10) Mhe. Joseph Michael Mkundi, Mb - Mjumbe
(11) Mhe. Felister Deogratius Njau, Mb - Mjumbe
(12) Mhe. Fakharia Shomar Khamis, Mb - Mjumbe
(13) Mhe. Muharami Shabani Mkenge, Mb - Mjumbe
(14) Mhe. Mustafa Mwinyikondo Rajab, Mb - Mjumbe
(15) Mhe. Ali Juma Mohamed, Mb - Mjumbe
(16) Mhe. Abdi Hija Mkasha, Mb - Mjumbe
(17) Mhe. Bupe Nelson Mwakang'ata, Mb - Mjumbe
(18) Mhe. Enossy Edwin Swalle, Mb - Mjumbe
(19) Mhe. Dkt. Alfred James Kimea, Mb - Mjumbe

**Mheshimiwa Spika,** nimebainisha majina ya Wajumbe ili kuzingatia misingi ya uandishi wa Taarifa za Kibunge. Misingi hiyo ni pamoja na uwazi na uwajibikaji katika uandishi wa Taarifa, kujenga uaminifu, kutambua mchango wa wahusika, kusaidia rejea pamoja na kuweka kumbukumbu sawa na rekodi za waliohusika na maudhui ya Taarifa hii.

**Majukumu ya Kamati**

**Mheshimiwa Spika,** ili kuweka bayana muktadha wa Taarifa hii pamoja na kuwezesha muunganiko wa majukumu, uchambuzi, maoni na mapendekezo kwa namna inayostahili, naomba kukumbusha majukumu ya Kamati hii. Kwa rejea, ya Bunge, Kamati hii ni miongoni mwa Kamati Kumi na Moja za Kisekta zilizotajwa katika Sehemu ya Pili ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge. Kwa mujibu wa kifungu cha 6(3) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge, Kamati hii inasimamia Wizara tatu zifuatazo:-

(i) Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki;
(ii) Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi; na
(iii) Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

**Mheshimiwa Spika**, Katika Kusimamia Wizara hizo, Kifungu cha 7(1) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge kimetaja majukumu manne ambayo ni:

(i) Kushughulikia Bajeti za Wizara inazozisimamia;

(ii) Kushughulikia miswada na mikataba ya Kimataifa inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyo chini ya Wizara inazozisimamia;

(iii) Kushughulikia Taarifa za Utendaji za kila mwaka za Wizara hizo; na

(iv) Kufuatilia utekelezaji wa majukumu ya Wizara hizo.

**Mheshimiwa Spika**, majukumu mengine matano ya Kamati hii yametajwa katika Kifungu cha 7 (2) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge. Majukumu hayo ni:-

(i) Kuimarisha ushirikiano kati ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mabunge ya nchi nyingine;

(ii) Kufuatilia mwenendo na hali ya Mtangamano wa Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo ya nchi za Kusini mwa Afrika;

(iii) Kushughulikia taarifa za Wawakilishi wa Tanzania katika Bunge la Afrika Mashariki, SADC na Bunge la Afrika;

(iv) Kushughulikia taarifa zote za Wawakilishi katika Vyama mbalimbali vya Kibunge ambapo Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni Mwanachama; na

(v) Kushughulikia Taarifa za hali ya Ulinzi na Usalama wa Mipaka ya Nchi na Usalama wa Raia na Mali zao.

**Mheshimiwa Spika**, majukumu hayo yanalenga kulisaidia Bunge ambalo ni Mamlaka ya nchi ya Kutunga Sheria na kusimamia utekelezaji wa shughuli za Umma kwa mujibu wa Ibara ya 4 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Utekelezaji wake unachangia kuliwezesha Bunge kusimamia lengo kuu la Serikali lililotajwa katika Ibara ya 8 (1) (b) ya Katiba ambalo ni kuwezesha

ustawi wa watu. Naomba kulihakikishia Bunge hili kwamba, kwa kipindi cha Februari, 2024 hadi Januari, 2025, Kamati ilifuatilia sekta inazozisimamia na kutathmini namna zinavyochangia uboreshaji wa maisha ya watu na ustawi wao.

**Njia zilizotumika**

**Mheshimiwa Spika,** Kanuni ya 142 ya Kanuni za Bunge imeweka sharti linalotaka Taarifa yoyote ya Kamati inayowasilishwa Bungeni ibainishe njia au mbinu zilizotumika katika kutekeleza majukumu yake yanayoripotiwa. Kwa kuzingatia masharti hayo, naomba kubainisha njia zilizotumika ambazo ni:-

(i) Uchambuzi wa Taarifa zilizopokelewa na kufanyiwa kazi;

(ii) Majadiliano katika Vikao pamoja na kuomba ufafanuzi kutoka mamlaka zilizohusika;

(iii) Urejeaji wa misingi ya kazi ikiwemo Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Kanuni za Bunge na Sheria zingine za nchi;

(iv) Ufuatiliaji wa mambo yanayojitokeza katika umma;

(v) Ufuatiliaji wa ahadi za Serikali Bungeni kuhusu sekta zinazosimamiwa na Kamati hii;

(vi) Ulinganisho wa hali halisi ya utekelezaji na Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020; na

(vii) Ulinganisho kati ya taarifa zinazoripotiwa kwa upande mmoja na Sera na miongozo kama vile Dira ya Taifa ya mwaka 2025 kwa upande wa pili.

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa hii imebainisha njia zilizotumika ili kuzingatia kanuni na msingi madhubuti ya kuripoti Bungeni. Kwa kufanya hivyo, Kamati imeweza:

(i) Kudhihirisha mchakato wa kazi yake ili kuruhusu tathmini ya matokeo yanayoripotiwa;

(ii) Kujenga msingi wa uhakika wa matokeo na mapendekezo ili Bunge liyakubali na kuwa Maazimio yake;

(iii) Kuweka msingi wa Bunge au wadau wengine kuthibitisha mchakato, matokeo na ustahili wa mapendekezo; na

(iv) Kurahisisha uelewa wa jumla kuhusu uchakataji wa taarifa na upatikanaji wa maoni ambayo ni msingi wa mapendekezo ya Kamati katika Taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na maelezo hayo, njia zilizotumika ziliiwezesha Kamati kufanikisha shughuli zake kwa kipindi kinachohusika. Matokeo ya matumizi ya njia hizo yameiwezesha taarifa hii kuwa na uthabiti wa maudhui na hivyo kuwa ya msingi wa uamuzi wa Bunge unaopendekezwa leo.

**Shughuli Zilizotekelezwa**

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa hii ni kwa ajili ya kuripoti shughuli zilizotekelezwa kwa mwaka 2024. Kwa msingi huo, naomba kulijulisha Bunge kuwa, Kamati ilitekeleza shughuli zifuatazo:-

### Mafunzo na Semina Mbalimbali

**Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Februari, 2024 hadi Januari, 2025, Wajumbe walipata fursa ya kujifunza kuhusu mambo yafuatayo:-

(i) Hali ya masuala ya Ugaidi pamoja na mikakati ya kuzuia na kupambana nao;

(ii) Uboreshaji wa Sera ya Mambo ya Nje ya mwaka 2002;

(iii) Hali ya Biashara haramu ya Usafirishaji wa Binadamu pamoja na usafirishaji wa magendo nchini na ulimwengu kwa ujumla;

(iv) Utekelezaji wa Mpango kazi wa Ujenzi wa Vitega Uchumi katika Balozi zetu;

(v) Mafunzo kuhusu Mfuko wa Jeshi la Polisi wa Tuzo na Tozo; na

(vi) Namna Jeshi la Zimamoto na Uokoaji linatekeleza majukumu yake.

**Mheshimiwa Spika**, Mafunzo hayo yamekuwa nyenzo muhimu katika utekelezaji wa majukumu ya Kamati. Kwa mfano, uelewa uliopatikana kuhusu uboreshaji wa Sera ya Mambo ya Nje umeiwezesha Kamati kufahamu ufanisi unaotarajiwa katika utekelezaji wa Sera iliyoboreshwa pamoja na changamoto tarajiwa. Uelewa uliopatikana unatumika kutoa ushauri bora wa kibunge kwa mambo yote ya kisera katika ushirikiano wa kimataifa na mtangamano wa kikanda.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa mwenendo wa kisiasa katika duru za Kimataifa, uelewa uliopatikana umejenga misingi bora wa kulishauri Bunge katika utekelezaji wa madaraka yake kwa namna inayowezesha ufanisi wa Serikali. Aidha, Kamati imetumia uelewa kutokana na mafunzo kuhusu masuala ya Zimamoto na Uokoaji nchini katika kutathmini afua (*interventions*) mbalimbali wakati wa majanga ya moto na mahitaji ya uokoaji.

**Kuchambua Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara**

**Mheshimiwa Spika**, Katika kipindi kinachoripotiwa, Kamati ilichambua utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2023/2024 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Matokeo ya kazi hiyo yalijumuishwa katika Taarifa ya Kamati iliyosomwa Bungeni wakati wa Mkutano wa Kumi na Tano wa Bunge.

Naomba kulijulisha Bunge lako tukufu kuwa, utekelezaji wa jukumu hilo, uliwezesha ufuatiliaji wa shughuli za umma kwa mujibu wa kifungu cha 7 (1) (d) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge.

**Kupokea na Kujadili Taarifa za Wizara Zinazosimamiwa na Kamati**

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa za Wizara ni nyenzo ya msingi katika kufuatilia na kujiridhisha kuhusu mchango wa sekta zinazohusika. Taarifa hizo zinawezesha kuona namna Wizara zinavyofanikisha lengo la Serikali la ustawi wa watu wanaowakilishwa katika Bunge hili. Kwa ujumla taarifa zilizopokelewa na kujadiliwa ziligusa masuala yafuatayo:

(i) Ulinzi na usalama wa raia na mali zao ikiwemo usalama barabarani;

(ii) uwezo wa uokozi na kukabiliana na majanga mbalimbali;

(iii) Uthabiti wa urekebu wa Wafungwa nchini;

(iv) Uimara wa usalama nchini;

(v) Hali ya wakimbizi na watafuta hifadhi nchini;

(vi) Usimamizi wa masuala ya uhamiaji ikiwemo wahamiaji haramu;

(vii) Hali ya biashara haramu ya usafirishaji wa Binadamu;

(viii) Usajili wa Jumuiya za Kidini na zisizo za kidini;

(ix) Ulinzi wa mipaka yetu;

(x) Hali ya Mtangamano wa Kikanda na uhusiano wa kimataifa; na

(xi) Hali ya siasa Duniani.

**Mheshimiwa Spika**, masuala hayo, yanahusika moja kwa moja na ustawi wa watu nchini. Kwa mfano, ulinzi na usalama wa raia na mali zao unaweka mazingira wezeshi ya shughuli za uchumi na kukuza uwezo wa huduma mbalimbali nchini. Aidha, uimara wa

usalama unafanikisha azma ya kuwezesha maisha bora na yenye utulivu na amani nchini.

**Kutembelea na Kukagua Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo**

**Mheshimiwa Spika**, ili kutekeleza masharti ya Kanuni ya 117 (1) ya Kanuni za Bunge, kuhusu Kamati za Kisekta kutembelea na kukagua utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha unaoishia, Kamati hii ilikagua Miradi ya Maendeleo iliyo chini ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ambayo ilitengewa fedha kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024. Matokeo ya shughuli hii yaliwasilishwa Bungeni wakati wa Mkutano wa Bajeti wa mwezi Aprili hadi Juni, 2024.

**Mheshimiwa Spika**, Vilivile, Kamati ilitembelea miradi mingine na kukagua uendeshaji wa shughuli za Shirika la MZINGA pamoja na Kituo cha Afya MZINGA. Maeneo mengine yaliyofuatiliwa na kukaguliwa na Kamati ni Ujenzi wa Makao Makuu ya Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu na Ujenzi wa Jengo la Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki-Mtumba Jijini Dodoma.

Ujenzi wa Jengo la Makao Makuu ya Idara ya uhamiaji – Dodoma, Ujenzi wa Kituo cha Zimamoto na Uokoaji –Mtumba Dodoma, ujenzi wa Ofisi za Idara ya Uhamiaji Unguja, vifaa na mashine za ukaguzi wa hati za kusafiria katika uwanja wa ndege wa kimataifa wa Amani Karume, utekelezaji wa shughuli za Gereza la Isanga Dodoma pamoja na ujenzi wa Gereza la Wilaya ya Karatu na Ofisi za Kamanda wa Polisi Mkoa wa Njombe.

**Mheshimiwa Spika**, Shughuli hizo zililenga ufuatiliaji wa sekta hizo na kubaini namna Wizara zinavyotekeleza majukumu yake. Kwa ujumla matokeo yake yametumika kupata maoni na ushauri wa Kamati wakati wa bajeti na Mapendekezo ya Kamati katika Taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika,** Vilevile, Kamati ilifanya ziara za kikazi katika nchi za Misri, Kenya na Zimbabwe. Ziara hizo ziliongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya Kamati.

**Kushughulikia Taarifa za Wawakilishi katika Vyama Mbalimbali vya Kibunge na Mabunge ya Kikanda**

**Mheshimiwa Spika**, katika utekelezaji wa jukumu la Kamati kwa mujibu wa Kifungu cha 7 (2) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilipokea na kujadili taarifa za wawakilishi wafuatao:-

(i) Wawakilishi wa Tanzania katika Bunge la Afrika Mashariki (EALA),

(ii) Wawakilishi katika Bunge la Afrika (PAP)

(iii) Wawakilishi kwenye Umoja wa Mabunge Duniani (IPU),

(iv) Wawakilishi kwenye Jukwaa la Kibunge la nchi za Ukanda wa Maziwa Makuu (*Great Lakes*);

(v) Wawakilishi kwenye chama cha mabunge ya Jumuiya ya Madola (CPA); na

(vi) Wawakilishi kwenye Bunge la Pamoja la Nchi za Afrika, Caribbean na Pasifiki na Umoja wa Ulaya (ACP EU).

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa hizo zimefanyiwa uchambuzi na matokeo yake yamechangia katika msingi wa maoni na mapendekezo ya Kamati nitakayoyasoma leo hii. Naomba kukiri kwamba, utaratibu huu umekuwa na tija kwa Bunge kwa kuwa uwakilishi unatambulika na kuliweka Bunge katika nafasi ya kufuatilia utekelezaji wa majukumu ya wawakilishi wake.

**Majumuisho ya Sehemu ya Kwanza**

**Mheshimiwa Spika**, sehemu hii imeeleza mambo makuu sita ambayo ni:

Msingi wa kuwasilisha Taarifa hii ambao ni masharti ya kanuni ya 136 (15) ya Kanuni za Bunge na madhumuni ya Kanuni hiyo;

(i) Lengo la Taarifa ambalo ni kuliwezesha Bunge kutekeleza majukumu yake ipasavyo;

(ii) Muundo wa Taarifa ili kubainisha mwelekeo wa mtiririko wa maudhui ambapo, imebainishwa kuwa Taarifa imegawanyika katika sehemu kuu tatu;

(iii) Njia kuu zilizotumika kupata maudhui ya Taarifa hii na sababu za kutumika kwa njia hizo;

(iv) Wajumbe 19 wa Kamati ili kuonesha wahusika wa maudhui na kujenga msingi wa uwajibikaji; na

(v) Majukumu ya Kamati na Shughuli zilizotekelezwa kwa kipindi cha Mwezi Februari, 2024 hadi Januari, 2025 ambayo ni kiini cha Taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika**, mambo hayo ni muhimu katika misingi ya taarifa zinazowasilishwa Bungeni. Kwa ujumla wake, yanadhihirisha namna taarifa inavyozingatia Kanuni na kuwasilishwa kwa uwazi katika muundo ambao unawezesha ufuatiliaji wa maudhui yake kwa urahisi. Aidha, mambo hayo yanaimarisha uwajibikaji kwa maudhui ya taarifa kutokana na kuwataja Wajumbe waliohusika na kazi inayoripotiwa Bungeni. Kwa msisitizo, mambo yote yanayoelezwa katika Taarifa hii kwa muundo uliobainishwa, yanastahili kufanyiwa kazi na Bunge kwa mujibu wa madaraka yake. Ufafanuzi zaidi unatolewa katika sehemu ya pili inayofuatia.

## SEHEMU YA PILI

## UFAFANUZI NA UCHAMBUZI WA MATOKEO YA SHUGHULI ZA KAMATI KIPINDI CHA FEBRUARI, 2024 HADI JANUARI, 2025

### Maelezo ya Jumla

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo ya jumla katika sehemu ya kwanza, sasa naomba kutoa ufafanuzi na uchambuzi wa matokeo ya shughuli za Kamati kwa kipindi kinachoripotiwa. Ufafanuzi huo unahusu maeneo makuu sita ambayo ni:-

(i) Ulinzi na Usalama wa Raia na Mali zao;

(ii) Wafungwa na Urekebu Magerezani;

(iii) Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa;

(iv) Mtangamano wa kikanda na uhusiano wa Kimataifa;

(v) Uwakilishi wa Bunge kwenye vyombo vya Uwakilishi wa kibunge;

(vi) Ushirikiano wa kibunge; na

(vii) Mambo ya Jumla kuhusu ufuatiliaji wa Kibunge chini ya Kamati.

**Ulinzi na Usalama wa Raia na Mali zao**

***Ufafanuzi wa Shughuli***

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inatambua kuwa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Tawala ni ahadi iliyotolewa kwa wananchi ambao waliikubali na kupiga kura. Kwa kuzingatia Ilani ya CCM, Serikali inatarajiwa kuimarisha ulinzi na usalama wa raia na mali zao kama ilivyoelezwa katika ukurasa wa 156, Sura ya Tano ya Ilani ya Uchaguzi wa mwaka 2020. Bunge kwa nafasi yake ya kufanya kazi kwa niaba ya wananchi linapaswa kufuatilia utekelezaji wa ahadi hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuwa Kamati hii ni injini ya Bunge katika sekta ya ulinzi na usalama, shughuli zake ni pamoja na kupokea Taarifa za hali ya ulinzi na usalama wa raia na mali zao. Naomba

kulijulisha Bunge lako tukufu kuwa Kamati ilifuatilia hali hiyo kwa kuchambua taarifa zilizohusu mambo yafuatayo:-

(i) Hali ya ulinzi na usalama wa Nchi;

(ii) Hali ya ulinzi na usalama wa mipaka ya nchi;

(iii) Mkakati wa kurasimisha waendesha bodaboda nchini;

(iv) Utekelezaji wa jukumu la kudhibiti ajali za barabarani nchini;

(v) Hali ya wakimbizi na watafuta hifadhi nchini;

(vi) Utendaji kazi wa Shirika la SUMA JKT;

(vii) Udhibiti wa biashara haramu ya usafirishaji wa Binadamu na biashara ya magendo; na

(viii) Hali ya miundombinu Magerezani na elimu ya Urekebu kwa wafungwa.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa taarifa hizo ulizingatia azma ya nchi kuwa na jamii salama inayolindwa dhidi ya matishio ya ndani na nje. Aidha, umuhimu wa kuihakikishia jamii haki na ustawi wa watu wote ulitiliwa maanani. Kwa misingi hiyo, Kamati ilitaka kujua masuala yafuatayo:

(i) Iwapo kuna ufanisi katika kulinda maisha ya raia dhidi ya hatari kama vile uhalifu na majanga ya asili;

(ii) Iwapo kuna uhakika wa ulinzi wa mali za raia na mali za umma;

(iii) Iwapo kuna usimamizi bora wa sheria na amani katika jamii; na

(iv) Iwapo kuna mazingira salama kwa ajili ya uwekezaji na maendeleo ya kiuchumi.

**Matokeo na Uchambuzi**

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa zilizowasilishwa kwenye Kamati zilionesha kuwa, hali ya usalama wa raia na mali zao kwa ujumla ni shwari na kwamba kuna utulivu, amani na usalama. Matokeo hayo yanaonesha kuwepo kwa  juhudi za pamoja za vyombo vya usalama, jamii, na Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi unaonesha kuwa ufanisi wa vyombo vya usalama, ushirikiano wa jamii, na uwekezaji katika miundombinu ya usalama wa raia ni miongoni mwa mambo yanayochangia utulivu, amani, na maendeleo endelevu nchini kwa sasa. Hata hivyo, bado kuna umuhimu wa kuendelea na uimarishaji wa ulinzi na usalama kwa ujumla. Msisitizo huu unatokana na ukweli kwamba, mambo hayo yasipoimarika, ni vigumu kufanikisha lengo la ustawi wa watu na maendeleo au kuwezesha maisha bora kwa kila Mtanzania.

**Changamoto Zilizobainika**

**Mheshimiwa Spika**, changamoto ni jambo la kawaida katika uendeshaji wa shughuli za umma duniani. Muhimu ni kuzibaini na kuzishughulikia ipasavyo. Kwa msingi huo, Kamati imebaini changamoto katika ulinzi na usalama wa raia na mali zao. Chagamoto hizo zinazohitaji ufumbuzi ni pamoja na:-

(i) Upungufu wa vifaa na vitendea kazi vya kisasa katika eneo la upelelezi na uchunguzi wa kisayansi;

(ii) Upungufu wa vyombo vya usafiri kama vile magari, helkopta, pikipiki na boti kwa vyombo vya ulinzi na usalama. Mathalani, Jeshi la Uhamiaji lina upungufu wa magari 348, pikipiki 390 na boti 13 na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji lina upungufa wa magari ya kuzima moto 156 na boti za uokozi 36;

(iii) Uchache wa vituo vya zimamoto na uokoaji nchini. Mathalani, nchi nzima kuna upungufu wa Vituo vya zimamoto na uokoaji 157;

(iv) Baadhi ya vifaa vya kitaalam vilivyopo kupitwa na wakati ikiwemo vya maabara ya sayansi ya uchunguzi;

(v) Uwepo wa uwiano usio sawa kati Askari na wananchi wanaohudumiwa. Kwa sasa uwiano ni 1:1,300 badala ya ule wa kimataifa ambao ni 1:45

(vi) Mwamko mdogo wa wananchi katika utoaji wa taarifa fiche kuhusu uhalifu na wahalifu;

(vii) Ongezeko la makosa mapya ya uhalifu yanayosababishwa na maendeleo ya sayansi na teknolojia, utandawazi, ukuaji wa miji, ongezeko la watu, ukosefu wa kazi na ujenzi holela wa makazi; na

(viii) Upungufu wa rasilimaliwatu kwa vyombo vya ulinzi na usalama; ambapo magereza ina upungufu wa askari 6000, Zimamoto Askari 7500, uhamiaji Askari 1200.

### Huduma za Magereza na Urekebu
### Ufafanuzi wa Shughuli

**Mheshimiwa Spika**, huduma za magereza na urekebu nchini zinasimamiwa na Jeshi la Magereza Tanzania (TPF). Huduma hii inahusika na usimamizi wa magereza, kuwezesha ulinzi wa wahalifu waliopo gerezani na kuwasaidia wafungwa kubadilika ili kurudi kwenye jamii kama raia wema Pamoja na kutoa ushauri wa Sera kuhusu uzuiaji wa uhalifu na ushughulikiaji wa wahalifu.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kutambua jukumu hilo, Aya ya 105, (n), uk. wa 158 wa Ilani ya CCM ya Uchaguzi wa mwaka 2020, ilitoa ahadi kwamba, Serikali italiwezesha Jeshi la Magereza kuendelea na majukumu ya kutunza, kuhifadhi na kufundisha wahalifu pamoja na kuzalisha mali. Ili kufuatilia utekelezaji wa ahadi hiyo, Kamati ilitaka kujua masuala yafuatayo:-

(i) Iwapo kuna ufanisi wa hifadhi na ulinzi wa wafungwa na mahabusu magerezani.

(ii) Iwapo jukumu la urekebu wa wafungwa kupitia elimu, mafunzo ya ufundi na msaada wa kisaikolojia linatekelezwa ipasavyo; na

(iii) Iwapo azma ya kuwajumuisha wafungwa waliomaliza kutumikia kifungo na kuingia kwenye jamii kama raia watiifu wa sheria inafanyiwa kazi ipasavyo.

### Matokeo na Uchambuzi

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ililinganisha miundombinu ya magereza nchini, majukumu ya urekebu na jitahada za kuwawezesha wafungwa wanapomaliza kifungo kuendana na kukubalika na jamii. Uchambuzi ulizingatia kuwa miundombinu ya magereza inapaswa kutoa mazingira bora kwa urekebu wa wafungwa. Ufanisi katika majukumu ya ulinzi, hifadhi, urekebu na ujumuishaji wa wafungwa wanapomaliza kifungo magerezani, unategemea miundombinu bora.

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi wa Taarifa zilizopokelewa kwa kipindi cha Februari, 2024 hadi Januari, 2025 unaonesha kuwa hali ya jumla ya miundombinu ya magereza nchini inaendelea kuimarika kutoka kwenye hali ngumu iliyokuwa imebainika. Aidha, juhudi hizo zimekwenda sambamba na kuliwezesha Jeshi la Magereza kuwa na nyezo na fedha zinazohitajika. Pamoja na hivyo, bado hali ya miundombinu ya Magereza inahitaji kuboreshwa zaidi ili kupata tija ya huduma za magereza.

### Changamoto Zilizobainika

**Mheshimiwa Spika**, miongoni mwa majukumu ya Jeshi la Magereza ni kuwarekebisha wafungwa ili wanapomaliza kutumikia adhabu zao wawe raia wema. Hata hivyo katika kutekeleza jukumu hili Jeshi hilo linakabiliwa na uchakavu wa miundombinu katika magereza. Magereza 85 kati ya Magereza zaidi ya 100 nchini yamejengwa kabla ya uhuru. Kwa msingi huo, miundombinu ya magereza hayo imekuwa chakavu kwa kuwa ilijengwa zaidi ya miaka 100 iliyopita. Kwa kipindi hicho, ujenzi wake haukuzingatia mahitaji ya huduma za urekebu na hifadhi salama kutokana na madhumuni ya utawala uliokuwepo. Hali hii

inapunguza ufanisi wa elimu ya urekebu inayopaswa kuendana na wakati wa sasa.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi zaidi ulibaini kuwa zaidi ya asilimia 85 ya Magereza nchini hayana mifumo ya TEHAMA na hivyo kuwa na changamoto katika eneo la kukusanya taarifa, kuchakata taarifa, kuhifadhi taarifa na kutumia taarifa kidigitali.

**Mheshimiwa Spika,** Kutokana na ukosefu wa TEHAMA, ufanisi wa Jeshi la Magereza katika kufuatilia kidigitali mienendo ya Wafungwa, Mahabusu, Wageni mbalimbali wanaotembelea Magereza na hata Askari, unapungua. Hali hii si nzuri katika kukabiliana na changamoto kiusalama ambazo zinabadilika kimfumo, muundo, uhusiano na asili yake kwa ujumla.

**Usafiri wa Bodaboda**

***Ufafanuzi wa Shughuli***

**Mheshimiwa Spika**, kama tunavyofahamu usafiri wa bodaboda nchini ni miongoni mwa njia kuu za usafiri wa haraka, uliozoeleka na wa bei nafuu mijini na vijijini. Usafiri huu unaendelea kutumika kusafirishia mizigo na abiria kwa umbali mrefu na mfupi katika shughuli za umma nchini. Aidha, usafiri wa bodaboda umepata umaarufu kutokana na mchango wake, kama vile kuwa wa bei nafuu, upatikanaji wake kwa haraka, urahisi wake kwenye msongamano wa magari na manufaa yake katika suala la ajira.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na hayo, sekta ndogo ya usafiri wa bodaboda imekuwa na rekodi kubwa ya kuchangia ajali za barabarani na mchango wake katika hatari na matishio ya kiusalama kwa raia, mali zao na kwa Taifa kwa ujumla. Hali hiyo ilihitaji kurasimisha masuala mbalimbali yanayohusu usafiri wa bodaboda. Kwa msingi huo, Kamati ilitaka kujua mikakati wa Serikali kurasimisha sekta ndogo ya usafiri wa bodaboda nchini. Kamati ilipokea maelezo ya Wizara ya Mambo ya ndani ya nchi kuhusu mkakati wa kurasimisha usafiri wa bodaboda nchini kwa upana wake. Lengo ni kuona mambo yafuatayo:-

(i) Iwapo mikakati hiyo inafanikisha kuwa na waendesha bodaboda wenye leseni halali, wanaozingatia Sheria na Kanuni za usalama barabarani;

(ii) Iwapo kuna uzingatiaji wa viwango vya udhibiti wa usalama barabarani kama vile masharti ya uvaaji wa helmenti;

(iii) Iwapo kuna misingi ya kuzingati katika kuimarisha usalama wa abiria, wanaendesha bodaboda na watumiaji wengine wa barabara;

(iv) Iwapo waendesha bodaboda wanawekewa mazingira ya kuboresha huduma ya usafiri wanaotoa;

(v) Iwapo juhudi za kuboresha miundambinu ya usafiri wa bodaboda kama vile maeneo ya maegesho;

(vi) Iwapo kunajuhudi za uandikishaji, utambuzi wa huduma; na

(vii) Iwapo kuna uendelezaji wa waendesha bodaboda kihuduma na uwezo wa kuzingatia usalama wao na wa abiria, mizigo na jamii kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika**, masuala hayo ni muhimu kwa manufaa ya umma, Serikali na Taifa yakifanyiwa kazi ipasavyo, usalama barabarani, utaimarika ajali za bodaboda zitapungua, hatari zilizopo zitadhibitiwa na manufaa ya usafiri huo yataonekana kiuchumi, kijamii na kisiasa.

**Matokeo ya uchambuzi wa shughuli**

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa taarifa na maelezo yaliyotolewa umebainisha mambo mbalimbali yanayofaa kuripotiwa Bungeni. Mambo hayo ni:-

(i) Kwa sasa hakuna mfumo rasmi wa kurekodi taarifa za waendesha bodaboda (utambuzi);

(ii) Waendesha bodaboda waliopo wanaainishwa katika kategoria ya wenye leseni na wasio na leseni;

(iii) Zaidi ya waendesha bodaboda, wapo wamiliki ambao pia wanapaswa kutambuliwa, kusajiliwa na kueleweka katika mikataba wanayoingia na waendesha bodaboda;

(iv) Hadi sasa hakuna utaratibu rasmi wa mafunzo kwa waendesha bodaboda kama sekta rasmi; na

(v) Serikali haijaweka baadhi ya miundombinu muhimu ya bodaboda kama vile maegesho au vituo rasmi vya bodaboda.

**Mheshimiwa Spika**, kwa matokeo hayo ya uchambuzi, sekta ndogo ya usafiri wa bodaboda inaendelea kuwa na rekodi za ajali, mazalia ya uhalifu kutokana na wachache miongoni mwa madereva wa bodaboda kutokuwa raia wema na hivyo kuwa hatarishi kwa usalama barabarani na usalama wa raia na mali zao.

### *Changamoto Zilizobainika*

**Mheshimiwa Spika**, kama ilivyo kwa mikakati ya jambo lingine lolote, suala la kuwa na mikakati ya kurasimisha usafiri wa bodaboda limebainika kukabiliwa na changamoto. Baadhi ya changamoto hizo ni kama ifuatavyo:-

(i) Kukosekana kwa mfumo rasmi wa utambuzi wa waendesha bodaboda pamoja na wamiliki;

(ii) Upungufu wa rasilimali fedha;

(iii) Changamoto za mtazamo ya kisiasa ambapo wanapovunja Sheria hutizamwa kama wapiga kura; na

(iv) Ukosefu wa matumizi ya teknolojia katika udhibiti na usimamizi wa bodaboda nchini.

Tathmini ya kamati inaonesha kuwa kwa sasa sekta hii kwa sehemu kubwa inajiongoza yenyewe kwani hata vituo huanishwa na bodaboda wenyewe na wamejiwekea taratibu mbalimbali ambazo wanazisimamia wenyewe.

**Udhibiti wa Ajali za Barabarani**

***Ufafanuzi wa Shughuli***

**Mheshimiwa Spika**, udhibiti wa ajali za barabarani ni muhimu katika kuboresha usalama na kuwezesha ustawi wa wananchi. Ajali za barabarani husababisha madhara makubwa kwa watu, mali, Serikali na Uchumi wa Taifa. Bunge la Tanzania lilitunga Sheria za kudhibiti usalama barabarani. Hata hivyo, rekodi zinaonesha kuwepo kwa matukio ya ajali za barabarani sambamba na madhara yake. Kwa msingi huo, Kamati ilipokea maelezo ya Serikali kuhusu mikakati ya kudhibiti ajali za barabarani.

**Mheshimiwa Spika**, katika taarifa hiyo Kamati ilifuatilia masuala yafuatayo:-

(i) Iwapo kuna utekelezaji tabiti wa Sheria na Kanuni za Usalama Barabarani.

(ii) Iwapo, adhabu zinazochukuliwa kwa wanaokiuka Sheria na Kanuni za Usalama Barabarani zinatekelezeka na zina tija.

(iii) Iwapo kuna elimu kwa umma kuhusu usalama barabarani inatolewa kwa mbinu na namna yenye ufanisi.

(iv) Iwapo kuna kampeni za kutosha na za mara kwa mara zinazohusisha wananchi kwa wigo mpana kuhusu usalama barabarani.

(v) Iwapo kuna juhudi za kuhusianisha ubora wa miundombinu inayojengwa na mahitaji ya viwango vya usalama barabarani.

(vi) Iwapo kuna utaratibu wenye tija wa ukaguzi wa magari kabla ya kupewa leseni au usajili wa shughuli za usafirishaji.

(vii) Iwapo kuna ukaguzi wa mara kwa mara wa magari ya abiria na mizigo ili kuona uzingatiaji wa viwango vya usalama.

(viii) Iwapo kuna ukusanyaji wa takwimu za ajali na uchambuzi kwa ajili ya kupata mazingatio muhimu katika kuendelea kudhibiti ajali za barabarani.

(ix) Iwapo kunajuhudi za kutumia teknolojia mpya kama vile kamera za usalama, rada za kuangalia kasi, au vifaa vingine.

### *Matokeo ya Uchambuzi*

**Mheshimiwa Spika**, matokeo ya uchambuzi yameonesha kuwa, kwa ujumla Serikali inaendelea na juhudi za kupunguza ajali na kudhibiti matukio ya ajali za barabarani.

Hata hivyo, yapo maeneo yaliobainika kuhitaji maboresho katika mkakati wa kupunguza ajali za barabarani maeneo hayo ni:-

(i) Matumizi ya teknolojia mpya katika kudhibiti ajali;

(ii) Elimu kwa umma yenye tija na kampeni mbalimbali kuhusu usalama barabarani;

(iii) Kujenga barabara pana zenye kukidhi mahitaji ya sasa na baadae;

(iv) Ukaguzi wa magari kabla ya kupewa leseni;

(v) Kufanya ukaguzi endelevu na wenye tija; na

(vi) Bima za ajali kwa magari ya abiria pamoja na elimu kuhusu kazi ya bima kwa abiria baada ya ajali.

### *Changamoto Zilizobainika*

**Mheshimiwa Spika**, baada ya Kamati kupokea taarifa kutoka serikalini kuhusu mkakati wa kudhibiti ajali za barabarani, changamoto zifuatazo zilibainika;

(i) Wembamba, uchakavu na ubovu wa barabara ambao unachangia kutokea kwa ajali;

(ii) Elimu ya usalama barabarani isiyo na tija na hivyo kutokuwa na ufanisi kwa mazingira ya sasa;

(iii) Ukaguzi wa magari usio na tija; hali hii husababisha hata magari yasiyokaguliwa kuwa na stika ya usalama barabarani ambayo ni nyaraka inayoonesha kuwa gari husika limekaguliwa;

(iv) Kuongezeka kwa makosa ya kibinadamu yanayotokana na uzembe ambayo yanachangia kutokea kwa ajali;

(v) Kutosimamiwa ipasavyo kwa Sheria ya Usalama Barabarani kutokana na ushawishi wa rushwa; na

(vi) Adhabu ndogo na zisizoendana na mazingira ya sasa kwa makosa yanayotokana na uvunjifu wa Sheria ya Usalama Barabarani.

### Udhibiti wa Biashara Haramu ya Usafirishaji wa Binadamu

### *Ufafanuzi wa Shughuli*

**Mheshimiwa Spika**, biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu ni changamoto kubwa duniani kote. Biashara hii inamadhara makubwa kwa watu binafsi, familia jamii, mataifa na ulimwengu mzima. Biashara hii inahusisha ukiukwaji wa haki za binadamu, utumwa na unyanyasaji na inakumbatia uhalifu. Kutokana na tatizo hilo, Bunge hili lilitunga Sheria ya Kuzuia na Kudhibiti Usafirishaji Haramu wa Binadamu, Sura ya 432.

**Mheshimiwa Spika**, Bunge ambalo ni chombo cha uwakilishi wa wananchi linapaswa kujua hatua za Serikali katika kudhibiti na kuzuia biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu ili kuliwezesha Bunge kufuatilia suala hilo, kamati ilipokea na kuchambua taarifa na maelezo ya Serikali kuhusu udhibiti wa biashara hiyo katika uchambuzi wake, kamati ilifuatilia masuala yafuatayo:-

(i) Iwapo Sheria za kudhibiti usafirishaji haramu wa binadamu zinatekelezwa kwa ufanisi;

(ii) Iwapo Maafisa wa Sekretarieti ya Kuzuia na Kupambana na Biashara Haramu ya Usafirishaji wa binadamu, Jeshi la Polisi, Uhamiaji na vyombo vingine vya Ulinzi na Usalama wanapewa mafunzo maalum ya kutambua na kushughulikia kesi za biashara ya binadamu;

(iii) Iwapo Serikali inaweka mikakati ya kuwalinda waathirika wa biashara ya binadamu dhidi ya unyanyasaji wa mara ya pili au kulipiziwa kisasi;

(iv) Iwapo Serikali inashirikiana na nchi nyingine, mashirika ya kimataifa (kama UNODC na INTERPOL), na mashirika ya kikanda kupambana na biashara hii;

(v) Iwapo Serikali imeimarisha udhibiti wa mipaka ili kuzuia biashara ya binadamu kuvuka mipaka ya nchi;

(vi) Iwapo Serikali inaendesha kampeni za kuelimisha umma kuhusu biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu, njia zinazotumiwa na wasafirishaji na jinsi ya kuripoti kesi zinazoshukiwa;

(vii) Iwapo Serikali inashirikiana na viongozi wa kijamii, mashirika ya dini na asasi za kiraia kuongeza uelewa na kushughulikia biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu;

(viii) Iwapo Serikali inaweka juhudi za kupunguza umasikini ambao mara nyingi huwalazimisha watu kuingia kwenye mazingira ya hatari ya biashara ya binadamu;

(ix) Iwapo Serikali inakusanya, kuchambua na kuripoti takwimu sahihi kuhusu biashara ya binadamu, ikiwa ni pamoja na idadi ya kesi, waathirika na wahusika waliokamatwa na kuhukumiwa; na

(x) Iwapo Serikali inashirikiana na sekta binafsi, kama vile sekta ya usafiri na mawasiliano, ili kudhibiti matumizi ya teknolojia katika biashara hii.

**Matokeo ya Uchambuzi**

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi unaonesha kuwa Serikali inachukua hatua kukabiliana na tatizo la usafirishaji wa binadamu. Sheria iliyotungwa na Bunge inasimamiwa ipasavyo na Sekretarieti ya Kuzuia na Kupambana na Biashara Haramu ya Usafirishaji wa Binadamu na vyombo vya Ulinzi na usalama vinashirikiana vizuri.

Juhudi za Serikali zinaendelea kuleta mafanikio katika kudhibiti biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu. Hali hii inathibitishwa na ukweli kuwa katika kipindi cha mwaka 2020-2024 zaidi ya Wahanga 1110 wa usafirishaji wa biashara haramu ya binadamu wameokolewa; ambapo 902 ni wa ndani ya nchi na 208 waliokolewa kutoka nje ya nchi. Halikadhalika katika kipindi hicho wahalifu 103 walifunguliwa kesi.

***Changamoto***

**Mheshimiwa Spika**, katika udhibiti wa biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu changamoto zilizobainika ni pamoja na:-

(i) Elimu ndogo kwa wananchi kuhusu ilivyo biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu;

(ii) Kampeni dhidi ya biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu kutofanyika kiasi cha kutosha hususan maeneo ya vijijini;

(iii) Bajeti isiyokidhi mahitaji inayotengewa Sektretariati ya Kuzuia na Kupambana na Biashara Haramu ya Usafirishaji wa Binadamu;

(iv) Uhaba wa vifaa na vitendea kazi unaoikabili Sektretariati ya Kuzuia na Kupambana na Biashara Haramu ya Usafirishaji wa Binadamu Pamoja na vyombo vingine vya ulinzi na usalama;

(v) Ukosefu wa matumizi ya teknolojia katika kukabiliana na baishara haramu ya usafirishaji wa binadamu;

(vi) Upungufu wa rasilimali watu katika sekretarieti ya Kuzuia na Kupambana na Biashara Haramu ya Usafirishaiji wa Binadamu; na

(vii) Kukosekana kwa mashirikiano ya kimkakati baina ya Serikali, mashirika ya kidini, mashirika ya kiraia pamoja na viongozi wa kijamii katika mapambano dhidi ya biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu.

**Wakimbizi Walio Nje ya Kambi**

***Ufafanuzi wa Shughuli***

**Mheshimiwa Spika,** kwa kawaida, wakimbizi walio nje ya kambi huwakilisha kundi la watu waliokimbia nchi zao kutokana na sababu kama vita, mateso au ukiukwaji wa haki za binadamu, lakini huamua au hulazimika kuishi nje ya kambi rasmi zilizoundwa na Serikali au Mashirika ya misaada. Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Wakimbizi (UNHCR) limeweka mwongozo na sera za kusaidia wakimbizi wanaoishi nje ya kambi ili kuhakikisha wanapata haki na huduma za msingi.

**Mheshimiwa Spika,** Bunge la nchi inayowahifadhi wakimbizi walio nje ya kambi lina wajibu mkubwa wa kufuatilia hali yao ili kuhakikisha haki za binadamu, usalama, na maslahi ya wakimbizi pamoja na jamii zinazowapokea zinalindwa. Kamati inayohusika na hilo ni Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama. Kwa sababu hiyo, Kamati ilipokea taarifa kuhusu hali ya wakimbizi na utambuzi wa wakimbizi waiishio nje ya kambi.

***Matokeo ya Uchambuzi***

**Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Septemba 30, 2024 nchi yetu ilikuwa na wakimbizi na waomba hifadhi 241,589; ambao wanaishi katika kambi mbalimbali za wakimbizi katika mikoa ya Kigoma, Tabora, Katavi na Tanga.

**Mheshimiwa Spika,** ufuatiliaji na uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa mbali ya wakimbizi hao walio katika makambi na makazi maalum wapo wakimbizi ambao wanaishi nje ya makambi na makazi ya wakimbizi kinyume na utaratibu. Wakimbizi hao wanaoishi nje ya makambi kinyume na utaratibu baadhi wameweza kuanzisha makazi ya kudumu na wanaendesha shughuli mbalimbali za kiuchumi kama wananchi wengine hasa katika mikoa ya Tabora, Kigoma, Katavi, Rukwa, Tanga, Geita na Kagera.

**Mheshimiwa Spika,** hali inakwenda kinyume na Sheria za kimataifa, Sheria za nchi pamoja na taratibu za wakimbizi.

***Changamoto Zilizobainika***

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inatambua Serikali inafanya juhudi kubwa katika kuwatambua wakimbizi walio nje ya kambi kinyume na utaratibu. Hata hivyo zoezi hilo linakabiliwa na changamoto zifuatazo;-

(i) Upungufu wa rasilimawatu na fedha unaoikabili Idara ya Huduma za Wakimbizi;

(ii) Wananchi kutokuwa na mwamko wa kutoa taarifa fiche kuhusu wakimbizi walio kwenye makazi yao;

(iii) Kukosekana kwa kitengo maalum katika muundo wa idara ya huduma kwa wakimbizi kinachohusika na wakimbizi walio nje ya kambi kinyume na sheria; na

(iv) Wakimbizi walio nje ya kambi kinyume na sheria wameachwa kwa muda mrefu pasipo kufuatiliwa na kuchukuliwa hatua stahili na hivyo wameweza kujipenyeza kwenye jamii na kunufaika na huduma nyingine kama wananchi wengine na hivyo kuweka mazingira magumu kuwatambua.

**Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa**

***Ufafanuzi wa Shughuli***

**Mheshimiwa Spika**, suala la ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa nchini linahusiana kwa karibu na kuweza na kuendelea kuwa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania yenye amani na usalama. Mwelekeo huo ndiyo dira ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa yenye wajibu unaogusa masuala ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa nchini.

**Mheshimiwa Spika,** Naomba kulikumbusha Bunge lako tukufu msingi wa kazi yake ya kufuatilia kwa karibu jukumu la Serikali kwenye eneo la ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Kazi hiyo inatokana na sababu kuu tatu.

**Kwanza** ni dhana ya usimamizi na uwajibikaji inayotambua wajibu wa Bunge kufuatilia masuala hayo.

**Pili**, nafasi ya Bunge katika uendeshaji wa nchi kwa kuwa chombo halisi cha uwakilishi wa wananchi.

**Tatu** ni falsafa ya udhibiti wa kiraia wa masuala ya kijeshi (*The doctrine of Civilian Control of the Military*). Falsafa hii inalenga kuwezesha utekelezaji wa majukumu ya ulinzi wa mipaka na yale

ya kiraia kwa pamoja katika namna inayoweka mbele maslahi ya umma na ya Taifa kwa misingi ya sheria za nchi.

**Matokeo ya Uchambuzi**

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi umefanyika kwa maeneo makubwa mawili kama ifuatavyo:-

**(a) Hali ya Ulinzi na Usalama wa Mipaka**

**Mheshimiwa Spika**, katika eneo la ulinzi, Kamati ilifuatilia ufanisi wa sekta ya ulinzi kwa maana ya usalama wa mipaka na Jeshi la Kujenga Taifa. Kamati ilipokea na kujadili Taarifa za Hali ya Ulinzi na usalama wa mipaka kila mara. Nafurahi kulijulisha Bunge kuwa uchambuzi unaonesha kwamba, hali ya ulinzi wa mipaka yetu kwa ujumla ni shwari na imara, na huku ikiendelea kuimarishwa inavyostahili. Serikali imeendelea kutekeleza ahadi yake kwa wananchi ya kuimarisha ulinzi na usalama wa nchi na mipaka yake kama ilivyoahidiwa katika Ilani ya Uchaguzi wa CCM, Aya ya 105, ukurasa wa 156.

**(b) Shughuli za Jeshi la Kujenga Tafa**

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa Jeshi la Kujenga Taifa, Kamati ilizingatia matarajio ya nchi kuliona Jeshi la Kujega Tafa linafanikisha azma ya kuwa na Tanzania yenye Jamii ambayo ina nidhamu, umoja, uzalendo, udugu, ukakamavu na kupenda kazi. Katika kufanya hivyo, Kamati ilitaka kujiridhisha iwapo Jeshi la Kujenga Taifa linafanikiwa kuwalea Vijana wa Tanzania, ili kuwajengea nidhamu, uzalendo, ukakamavu pamoja na kuwafundisha ujuzi, ambao utawawezesha kuchangia katika ulinzi wa Taifa na maendeleo ya kiuchumi.

**Mheshimiwa Spika,** historia inaonesha kuwa shughuli za mafunzo, malezi ya vijana na uzalishaji mali katika Jeshi la Kujenga Taifa zilipata kukabiliwa na uhaba au ucheleweshaji fedha za kujiendesha. Hali hiyo ilisababisha kutofikia malengo ya kuanzishwa kwa kambi za JKT nchini. Ili kukabiliana na

changamoto hiyo, lilianzishwa Shirika la Mkuu wa JKT kupitia Tangazo la Serikali Namba 94 la Julai mosi, 1981. Baadaye, mwaka 1985 Shirika lilibadilishwa na kuwa Shirika la Uzalishaji Mali la JKT (SUMAJKT).

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia historia hiyo, Kamati ilitaka kujiridhisha iwapo SUMAJKT linaendelea kukidhi madhumuni ya kuanzishwa kwake na kuongeza ufanisi katika Ulinzi na mafunzo ya JKT.

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa zilizopokelewa zinaonesha kuwa SUMAJKT imeendelea kutekeleza majukumu yake. Katika maendeleo hayo, Shirika hilo lina Kampuni Tanzu zaidi ya kumi na Tatu ambazo zinatekeleza majukumu ya uzalishaji mali pamoja na kuchangia uchumi wa Taifa kupitia Sekta ya Ujenzi, Sekta ya Viwanda, Sekta ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi, Sekta ya Biashara na Huduma pamoja na Sekta ya Elimu.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi ulibainisha kwamba, mchango wa SUMAJKT katika kugharimia uendeshaji wa shughuli za malezi ya vijana wa JKT, kwa Mwaka wa Fedha 2023/24 ulikuwa ni **Shilingi Milioni 803**. Vilevile, Shirika hilo limeendelea kushiriki katika ujenzi wa miundombinu ya kambi za JKT, na kutoa mafunzo ya vitendo kwa vijana wa JKT kupitia kampuni zake Tanzu.

## Changamoto Zilizobainika

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo mabadiliko ya muktadha na mazingira, changamoto katika sekta ya ulinzi haziepukiki. Jambo la maana zaidi ni hatua za kuzikabili changamoto hizo kadiri zinavyobainika.

Kutokana na umuhimu wa kuzitambua changamoto za sekta ya ulinzi, Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa miaka mitano 2021/22 – 2025/2026 umetambua uthabiti wa vyombo vya ulinzi na usalama kama hatua muhimu ya kufanikisha azma ya amani, utulivu na usalama.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Jeshi la Kujenga Taifa, hususan SUMAJKT, zipo changamoto zinazohitaji kufanyiwa kazi. Changamoto hizo ni:

(i) Kuzidai Taasisi binafsi, Taasisi za Umma na Wizara za Serikali zilizopatiwa huduma na kampuni tanzu zaidi ya Shilingi Bilioni 40. Kiasi hiki ni kikubwa na kinafifisha shughuli za Shirika katika uzalishaji na kushindwa kutekeleza malengo iliyojiwekea; na

(ii) Ukosefu wa mitaji mkubwa ya kuanzisha miradi ya kimkakati ikiwemo kiwanda cha Madawa, vifaa tiba na Mbolea.

**Hali ya Mtangamano wa Kikanda**

**Mheshimiwa Spika**, Bunge lako tukufu ambalo ni chombo cha uwakilishi wa wananchi, lina maslahi katika mtangamano wa kikanda (Mtangamano wa Afrika Mashariki na Mtangamano wa SADC). Msingi wake ni kuwa mtangamano wa kikanda una athari kubwa za kisiasa, kiuchumi, kijamii, na kitamaduni ambazo zinagusa maendeleo na utawala wa nchi. Kwa msingi huo, Kamati ilijielekeza katika ufuatiliaji wa hali ya Mtangamano na hivyo taarifa hii inaripoti shughuli hiyo na matokeo ya uchambuzi kama ifuatavyo:-

**Ufafanuzi wa Shughuli**

**Mheshimiwa Spika**, katika utekelezaji wa majukumu yake, Kamati ilipokea Taarifa kuhusu hali ya mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na mtangamano wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika. Lengo la shughuli hii ni kuliwezesha Bunge kujiridhisha iwapo ahadi, manufaa, na majukumu ya taifa ndani ya mifumo ya ushirikiano wa kikanda yanalingana na maslahi ya kitaifa, malengo ya maendeleo na mamlaka ya kikatiba. Katika shughuli hii, Kamati ilitaka kujiridhisha na masuala yafuatayo:-

(i) Iwapo Serikali inatekeleza ipasavyo majukumu yake chini ya makubaliano ya kikanda.

(ii) Iwapo juhudi za ushirikiano wa kikanda zinachangia kwa kiasi kikubwa ukuaji wa uchumi, biashara, usalama, na ustawi wa kijamii nchini.

(iii) Iwapo utekelezaji wa makubaliano, itifaki, na mikataba ya kikanda unakwenda inavyostahili.

(iv) Iwapo kuna manufaa ya kutosha kiuchumi, kisiasa, na kijamii kwa nchi kutokana na ushiriki wa nchi kwenye shughuli za Jumuiya hizo za kikanda.

**Matokeo ya Uchambuzi**

**Mheshimiwa Spika,** Matokeo ya uchambuzi yanaonesha kwamba, nchi wanachama wa Jumuiya hizo za kikanda: Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika zimenufaika kwa namna mbalimbali. Ufafanuzi wa manufaa hayo kwa kila Jumuiya ni kama ifuatavyo:-

**(a) Jumuiya ya Afrika Mashariki**

**Mheshimiwa Spika**, Tanzania imeendelea kunufaika na kuwa mwanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki katika nyanja za kibiashara, sekta za uchumi pamoja na uhusiano kati ya Tanzania na nchi wanachama wa Jumuiya hiyo. Uanachama umeendelea kuleta manufaa mbalimbali kwa nchi katika kipindi cha mwaka 2024. Manufaa hayo ni pamoja na yafuatayo:-

(i) Kukua kwa soko la bidhaa na huduma mbalimbali ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki;

(ii) Urahisi wa Watanzania kusafiri ndani ya nchi wanachama umeongezeka:

(iii) Mchango wa Tanzania kwenye juhudi za kuleta amani na utulivu katika ukanda wa Maziwa Makuu umeiwezesha Tanzania kuwa na heshima na kuimarisha utulivu na amani ndani ya nchi; na

(iv) Manufaa ya ufanisi wa biashara katika soko la kikanda kutokana na kuongezeka kwa urahisi wa kufanya biashara ndani ya kanda.

**(b) Mtangamano wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC)**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipokea na kujadili taarifa ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kuhusu Hali ya Mtangamano wa SADC. Uchambuzi ulionesha kuwa Jumuiya ya Maendeleo kusini mwa Afrika inatekeleza hatua moja tu ya mtangamano ambayo ni eneo huru la biashara.

**Mheshimiwa Spika**, Tanzania imenufaika katika kuuza bidhaa zake kwa nchi wanachama kwa urahisi kutokana na utaratibu wa kuondoleana ushuru. Mathalani, katika kipindi cha miaka 5 kuanzia mwaka 2019-2023, uraimu wa biashara umefikia wastani wa dola za marekani milioni 783. Bidhaa zinazoongozwa kwa kuuzwa ni pamoja na dhahabu, pamba, nguo, chai, kahawa na bidhaa za viwandani.

**Changamoto Zilizobainika**

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na mafanikio makubwa ya uanachama wa Tanzania katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, na Jumuiya ya Mandeleo Kusini mwa Afrika. zipo changamoto kwa Jumuiya hizo na nchi wanachama.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa Jumuiya ya Afrika Mashariki changamoto hizo ni Pamoja na;-

(i) Kasi ndogo ya utekelezaji wa Itifaki ya Soko la pamoja kutokana na kukosekana kwa Sheria moja ya Jumuiya ya kutekeleza itifaki hiyo kama ilivyo kwa itifaki ya umoja wa Forodha;

(ii) Baadhi ya nchi kuendelea kuweka vikwazo vya biashara visivyo vya kodi kinyume na itifaki ya Forodha;

(iii) Baadhi ya nchi wanachama kuwa na migogoro ya ndani ya kisiasa inayochangia kuzorota kwa hali ya usalama; na

(iv) Kasi ndogo ya nchi wanachama katika utoaji wa michango ya bajeti katika Jumuiya.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa SADC, changamoto ni Pamoja na:-

(i) Baadhi ya nchi wanachama kutowasilisha kwa wakati michango yao na hivyo kupunguza kasi ya utekelezaji wa program za mtangamano na baadhi ya taasisi kushindwa kutekeleza majukumu yake ipasavyo;

(ii) Kukosekana kwa miundombinu imara ya kufanikisha biashara kama vile reli na barabara hali ambayo inaathiri uhusiano wa kibiashara katika SADC,

(iii) Mabadiliko ya tabianchi ambayo yanaathiri uzalishaji wa chakula na shughuli nyingine za kiuchumi;

(iv) Sekta binafsi kutochangamkia ipasavyo fursa zitokanazo na mtangamano wa kikanda na uhusiano wa kimataifa; na

(v) Baadhi ya nchi wanachama kuwa na migogoro ya ndani ya kisiasa inayochangia kuzorota kwa hali ya kiusalama.

**Uwakilishi wa Bunge kwenye Vyombo vya Uwakilishi wa Kibunge**

**Ufafanuzi wa Shughuli**

**Mheshimiwa Spika**, Wawakilishi wa Bunge letu kwenye vyombo vya kiuwakilishi, wanatumwa na Bunge na wanawajibika kwa Bunge. Kifungu cha 7(2)(c) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge kimeweka masharti yanayoitaka Kamati hii kushughulikia Taarifa za wawakilishi hao. Kwa msingi huo, Kamati ilipokea taarifa za wawakilishi wa Bunge zifuatazo:-

(i) Taarifa za Wawakilishi wa Tanzania katika Bunge la Afrika (PAP);

(ii) Taarifa za Wawakilishi wa Tanzania katika Bunge la Afrika Mashariki (EALA);

(iii) Taarifa za Wawakilishi wa Bunge katika Umoja wa Mabunge Duniani (IPU);

(iv) Taarifa za Wawakilishi wa Tanzania katika Jukwaa la Kibunge la Nchi za Ukanda wa Maziwa Makuu;

(v) Taarifa za wawakilishi wa Tanzania katika Umoja wa Mabunge wa Jumuiya ya Madola (CPA);

(vi) Taarifa za Wawakilishi wa Tanzania katika Umoja wa Mabunge wa Nchi za Afrika, Caribbean na Pacific na Jumuiya ya Ulaya (ACP EU); na

**Uchambuzi wa Matokeo**

**Mheshimiwa Spika**, Kutokana na uchambuzi wa Taarifa zilizowasilishwa, Kamati imethibitisha kuwa, ushiriki wa wawakilishi wa Bunge kwenye vyombo vya Kibunge umesaidia kuimarisha ushirikiano na Vyombo vya Kibunge vya kikanda na Bunge letu. Matokeo ya uimara huo, yanaongeza manufaa ya Tanzania kushirikiana na nchi wanachama wa Jumuiya za Kikanda. Aidha, utaratibu huu wa wakilishi kuripoti kwenye Kamati umesaidia kuhakikisha kwamba wawakilishi wanawajibika ipasavyo kusimamia maslahi ya kitaifa kwa kadiri Bunge hili linavyotarajia. Uzoefu huo, umeongeza usimamizi wa kibunge wa masuala ya kisera kuhusu ushirikiano wa kikanda na kimataifa.

**Ushirikiano wa Kibunge**

**Ufafanuzi wa Shughuli**

**Mheshimiwa Spika**, ushirikiano wa kibunge unahusisha ushirikiano kati ya Bunge la nchi moja na Bunge la nchi nyingine (*Bilateral*

*relation*) au Ushirikiano wa Bunge na Mabunge mengine katika Jumuiya au taasisi za Kibunge za kimatiafa ama za kikanda (*Multilateral relations*). Kama ilivyobainishwa awali, mojawapo ya majukumu ya Kamati hii ni kuimarisha ushirikiano kati ya Bunge la Tanzania na Mabunge ya nchi nyingine. Ushirikiano huu unajumuisha:-

(i) Ziara za kubadilishana uzoefu baina ya Wabunge wa Tanzania na wenzao wa nchi nyingine.

(ii) Shughuli za Vyama vya Urafiki wa Kibunge (Parliamentary Friendship Groups) kati ya Bunge la Tanzania na Mabunge ya nchi nyingine

(iii) Mifumo ya kubadilishana taarifa na nyaraka za kibunge kupitia teknolojia ya kidijitali, kama vile majukwaa ya mtandaoni ya kushirikishana taarifa za utungaji wa sheria, na ripoti za Kamati.

(iv) Warsha na semina za pamoja kuhusu changamoto za kikanda na kimataifa kama vile mabadiliko ya tabianchi, masuala ya usalama, na maendeleo ya uchumi.

(v) Mikataba na Makubaliano rasmi ya ushirikiano (MoUs) kati ya Bunge la nchi moja na Mabunge ya nchi nyingine.

(vi) Vikao vya pamoja vya majadiliano na Mabunge ya nchi jirani ili kushughulikia masuala ya kikanda kama usalama wa mipaka, biashara na usimamizi wa rasilimali.

**Matokeo ya Uchambuzi**

**Mheshimiwa Spika**, Matokeo ya uchambuzi yanaonesha kuwa, Bunge lako tukufu limefanikiwa kuimarisha ushirikiano kati yake na mabunge ya nchi jirani ndani ya Afrika Mashariki pamoja na Nchi za SADC. Aidha, ushirikiano umekuwa mzuri kati ya Bunge la Tanzania na Mabunge ya nchi nyingine za Afrika, Asia na Ulaya. Mfano wa mambo yanayojenga ushirikiano huo ni ziara za

kibunge na mawasiliano ya kibunge kwa baadhi ya nchi kama vile, Malawi, Uganda, Zimbabwe, China na Ghana kwa kipindi cha mwaka 2024.

**Mheshimiwa Spika**, Hadi sasa Bunge la Tanzania lina vyama vya urafiki wa kibunge na mabunge mbalimbali vipatavyo 13. Kwa mwaka 2024, Bunge lilianza mchakato wa kuwa na Vyama vya urafiki wa Kibunge kati yake na Bunge la Misri na Rwanda.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaridhishwa na maendeleo ya ushirikiano wa kibunge kati ya Bunge la Tanzania na mabunge ya nchi nyingine ambayo yamefanyika kwa mwaka huu. Kupitia ushirikiano huo, masuala muhimu kama vile mijadala ya kuimarisha usalama na ulinzi wa amani katika ukanda wa Afrika, kuboresha mazingira ya biashara ya kikanda, kuvutia wawekezaji, namna ya kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi na kukuza elimu ya viwango vya kimataifa yamejadiliwa na kueleweka na hivyo kufikia makubaliano kibunge.

**Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge yaliyotolewa katika Mkutano wa Kumi wa Bunge**

**Ufafanuzi wa Shughuli**

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa Bunge ni mamlaka ya kusimamia shughuli za umma, linapaswa kufuatilia utekelezaji wa maazimio yake. Miongoni mwa njia za Bunge kufuatilia utekelezaji huo, ni Kamati zinazohusika kupokea na kujadili taarifa za Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge. Kwa vile maazimio ya Bunge yaliyotokana na Taarifa za Kamati za Bunge yalipitishwa mwezi Februari, 2024, Kamati hii ilifuatilia utekelezaji wa maazimio hayo uliopaswa kufanywa na Wizara tatu kwa kipindi tajwa. Wizara hizo ni Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

**Matokeo ya Uchambuzi**

**Mheshimiwa Spika**, matokeo ya uchambuzi yanaonesha kuwa Wizara zote tatu zimetekeleza maazimio ya Bunge kwa viwango

tofauti. Yapo maazimio yaliyotekelezwa kikamilifu, yapo yaliyaanza kutekelezwa lakini hayajakamilika na yapo machache ambayo hayajaanza kutekelezwa. Hali ya utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kutokana na Taarifa ya Kamati hii mwezi Februari, 2024 ni kama ifuatavyoonekana katika Jedwali Na. 1.

**Jedwali Na. 1: Hali ya Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kwa Sekta zinazosimamiwa na Kamati**

| WIZARA | JUMLA YA MAAZIMIO | YALIYOTEKELEZWA | UTEKELEZAJI UNAENDELEA | HAYAJATEKELEZWA |
|---|---|---|---|---|
| **Mambo ya Nje** | 12 | 6 | 5 | 1 |
| **Mambo ya Ndani** | 14 | 2 | 9 | 3 |
| **Ulinzi na JKT** | 3 | 1 | 1 | 1 |
| **Jumla ya idadi** | 29 | 9 | 15 | 5 |

**Chanzo**: Taarifa zilizopokelewa na Kamati

**Mheshimiwa Spika**, kwa jedwali hilo, uchambuzi ni kama ifuatavyo:-

**a. Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi**

Wizara hii imetekeleza kikamilifu maazimio mawili (2) sawa na asilimia 14 na imeanza kutekeleza bila kukamilisha maazimio 9 sawa na asilimia 64 Kwa takwimu hizo, Wizara hii haijaanza kabisa kutekeleza maazimio 3 Sawa na asilimia 21. Mfano wa maazimio yaliyotekelezwa ni Pamoja na kufanya tathmini ya mifumo ya urekebu kwa lengo la kuona namna ya kuiboresha.

**b. Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki**

Wizara hii imetekelezakikamilifu maazimio 6 sawa na asilimia 50 na imeanza kutekeleza bila kukamilisha maazimio 5 sawa na asilimia 42, Kwa takwimu hizo, Wizara hii haijaanza kabisa kutekeleza azimio 1 sawa na asilimia 8. Mfano wa maazimio yaliyotekelezwa ni pamoja na kuandaa mpango wa ujenzi, ukarabati na

uendelezaji wa Chuo cha uhusiano wa Kimataifa cha Dkt. Salim Ahmed Salim na kuanisha utaratibu mahsusi wa kimkakati kufanya tathmini ya mikataba iliyosainiwa na nchi na kuridhiwa na Bunge ili kubaini tija, ufanisi, manufaa au changamoto kwa dhumuni la kujiimarisha kwa maslahi ya nchi.

**c. Wizara ya Ulinzi na JKT**

Wizara hii imetekeleza kikamilifu Azimio 1 sawa na asilimia 33.3 na imeanza kutekeleza bila kukamilisha Azimio 1 sawa na asilimia 33.3 Kwa takwimu hizo, Wizara hii haijaanza kabisa kutekeleza Azimio 1 Sawa na asilimia 33.3 Mfano wa maazimio yaliyotekezwa ni Wizara kushirikiana na TAMISEMI, Wizara ya Elimu pamoja na wadau wengine kufanya tathmini ya jumla kuhusu mafunzo ya JKT ikilinganishwa na dhamira ya nchi kuwa na utaratibu wa mafunzo hayo.

**Mheshimiwa Spika**, kwa ujumla hali ya utekelezaji wa maazimio ya Bunge kwa wizara zote tatu inabainishwa katika Jedwali Na. 01.

**Majumuisho Sehemu ya Pili**

**Mheshimiwa Spika**, Sehemu hii ya ripoti ninayoimalizia ni muhimu na inajenga msingi wa maoni ya Kamati ambayo ni egemeo la mapendekezo nitakayoyatoa kwa ujumla sehemu hiyo imeeleza ilivyo hali ya ulinzi na usalama, miundombinu ya magereza nchini na hali ya huduma ya usafiri wa Boda boda kwa usalama wa Raia. halkadhalika, suala la Huduma za wakimbizi, shughuli za Jeshi la kujenga Taifa, mtangamano wa kikanda, ushirikiano wa kimataifa na uwakilishi wa Bunge kwenye vyombo vingine vya uwakilishi, vimefafanuliwa pia katika taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika**, mambo hayo yameeleza hali ilivyo, kuonesha mafanikio na changamoto na kuhusisha na matarajio ya watu na miongozo mingine ya nchi. Kufanya hivyo kumeiweka Kamati katika nafasi ya kuwa na mtazamo na maoni ya jumla yenye msingi na kutoa mwelekeo wa mapendekezo kama inavyojitokeza katika sehemu ya tatu ya taarifa hii.

## SEHEMU YA TATU

## MAONI NA MAPENDEKEZO

### Maoni

**Mheshimiwa Spika,** matokeo ya shughuli za Kamati kwa mwaka 2024 yameipa Kamati mtazamo wa jumla kuhusu dhima na majukumu ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Wizara ya Mambo ya Ndani na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Maoni hayo ambayo ndiyo msingi wa hoja ya Kamati ni kama ifuatavyo:-

### Wizara ya Mambo ya Nje, na Ushirikiano wa Afrika Mashariki

**Mheshimiwa Spika**, Kwa kuzingatia matokeo ya ufuatiliaji wa utekelezaji wa Majukumu ya Wizara hii, Kamati ina maoni kwa maeneo mbalimbali. Kwanza ni maoni ya Kamati kuwa, kuimarisha Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa kushawishi utekelezaji wa masharti ya Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya hiyo pamoja na Itifaki zake ni jambo muhimu kwa Tanzania. Ushawishi huo uguse pia msukumo wa kuboresha uwiano wa tozo, ushuru, na ada kwa bidhaa zinazokumbwa na vikwazo, na kuhimiza juhudi za kidiplomasia ili kutatua migogoro ya kikanda.

### Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi

**Mheshimiwa Spika**, kwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya nchi, ni mtazamo wa Kamati kuwa, Wizara hii itaendelea kufanikiwa kulinda maisha na mali, kuwezesha na kudhibiti utokaji na uingiaji nchini kwa raia na wageni, kuwarekebisha wafungwa na kutoa huduma kwa wakimbizi waliopo nchini. Hata hivyo, mafanikio hayo yanahitaji ufanisi wa vyombo vya ulinzi na usalama nchini kutokana na kuwa na bajeti ya kutosha, vifaa vya kisasa, na matumizi ya sayansi na teknolojia.

**Mheshimiwa Spika,** Juhudi za kuendeleza miundombinu ya usalama, ikiwemo ujenzi wa vituo vya zimamoto, kuboresha

miundombinu ya magereza na kuanzisha mikakati ya kudhibiti ajali barabarani kupitia matumizi ya teknolojia ya kisasa ni mambo muhimu katika usalama wa raia na mali zao. Aidha, ushirikiano kati ya Serikali, sekta binafsi, na wadau wengine unahitajika ili kuimarisha usalama na kuzuia uhalifu, hasa kupitia uwekezaji katika TEHAMA unaodhibiti usafirishaji haramu wa binadamu na ufuatiliaji wa wakimbizi wanaohifadhiwa nchini.

**Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa**

**Mheshimiwa Spika,** Kutokana na uchambuzi**,** Kamati ina maoni kuwa, kuendelea kuimarisha mifumo ya ulinzi, kutoa elimu kwa jamii za mipakani kuhusu umuhimu wa alama za mipaka, kufanya mageuzi madhubuti ya mifumo ya usimamizi wa madeni ambayo SUMA JKT inazidai taasisi mbalimbali ni mambo yanayohitaji msukumo na mwendelezo. Kufanya hivyo, kutachangia usalama wa mipaka, ufanisi wa kifedha na uendeshaji bora wa SUMA JKT.

**Maoni Yatokanayo na Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge**

**Mheshimiwa Spika,** Shughuli ya Kamati inayohusu kufuatilia utekelezaji wa Maazimio ya Bunge imechangia maoni ya Kamati katika maeneo makuu mawili. Maoni hayo ni kama ifuatavyo:-

(i) Kutokutekelezwa kwa baadhi ya maazimio ya Bunge yaliyotokana na Taarifa ya Shughuli za Kamati kwa mwaka 2023, ni jambo linalohitaji kufanyiwa kazi ili kuboresha ufanisi wa sekta inayohusika katika kuwezesha ustawi wa watu kwa mujibu wa Ibara ya 8 (1)(b) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; na

(ii) Kuendelea kwa changamoto zinazobainishwa na Bunge kupitia taarifa ya Kamati hii licha ya maazimio ya kuzitatua ni jambo linaloweza kuathiri mtazamo wa jumla wa umma kwa Bunge iwapo hakuna ufafanuzi.

**Mapendekezo**

**Mheshimiwa Spika,** Maelezo yote niliyoyatoa katika taarifa hii yamejenga msingi wa hoja ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama. Kutokana na maelezo hayo niliyoyamalizia kwa maoni, sasa naomba kutoa hoja kwamba Bunge liyapokee mapendekezo ninayoyatoa yawe maazimio ya Bunge kama ifuatavyo:-

**Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki**
**a) Vikwazo vya Kibiashara Visivyo vya Kikodi**

**KWA KUWA,** baadhi ya nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zinaweka vikwazo vya kibiashara visivyo vya kikodi, lakini ushawishi wa kutosha haufanyiki kuzitaka zizingatie masharti ya Itifaki zinazohusika,

**NA KWA KUWA,** Tanzania isipozishawishi nchi wanachama katika suala la kuondoa vikwazo vya kibiashara visivyo vya kikodi kwa mujibu wa Itifaki za Jumuiya, itakuwa imeacha kutekeleza wajibu wa msingi katika kuimarisha ushirikiano na uhusiano ndani ya kanda,

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba, Serikali ya Tanzania ifanye mambo yafuatayo:-

(i) Kuendelea kuzishawishi nchi wanachama ili zizingatie inavyostahili masharti ya Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuia ya Afrika Mashariki pamoja na Itifaki zake; na

(ii) Kuzishawishi nchi wanachama kukamilisha zoezi la kuwianisha tozo, ushuru na ada kwa bidhaa ambazo zinawekewa vikwazo zaidi visivyo vya kikodi.

**b) Ufinyu wa Bajeti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki**

**KWA KUWA,** Jumuiya ya Afrika Mashariki inakabiliwa na changamoto ya ufinyu wa bajeti kwa ajili ya utekelezaji wa

shughuli muhimu za kimkakati na uendeshaji wa Jumuiya na taasisi zake,

**NA KWA KUWA,** upungufu huo wa bajeti unaotokana na baadhi ya nchi wanachama kutokulipa michango kwa wakati kinyume na masharti ya Mkataba, unakwamisha malengo ya Jumuiya ya Afrika Mashariki,

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba, Serikali ya Tanzania iendelee kushawishi nchi wanachama zitekeleze ipasavyo masharti ya Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya, ikiwemo kutoa michango ya Jumuiya kwa wakati.

**c) Migogoro ya Ndani kwa Baadhi ya Nchi Wanachama wa Jumuiya**

**KWA KUWA,** Jumuiya ya Afrika Mashariki inakabiliwa na changamoto ya migogoro ya ndani kwa baadhi ya nchi wanachama, ilhali migogoro hiyo inaweza kupungua au kumalizika iwapo zitatumika juhudi za ushawishi,

**NA KWA KUWA,** kuendelea kwa migogoro hiyo ni jambo linaloigharimu Jumuiya kiasi kikubwa cha fedha kwa ajili ya utatuzi wake na kuathiri uwezo wa Jumuiya kufadhili shughuli za maendeleo,

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba, Serikali ya Tanzania itumie ushawishi wake kushirikiana na nchi nyingine wanachama na wadau mbalimbali ili kutumia juhudi za kidiplomasia kwa kuzingatia mazingira yaliyopo kutafuta suluhu ya kudumu ya migogoro hiyo.

**d) Sekta Binafsi Kushindwa Kutumia Ipasavyo Fursa za Kiuchumi katika Jumuiya za Kikanda**

**KWA KUWA,** sekta binafsi hainufaiki ipasavyo na fursa za kiuchumi katika mtangamano wa Afrika Mshariki kutokana na kutozitambua au kukosa hamasa ya kuzitumia,

**NA KWA KUWA,** hali hii inayotokana na nchi kukosa mpango mkakati unaoainisha fursa mbalimbali zilizopo na namna Sekta Binafsi inavyoweza kunufaika na fursa hizo, inapunguza manufaa yaliyotarajiwa kiuchumi na kijamii,

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba, Serikali iandae mpango mkakati unaotekelezeka ambao utabainisha fursa za kiuchumi katika mtangamano wa kikanda na namna Sekta binafsi zitakavyoweza kuzitumia fursa hizo.

**Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi**

**a) Kuendeleza Uwezo wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama wa Raia na Mali Zao**

**KWA KUWA,** kuviwezesha vyombo vya ulinzi na usalama kwa teknolojia, bajeti, vifaa na vitendea kazi ni jambo endelevu ambalo linastahili kupewa kipaumbele kama inavyofanyika nchini,

**NA KWA KUWA,** hatua yoyote ya kutoongeza uwezeshaji huo inaweza kuathiri ufanisi wa juhudi za kuimarisha usalama wa raia na mali zao nchini,

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba, Serikali iendelee kuviwezesha vyombo vya ulinzi na usalama wa raia na mali zao kwa kufanya yafuatayo:-

(i) Kuvipa uwezo wa kuendana na maendeleo ya sayansi na teknolojia duniani katika utekelezaji wa majukumu yao;

(ii) Kuvipatia bajeti ya kutosha kuendelea kuimarisha ulinzi na usalama wa raia na mali zao; na

(iii) Kuendelea kuvipatia vifaa na vitendea kazi vya kutosha na vya kisasa zaidi.

**b) Uchache wa Vituo vya Zimamoto na Uokoaji**

**KWA KUWA,** hali ya jumla ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji inaonesha kuwa jumla ya wilaya 97 hazina vituo vya Jeshi hilo nchini,

**NA KWA KUWA,** kukosekana kwa vituo vya Jeshi hilo katika baadhi ya Wilaya, kunathiri uwezo wa kulinda maisha na usalama wa raia na mali zao dhidi ya matukio ya moto na majanga mengine,

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba Serikali iandae Mpango wa Ujenzi wa Vituo vya Zimamoto na Uokoaji katika Wilaya zote ambazo hazina vituo hivyo nchini.

**c) Miundombinu Chakavu ya Magereza**

**KWA KUWA,** uchakavu wa miundombinu ya magereza nchini unaongezeka kutokana na ukosefu wa mpango mahususi wa kuboresha miundombinu hiyo,

**NA KWA KUWA,** hali hiyo ya miundombinu kuendelea kuchakaa inaathiri dhima ya huduma za magereza kutokana na:-

(i) Baadhi ya Magereza kuwa na wafungwa na mahabusu kuliko uwezo wake jambo linalohatarisha afya na usalama wa wafungwa;

(ii) ukosefu wa huduma bora za maji safi, vyoo, na usafi wa mazingira unaosababisha magonjwa ya mlipuko;

(iii) kupungua kwa ufanisi wa ulinzi na kusababisha hatari ya wafungwa kutoroka au kushambulia maafisa wa magereza;

(iv) ukosefu wa mazingira bora ya kuwezesha huduma za urekebu ambalo ni jukumu la msingi la Jeshi la Magereza;

(v) changamoto za lishe na huduma za kijamii zinazotokana na miundombinu duni ya maghala ya chakula, jiko na huduma za msingi;

(vi) ukosefu wa ofisi bora, makazi na vifaa vya kazi unaoweza kushusha morali ya maafisa na Askari wa Magereza;

(vii) Mzigo kwa Serikali wa gharama kubwa za uendeshaji kutokana na kuharibika kwa miundombinu mara kwa mara na matibabu ya magonjwa yanayoweza kuzuilika,

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba, Serikali iandae mpango mahsusi unaotekelezeka wa kuboresha miundombinu ya Magereza nchini.

**d) Matumizi ya TEHAMA Magerezani**

**KWA KUWA**, zaidi ya asilimia 85 ya magereza nchini hayanufaiki na matumizi ya TEHAMA kutokana na kukosa miundombinu stahiki kama vile:-
(i) Kamera za CCTV;
(ii) mashine za ukaguzi;
(iii) miundombinu ya mawasiliano; na
(iv) miundombinu ya mifumo ya kidijitali,

**NA KWA KUWA,** kukosekana kwa matumizi ya TEHAMA katika magereza hayo ni changamoto inayoweza kuathiri:
(i) haki za wafungwa;
(ii) usalama wa magereza;
(iii) huduma za urekebu; na
(iv) ufanisi wa utendaji wa maafisa wa magereza,

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba Serikali kwa kuwashirikisha wadau wa maendeleo iongeze uwekezaji katika TEHEMA na mifumo ya kidijitali ili kuliwezesha Jeshi la Magereza kuwa na mifumo na nyenzo za kiteknoljia zinazowezesha huduma za kisasa.

**e) Utambuzi wa Waendesha Bodaboda nchini**
**KWA KUWA,** kukosekana kwa mfumo wa utambuzi wa waendesha bodaboda kidijitali nchini ni changamoto inayosababisha kutokuwepo kwa takwimu rasmi za waendesha bodaboda,

**KWA KUWA,** kukosekana kwa mifumo ya kidijitali kunachochea kutokuwa na utambuzi wa waendesha bodaboda kwa kudhoofisha usajili, udhibiti, na ufuatiliaji wao**.**

**NA KWA KUWA,** hali hiyo ya usajili, udhibiti na ufatiliaji wa waendesha bodaboda inasababisha athari kubwa kwa jamii na maendeleo ya nchi kama vile:-

(i) Kuongezeka kwa ajali za barabarani ambazo huleta vifo, ulemavu na mzigo mkubwa kwa sekta ya afya kutokana na matibabu ya waathirika katika ajali,

(ii) Kushamiri kwa uhalifu wa kutumia bodaboda kutokana na kuwepo kwa waendesha bodaboda wasiosajiliwa ambao hutumiwa na wahalifu kufanya ujambazi, wizi wa simu, na uporaji;

(iii) Kuongezeka kwa migongano kati ya Serikali na waendesha bodaboda kutokana na taratibu za usajili na utoaji wa leseni kukosa uwazi,

(iv) Kudhoofisha utekelezaji wa Sheria za Usalama Barabarani na kuhatarisha maisha ya waendesha bodaboda, abiria na watumiaji wengine wa Barabara

**NA KWA KUWA** kukosekana kwa utambuzi rasmi kunasababisha sekta hiyo kukosa udhibiti na hivyo Waendesha bodaboda kutumia mwanya huo kutofuata sheria mbalimbali za nchi ikiwemo Sheria ya usalama barabarani na pia baadhi yao ambao sio waadilifu kushiriki kwenye matukio ya uhalifu pasipo kutambulika kwa urahisi.

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba, Serikali ilisimamie Jeshi la Polisi ili liweze kushirikiana na LATRA, Halmashauri za Miji na Wilaya na Taasisi nyingine za Serikali pamoja na wadau mbalimbali, kuandaa mfumo rasmi wa kisasa wa kidijitali kwa ajili ya utambuzi wa waendesha bodaboda nchini.

**f) Hali ya Barabara Kuu nchini**

**KWA KUWA,** barabara nyingi zinazounganisha mikoa pamoja na zinazounganisha Tanzania na nchi jirani (Barabara kuu) ni nyembamba kwa kuwa na njia moja kwenda na nyingine ya kurudi pasipo kuwa na utengano,

**NA KWA KUWA,** hali hiyo ya barabara kuu nyingi kutokufikia viwango vya nyota tatu inaweza kuathiri ustawi wa Taifa, usalama wa wananchi, maendeleo ya uchumi na ufanisi wa sekta mbalimbali,

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba:

(i) Serikali itumie utaratibu wa kujenga barabara za viwango vya nyota tatu kuanzia sasa; na

(ii) Kwa barabara kuu ambazo zilijengwa kipindi kilichopita, Serikali iziboreshe inavyostahili ili kufikia azma ya kuwa na barabara kuu zenye nyota tatu.

**g) Teknolojia katika Udhibiti wa Ajali za Barabarani**

**KWA KUWA,** kutokutumika kwa teknolojia ya kisasa katika udhibiti wa ajali za barabarani kunasababisha na ugumu wa kuwabaini madereva na watumiaji wengine wa barabara wanaokaidi sheria za usalama barabarani

**NA KWA KUWA,** matokeo ya kutokutumika kwa teknolojia ya kisasa ili kudhibiti vichocheo vya ajali yanasababisha vifo, ulemavu na mzigo kwa Serikali kugharamia matibabu ya waathrika wa ajali,

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba**,**

(i) Jeshi la polisi lifanye tathmini ya mpango wake wa kudhibiti na kuzuia ajali barabarani kwa lengo la kubaini kama

mpango huo unafanikisha tija iliyokusudiwa katika kudhibiti na kuzuia ajali za barabarani

(ii) Serikali iweke mpango mkakati unaotekelezeka wa ununuzi wa vifaa vya kisasa kwa kuzingatia teknolojia mahsusi kwa uhalisia wa barabara zetu na kuvifunga katika barabara kwa kuanzia na barabara kuu ikiwa ni sehemu ya mkakati wa kupambana kudhibiti ajali za barabarani; na

(iii) Serikali iandae mpango wa kuwapatia mafunzo Askari wa usalama wa barabarani ili kuwa na uelewa na ujuzi wa kutumia na kufuatilia vifaa vya kitekonolojia vitakavyofungwa kwa ajili ya usalama barabarani.

**h) Biashara haramu ya usafirishaji wa Binadamu**

**KWA KUWA,** biashara haramu ya binadamu inaendelea kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo:

(i) Umasikini na ukosefu wa ajira kwa watu wanaoingizwa katika mitandao ya biashara hiyo;

(ii) Watu wengi, hasa wa vijijini, kukosa uelewa kuhusu mbinu zinazotumiwa na wasafirishaji haramu;

(iii) Ufinyu wa bajeti ya Sekretarieti ya Kupambana na Biashara Haramu ya Usafirishaji wa Binadamu nchini; na

(iv) Wafanyabiashara wa usafirishaji haramu wa binadamu kutumia teknolojia ya kisasa kuliko inayofanyika katika vyombo vya udhibiti wa biashara hiyo,

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba, Serikali ifanye mambo yafuatayo:-

(i) Kuendeleza ushirikiano kati yake na sekta binafsi na wadau wengine ili kujenga mazingira wezeshi ya kiuchumi kwa vijana na makundi maalumu;

(ii) kushirikiana na mashirika ya kidini, asasi za kiraia na wadau wengine ili kuelimisha umma kuhusu mikakati inayotumiwa na wahalifu pamoja na madhara ya biashara hiyo kwa jamii na taifa;

(iii) Serikali itenge fedha za kutosha kwa Sekretarieti ya Kuzuia na Kupambana na Biashara Haramu ya Binadamu ili iweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo sambamba na kununua vifaa na vitendea kazi vya kisasa; na

(iv) Kuwezesha matumizi ya vifaa na kiteknolojia ya kisasa katika shughuli za udhibiti na uzuiaji wa usafirishaji haramu wa binadamu.

**i) Wakimbizi walio nje ya kambi**

**KWA KUWA,** kuwepo kwa wakimbizi wanaoishi nje ya kambi kinyume na sheria na taratibu za ukimbizi ni jambo linalohitaji juhudi na mbinu za kimuundo na kibajeti,

**NA KWA KUWA,** kutokutumika kwa mbinu za kimuundo na kibajeti kwa ajili ya kushughulikia suala la wakimbizi waliotoka nje ya kambi kunaweza kuathiri kwa kiasi kikubwa usalama, utawala bora, na maendeleo ya jamii zinazowahifadhi wakimbizi hao,

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba, Serikali ifanye yafuatayo: -

(i) Idara ya Wakimbizi Iwe Idara inayojitegemea na kujiendesha kwa namna inayoiwezesha kusimamia masuala ya wakimbizi kwa ufanisi;

(ii) Iwezeshe upatikanaji wa Fungu maalumu la kibajeti (Vote) kwa Idara ya Wakimbizi tofauti na sasa ambapo Idara hiyo inapata fedha zake kupitia Fungu 51(Wizara); na

(iii) Serikali itenge bajeti ya kutosha kwa idara ya wakimbizi ili iweze kutekeleza majukumu yake kama ilivyokusudiwa.

**Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa**

**(a) Kuendeleza Juhudi za Ulinzi wa Mipaka**

**KWA KUWA**, ulinzi wa mipaka ya nchi yetu umeendelea kuimarika kutokana na mambo mbalimbali ikiwemo:-

(i) Ushirikiano na uhusiano mzuri wa kidiplomasia baina ya Tanzania na nchi za jirani; na

(ii) Hatua ya Serikali kuendelea kuwezesha bajeti ya ulinzi,

**NA KWA KUWA,** kutoendeleza juhudi hizo za Serikali kutasababisha changamoto za kidiplomasia na ulinzi,

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba, Serikali iendeleze juhudi zake za kuimarisha ulinzi wa mipaka kwa kuwezesha ulinzi na elimu kwa jamii zinazoishi mipakani.

**(b) Madeni ya SUMAJKT inazodai Taasisi za Umma na Binafsi**

**KWA KUWA,** SUMAJKT ambayo ilianzishwa kwa madhumuni maalumu yanayoendana na lengo la kuwa na Jeshi la Kujenga Taifa nchini inazidai Taasisi za Umma na Binafsi zaidi ya Shilingi bilioni 40,

**NA KWA KUWA,** deni hilo lisipolipwa inavyopaswa litaathiri ukuaji na ufanisi wa SUMAJKT katika miradi ya kimkakati, jambo ambalo linakwamisha azma ya kuanzishwa kwake na taifa kwa ujumla,

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba, Serikali –

(i) Ihakikishe kuwa, Taasisi zote za umma na Binafsi zinazodaiwa na SUMAJKT zinalipa madeni yao haraka na kwa ukamilifu;

(ii) Ilisimamie Shirika kufanya tathmini ya sera yake ya madeni kwa kuzingatia azma ya kukusanya madeni na kuzuia au kupunguza uwezekano wa ongezeko la madeni; na

(iii) Iliwezeshe Shirika kuweka mfumo madhubuti na endelevu ambao hautaruhusu utoaji wa huduma unaochangia ongezeko la madeni.

**Majumuisho na Hitimisho**

**Majumuisho sehemu ya tatu**

**Mheshimiwa Spika**, Sehemu ya tatu imejengeka kutoka sehemu ya kwanza na ya pili kwa kubainisha mazingatio ya msingi na mtazamo unaotokana na uchambuzi kwa kutegemea Ushahidi uliodhihirika kwenye shughuli za Kamati. Kwa msingi huo, sehemu hii imebainisha hatua stahiki kwa lengo la kuimarisha ustawi wa watu, mustakabali wa Taifa na maendeleo halisi kwa ujumla.

**Hitimisho**

**Mheshimiwa Spika**, napenda kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha Taarifa ya Mwaka ya Kamati kuhusu utekelezaji wa shughuli zake kwa kipindi cha Januari, 2024 hadi Februari, 2025. Ni imani ya Kamati kuwa fursa hii inayotokana na masharti ya Kanuni ya 136 (15), ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 itasaidia kuliwezesha Bunge lako Tukufu kutekeleza wajibu wake wa kuisimamia Serikali ipasavyo.

**Mheshimiwa Spika**, napenda pia kuchukua nafasi hii kuwashukuru Waziri wa Mambo ya Ndani Mhe. Innocent Bashungwa (Mb), pamoja na Naibu Waziri wake Mhe. Daniel Baran Sillo (Mb) kwa ushirikiano walioutoa kwa Kamati katika kipindi ambacho Kamati imefanya kazi nao.

Vilevile, namshukuru Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa Mhe. Dkt. Stagomena Lawrence Tax, (Mb) na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki Mhe. Mahmoud Thabit Kombo (Mb), na Naibu Waziri wake Mhe. Cosato David Chumi (Mb) na Mhe. Denis Lazaro Londo Mb) pamoja na watendaji wote wa Wizara hizo kwa ushirikiano waliouonesha katika kipindi chote ambacho Kamati imekuwa ikitekeleza majukumu yake.

**Mheshimiwa Spika,** mwisho, lakini si kwa umuhimu, nawashukuru Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge chini ya Uongozi wa Ndg. Baraka Idelfornce Leornad, Katibu wa Bunge kwa kuisaidia Kamati kutekeleza majukumu yake.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kueleza shughuli zilizotekelezwa, Uchambuzi wa matokeo ya utekelezaji wa shughuli za Kamati, Maoni na Mapendekezo sasa naomba kutoa hoja kwamba Bunge sasa liipokee, kujadili na hatimaye kuikubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama pamoja na Maoni na Mapendekezo yote ya Kamati kama yalivyo katika Taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja.

..............................
Vita R. Kawawa, Mb
**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA**
06 Februari, 2025

**MHE. VINCENT P. MBOGO:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono, ahsanteni sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kuwasilisha hoja hiyo ya Kamati. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kama ilivyo ada, tuna hoja mbili mbele yetu na nina majina hapa ya Waheshimiwa Wabunge ambao wameomba kuchangia. Kwa hiyo, tutaanza na huo uchangiaji. Tutaanza na Mheshimiwa Janejelly James Ntante, atafuatiwa na Mheshimiwa Zahor Mohammed Haji. Mheshimiwa Kunti Yusuph Majala ajiandae.

**MHE. JANEJELLY J. NTATE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa fursa ya kuwa mchangiaji wa kwanza.

Mheshimiwa Spika, ninaanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye amenipa uhai na uwezo wa kusimama hapa leo. Nampongeza Mheshimiwa Rais kwa juhudi anazofanya kwenye sekta hizi tatu za viwanda, kilimo, mifugo na uvuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia ninawapongeza Mawaziri wanaosimamia Wizara hizo; Mheshimiwa Dkt. Jafo na Msaidizi wake Mheshimiwa Kigahe; Mheshimiwa Hussein Bashe na Msaidizi wake Mheshimiwa Silinde; Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji na Msaidizi wake Mheshimiwa Mnyeti, wamefanya kazi ya kubeba maono ya Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaanza kwa kuichangia hoja ya Liganga na Mchuchuma. Huu ni mfupa uliomshinda fisi, lakini tunapokwenda Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan chini ya Serikali yake ya Chama cha Mapinduzi anaenda kuutafuna na kuumaliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye Kamati, Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na wataalam wake walikuja na taarifa ambayo tangu tuwe kwenye hiyo Kamati hatujawahi kupata taarifa ya aina hiyo. Hiyo ilitokana na nini? Katibu Mkuu wa Wizara ya Viwanda Dkt. Hashil hakuwa mchoyo alipopewa Naibu Katibu Mkuu ambaye ni Dkt. Suleiman kumpa mawazo na nafasi ya kusimamia zile taasisi muhimu ndani ya Wizara ya Viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika wetu, Dkt. Tulia Ackson, yule kijana ni mahiri wa sheria, nimemlinganisha na wewe. Pia ni mahiri wa uchumi, na alichoongeza pale ni mahiri wa lugha ya watu ambao tunaenda ku-*negotiate* nao kuhusu mikataba ya Liganga na Mchuchuma. Kwa hiyo, sasa hawana kona ya kupindapinda. Wakipinda kwa lugha yao, anao. Kwa hiyo, Liganga na Mchuchuma inaenda kufika mwisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, tulitoa maelekezo kwa Mheshimiwa Waziri Jafo kwamba, hii taarifa tuliyoipata Kamati, akuombe kibali na ninajua wewe unavyopenda Waheshimiwa Wabunge wako waende kwa pamoja, hutakataa. Hii taarifa ije kwa Waheshimiwa Wabunge wote, ili wote twende na uelewa mmoja kwenye Liganga na Mchuchuma. Tungekuwa na uelewa mmoja, juzi Mheshimiwa Mbunge wa eneo husika asingeweza kuuliza swali la msingi kwamba sasa tunaenda wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nina imani kabla ya Bunge hili kuahirishwa, ruhusa itatoka na Mheshimiwa Jafo atajipanga na wataalam wake hao waje wawape Waheshimiwa Wabunge ile taarifa ya Liganga na Mchuchuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia niiongelee *SIDO*. Nchi yoyote iliyoendelea ni lazima iwe na taasisi kama *SIDO*. Hata hivyo, *SIDO* ya kwetu Tanzania ndiyo tunaitegemea iandae viwanda vidogo vidogo kusaidia akina mama na vijana. Hata hivyo, inahemea kwenye *oxygen*. Kwa sababu gani? *SIDO* inatakiwa iwe na wafanyakazi 456 lakini sasa hivi ina wafanyakazi 277, pungufu ya wafanyakazi 179.

Mheshimiwa Spika, hili linaenda na taasisi zote zilizo chini ya Wizara ya Viwanda; *TIRDO*, *TEMDO*, *KMTC*, *CAMARTEC* na *NDC* yenyewe inayowasimamia. Vile vile Suala la watumishi inabidi Serikali iliangalie kwa mapana zaidi. Pia, *SIDO* wanakabiliwa na madeni ya pango la ardhi kwenye sehemu ambazo ofisi zao zipo.

Mheshimiwa Spika, sasa nilichoshangaa, hawa hawafanyi biashara. Hizi ni taasisi za Serikali, lakini zina madeni lukuki kwamba ni pango la ardhi. Wanapata wapi mapato ya kulipa pango la ardhi? Naiomba Serikali ifute yale madeni yaliyopo na iende ikachakate sheria za kodi, taasisi za Serikali ambazo hazifanyi biashara zisiwe zinalipa pango la ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia kuna uchakavu wa miundombinu kwenye hizi taasisi zetu, na lenyewe liangaliwe kwa sababu

tunategemea hawa ndio watengeneze mitambo, vifaa lakini hawana vifaa vya kuwasaidia.

Mheshimiwa Spika, changamoto nyingine iliyopo ni kwamba, bado Serikali hatujaamini zana zinazozalishwa na hizi taasisi zetu. mfano mzuri ni *TEMDO*, wanazalisha mpaka majokofu ya kutunza maiti, lakini Wizara ya Afya bado haijachukua jukumu sahihi kununua hayo majokofu ili tu-*save* fedha za kigeni. Ni Wizara ya Ulinzi tu ndiyo imeanza kununua yale majokofu. Kwa hiyo, tunaiomba Serikali kupitia viwanda na Wizara ya Afya wachukue mkakati thabiti wa kuweza kununua hivyo vifaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hawa *TEMDO* wameweza kutengeneza viwanda vidogo vidogo vya sukari. Tunawapongeza Wizara ya Kilimo kwa sababu wao waliweza kuwekeza fedha za kusaidia *TEMDO* kuunda mitambo hiyo ya viwanda vidogo vidogo vya kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naenda kwenye kilimo. Nawapongeza sana Wizara ya Kilimo, leo hii tumeona kwenye magazeti Tanzania tumekuwa wazalishaji wa pili Afrika kwa zao la mahindi. Hili siyo jambo dogo. Kwa hiyo, waliokuwa wanabeza nguvu anazoweka Mheshimiwa Dkt. Samia kwenye kilimo, wameanza kuona matokeo chanya. Naamini itachukua muda kidogo, baada ya umwagiliaji kukaa sawa, tutakuwa namba moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, twende kwenye uvuvi na mifugo. Nawapongeza sana Wizara ya Uvuvi na Mifugo, mmeweza kufanya, mnataka kuja na chanjo. Nampongeza Mheshimiwa Waziri, tulipomwambia kwenye Kamati kwamba Halmashauri sasa zinataka kuitumia chanjo ya mifugo kuifanya chanzo cha mapato, mara moja ametoa tangazo na tumeliona, kuwaambia kuna bei elekezi iliyoelekezwa na Wizara ya Mifugo. Kwa hiyo, halmashauri wasiweke bei elekezi za kwao wanazojua. Hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia kuna maabara ya uvuvi wa Kitaifa. Hii ndiyo maabara kubwa katika Ukanda wa Afrika Mashariki na

Kusini lakini maabara hii bado inasuasua. Haijapewa bajeti ya kutosha na vifaa vya kisasa, kwa hiyo, tunakosa soko la Samaki. Hao wanaotaka kuja kupima samaki wao, hatuna vifaa vya kutosha kuweza kupima Samaki. Kwa hiyo, tunapoteza mapato kupitia hapa. Sasa Serikali iweke juhudi ya kuwapa vifaa vya kisasa, teknolojia ya kisasa na watumishi wa kutosha ili tuweze kuitumia hii maabara kwa malengo ambayo tumejiwekea wenyewe.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, niseme tu kwamba kilimo, viwanda na uvuvi, washirikiane, wao ndio sekta mahiri za kuendeleza uchumi wa Tanzania, waweke maono ya Mheshimiwa Rais, waweze kuungana na hizi sekta zao zifanye kwa pamoja ili tuweze kusonga mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaendelea na uchangiaji tuna wageni ambao wameingia baada ya tangazo la awali la wageni.

Waheshimiwa Wabunge, nawaleta kwenu sasa wageni walioingia baada ya matangazo. Kwanza, tutaanza na wageni wangu. Yupo Chifu Allan Ndenjela Mwaigaga, ameambata na mwanaye anaitwa Asha, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wengine 14 waliokaa Jukwaa la Spika, ambao ni wa Mheshimiwa Naibu Spika. Hawa ni viongozi wa Chama cha Mapinduzi kutoka Wilaya ya Ilala. Kwanza, kuna Madiwani wa Jiji la Dar es Salaam wakiongozwa na Mheshimiwa Eva Nyamoyo, karibuni sana. Pia, wapo viongozi wa Kata ya Jangwani, Kariakoo. Karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Tunao wageni mbalimbali wa Waheshimiwa Wabunge ambao nao hawakupata nafasi ya kutangazwa asubuhi. Kwanza ni wageni 47 wa Mheshimiwa Jerry William Silaa ambaye ni Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. Hawa ni wanafunzi wa

Utawala wa Umma wa Chuo Kikuu cha Kimataifa cha Kampala kutoka Jijini Dar es salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wageni wawili wa Mheshimiwa Hamza Khamis Khamis ambaye ni Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira. Hawa ni Ndugu Hillary Lesakwi na Ndugu Frank Chacha kutoka Arusha, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 12 wa Mheshimiwa Judith Salvio Kapinga ambaye ni Naibu Waziri wa Nishati. Hawa ni Madiwani wa Viti Maalumu wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga, wakiongozwa na Wenyeviti wa Umoja wa Wanawake Tanzania wa Wilaya ya Nyasa na Mbinga. Yupo pia Katibu wa Umoja wa Wanawake Tanzania wa Wilaya ya Mbinga Mkoa wa Ruvuma, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 13 wa Mheshimiwa Kasalali Emmanuel Mageni ambao ni Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake Tanzania na Madiwani wa Viti Maalum kutoka Kwimba Mkoa wa Mwanza. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wengine ni wageni tisa wa Mheshimiwa Maulid Saleh Ali ambao ni wanafunzi wa Chuo cha Mipango Jijiji Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wanne wa Mheshimiwa Ravia Idarus Faina ambaye ni Katibu wa CCM kutoka Mtende Mkoa wa Kusini, Zanzibar.

Wapo wageni 21 wa Mheshimiwa Ali Juma Mohamed ambao ni waalimu na wanafunzi wa shule ya Msingi Shaurimoyo waliopata ufaulu mkubwa na kupata nafasi za vipaji maalum, karibuni sana, lakini pia hongereni sana watoto kwa kufanya vizuri katika masomo yenu, na waalimu pia tunawashukuru kwa kazi nzuri ya kuwafundisha hao watoto.

Nilikuwa najaribu kuwatazama, nimeona kama umri wao ni mdogo sana, Mheshimiwa Kishimba angekuwepo angesema umri

wa kuanza shule, pengine siyo lazima uanzie pale unapoanzia sasa. Haya hongereni sana watoto wetu. *(Makofi)*

Tunaye Mgeni wa Mheshimiwa Abubakari Asenga ambaye ni Balozi wa Kiswahili kutoka Baraza la Kiswahili Tanzania (BAKITA), Joram Mkumbi. Karibu sana Bungeni.

Waheshimiwa Wabunge, huyu pia ni Balozi wa Baraza la Kiswahili Tanzania (BAKITA). Pamoja na hayo kwa kweli anafanya kazi nzuri ya kutuongezea msamiati sisi ambao huwa hatuna nafasi ya kuutafuta kila wakati.

Tunashukuru sana kwa kutuongezea msamiati wa Kiswahili na kukisema Kiswahili fasaha mpaka pale Watanzania wote tuelewe Kiswahili fasaha na namna ilivyo lugha adhimu kabisa. Ahsante sana kwa mchango wako, na karibu sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni saba wa Mheshimiwa Simon Songe Lusengekile ambao ni Madiwani wa Viti maalum na Viongozi wa Umoja wa Wanawake Tanzania Wilaya ya Busega, Mkoa wa Simiyu, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo. Wapo wanafunzi 80 na walimu saba kutoka Shule ya Msingi *Victory Christian* ya Jijini Dar es Salaam. Karibuni sana watoto wazuri, tunaamini nanyi mtafanya vizuri kwenye masomo yenu. *(Makofi)*

Tunao wageni wawili wa Taasisi ya *Tanzania Artist Unit for Community Development (TAFOCDE)* kutoka Wilaya ya Ubongo Jijini Dar es Salaam, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hao ndio wageni walioingia baada ya tangazo la awali. Sasa tunaendelea na uchangiaji. Mheshimiwa Zahor Mohammed Haji, atafuatiwa na Mheshimiwa Kunti Yusuph Majala, Mheshimiwa Joseph Michael Mkundi ajiandae.

**MHE. ZAHOR MOHAMMED HAJI:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchukuwa nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ili nami kuwa miongoni mwa wachangiaji.

Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nianze mchango wangu kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu, lakini pia nampongeza kama Amiri Jeshi wa Majeshi yetu ya Ulinzi na Usalama kwa kuendelea kuhakikisha kwamba nchi yetu pamoja na majirani zetu wanaendelea kuwa salama. Hilo ndilo jukumu la msingi la kikatiba la Rais wetu. Ninampongeza sana.

Mheshimiwa Spika, vile vile naomba nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kuwa kinara katika kuhakikisha pamoja na kwamba analilinda Taifa letu na majirani zetu, lakini pia na ukanda wetu wa *East Africa* pamoja na *SADC*. Kwa kweli amekuwa kiongozi kinara anayeonyesha kwamba amekusudia kuwa sehemu ya uongozi bora.

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo hiyo, utakumbuka kwamba tunayo changamoto. Bado nasema ni changamoto kwa upande wa majirani zetu wa *DRC* na wenzetu wa Rwanda. Ni changamoto za kimaisha, lakini Mheshimiwa Rais amesimama kinara na kuhakikisha kwamba jambo hili linapatiwa ufumbuzi na ametoa wazo. Vile vile amekubali kuhodhi mkutano huu ili kuweza kulitatua jambo hili kama Rais, kama Tanzania. Nampongeza sana Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, kwenye taarifa yetu tumezungumza mambo mengi sana. Moja katika hayo, naomba nivipongeze nyombo vyetu vya ulinzi na usalama, vyote kabisa, kwa sababu vyenyewe vinafanya kazi kwa kushirikiana na Mheshimiwa Rais ili kuhakikisha kwanza vinafuata Katiba yetu.

Mheshimiwa Spika, pili, vinafuata sheria ili kuhakikisha kwamba haki na wajibu wao unatendekea, lakini vile vile kuwafanya wananchi waendelee kutambua kwamba usalama wao ndiyo suala namba moja. Nawapongeza sana viongozi wetu hao.

Mheshimiwa Spika, taarifa yetu imesema mambo mengi sana, lakini moja ya mambo ambayo ningependa kuipongeza Serikali ni juu ya kuviwezesha vyombo vyetu hivi kutekeleza majukumu yake vizuri kabisa.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba tunayo changamoto ya upatikanaji wa fedha, lakini Serikali imeendelea kujitahidi. Sasa kwenye hili, ombi langu ni kwamba, yapo maeneo ambayo ni lazima tuyape kipaumbele. Kwa mfano, taarifa yetu inasema kwa upande wa Magereza, tunayo Magereza yetu ambayo yamejengwa zaidi ya miaka 100 iliyopita. Tumetembelea kwenye baadhi ya Magereza haya, tumeangalia wafungwa walivyo, tumeangalia na hali zao.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali kwamba, pamoja na kwamba inaendelea kujitahidi, bado hoja ya kuhakikisha kwamba tunaviwezesha vyombo hivi, tunatengeneza miundombinu bora kama tulivyoanza ili tuweze kuondokana na hili kwa sababu sheria pia zinatuhitaji, watu hawa waweze kupatiwa haki zao kama wafungwa, kwa sababu ufungwa ni adhabu, lakini huwezi ukapata adhabu ndani ya adhabu. Kwa hiyo, naomba Serikali iendeleze jitihada zake za kuhakikisha kwamba Magereza haya yanakwenda kwa mujibu wa sheria kwa kadri inavyohitajika.

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo hiyo, napenda kwenda kwenye upande wa Wizara yetu ya Mambo ya Nje. Naomba niwapongeze wenzetu wa Wizara hii, kwa sababu, kule nyuma tuliwahi kusema kwamba Wizara hii ndicho kioo chetu, inapimwa kwa mazuri na mabaya, ya ndani na nje. Sasa kwa hapa, na kwa haya yanayoendelea ndani ya nchi yetu, ndani ya Afrika Mashariki na ndani ya *SADC* maana yake kiungo kikubwa ni Wizara yetu ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, wenzetu hawa wanafanya kazi kubwa sana, kwa kuelewa kwamba sheria zetu na majukumu yao yanawataka kuendelea kuitunza au kutunza majirani zetu ili kuhakikisha kwamba tunaendelea kuishi salama; lakini kwa

maana hiyo hiyo ni sehemu inayoweza kutuwezesha kufanya biashara na wenzetu hawa. Kwa sababu pamoja na siasa, lakini hoja ya kuendeleza uchumi ni nzuri zaidi kwa sababu itatusaidia kuweza kuishi na majirani zetu vizuri.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza sana Wizara ya Mambo ya Nje kwa hoja ya Wizara hiyo ya kuhakikisha kwamba inamsaidia Rais ili kuweza kupambana na matukio ya ndani na ya nje ili kuhakikisha ukanda wetu wote wa Afrika Mashariki na *SADC* unabaki salama, na waendelee na hili.

Mheshimiwa Spika, mwisho kuliko yote, tumesikia kuhusu upungufu wa vitendea kazi, taarifa yetu imesema. Naomba tujitahidi kwa sababu sasa tumeboresha jeshi letu. Kwa mfano, katika Jeshi letu la Zimamoto kumekuwa na Idara ya Uokozi. Idara hii ukiitizama ni ndogo, lakini ukweli ni kwamba ina kazi kubwa, kwa sababu inatakiwa kuhakikisha inasimamia uokozi kwenye bahari, pamoja na kusimamia uokozi kwenye mito na maziwa. Bado chombo hiki ni kipya. Nadhani ni mwaka mmoja au miwili tumeweza kukifanya kuwa jeshi kamili. Maana yake ni kwamba ni lazima tuendelee kuviwezesha ili viweze kuwa matumaini kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii ni kwa sababu mvua zinaendelea kunyesha na wananchi wanaishi maisha yao kwa kutegemea maji. Tunahitaji kuviwezesha vyombo hivi ili viweze kuwasaidia, pamoja na kuwaokoa, kwa sababu ajali zinatokea, baharini na angani, lakini kwetu sisi naomba Serikali iongeze jitihada za kuhakikisha kwamba inawapatia watumishi wanaostahili, na vitendea kazi.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, tumezungumza kuhusu boti, helkopta, na ndege, ili iweze kufanya kazi zake vizuri na kuhakikisha kwamba wananchi wanaendelea kubaki salama na kuwa na imani na Serikali yao na Rais wao na Chama chao cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Kunti Yusuph Majala, atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Michael Mkundi, Mheshimiwa Balozi Liberata Mulamula ajiandae.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ili niweze kutoa mchango wangu kwenye Kamati zetu hizi mbili. Kwanza, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya na kuweza kukutana tena hapa kwa ajili ya lengo la kuendelea kulipigani Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze na Wizara ya Kilimo kwenye Kamati ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo. Natamba juhudi kubwa ambazo zinafanywa na Serikali kwenye suala lote la kuboresha sekta yetu ya kilimo kwenye taasisi zake mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, bado tuna changamoto kubwa sana kwenye sekta ya kilimo, kwa mfano kwenye umwagiliaji, tulijiwekea malengo ili tuweze kulisha Afrika, na tukasema ili tuweze kutimiza lengo hilo ni lazima tutoke kwenye kilimo cha kutegemea mvua ya Mungu na badala yake twende kwenye kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, mpaka sasa hali ni ngumu kwenye sekta ya umwagiliaji, fedha bado ni changamoto. Wizara imetangaza miradi mingi ambayo yote imebaki, haiendelei, hakuna mradi unaotekelezeka kwa sababu ya ukosefu wa fedha. Sasa kwenye suala la utoaji wa fedha, naiomba Serikali kwa maana ya Wizara ya Fedha wasaidie kutoa fedha kwenye sekta ya umwagiliaji ili tufikie hilo lengo.

Mheshimiwa Spika, leo tumetangazwa kwamba ni nchi ya pili kwenye suala zima la uzalishaji wa zao la mahindi. Laiti Serikali ikiiona sekta ya umwagiliaji na ikatoa fedha hizi tukajenga miradi yetu ya umwagiliaji, Tanzania tutaongoza, tutakuwa wa kwanza kwenye uzalishaji, siyo wa mahindi tu, itakuwa ni mazao yote ya chakula pamoja na mazao mengine ya biashara. Kwa hiyo, naomba sana Wizara ya Fedha iweze kutusaidia hizo fedha ili tuweze kwenda kutimiza hayo malengo yetu.

Mheshimiwa Spika, pia fedha hizi zinapotoka, naomba Wizara ya Kilimo, tusiende na miradi mingi kwa wakati mmoja. Tuchague miradi ya kipaumbele, iende itolewe fedha ambazo zitakamilisha miradi ile ili ianze kuzalisha na kuleta fedha kwa Watanzania badala ya kwenda na miradi mingi ambayo mwisho wa siku kunakuwa na miradi yote isiyotekelezeka.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ninalotamani kulisema siku ya leo ni kuhusu suala la uanzishwaji wa Mamlaka ya Usimamizi wa Shughuli za Kilimo, hususan masuala ya ugani. Tumeona tija kubwa iliyotokea kwenye taasisi kwa mfano *RUWASA,* baada ya kuanzishwa. Leo tunaona namna ambavyo angalau kwenye maeneo machache, maji yanaanza kupatikana; pia *TARURA* hali kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba sana Serikali ione umuhimu wa kuanzisha mamlaka hii ili iweze kutusaidia kusimamia kule chini kwenye halmashauri zetu. Hii itawezesha, kwanza, hawa wataalamu wetu kuwa karibu na wale wakulima. Pili, Wizara, kama msimamizi wa sera atakuwa yupo pale, anaweza kusimamia na kuona ni namna gani shughuli zake za kilimo zinavyokwenda na kutekelezeka. Pia litasaidia kwenye suala la uchukuwaji wa hatua kwa wale viongozi ambao watakuwa hawatimizi wajibu na majukumu yao kwenye maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba sana, suala hili la uanzishwaji wa mamlaka ya kilimo liwe ni kipaumbele ili tuweze kuisaidia sekta ya kilimo kwa wakulima wetu wadogo kule chini.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo natamani kulisema ni suala zima la usimamizi wa sekta ya sukari. Pamoja na kwamba hali imetulia, lakini ni ukweli kwamba bado hali siyo shwari sana kwenye sekta ya sukari.

Mheshimiwa Spika, bado tuna changamoto ya uzalishaji wa miwa kwenye mashamba tuliyonayo. Bado mashamba tuliyonayo yanazalisha chini ya kiwango, hayafikii lengo. Hata hivyo,

viwanda tulivyonavyo bado havizalishi vizuri kwenye hiyo miwa tuliyonayo kwenye viwanda vyao.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba Wizara watafute namba ya kutengeneza mkakati madhubuti wa kuweza kuwasimamia hawa watu wa tasnia ya sukari. Mashamba au maeneo waliyonayo, moja yazalishe kama walivyojiwekea malengo yao. Pili, na viwanda vyetu pia viweze kupata *material* na viweze kuzalisha ili tupunguze fedha nyingi tunazoendelea kuagiza sukari nje ya nchi na kuendelea kupoteza fedha nyingi za kigeni.

Mheshimiwa Spika, tunatakiwa tuzalishe sisi wenyewe tuweze kuuza kwa majirani zetu nasi tuweze kuongeza hizo fedha za kigeni, lakini pia tuweze kujitosheleza na bei iweze kushuka kwa Watanzania wetu hapa ndani ili wote waweze kutumia sukari.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine pia ni kwenye sekta ya mafuta. Serikali ilikuja na mpango mzuri sana wa kuhamasisha wakulima kwa ajili ya uzalishaji wa mbegu za uzalishaji wa mafuta. Wananchi walihamasika wakalima kwa msimu mmoja. Baada ya hapo, msimu wa pili bei iliporomoka. Baada ya bei kuporomoka Serikali ikatoa fursa ya kupunguza kodi kwenye uagizaji wa mafuta nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, leo tunapozungumza, wananchi wamekata tamaa kulima mchikichi, kulima alizeti kwa sababu bei imeporomoka. Pili, wale waagizaji wa mafuta au watu wenye viwanda vya mafuta ambao wanapewa fursa ya kuagiza wameona, ni rahisi kuagiza mafuta nje kuja kuyaleta humu ndani na kuyachakata na kuuza badala ya kununua mazao yaliyomo humu ndani.

Mheshimiwa Spika, sasa kama Taifa tukiendelea na hali hii, hakika hatutafikia lengo ambalo tulikuwa tumejiwekea kama nchi, la kuhakikisha kwamba tunatamani tuzalishe vya kwetu, kwa sababu uwezo tunao, ardhi tunayo, nguvukazi tunayo. Ni kwa nini Serikali tuendelee kuagiza mafuta nje, huku tukiwa tunatumia

fedha nyingi kuagiza mafuta nje? Kwa hiyo, naomba Wizara ya Kilimo irudi kwenye mkakati wake na malengo yake ya kuhakikisha kwamba tunapata mbegu zilizo bora. Pili, tunahakikisha kwamba zao hili linasimamiwa na linakuwa na bei, na tunahakikisha wanunuzi wanakuwepo na tuweke bei elekezi, hususan kwenye zao la alizeti.

Mheshimiwa Spika, leo zao la alizeti limekuwa kila mmoja anakwenda kununua kwa bei yake. Kwa hiyo, naiomba sana Wizara ya Kilimo watusaidie kwenye hili ili tuweze kuondokana na adha kubwa ya upatikanaji wa mafuta kwenye Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, sasa nihamie kwenye Wizara ya Viwanda, ambayo hii pia itakuwa na Wizara ya Kilimo. Suala la Stakabadhi Ghalani, nina mambo mawili kwenye suala hili.

Mheshimiwa Spika, kwanza, ni lazima kwa *either* ni wadau ama mtu mwingine yeyote, wanapokwenda kujenga maghala haya wasiyajenge mjini, wajenge vijijini ambako ndiko wananchi wanakolima na ndiko mazao yao yalipo, ili tuweze kuwasaidia wakulima wetu kutokupoteza mazao mengi wakati wa usafirishaji.

Mheshimiwa Spika, maghala yakiwa kule, mazao ya hawa wananchi hayatapotea kwa sababu watakuwa wanapeleka eneo ambalo ni karibu, lakini wakiyapeleka huku mjini kwa kweli kusafirisha kutoka mashambani mpaka kuyafikisha kwenye haya maeneo ya maghala gharama inakuwa ni kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba Wizara ya Kilimo pamoja na Wizara ya Viwanda, wanapokwenda kujenga maghala ama kuhamasisha wadau kutujengea maghala, waende wakajenge maeneo ambayo wakulima wanapatikana.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni kuhusiana na suala la mazao yanayokwenda kwa msimu kwenye mfumo wa Stakabadhi Ghalani, ama yatakayouzwa kwa kutumia mfumo wa Stakabadhi Ghalani. Mfumo huu ni mzuri, na tunatamani Watanzania wote leo kwa mazao yote yaweze kutumia mfumo

huu ili wakulima wetu waweze kupata tija ama waweze kupata faida.

Mheshimiwa Spika, changamoto iliyopo, elimu bado iko chini sana. Kwa hiyo, tunaomba, Serikali, Wizara ya Viwanda pamoja na Wizara ya Kilimo watusaidie. Kwa mfano, sasa hivi wakulima wetu ndio wako kwenye msimu, wanalima. Tunaomba Serikali ianze kutoa elimu, iwaambie ni mazao gani msimu huu yataingia kwenye mfumo wa Stakabadhi Ghalani.

Mheshimiwa Spika, Serikali iwape elimu, na pia bei zitakazouzwa kwenye huo Mfumo wa Stakabadhi Ghalani badala ya kwamba wakulima wameshajilimia, wamemaliza, wakitaka kwenda kuuza kwa bei fulani, Serikali inakuja kuleta watu kununua kwa bei nyingine. Hiki kitu kinaleta mkanganyiko na inakuwa siyo sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, mtu anakuwa ameshajipangia kwamba naenda kuuza leo, nikafanye mahitaji yangu fulani, wewe unaenda unamzuia ndani ya wiki, wiki mbili, mwezi hujamlipa fedha yake. Inakuwa siyo sawa, na hatuwatendei haki wakulima. Kwa hiyo, naomba Serikali ianze elimu leo, itangaze mazao ya msimu huu yatakayokwenda kuuzwa kwa Mfumo wa Stakabadhi Ghalani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo natamani kulisema ni suala zima la ununuzi wa *scanner* kwenye mipaka yetu yote. Tuna mipaka mikubwa tisa. Kati ya mipaka hii tisa, tuna mpaka mmoja tu ndiyo wenye *scanner,* ambapo ni mpaka wa Tunduma. Mipaka yote haina *scanner*, bandarini hakuna *scanner*.

Mheshimiwa Spika, ukosefu wa *scanner* unasababisha moja, kupoteza mapato ndani ya Taifa letu; pili, mizigo, namna ya ukaguzi, tunafungua kontena, tunaanza kufungua kama ni friji tushushe moja moja. Pia, uingizaji wa vitu *fake* ambavyo vinaweza kuingia unakuwa ni mkubwa sana; tatu, kunakuwa na malipo yale ya wateja wetu ambao wameingiza mzigo kukaa kule bandarini kwa muda mrefu ama kwenye zile *yard* zilizowekwa kule

pembezoni ambapo wao wanatakiwa kulipa baada ya mwezi mmoja.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba pia Wizara ya Viwanda kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha, watoe fedha ili twende tukanunue hizi *scanner* ziweze kusaidia na ziweze kuleta tija kwenye ukusanyaji wa mapato, na urahisishaji wa kazi za viwandani pamoja na bandarini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ni suala la ununuzi wa meli kwa Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Tangu nimeingia Bunge hili mwaka 2015 nilikutana na suala zima la ununuzi wa meli za uvuvi zikiwa nane; nne zikiwa zinanunuliwa upande wa Zanzibar, nne Tanzania Bara. Zikaja zikapungua tukaambiwa zitanunuliwa mbili. Leo zimepungua, tuliambiwa zinakuja nne, sasa tumeambiwa ni mbili, lakini hata hizo mpaka leo kimya.

Mheshimiwa Spika, tunaomba Serikali hebu shikeni hili, tusaidieni hizo meli zinunuliwe zije, changamoto ni nini? Kwa nini hizi meli hazinunuliwi? Shida iko wapi? Nunueni meli hizi ili tuweze kupata hayo mafao, tuweze kupata hizo fedha zinazopatikana kwenye hao samaki walioko bahari kuu.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni boti kwa ajili ya doria. Pia, kulikuwa na ununuzi wa boti kwa ajili ya doria kwenye bahari, mpaka leo nazo kimya. Shida iko wapi? Tusaidieni Wizara ya Fedha, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, tunaomba mshirikiane, nendeni kwa vipaumbele, ni kipi kinachotakiwa kuanza ili tuweze kupata nini? Tukinunua meli za wavuvi, tukanunua na boti za doria hakika tutapata mapato mengi na mambo mengine yataenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine nirudie tena kwenye suala la uanzishaji wa mamlaka za mifugo. Pia, tunaomba Serikali ianzishe mamlaka kwa ajili ya mifugo yetu ili tuweze kusimamia masuala mazima yanayohusiana na mifugo yakiwamo majosho na hata elimu kwa wafugaji wetu. Bado tunatamani sana tupate hii mamlaka ili ziweze kusaidia wafugaji wetu.

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho ni chanjo kwa mifugo. Wafugaji wetu wanatamani sana kupata chanjo ama mifugo yao iweze kupata chanjo. Changamoto kubwa zilizopo ni uwepo wa chanjo *fake* na gharama za chanjo. Sasa naomba kwa wafugaji wetu na Wizara, mtusaidie. Moja, elimu kwa wafugaji. Pia kuwaelimisha kwamba chanjo zinazotolewa ni chanjo zitakazoleta tija kwa hao wafugaji. Pili, ni chanjo zitakazoleta tija kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, leo tunashindwa kuuza nyama nje kwa sababu tu wenzetu hawaamini kwamba mifugo yetu inatunzwa na inapata chanjo kwa namna gani? Kwa hiyo, tukipata chanjo na wananchi wetu wakipata chanjo, tutapata soko la nje. Kwa hiyo, tutanufaika sisi wafugaji, lakini litanufaika Taifa kwa maana ya kupata fedha za nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru kwa muda wako, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Joseph Michael Mkundi atafuatiwa na Mheshimiwa Balozi Liberata Mulamula, na Mheshimiwa Charles John Mwijage ajiandae.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Nianze kwa kuwapongeza Wenyeviti wa Kamati zote mbili kwa uwasilishaji wao mzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2025, Sura ya Tano, Ibara ya 105 inaipa jukumu Serikali kusimamia amani na usalama wa Taifa letu. Inatoa jukumu hili kwa sababu kuna uwiano mkubwa sana kati ya amani na maendeleo ya kijamii na kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutekeleza vizuri sana Ilani yetu ya uchaguzi. Mheshimiwa Rais amefanya uwekezaji mkubwa sana kwenye vyombo vyetu vya ulinzi na usalama, ndiyo maana leo

Taifa letu lina hali iliyo shwari. Sisi Kamati tumepitia mambo mbalimbali, tumejiridhisha hali ya ulinzi na usalama wa Taifa letu inaridhisha sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna hatua kubwa sana ya mabadiliko chanya kwenye vyombo vyetu vya ulinzi na usalama. Ndiyo maana siyo ajabu leo hii Mataifa mbalimbali na viongozi wa Mataifa mbalimbali hawaoni kigugumizi kuja Tanzania kutembelea, lakini hata kushiriki mikutano mbalimbali ya Kimataifa inayofanyika kwenye Taifa letu. Nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na mambo mazuri sana yanayofanyika, nalipongeza Jeshi la Polisi, wanafanya kazi kubwa sana. Hii ni kutokana na uwekezaji mkubwa ambao Serikali imewekeza kuhakikisha vyombo vyetu vya ulinzi na usalama vinafanya kazi zake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Magereza linafanya vizuri pamoja na changamoto zake; na Uhamiaji wanafanya vizuri. Nimekuwa nazunguka kwa siku kadhaa kwenye mji wetu wa Dodoma, lakini hata miji mikuu mingine naona Jeshi la Polisi watu wake wako kwenye kila kona wakiwa na vifaa kwa ajili ya kuhakikisha Taifa letu linakuwa salama. Niendelee kumpongeza Mheshimiwa Rais na vyombo vyote vya ulinzi na usalama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na haya ambayo ni mazuri, bado kuna changamoto ambazo tunatakiwa tuzifanyie kazi. Majeshi yetu yanafanya kazi vizuri, lakini kuna mabadiliko makubwa sana ya kijamii. Kuna ongezeko la watu, kuna mabadiliko ya teknolojia na mabadiliko mbalimbali ya kijamii yanayotokea. Jambo hili linasababisha kuwe na uhitaji mkubwa wa vifaa vya kisasa na kisayansi kwa ajili ya kufanya upelelezi na kufanya uchunguzi wa kisayansi ili kuweza kukabiliana na uhalifu wa kisasa tofauti na huko tunapotoka.

Mheshimiwa Spika, leo kwa mfano Jeshi la Polisi lina vifaa ambavyo kwa uwekezaji uliofanyika na Serikali, wanafanya

shughuli zao, lakini bado vinahitajika vifaa vya kisasa vya kiupelelezi na kiuchunguzi ili kuweza kuendana na mabadiliko ya kisasa na mabadiliko ya kisayansi. Pia, kama nilivyosema, kwa ongezeko la watu, ukosefu wa ajira unafanya kuwe na makosa mengine mengi sana yanayotokana na changmoto kama hizo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, sisi Kamati tuliona bado kunahitajika uwekezaji mwingine mkubwa ili kuhakikisha majeshi yetu, hasa Jeshi la Polisi linapata vifaa vya kisasa ili kuweza kukabiliana na changamoto hizi zinazotokana na mabadiliko ya kidunia.

Mheshimiwa Spika, amesema Mheshimiwa Zahor, bado kuna upungufu wa vifaa hasa magari kwenye majeshi yetu. Jeshi la Magareza kwa mfano lina upungufu mkubwa wa magari, Jeshi la Zimamoto lina upungufu mkubwa wa magari, hasa ikiwa ni pamoja na boti za uokoaji, vitu ambavyo ni muhimu sana kwa shughuli zao na ukizingatia kwamba jamii yetu kwenye Taifa letu kuna changamoto kadhaa zinatokea majini na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kupatikana kwa vifaa hivi kutafanya majeshi yetu yaweze kufanya kazi zake vizuri. Kwa hiyo, naomba Serikali pamoja na mipango na mikakati iliyopo, lakini bado kunahitajika uwekezaji mkubwa kwenye majeshi yetu ili waweze kupata vifaa vya kufanyia kazi kwa ubora mkubwa zaidi.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kuunda Tume ya Haki Jinai. Jambo ambalo limeboresha sana utendaji kazi wa majeshi yetu na kutoa haki kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu hiyo, nitoe rai kwa wananchi ili kuweza kufanya vyombo hivi viweze kufanya kazi zake vizuri hasa Jeshi la Polisi, wananchi watoe ushirikiano kwa kutoa taarifa za uhalifu kwa majeshi yetu ili majeshi haya yaweze kufanya kazi yake vizuri na kufikia lengo tulilolitarajia kulingana na maelekezo ya ilani yetu, Mheshimiwa Rais aweze kuendelea kutenda majukumu yake kwa ubora mkubwa ili kuhakikisha kwamba majeshi haya yanafanya kazi yake, yanalinda amani na Taifa letu

linaendelea kuwa kinara kwenye ukanda huu na dunia nzima kama kisiwa cha amani.

Mheshimiwa Spika, yangu yalikuwa ni hayo machache, nashukuru kwa nafasi, Mwenyezi Mungu akubariki sana.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Balozi Liberata Mulamula atafuatiwa na Mheshimiwa Charles John Mwijage.

**MHE. BALOZI LIBERATA R. MULAMULA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi nami niweze kuchangia kwenye Taarifa ya Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kama ilivyowasilishwa vizuri na kwa ufasaha na Mwenyekiti wetu Mheshimiwa Vita Kawawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, naomba nimshukuru Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa namna anavyoikuza diplomasia yetu ya Tanzania. Pia, napenda kumshukuru kama Amiri Jeshi Mkuu kwa kuhakikisha kwamba nchi yetu iko salama na imara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kuchangia taarifa ya Kamati hii kama Mjumbe, naomba nikushukuru wewe binafsi kwa kunipangia Kamati hii ambayo inahusika na masuala ya diplomasia, masuala ya usalama na ulinzi, eneo ambalo nimehudumu kwa muda mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, natambua umuhimu wa Kamati hii katika kusimamia utekelezaji wa kazi za Wizara husika, katika kukuza mahusiano ya Kimataifa, kulinda amani na usalama wa nchi yetu na watu wake.

Mheshimiwa Spika, bila kupoteza muda, naomba kwanza niunge mkono hoja ya Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama. Pia, nakubaliana na taarifa na mapendekezo kama yalivyowasilishwa na Mwenyekiti wetu.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kuongeza mchango wangu kama Mjumbe wa Kamati, katika maeneo matatu. Moja, inahusu diplomasia yetu ya Uchumi; pili, amani na usalama kwenye kanda yetu ya maziwa makuu; tatu, muda ukiruhusu nitagusia masuala ya mtangamano wa kikanda, yaani Jumuiya ya Afrika Mashariki na *SADC* kwa ajili ya tafakuri ya Bunge na kuishauri Serikali yetu ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naomba kuipongeza Serikali na Wizara husika kwa taarifa walizotupatia kwenye Kamati pamoja na ziara za mafunzo na semina zilizotolewa na taasisi mbalimbali za Wizara hizo tatu, katika kutuelimisha kuhusu utekelezaji wa majukumu yao na mipango ya maendeleo katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, niseme tumepata wasaa wa kupokea taarifa za Wizara hizo tatu na kuzichambua. Niseme katika utekelezaji wa Maazimio ya Bunge, hatua mbalimbali zimechukuliwa na inaashiria kuna mwitikio mzuri wa kuyatekeleza na pia kuna changamoto kama zilivyoainishwa na Mwenyekiti wetu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu diplomasia ya uchumi, naomba kwanza nimpongeze sana kwa dhati Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, mwanadiplomasia namba moja kwa kuipaisha diplomasia yetu ya uchumi kwa maono yake, kwa wepesi wake wa kufanya ziara mbalimbali nje ya nchi, kwa kujenga na kukuza mahusiano na nchi mbalimbali duniani na mashirika ya Kimataifa, pamoja na kuhamasisha uwekezaji na kujenga mahusiano mazuri ambayo yamechochea kupata misaada mingi sana katika kujenga uchumi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, naomba nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kuvutia mikutano mikubwa ya Kimataifa nchini, ikiwemo *Africa Energy Summit* iliyomalizika juzi ambayo ilihudhuriwa na viongozi wa juu wa nchi kutoka Bara la Afrika na duniani kote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii imeonyesha kutambulika na kuheshimika kwa Rais wetu, na kukubalika ulimwenguni kote. Hakika mwenye macho haambiwi tazama, kama Waingereza wasemavyo, *"it is economic diplomacy at its greatest height and at its best."* *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba pia niwapongeze Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, chini ya uongozi mahiri wa Mheshimiwa Mahmoud Thabit Kombo na Manaibu wake, Mheshimiwa Cosato Chumi, Mbunge; namwona na Mheshimiwa Dennis Lazaro Londo pamoja na Mabalozi wetu na Watumishi wote wa Wizara kwa kazi nzuri wanayoifanya katika kuendeleza diplomasia yetu ya uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hizo, tathmini ya Kamati kutokana na taarifa tulizopokea zinaonesha wazi kwamba, bado kuna uelewa mdogo kwa wadau hususan sekta binafsi na wanaNchi kwa ujumla kuhusu manufaa ya diplomasia ya uchumi na fursa nyingi zinazotokana na mtangamano na mahusiano yetu ya Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, tumeona kwamba, Wizara kwa kweli inahitaji kufanya mawasiliano makubwa kuweza kuhamasisha hasa sekta binafsi kuweza kuchangamkia hizi fursa. Kwa mfano, utakuta kwamba, pamoja na kuwa Sudan ni mwanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, lakini wengi hawajui kwamba huku nako kuna soko. Pamoja na matatizo yao, kuna soko kubwa la mchele na mahindi, lakini wanafikaje?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, sisi kama Kamati tumeshauri kwamba Wizara ikishirikiana na Wizara nyingine za kisekta, zije na mkakati wa kuweza kuelimisha wananchi wetu kuhusu hizi fursa zilizopo.

Mheshimiwa Spika, pia, tumesikitishwa na vikwazo visivyo vya kikodi vinavyoendelea, pamoja na kwamba Jumuiya ya Afrika Mashariki imetoa mwanya na soko huru, lakini juzi tulikuwa mpakani Mtukula tumekuta mlundikano wa malori ya mizigo na

magari mapya ambayo yametoka bandarini kwetu kwenda Uganda hayajavuka. Kwa kweli tunasema kwamba, pamoja na kuwa na *One Stop Center* au *Border Post,* lakini bado kwa kwa kweli kuna changamoto nyingi sana.

Mheshimiwa Spika, vikwazo ni vingi na ukipita kwenye barabara ya kutoka Mtukula mpaka kwenda Bukoba utakuta kwamba bado kuna vizuizi vingi sana ambavyo vimekuwa ni kero sana. Kwa hiyo, niseme pia kwamba pamoja na juhudi za Mabalozi wetu kuimarisha diplomasia ya Uchumi, lakini wengi bado wanalalamika sana kutojibiwa wanayopeleka kwenye Wizara mbalimbali na Serikalini. Kwa kweli inawakatisha tamaa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nami nasema kwamba Diplomasia ya Uchumi haitekelezwi na Balozi zetu peke yake au Wizara ya Mambo ya Nje, bali inahitaji ushirikiano wa sekta zote, na Wizara zinazohusika kama vile Wizara ya Viwanda na Biashara, Uwekezaji na Mipango. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nihitimishe kwa kusema kwamba Diplomasia ya Uchumi ni muhimu kuanzia ndani kwanza, kana kwamba wasemavyo, *foreign policy is an extension of domestic policy.* Kwa hiyo, nashukuru sana kwa fursa hiyo na ninaunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Charles Mwijage.

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa fursa ya kuchangia Taarifa za Kamati mbili; hivyo, kwa sababu ya faida ya muda, nitachangia sekta za kiuzalishaji kilimo na mifugo. Nikijaliwa kidogo nitajikumbusha kama bado biashara naifahamu.

Mheshimiwa Spika, nami nitajikita kwenye kuungana na Kamati, lakini nitaungana nao baada ya kufanya marekebisho. Sitaungana nao kijumla jumla, lazima nitoe mapendekezo yangu. Hata hivyo, kuna uandishi mzuri uliyoonyesha mafanikio na changamoto. Nianzie kwenye mafanikio. Binafsi, nafarijika kwa

mafanikio tuliyoyapata kama nchi kutokana na zao la kahawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tulizoea kuuza kahawa nje ya nchi na kupata dola bilioni 240, lakini kwa mujibu wa taarifa za Kamati, tumepata dola milioni 791. Hii ni kazi kubwa imefanyika, na nitaelezea tumefikaje hapo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kilichokuwa kinaniuma zaidi, siyo kupata mapato zaidi, ila mafanikio ya jirani yetu nchi ya Uganda, wamepata dola bilioni 1.14. Sasa namwambia Mtumishi wa Bwana, hawa watu unawakamata, huhitaji muda mrefu. Uganda tutafika huko, kwa sababu, mwaka 2024 walipata dola milioni 800, na mwaka huu wamepata dola bilioni 1.14. Hivyo, nawe unaweza ku-*leapfrog* na kufika huko ndani ya miaka miwili, au mitatu. Mtumishi wa Bwana, unajua nilikuwa silimi kahawa, lakini mwaka huu nimepanda miche 2,600, na kufika Desemba tapanda miche 5,000. Hivyo, nitakuwezesha kufika hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumefikaje hapo? Tumefika hapo baada ya Mheshimiwa Rais, kwa juhudi zake binafsi, kuweza kufungua soko la China. China sasa wanakwenda kunywa kahawa ya Tanzania, kutoka Kagera, Muleba.

Mheshimiwa Spika, hivyo, nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa jambo hilo alilotutendea. Pia niwaeleze kuwa nimeyasikia mapendekezo ya Kamati. Baada ya bei ya kahawa kuwa nzuri, hakuna cha uhamasishaji. Mtu asichukue fedha yako kwamba anakwenda kuhamasisha. Bei ambayo Mheshimiwa Rais aliwezesha kupatikana, ni hamasa tosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mafanikio mengine niliyoyaona sijui hayajaandikwa vizuri! Hapa ni haya yanayo-*trend* leo kwamba sisi tumezalisha tani milioni 11 za mahindi kutoka tani milioni sita tulizokuwa tunapata. Pia, tumekuwa tukijadili kama Bunge, tukiongozwa na Kamati hii. Mojawapo ya maeneo yaliyotuletea mafanikio, ni ile ruzuku ya mbolea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nami mapendekezo yangu kwa Serikali kwamba tusiishie kuwa wa pili, hoja yangu siyo kuwa wa pili. Kwa imani yangu, nimeshamwambia Mheshimiwa Waziri anayehusika, tunaweza kuzalisha tani milioni 30, inawezekana.

Mheshimiwa Spika, tani milioni 30 inawezakana, na hapo ndiyo tutatengeneza *synergy* ya kufungamanisha mifugo na kilimo, kwa maana ya chakula, kwamba wananchi wanaweza kula hayo mahindi, lakini tunaweza kutumia mahindi na *by-product* za mahindi kulisha mifugo yetu. Hivyo ili tu-*take advantage* ya kuweza ku-*export* mifugo katika nchi za Ghuba ambazo zinahitaji nyama ya Tanzania ya wanyama wadogo wadogo kama mbuzi, kondoo, na ng'ombe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimewahi kusema na ninarudia kusema *potential* ya soko la nyama Ghuba ni dola bilioni tisa. Kama Tanzania, tungeweza kupata nusu yake, tungefika pale tunapopaswa kuwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nazungumzia Sekta ya Sukari na natumia fursa hii kuipongeza Wizara kwa kile kitendo cha kuihamasisha *TEMDO*. *TEMDO,* kile kiwanda chao siyo kiwanda kidogo. Vile tulikuwa tunaviita Viwanda Ngazi ya Tarafa, yaani mnaweza kuwanacho kwenye yale maeneo oevu yanayoweza kulima miwa, na kila tarafa inakuwanacho hicho kiwanda. Hiyo ndiyo mojawapo ya sekta ambazo unaona zitatupeleka kuwa na utoshelevu wa sukari ya kutosha.

Mheshimiwa Spika, *potential* ya sukari Tanzania ni tani milioni mbili tuki-*explore* shughuli zote. Mwenyekiti wa Kamati amekaa mbali nami, alijua nitazungumza naye. Hoja ya *white sugar* na *Industrial sugar* ni tofauti. Hoja ya *Industrial Sugar* siyo miujiza, ni kwamba hatuna sukari ya kutosha. Kwa hiyo, huwezi ku-*refine* sukari kwanza ili kupata *industrial sugar.*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, suluhisho ni kuzalisha sukari nyingi kama tulivyozungumza, Viwanda vya *TEMDO,* hivi vya kuzalisha tani 4,000, au 5,000. Tulianza na Manyara ambapo

walikuwa na tani 2,000 kwa mwaka. Leo wameshapanda. Kwa hiyo, Serikali sasa tuwasukume hawa watu. Ili kumsukuma, lazima umlinde. Kama una msukuma, lakini humlindi, utamuua kwa *pressure*, yaani atapata kiharusi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lazima mtu unapomwambia kajenge kiwanda, umhakikishie kwamba utamlinda. Kama unataka kumuua mtu, usitafute sumu, mwambie anzisha kiwanda, halafu usimlinde. Atakufa *immediately* na atajuana na Mungu wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ndiyo ninalowaambia kuhusu viwanda vya sukari. Nimefurahishwa huu Mpango wa Sukari wa Miaka Kumi na Mbili, tunakaribia kufika pale tulipopaswa kuwa. Pia, nafurahi kazi ya Rufiji, wameanza kulima. Nafurahi tumeanza kufanya kazi Songea, nafurahi Kigoma *Sugar* ya Kasulu inaanza kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nizungumze kidogo kuhusu uvuvi. Imesemwa changamoto ya uvuvi, lakini nyingine Mwenyekiti hakuziandika. Changamoto yetu sisi wavuvi ni magugu maji, na mnajua nina *square* kilomita 7,200 za Ziwa Victoria na Uvuvi wa Samaki ni Ziwa Victoria. Hivyo magugu maji yanaua samaki kwa kiwango kikubwa na haijaandikwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napendekeza uwatume Wajumbe wa Kamati *weekend* hii waende wakaangalie magugu maji, tunakwisha! Hakuna samaki, hakuna *navigation,* tunakwisha na magugu maji. Mwenyekiti unapohitimisha, uombe Spika akuruhusu ukaangalie magugu maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la uvuvi haramu, Kamati imependekeza udhibiti. Nani anadhiti uvuvi haramu Tanzania hii? Hakuna anayedhibiti, na sisi wanasiasa ni wahanga. Kila unapojaribu kusema udhibiti, unakuwa mhanga.

Mheshimiwa Spika, tulipendekeza kwamba ianzishwe Mamlaka ya kudhibiti ziwa, tudhibiti magugu. Nchi jirani kwa

Mjomba, ziwa linalindwa kwa bunduki na kofia zao zimeandikwa UA. Huwezi kugusa samaki. Samaki wa Uganda ukiwekewa kwenye sahani, inabidi uwaambie watu wafiche simu zao wasipige picha, samaki ni mkubwa. Lazima tulinde Ziwa ili tulinde viwanda vyetu. Viwanda vyetu havina kazi vinavyofanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu Sekta ya Chai. Mheshimiwa Waziri, nenda kwenye *niche bucketing,* soko la chai huko duniani limeharibika, lazima hawa watu uwasimamie, lakini uwalinde waende kwenye *niche marketing.* Wakienda ovyo kwenye Soko la Dunia, wanakwenda kutafuta *stroke*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, nipongeze shamba letu la Binengo, mwekezaji aliyeletwa anaelewa na amekuja kwangu, nimemshauri namna ya kufanya, lakini *niche marketing* ni muhimu. Bila kwenda kwenye *niche marketing* soko la dunia haliko salama sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuzungumzie mazingira mazuri ya biashara. Kweli nawapongeza Kamati kwa kuzungumzia *cargos scanner,* na nilizungumza hapa juzi na Waziri wa Fedha, alisema *cargos scanner* inataka kujengwa Mtukula, lakini tumechelewa. Pamoja na mizigo kutafuta ushuru, lakini wepesi wa kufikisha mzigo kwa mteja ndiyo unafanya Tanzania tuweze kupendwa, watu wapende Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mtumishi anajua, hata Rais wa nchi fulani ameamua kuwa *promoter* wa mchele wetu, akisema mchele mzuri duniani uko Tanzania. Sasa, kama unapigiwa kampeni na mtu mkubwa namna hiyo, basi ondoa urasimu, ondoa vikwazo kusudi bidhaa iende sokoni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hayo mawili, naunga mkono hoja kwa marekebisho hayo niliyoyatoa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, majina ni mengi sana hapa, hivyo tutarejea leo jioni. Tutakaporejea,

tutaanza na Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud, Mheshimiwa Vincent Paul Mbogo, Mheshimiwa Dkt. Pius Stephen Chaya, Mheshimiwa Grace Victor Tendega, kisha wengine wataendelea kuitwa kadiri muda utakavyokuwa unakwenda.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, nasitisha Shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni leo.

*(Saa 7.09 Mchana Bunge Lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia)*

*Mwenyekiti (Mhe. Joseph K. Mhagama) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tuketi.

Katibu.

**NDG. MKUTA MASOLI – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA KAMATI**

**Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2024**

**Na**

**Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2024**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano kwa taarifa mbili za Kamati zilizopo mbele yetu kama ambavyo zimeelezwa. Tutaanza na Mheshimiwa Khadija Hassan

Aboud, atafuatiwa na Mheshimiwa Vincent Paul Mbogo na Mheshimiwa Dkt. Pius Stephen Chaya, ajiandae.

**MHE. KHADIJA HASSAN ABOUD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Awali ya yote napenda kuchukua fursa hii kuwapongeza wawasilishaji wetu wawili kwa taarifa zetu hizi mbili za leo za Kamati tunazozijadili. Ninazipongeza Wizara zote zinazosimamia sekta mbalimbali katika Kamati zetu hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianzia na Sekta za Kilimo, Mifugo, Viwanda na Biashara tumegundua kwamba, kuna sheria nyingi ambazo zinakinzana kati ya sheria za sekta na sekta nyingine. Pia, sheria hizi zimepitwa na wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, kuna sheria ambazo haziendani na teknolojia ya sasa. Naomba sana hatua zichukuliwe kurekebisha sheria hizi ili twende na kasi ya maendeleo na ukuzaji wa uchumi katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sekta ya kilimo ninasisitiza kama ushauri wa Kamati ulivyosema kwamba, huduma za ugani, ule uwakala uharakishwe ili uanze kazi. Sambamba na hilo, kuajiri zaidi Maafisa Ugani wa sekta za kilimo, mifugo na uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiendelea, kuna Vituo vya Rasilimali vya Kilimo vya Kata. Vituo hivi vipo kwenye kata zetu na maeneo yote ya nchi, lakini ukweli ni kwamba havifanyi kazi inayokusudiwa. Vituo hivi vinafanya kazi nyingine ambazo hazimsaidii mkulima kama lengo lililokusudiwa kuanzisha kwa vituo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ushauri wa Kamati unavyosema, vituo hivi vimebadilishwa matumizi. Kama Kamati ilivyoshauri, nami ninaongezea hapo kwamba vipelekwe kwenye Wizara ya Kilimo ili vikafanye kazi iliyokusudiwa na Wizara ya Kilimo ifanye kazi ya kuviendeleza zaidi, kuviwekea miundombinu na vifaa vya kisasa ili vitoe huduma za ugani na mafunzo ya kilimo

kama ilivyokusudiwa. Uwekezaji mkubwa umefanyika, lakini kazi iliyokusudiwa haifanyiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiendelea kwenye huduma hizi za kilimo cha umwagiliaji maji, ni muhimu sana. Ninashauri kama ilivyosema Kamati, tuongeze kuajiri wataalamu wa umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatenga fedha nyingi kwa ajili ya umwagiliaji, kujenga mabwawa, lakini tuna uhaba wa wataalamu wa elimu ya umwagiliaji. Hapa tutaokoa fedha nyingi za Serikali kuona miradi hii inafanya kazi iliyokusudiwa na inatoa huduma za kilimo bora kwa wakulima na wananchi wetu ambao tuna hamu ya kujifunza kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye sekta ya mifugo, hamasa kubwa iwekwe kwenye kuongeza viwanda vya usindikaji maziwa, ili tuweze kunusuru upotevu wa maziwa tulionao hivi sasa. Pia, tutaongeza ajira kwa vijana wetu na pato la Taifa kwa kupunguza uagizaji maziwa kwa fedha za kigeni ambazo tunazo hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna changamoto, tunampongeza mwekezaji wa ndani Ndugu Asas kwa kuanzisha kiwanda kikubwa sana cha usindikaji wa maziwa ya unga, lakini changamoto iliyokuwepo maziwa ya unga na bidhaa ambazo zinazalishwa na maziwa, kwa mfano jibini na vitu vingine, inaonekana kama ni maziwa ya anasa au ya kujistarehesha. Kwa hiyo, kodi imekuwa kubwa sana, ambapo uzalishaji na uunzaji wa maziwa unakuwa changamoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maziwa ya unga ni chakula kama maziwa mengine, kwa sababu wananchi wetu, sio wote wana majokofu ya kuhifadhi maziwa ya kawaida. Wakinunua maziwa ya unga wakayaweka ndani, wanaweza kuyatumia mwezi mmoja mpaka mitatu. Kwa hiyo, ile hali ya kuwa na lishe bora itakuwa inakwenda sambamba na yule ambaye anatumia maziwa ya maji na unga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sasa hivi dunia imefunguka, wananchi wetu wanajua kutumia hivi vitu; jibini na vitu vingine. Sasa kodi inapokuwa kubwa, wanashindwa kumudu na hii itasababisha wawekezaji wengine washindwe kuja kuwekeza kwa sababu ya changamoto hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najielekeza kwenye uvuvi na hasa uvuvi wa Bahari Kuu. Naipongeza Serikali kwa dhati kabisa kwa kufikia hatua kubwa ya ujenzi wa Bandari ya Uvuvi kule Kilwa. Ni fahari kwa Tanzania, tutawekeza sasa kwenye uvuvi wa Bahari Kuu na tutapata fedha za kigeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bandari yetu ya uvuvi inakaribia kukamilika, lakini bado meli za uvuvi hazijawa tayari. Ni vyema basi mambo haya yaende sambamba; meli za uvuvi na bandari yenyewe ya uvuvi, ili tuweze kufikia yale malengo tuliyoyakusudia na tunayoyatarajia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo, Shirika la *TAFICO* liwekewe miundombinu na vitendea kazi vya kutosha ili liende sambamba na uvuvi wa Bahari Kuu kwa maana vitu vyote vitakuwa vimekamilika. Shirika hili limeanza zamani kufufuliwa, lakini bado uwekezaji wake unakuwa taratibu. Hofu yangu ni kwamba, tunawekeza fedha nyingi, lakini hatukamilishi. Kuna hatari sasa na vile vya mwanzo vikaharibika kabla hivi vya mwisho havijatokea. Tunachohitaji ni uzalishaji, tuwekeze hapa kwenye uvuvi wa Bahari Kuu, tuingize fedha za kigeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo chetu cha Mbegani Bagamoyo kinakabiliwa na changamoto nyingi zikiwemo uchakavu wa majengo na miundombinu, na uchakavu wa vifaa vya kufundishia zikiwemo meli. Kwa hiyo, ni vyema chuo hiki kikapatiwa miundombinu hiyo ili wanafunzi wetu wapate ile fursa tunayoisema ya kujiajiri ili kupunguza changamoto hii ya ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo, kwenye Chuo chetu cha Mbegani wanafunzi wapatiwe mikopo kama vyuo

vingine vya kati. Sasa hivi kwenye chuo kile, wanafunzi hawawezi kupata mkopo, wanajifunza ujasiriamali wa kuvua na kufuga Samaki, lakini kwa sababu ya uwezo mdogo wa wazazi wao, wanashindwa kuomba kusoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, chuo hiki kinatakiwa sasa kiwe sambamba na vile vyuo vingine vya kati. Wapatiwe mafunzo hawa vijana waweze kujisajili na wakasome haya mafunzo ya ujasiriamali wa uvuvi na mambo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, najielekeza kwenye sekta ya viwanda. Kuna Kiwanda chetu cha Kibaha cha Viuadudu. Uwekezaji mkubwa umefanyika, lakini bado kinakabiliwa na changamoto za madeni na vitu vingine. Nashauri tuendelee kuishauri Serikali kama maazimio ya Kamati, madeni yale yalipwe. Pia kipanuliwe zaidi ili kuzalisha dawa za viuadudu nyingine kwenye mazao ya kilimo, ili tuweze kuzitumia badala ya kuagiza vitu kutoka nje, kwani vingine vinakuja havina ubora, wakulima wetu wanapata hasara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna taasisi zetu kama *CAMARTEC, TEMDO, KMTC, SIDO* na *TIRDO*. Hizi ziongezewe bajeti kwa sababu tumeziona na tumezikagua. Tumeona utekelezaji wake, na hamu waliyonayo wafanyakazi wa sekta hizi, ni kutaka kuhakikisha kwamba Tanzania tunajitegemea kwa vifaa vyetu mbalimbali ambavyo tunavitumia humu nchini vikiwemo vya kilimo na viwanda vidogo vidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumesikia hivyo viwanda vya sukari wanatengeneza majokofu. Sasa hivi wana mpango wa kutengeneza majokovu ya kuhifadhia barafu kwa ajili ya samaki wengi watakaovuliwa wakati wa uvuvi wa Bahari Kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiwekeza hapa, tutarejesha fedha mara tatu au nne ya hizo ambazo tumewekeza na itatupunguzia Tanzania kutumia fedha zetu za kigeni za ndani kuagiza vifaa hivyo ambavyo wananchi wetu wana ujuzi na uwezo wa kuzalisha hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, tuongeze bajeti na vifaa vya kutosha kwenye hizi sekta. Pia tuongeze wataalamu wa fani mbalimbali wa kutosha ili waweze kumudu kazi zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, nazipongeza Wizara zote hizi: Kilimo, Uvuvi na Viwanda. Serikali imeongeza bajeti kubwa katika sekta ya uzalishaji, lakini tumeona mafanikio na faida ya fedha hizo zilizowekezwa. Kilimo sasa kinakua, uvuvi unakua na ufugaji unakua pia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud. Sasa namwita Mheshimiwa Vincent Paul Mbogo, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Pius Stephen Chaya. Mheshimiwa Grace Victor Tendega ajiandae.

**MHE. VINCENT P. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi nami niweze kuchangia taarifa yetu ya Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama. Kipekee nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa anayoifanya ya kuendelea kuviboresha vyombo vyetu vya ulinzi hasa kwa kuendelea kutoa ajira mpya ili kuleta ufanisi ndani ya vyombo vyetu vya ulinzi na usalama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, nawapongeza Mawaziri wote wa Wizara tatu: Wizara ya Mambo ya Nje, Wizara ya Mambo ya Ndani, Wizara ya Ulinzi pamoja na timu nzima ya Makatibu Wakuu na wataalamu wote kwa kuendelea kumsaidia Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaona mambo ya maendeleo wanayoyafanya na yanaonekana kwa macho, kuanzia vyombo vya usafiri ndani ya vyombo vyetu vya ulinzi na usalama vinaboreshwa kwa kasi kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Nkasi Kusini na Mkoa wa Rukwa. Jimbo la Nkasi Kusini Mheshimiwa Rais ametufanyia mambo makubwa sana ya maendeleo. Jimbo la Nkasi Kusini kwa niaba ya wananchi, tunamshukuru Mheshimiwa Rais kwa sababu halikuwa na Kituo cha Afya hata kimoja. Mheshimiwa Rais ametujengea vituo vya afya sita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kata nne hazikuwa na barabara, Mheshimiwa Rais amefungua barabara mpya nane. Shule za Msingi mpya nne, vijiji 32 havikuwa na umeme, kote umeme umefika. Tunasema ahsante sana, 2025 wananchi wanasema wanaenda na Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na usalama ndani ya Ziwa Tanganyika. Jimbo la Nkasi Kusini na Mkoa wa Rukwa unapakana na nchi nne: Burundi, Zambia, Congo hadi Mpaka wa Rwanda Kigoma huko. Kuna changamoto kubwa sana ya usalama ndani ya Ziwa Tanganyika. Wavuvi wetu wanaokwenda kufanya shughuli za uvuvi, wanavamiwa na kunyang'anywa nyavu zao, fedha na rasilimali hadi kuvuka upande wa pili wa Tanzania, wanapata hasara sana wanapovamiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru Wizara ya Ulinzi. Niliomba ujenzi wa Kambi ya JKT Tarafa ya Wampembe, katika Taarifa yao wameiweka. Naomba Kambi hii ianze kujengwa mapema kwa ajili ya usalama ndani ya Ziwa Tanganyika. Vilevile, Barabara ya Wampembe ipandishwe hadhi iwe barabara ya kiulinzi, ikarabatiwe wakati wote; masika na kiangazi, iweze kupitika ili ulinzi Ukanda wa Ziwa Tanganyika ufanyike kwa sababu kuna uhalifu wa mara kwa mara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru Wizara ya Mambo ya Ndani, niliomba ujenzi wa Kituo cha Polisi Kata ya Kala Kijiji cha Mpasa. Kituo cha Polisi Kata ya Mpasa kimejengwa vizuri, changamoto inakuja kwenye vifaa. Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani aliniahidi kupeleka boti Ukanda wa Ziwa

Tanganyika, Kituo cha Polisi Mpasa, lakini mpaka sasa bado hazijafika. Naomba Mheshimiwa Waziri Bashungwa apeleke boti kwa ajili ya *patrol* ndani ya Ziwa Tanganyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa yetu imegusia Jeshi la Polisi pamoja na Jeshi la Zimamoto. Kuna changamoto kwa Jeshi la Zimamoto kutokuwa na ofisi vijijini, na kwa sasa kuna ukuaji mkubwa sana wa vijiji pamoja na maendeleo yanayokuja na kasi ya ujenzi wa nyumba za umeme. Kwa hiyo kuna majanga yanayotokea mara kwa mara. Kuna majanga ya asili na majanga yasiyo ya asili. Upande wa umeme kuna majanga ambayo yanatokea ya moto. Jeshi la Zimamoto halina ofisi mpaka vijijini. Kwa hiyo, elimu kufika vijijini bado ni changamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwenye vile vituo vya Polisi vya kisasa vilivyojengwa, Jeshi la Zimamoto lipewe nafasi na ofisi ili liweze kwenda kutoa elimu vijijini. Pamoja na hayo, Jeshi la Zimamoto liongezewe fedha ili lianzishe Kitengo cha Zimamoto Jamii, kwa sababu Zimamoto Jamii itaweza kufika hadi vijijini kutoa elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna majanga mengi yanayowapata watoto na vijana kama kuangukia kwenye visima na mito wakati wa masika, lakini elimu ya uokoaji bado kwa sababu Jeshi la Zimamoto ndilo tumelihuisha sasa hivi kuwa idara. Kwa hiyo, bado halijatanua wigo kufika hadi vijijini. Sasa, kupitia Zimamoto Jamii, vile vikundi vitapata elimu na vitaweza kuokoa mapema kabla jeshi halijafika kuokoa maisha ya watu, litafika mapema na jamii itakuwa sehemu husika ya tukio. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo biashara haramu ya binadamu, imekuwa ni biashara kubwa sana, inatishia, na watu wengi wanauzwa kimya kimya. Jamii hasa huko vijijini bado haijapata elimu. Naomba iundwe idara kamili ya kuweza kukabiliana na hii changamoto kwa sababu ni kubwa sana. Taarifa na elimu ya wale waliouzwa wakaokolewa, itolewe kwenye vyombo vya taarifa ya habari, *TV* na magazeti; na viongozi wapewe elimu na

ishuke chini mpaka kwa Madiwani ili wananchi vijijini wapate elimu kwamba kuna biashara haramu ya binadamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya kata zipo kwenye mazingira magumu ambapo zinatakiwa zijengewe vituo vya Polisi. Kwa mfano, Kata ya Kate, wananchi wamejitolea, wamejenga lakini bado. Naomba Wizara hii itenge angalau shilingi milioni Hamsini hamsini kwa kila kata, ipelekwe ikaunganishe nguvu za wananchi kwenye hivi vituo vya Polisi ili wananchi wapate ulinzi katika vijiji vyao, kwa sababu uhalifu upo mara kwa mara kutokana na jiografia ngumu ya kata zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mbogo. Mheshimiwa Dkt. Pius Stephen Chaya, atafuatiwa na Mheshimiwa Grace Victor Tendega, na Mheshimiwa Edwin Enosy Swalle ajiandae. *(Makofi)*

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipatia hii nafasi ya kuchangia kwenye taarifa hizi mbili za Kamati zetu. Vilevile, nawashukuru Wenyeviti wetu wawili ambao wamewasilisha hizi taarifa muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee namshukuru Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa ambayo ameifanya hususan katika Jimbo la Manyoni Mashariki. Nikisema nianze ku-*mention* miradi yote ambayo ameifanya, naweza nisimalize, lakini nskiri kwa kusema kwamba sisi watu wa Manyoni mwaka huu ni Mwaka wa Uchaguzi na tumepeana ahadi kwamba, tutahakikisha Mheshimiwa Rais tunampatia heshima kubwa kwa kazi kubwa ambayo ameifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina maeneo mawili ambayo ningependa kuchangia kwenye Taarifa ya Kamati, hususan kilimo na upande wa mifugo. Upande wa kilimo, kwanza nampongeza

Waziri pamoja na timu yake, kaka yangu Mheshimiwa Bashe. Kwa kweli, Mheshimiwa Bashe hajasomea kilimo, nadhani tunatakiwa tum-*award Ph.D* ya kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa taarifa niliyonayo, najua Mheshimiwa Waziri amesoma Mzumbe, mambo ya *administration*, lakini kimsingi ame-*master* sana hii Wizara ya Kilimo. Ukiacha hilo, Mheshimiwa Bashe umekuwa *very aggressive*, *very innovative*, *very strategic* na nina mifano kwa nini ninasema hilo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande wa Tume ya Umwagiliaji, wote ni mashahidi, huko nyuma Tume ya Umwagiliaji kimsingi ilikuwa imekufa, lakini kwa ushawishi wake kwa Mheshimiwa Rais, akamshawishi pamoja na Wizara yake, wakaongezewa fedha za umwagiliaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka tulikuwa na shilingi bilioni 42 wakati tumeingia. Sasa hivi anachezea shilingi bilioni 500 na kitu. Hii ni kwa sababu, yupo *aggressive*, *innovative* na yupo *result based.* Ndiyo maana Mheshimiwa Rais amemwelewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule kwangu kuna mradi mmoja wa Umwagiliaji wa Mbwasa. Kila Ilani ya Uchaguzi huwa unawekwa. Mimi tangu nimeanza kukua nasikia tu unatajwa, Mradi wa Mbwasa *Irrigation*, Mradi wa Umwagiliaji wa Mbwasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2024, Mheshimiwa Rais ali-*commit* ile *tender* ya zaidi ya shilingi bilioni 18 ikatangazwa, na mkandarasi ameshapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii nimepewa taarifa, *next week* mkandarasi anaenda kukabidhiwa *site* na watu wa Manyoni wameniomba wakasema kwamba, Mheshimiwa Bashe kwa sababu, hii historia ameiweka mwenyewe, tunaomba yeye mwenyewe aje awe mgeni rasmi kwenye kumkabidhi *site* huyo mkandarasi, tarehe 13. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa heshima hii ambayo anaenda kuiweka. Ule ni mradi mkubwa sana wa kihistoria, tangu Mzee Chiligati akiwa Mbunge, akiwa Waziri, *for 15 years* alikuwa akipigia kelele, lakini ndani ya hii miaka minne ya Mheshimiwa Rais. Dkt. Samia Suluhu Hassan, anaenda kuweka historia nyingine kubwa sana ya kilimo cha umwagiliaji kwenye eneo letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbali ya hiyo, kuna mradi mwingine wa Udimaa. Nao mwaka 2024 ulitangazwa, ambapo kimsingi tunasubiri mkandarasi naye asaini *contract,* kwa ajili ya kuanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, haya ni mafanikio makubwa sana upande wa kilimo, nami nimekuwa mdau wa Kilimo cha Umwagiliaji. Mara nyingi ninam-*challenge* Mheshimiwa Bashe, namwambia, kama hauta-*focus* kwenye suala la umwagiliaji, kilimo cha Tanzania tutakuwa waongo. *We have to transform our agriculture,* twende kwenye umwagiliaji kwa sababu, mvua hazitabiriki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbali ya hayo kuna maeneo ya umwagiliaji, Mheshimiwa Bashe ni shahidi. Kule bondeni kwetu, Tarafa ya Kintinku, kuna maeneo ya umwagiliaji ambayo kimsingi yanahitaji kuwa *developed*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, *Scheme* ya Walak, *Scheme* ya Msemembo, *Scheme* ya Udimaa, *Scheme* ya Ziale, *Scheme* ya Makanda na hata Ngaiti na kwingine. Haya ni maeneo ambayo kimsingi naomba ayachukue kama changamoto, *in the future* tuangalie ni jinsi gani tunaweza tukaendeleza?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Tume ya Umwagiliaji, nimekuwa nikichangia mara nyingi. Ukiangalia sasa hivi haina *investment* ambayo tume ina-*manage*, *is a very huge investment*. Halafu bado tunadili na tume. *Scope* imeongezeka, lakini bado tuna-*deal* na tume. Ushauri wangu ni kwamba, kwa nini tusi-

*transform* hii tume, tukatengeneza *a very giant institution,* mamlaka ambayo itaenda sasa kusimamia huu uwekezaji ambao tumeshauweka kwenye maeneo mengi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii shilingi bilioni 18 siyo Manyoni tu, mimi ninajua kule Mkalama kuna mradi mkubwa sana wa umwagiliaji, na Iringa kuna mradi mkubwa sana wa umwagiliaji. Nashauri, na ninaona hapo Mheshimiwa Waziri yupo karibu na Spika, naye ndiyo anahusika kwenye kushawishi hivi vitu, naomba tuletewe sheria ya kutengeneza Mamlaka ya Usimamizi wa Umwagiliaji Tanzania, ili tuweze kuipa nguvu Tume ya Umwagiliaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili ni suala la korosho. Kwa kweli, ninamshukuru Mheshimiwa Rais, na pia namshukuru Mheshimiwa Bashe. Watu wa Mtwara na Lindi walikuwa wanatudharau Manyoni kwamba, ninyi Manyoni hamwezi kulima korosho. *Frankly speaking*, sasa hivi Kilimo cha Korosho Manyoni kime-*peak*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka huu tumeenda kuuza korosho zaidi ya tani 100,000 kwa shilingi 3,167/=. Mimi wakati ninaingia Ubunge, nakumbuka tuliuza korosho kwa shilingi 1,600/= na mwaka 2024 tuliuza kwa shilingi 1,300/=, lakini mwaka huu wakulima wameuza kwa shilingi 3,167/=, ndani ya wiki hii iliyopita. Kwa hiyo, haya ni mafanikio makubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiacha hilo, Mheshimiwa Rais ametujengea ghala kubwa sana la kisasa pale. Watu wa *TARI* wamewekeza kwenye huu Mradi wa Korosho. Tuna zaidi ya ekari 22,000 ambazo tumeweka kule kwenye Mradi wa Korosho na tumejenga nyumba mbili za watumishi kule kwenye *site* za korosho. Haya ni mafanikio makubwa sana upande wa korosho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina changamoto chache ambazo ningeweza kumshauri Mheshimiwa Waziri, kwanza, ni vile viuatilifu vya ruzuku wanavyoleta, hawaangalii ukubwa wa ekari ambazo

mtu anazo. Mwenye ekari 10 anapewa *the same quantity* na mwenye ekari mbili. Sasa wakulima wangu wanalalamika. Nadhani iangaliwe, kama mkulima ana ekari 50, idadi ya viuatilifu atakavyopewa iendane, iwe *proportional* na idadi ya ekari ambazo anazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili ni kuhusu mnada. Tulifanya mnada *last week*, lakini kuna wakulima wengi bado wanaendelea kuvuna. Wanashauri, ni kwa nini tusiwe na minada mitatu? Kwa mfano, tukawa na mnada wa kwanza *mid-February*, mnada wa pili *end of March* na mnada wa tatu *end of May*, ili angalau tuweze ku-*capture* wakulima wote kulingana na vipindi tofauti tofauti vya uvunaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la tatu ni magunia. Gunia moja la kuhifadhia korosho linauzwa shilingi 10,000/= Manyoni. Najua kule kwenye tumbaku Mheshimiwa Bashe anatoa magunia ya ruzuku. Anawakopesha wakulima, wanachukua, *then* anakuja kuwakata wakati wa kuuza, kwa sababu sisi tunauza kwa kutumia Stakabadhi Ghalani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ni kwamba, kwa nini tusitoe haya magunia kwa kuwakopesha, *then* wakati wanauza kwenye ule mnada wa Stakabadhi Ghalani wakatwe? Ile bei ya shilingi 10,000/= *is very expensive*. Kwa hiyo, wakulima wengi wanalalamika. Ningeshauri hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, tembo wanasumbua wakulima wa korosho. Sasa, hili siyo la Mheshimiwa Bashe, namwona kaka yangu hapo Mheshimiwa Kitandula ananiangalia. Tembo wanasumbua wakulima wa korosho, ninaomba nisaidiwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ni Wizara ya Mifugo. Nampongeza Waziri wa Mifugo. *Honestly speaking*, Wizara ya Mifugo sasa hivi ina *a very significant contribution* kwenye uchumi wa Taifa. Mimi natoka kwenye ukanda ambao tuna mifugo wengi sana na nimekuwa nikilisema hili. Kama nilivyosema kwenye suala

la Tume ya Umwagiliaji, Wizara ya Mifugo imekuwa mtoto yatima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia tuna-*deal* na vitu vikubwa; majosho, malisho, sijui chanjo, masoko, mabwawa na kadhalika, lakini yapo ndani ya Wizara kama vi-*unit* tu. *It is a high time* sasa, tunahitaji vilevile kutengeneza *an authority* (mamlaka) ambayo itasimamia Sekta ya Mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Mifugo ni sekta ambayo kimsingi kama tutaitengenezea *a very giant institution*, kama ilivyo *TANESCO, TARURA, LATRA, RUWASA*, nina uhakika mkubwa sana Sekta ya Mifugo ita-*develop* na inaweza ikawa na *a very significant contribution* kwa uchumi huu wa Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niliona niliseme hilo na ninamwona pale daktari, Waziri wa Mifugo. Najua yeye ni Mchumi na Sekta ya Mifugo kimsingi ni ya uchumi *perse*. Kwa hiyo, najua kabisa ataenda kuitendea haki. Hebu tuanzishe hii mamlaka, *then* tuone ni jinsi gani itaenda ku-*transform* Sekta ya Mifugo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, nirudie kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa ambayo ameifanya katika Taifa letu la Tanzania. Sisi watu wa Manyoni tunamwahidi ushindi wa kishindo mwaka huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, ninaunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Pius. Sasa namwita Mheshimiwa Grace Victor Tendega, atafuatiwa na Mheshimiwa Edwin Enosy Swalle, na Mheshimiwa Muharami Shabani Mkenge wajiandae. *(Makofi)*

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa nami niweze kuchangia katika taarifa hizi mbili. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye

ametuwezesha kuwa mahali hapa muda huu, kuweza kufanya kazi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee kabisa napenda kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa anayoifanya kama Amiri Jeshi Mkuu wa nchi hii ya kuhakikisha usalama wa nchi yetu uko sawasawa. Kwa hiyo, napenda nimpongeze kwa kazi hiyo na vyombo vya ulinzi na usalama viko sawa na mipaka yetu yote iko salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee kabisa, nampongeza Mheshimiwa Spika wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa anayoifanya ya kuliongoza Bunge hili, kutuongoza vyema na kuhakikisha kwamba, Kamati zetu zinatoa taarifa ambazo zimefanyiwa kazi. Hongera sana kwa Mheshimiwa Spika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitajikita katika Taarifa ya Wizara ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, hasa katika kipengele kinachohusu biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu. Biashara hii ni kubwa kabisa duniani, ni biashara ya tatu kwa ukubwa duniani. Ninavyosema hivi ninamaanisha kwamba, kuna biashara nyingine, lakini hii ni kubwa sana na ipo. Watanzania wengi hatuelewi kwamba, ni biashara kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii biashara inatokana na mambo gani? Biashara hii inatokana na umaskini, kutokuwa na uelewa wowote, hali ngumu ya maisha na masuala mbalimbali ambayo mtu huna uelewa nayo, itakukuta biashara hii. Hii biashara hasa inawakuta vijana wengi na vijana wetu wengi wamekwenda wakipotea, wakipata adha, wakitumiwa ndivyo sivyo na kuweza kuhatarisha maisha yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukulie mfano, kuna Watanzania wanaolaghaiwa, wanaambiwa kuna kazi nje ya nchi, kazi nzuri kabisa na anakuja anapewa maelekezo kwamba, hiyo kazi itamsaidia. Bila kujitambua, anaweza akauza vitu alivyonavyo

akapata nauli na kwenda kule. Kumbe akifika anaenda kutumikishwa na hatimaye hawezi kurudi nyumbani, anakuwa hana nauli, hana anachoweza kufanya, hana mawasiliano, hana kila kitu. Hii inatokea, na tumeiona kwenye kamati yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, biashara hii inafanyika ndani na nje ya nchi. Kwa ndani ya nchi kuna vijana wanachukuliwa, hata watoto wadogo wanachukuliwa, wanaletwa kwenye maeneo mbalimbali, iwe mijini au maeneo mengine. Wanapoletwa pale wanatumikishwa kazi kwa ujira mdogo sana. Wanapotumikishwa hizo kazi, unafikiri watalipwa kitu kizuri, wanajua wanaenda kupata ujira mzuri, kumbe wanaenda kutumikishwa ndivyo sivyo na yanawakuta madhara makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna watu wenye ulemavu pia, wanaweza wakachukuliwa kutoka ndani au nje ya nchi wakaenda kutumikishwa. Unapoenda labda mtu anaomba, unafikiri unamsaidia, kumbe yule mtu ana watu, maajenti, nyuma ambao ndiyo wanapokea zile fedha baada ya yeye kupata ujira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hii biashara ni kubwa mno na inatesa Watanzania walio wengi. Naipongeza Serikali, hasa chombo cha Sekretarieti ya Kuzuia na Kupambana na Biashara Haramu ya Usafirishaji wa Binadamu, ikishirikiana na vyombo vya ulinzi na usalama. Wameweza kubaini zaidi ya wahanga 1,110 ambao walikutwa na biashara hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya hao, 902 walikutwa kutoka nje ya nchi, 208 kutoka ndani ya nchi na wahalifu 103 wanaofanya hiyo biashara walipatikana. Kwa hiyo, nawapongeza. Pamoja na kufanya kazi yote hiyo, lakini bado biashara hii imeshamiri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naiomba Serikali, pamoja na juhudi kubwa wanazozifanya kwa chombo hiki cha Sekretarieti ya Kuzuia na Kupambana na Biashara Haramu, waweze

kushirikiana vizuri na Wizara ya Mambo ya Ndani kuweza kufanya mambo yafuatayo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, waweze kushirikiana kutoa elimu kwa jamii, watoe elimu kwenye halmashauri zetu, kwenye Wilaya zetu, kwenye vijiji vyetu, kwenye kata zetu na kwa jamii kwa ujumla iweze kujua. Watoe elimu ili wananchi wajue kwamba, kuna madhara kama hayo yanawakuta ili waweze kuwasaidia wananchi. Serikali iweze kutenga fedha za kutosha kuhakikisha chombo hiki kinatoa elimu, na pia wananchi wapate elimu hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaposema chombo hiki kipate fedha za kujiendesha, ni kwa kuwa kinahitaji kujenga eneo maalumu la hawa wahanga kuweza kupata masuala ya unasihi, kufanyiwa *counselling* kwa sababu, mtu akikutwa ametoka huko, anakuwa amechanganyikiwa. Kwa hiyo, hilo ni eneo ambalo wataweza kulijenga kusaidia watu kupunguza mawazo na changamoto zile, ili waweze kujiunga na jamii wakiwa salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni la Wizara ya Ulinzi na Usalama na Jeshi la Kujenga Taifa. Nalipongeza Jeshi letu, limekuwa likifanya kazi kubwa sana kwa weledi mkubwa wa kulinda nchi yetu na mipaka yake, wanafanya kazi kubwa sana. Jeshi letu la Kujenga Taifa wameweza kufanya kazi kubwa ya kuchukua vijana wetu na kwenda kuwapa elimu hiyo ya kujitegemea katika maeneo mbalimbali, japo haitoshelezi, lakini wamekuwa wakifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *SUMA-JKT* inadai mashirika na taasisi za umma na za binafsi shilingi bilioni 40. Pesa hizo ni nyingi sana. Wanashindwa kujiendesha katika mambo na mipango yao ambayo wamejipangia, wanashindwa kutekeleza huduma zao ambazo wameweka ziendelee. Kwa hiyo, deni hili ni kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaiomba Serikali iweze kuchukulia kwa umakini mkubwa kuhakikisha hilo deni linalipwa.

Taasisi hizo zinazodaiwa ziwalipe *SUMA JKT;* na pia asasi za kiraia ambazo zimeikopa *SUMA JKT* zilipe hizo fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni miundombinu chakavu katika magereza na vyombo vyetu vya ulinzi na usalama. Magereza zetu nyingi ni chakavu, na zilizo nyingi zimejengwa miaka 100 iliyopita ambao ni karibu 85%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaiomba Serikali ihakikishe kwamba, katika bajeti zake nyingi zinazotengwa, kuna fedha za kutosha za kuwasaidia ili Jeshi la Magereza waweze kukarabati majengo ili yaendane na wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nashauri kuwe na mifumo ya TEHAMA na kuwe na maeneo ambayo watatolea urekebu. Kwa sababu, sasa hivi tunataka tutoe urekebu, kwa maana wale wafungwa waweze kupata mafunzo ambayo yatawasaidia wakitoka nje ya Magereza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, naishukuru Serikali, kupitia Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, chini ya Jeshi la Uhamiaji kwa udhibiti wa wahamiaji haramu nchi hii. Wameweza kuanzisha programu inayoitwa mjue jirani yako, inayoendana na mazingira husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hii programu imesaidia sana kwa sababu, wahamiaji haramu wamekuwa wakija nchini kwetu, wakijumuika na kuwa kama Watanzania. Kwa hiyo, hiyo ni programu ambayo Mheshimiwa Rais aliisisitiza na Jeshi letu la Uhamiaji limeweza kufanya hivyo. Tunalishukuru limeweza kufanya kazi kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mwisho ni Majeshi ya Polisi na Zimamoto. Tunashukuru Jeshi la Polisi limepata magari, lakini magari hayo hayatoshelezi. Ni magari mazuri, mtawaona wanajeshi wamekuwa katika magari mazuri, lakini pia, wana *uniforms* ambazo zinaridhisha, lakini bado haitoshelezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji lina upungufu wa magari 156, wana upungufu wa maboti 36 na pia, wana uchache wa vituo vya zimamoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, lakini nawapongeza Mawaziri ambao wameweza kufanya kazi yao ipasavyo, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Grace Tendega. Mheshimiwa Edwin Enosy Swalle, atafuatia Mheshimiwa Muharami Shabani Mkenge. Mheshimiwa Mohamed Saidi Issa ajiandae.

**MHE. EDWIN E. SWALLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi jioni hii nami niweze kuchangia taarifa mbili za Kamati ambazo leo zimewasilishwa ndani ya Bunge lako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze na Taarifa ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama. Naungana na Wajumbe wa Kamati hii ya NUU kwanza kumpongeza sana Mwenyekiti wa Kamati ya NUU, Mheshimiwa Vita Rashid Mfaume Kawawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwenyekiti wetu, Mheshimiwa Kawawa anafanya kazi nzuri sana, ni kiongozi makini. Natuma salamu kwa wananchi wa Jimbo la Namtumbo kwamba, tunatamani Mheshimiwa Kawawa aendelee kuwepo ndani ya Bunge lako Tukufu. Sisi tunamwamini sana Mheshimiwa Vita Kawawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya salamu hizo kwa wananchi wa Jimbo la Namtumbo, naomba sasa pia nitumie nafasi hii kuvipongeza vyombo vyetu vya ulinzi na usalama, nikianza na Ofisi ya *DGIS, IGP, CGP, CGF* pia *CDF* kwa kazi nzuri ambazo wanafanya kwa ajili ya ulinzi na usalama wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taifa letu limekuwa na utulivu mkubwa sana, na haya mambo hayatokei kwa bahati mbaya. Tumekuwa na mikutano mingi sana hapa nchini ambayo

imekuwa na wageni wengi mbalimbali kutoka Afrika na nje ya Afrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa na mkutano mkubwa sana mwaka 2003 ambao ni mkutano wa Kilimo na Chakula, ulikuwa na wageni zaidi ya 3,000, hakuna mtu hata mmoja aliyeondoka hapa akiwa na hali mbaya ya kiusalama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tumekuwa na Mkutano mkubwa sana wa Nishati mwaka huu ambao ni *Energy Summit Mission 300* ya mwaka huu. Tumekuwa na wageni wengi na Marais wengi wa Afrika; na wageni wetu wote wameondoka salama Tanzania, kwa sababu ya kazi nzuri ya vyombo vya ulinzi na usalama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tumekuwa na Wajumbe wa Chama cha Mapinduzi zaidi ya 5,000 katika Mkoa wa Dodoma, waliokuja kwa kishindo kumpitisha Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kuwa mgombea wa Urais. Tumeshuhudia Dodoma imekuwa shwari, hakuna aliyepoteza simu wala shati, wameondoka salama. Hongera sana vyombo vya ulinzi na usalama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nitumie nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais, kwa kazi nzuri ya kuimarisha diplomasia ya Kimataifa. Yamesemwa mambo mengi hapa, na wahenga wanasema, mwenye macho haambiwi tazama. Watoto wa mjini pia wanasema kama huwezi kusoma, angalia picha; kama huwezi kuangalia picha, basi unaweza ukanusa hata ukasikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitazama takwimu na heshima ya nchi ambayo sasa dunia wanaitazama, hakuna mashaka kama Mheshimiwa Rais amejenga diplomasia kubwa sana duniani kwa ajili ya Taifa letu. Wale ambao pengine hawafuatilii, ukitazama kwenye sekta ya utalii, kwa mfano kutoka mwaka 2021 Mheshimiwa Rais, amefanikiwa kuongeza watalii kutoka Mataifa mbalimbali, kutoka 922,000 mpaka 2,140,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii maana yake nini? Ni kwamba diplomasia yetu inazidi kuimarika na Taifa letu linazidi kuwa na taswira nzuri duniani. Mheshimiwa Rais, hongera sana kwa kazi nzuri ambayo unaifanya kwa ajili ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nitumie nafasi hii kusema kwamba, kwa wakati huu ambao tunaelekea kwenye uchaguzi na wakati huu ambao nchi yetu itakwenda kuwa na masuala mbalimbali ya kuongeza ulinzi na usalama katika ukanda huu wa Maziwa Makuu, tumeona hapa ndani vyombo vyetu vya Ulinzi na Usalama vimeongezewa magari mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitazama Askari wetu sasa hivi huko barabarani wanayo magari mazuri, wanakaa kwa amani na hii ni kuongeza ulinzi wa raia na mali zao. Mheshimiwa Rais hongera, lakini pia Mawaziri wote; Waziri wa Mambo ya Ndani, Waziri wetu wa Ulinzi na Jeshi la Kujeta Taifa, Waziri wa Mambo ya Nje, hongereni sana kwa kumsaidia Mheshimiwa Rais kwa kazi mbalimbali za Wizara hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine kwenye hii Sekta ya Mambo ya Nje Ulinzi na Usalama, nitumie nafasi hii pia kumshukuru Mheshimiwa Rais, kwani wananchi wangu wa Kata ya Mtwango, Kata ya Kichiwa, Kata ya Igongolo, Ikuna na Ninga walikuwa na kero ya Kituo cha Polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninazo taarifa njema kwamba Mheshimiwa Rais, ametupatia zaidi ya shilingi milioni 250 kuanza ujenzi wa Kituo cha Polisi pale Mtwango, ahsante sana Mheshimiwa Rais. Sasa kata hizi zitakuwa na usalama mwingi kwa wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili naomba niingie kwenye Sekta ya Kilimo kwa maana ya Biashara na Viwanda, Kilimo na Mifugo. Hapa pia namshukuru sana Mheshimiwa Deo Mwanyika, Mbunge wa Njombe Mjini, Kaka yangu, ahsante sana kwa taarifa nzuri. Nasi wananchi, hasa wakulima wa chai, mmetutendea haki sana, ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijikite kwenye ukurasa wa 81 kwenye Taarifa ya Kamati hii ya Biashara na Viwanda, Kilimo na Mifugo. Kuhusu tasnia ya chai nchini, kwanza naunga mkono kwamba zao la chai hapa nchini kama ambavyo taarifa imesema, limeenda likidorora siku hadi siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafahamu zipo kazi na juhudi nzuri ambazo Mheshimiwa Waziri wa Kilimo amezifanya, na ninaungana kabisa na kauli ya Mheshimiwa Dkt. Chaya, aliyesema kama Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Bashe *is very strategic*, *very innovative, very focused,* nami naongeza kusema kuwa Mheshimiwa Bashe *is very bold*, ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, sifa zote hizi unastahili na amefanya kazi nzuri. Kule Lupembe alitoa maelekezo kwamba wananchi wa *AMCOS* ya Lwafi na Ikami waende kwa sehemu ya kiwanda cha kule Kabambe. Nataka nitoe taarifa kwa Mheshimiwa Waziri Bashe, kwamba wananchi wale sasa wameshaingizwa rasmi kwenye huu mradi na wanaanza kupata pembejeo na mafunzo ya ugani. Mheshimiwa Bashe, Waziri wa Kilimo, ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, Mheshimiwa Waziri, alitoa maelekezo ya msingi sana kwamba kile kiwanda cha wananchi wa Lupembe kirejeshwe kwa wakulima wa Lupembe. Uamuzi ule ulienda vizuri, uhakiki ukafanyika, lakini mpaka leo kile kiwanda hatujajua nini kimekwamisha kurejeshwa rasmi kwa wananchi wa Lupembe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Lupembe wamenituma kwamba, pamoja na kazi nzuri ambayo Mheshimiwa Waziri anaifanya, kwa sababu kila alikoenda kwenye zao la korosho, kwenye zao la pamba umetatua na changamoto zile, na zimeenda zikiisha, wanaomba baada ya Bunge hili afike Lupembe kuona kazi nzuri ambayo ameanza kuifanya aikamilishe, chai ipate soko zuri hapa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, namwomba sana Mheshimiwa Waziri, wale watu wa kampuni ya *LIPTON* au *NOSCI* ambao wamekuwa msaada mkubwa kwa wakulima wa chai Lupembe, licha kwamba chai sasa hivi inachukuliwa kwa mgao ndani ya wiki mara mbili mbili, hawa ni wadau muhimu sana. Mwaka 2024 wamesaidia kulipia wakulima *certificate* ya Kilimo ili wakauze mazao yao ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tena zipo kata kadhaa, kata kama ya Lupembe, Matembwe, na Ukalawa. Hawa wote watahitaji tena kufanyiwa *certification* kwa ajili ya mazao yao. Naiomba Serikali, kwa sababu huyu ni mdau, anasaidia wakulima, apewe ushirikiano akomboe wananchi wa Lupembe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri, kwa sifa alizonazo na uwezo alionao, wananchi wa Lupembe wanachuma chai, lakini wanaelekea kukata tamaa. Tusipochukua hatua, zao hili linaweza kwenda kufa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naunga mkono kwamba vile viwanda kama vya Ikanga, Kiwanda cha Kibena ambacho *DL* ameshindwa kukiendesha, Serikali ichukue hatua viwanda hivi, vichukuliwe wapate wawekezaji wengine ili wawasaidie wakulima wetu wa chai Mkoa wa Njombe na nchi yetu kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo, Mheshimiwa Waziri nashukuru sana, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Edwin Enosy Swalle, ahsante sana. Mheshimiwa Muharami Shabani Mkenge, atafuatiwa na Mheshimiwa Mohamed Said Issa na Mheshimiwa Samweli Xaday Hhayuma, ajiandae.

**MHE. MUHARAMI S. MKENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kupata nafasi hii kuchangia taarifa ya Kamati zetu hizi mbili ambazo zimewasilishwa hii leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda nichukue nafasi hii kutoa pongezi nyingi sana kwa Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa ambayo anaifanya. Pia napenda kuchukua nafasi hii nimpongeze kwa kuchaguliwa na Mkutano Mkuu wa Chama cha Mapinduzi kuwa mgombea wa kuipeperusha bendera ya Chama cha Mapinduzi katika uchaguzi wa mwaka huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Dkt. Emmanuel Nchimbi, kwa kuteuliwa kuwa mgombea mwenza katika safari moja na Mheshimiwa Rais. Vilevile sitasahau kumpongeza Mheshimiwa Makamu Mwenyekiti, ndugu yetu Mheshimiwa Wasira naye kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Chama chetu Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii kutoa pongezi kwa vyombo vyetu vya Ulinzi na Usalama. Vyombo vyetu vya Ulinzi na Usalama vinafanya kazi kubwa ya kulinda nchi yetu, tunaona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda vilevile nimpongeze Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuendelea kuitunza amani ya nchi yetu Tanzania, pamoja na kujitahidi kuhakikisha kwamba majirani zetu nao wanakuwa na amani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni anaendelea kupambana kuhakikisha kwamba amani ya Congo inapatikana kwa kuitisha mikutano na viongozi wenzake ili hali ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo iweze kuimarika. Tunampongeza sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile naomba nilipongeze Jeshi letu la Polisi kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya. Kwa kweli nchi imetulia, watu na mali zao wametulia kwa sababu Jeshi letu linafanya kazi usiku na mchana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na changamoto nyingi ambazo zimejitokeza, changamoto za vifaa ni ukweli usiopingika, Polisi wanafanya kazi kubwa, lakini vifaa ni vichache. Kwa hiyo, tunaiomba Serikali walitupie macho Jeshi la Polisi kwa ajili ya vifaa vitakavyowawezesha kufanya kazi zao kwa weledi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi la Polisi linajitahidi, linakusanya fedha za tuzo na tozo, tunaona vituo vya Polisi vinajengwa, kwa kweli wanajitahidi sana, lazima tuwape maua yao. Ni kazi nzuri ambayo wanaifanyia nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudi katika hali ya usalama. Jeshi la Polisi na hasa usalama wa barabarani, ni kweli ajali nyingi za barabarani zimeendelea kupungua siku hadi siku kutokana na kazi kubwa ambayo Jeshi la Polisi linaifanya, lakini bado Serikali ina jukumu kubwa sana la kulisaidia jeshi hili kupata vifaa kuachana na Habari ya *traffic* ambao wengi wanakaa barabarani na hatimaye wanapata kashifa nyingi kwa ajili ya kuchukua chochote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watafute vifaa, kwa mfano sasa hivi kuna changamoto kubwa barabarani huko, watu wana-*overtake* ovyo, lakini kama wangekuwa na *camera* sehemu zote za barabara ingesaidia sana Polisi hawa kupata nafuu katika ufanyaji wa kazi zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo nataka kuligusia ni bodaboda. Unatambua kuwa zaidi ya 60% katika nchi yetu usafiri wa bodaboda unategemewa sana na watu, lakini bodaboda hawa wanaishi katika mazingira ambayo siyo sahihi. Bodaboda hawa hawatambuliki. Tunaiomba Serikali ianzishe mfumo maalumu sasa hivi wa kuwatambua bodaboda kwa ajili ya usalama wao pamoja na usalama wa abiria ambao wanawachukua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii bodaboda anaweza akatokea kituoni hajulikani, akafika pale akafanya jambo lolote la kihalifu, akawaponza bodaboda wenzake, wakaingia katika

matatatizo kwa sababu tu hakuna utambuzi sahihi katika hivi vituo vya bodaboda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Jeshi la Polisi pamoja na Serikali ihakikishe kwamba bodaboda wanapata utambuzi ili waweze kufanya kazi zao vizuri kwa sababu ni watu ambao ni wengi sana katika nchi yetu, wanatusaidia sana sisi wengine katika suala zima la usafiri mijini pamoja vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kidogo suala moja ambalo amezungumzia mjumbe mwenzangu kuhusu deni ambalo SUMA JKT wanadai. Mheshimiwa Mjumbe mwenzagu aliyepita alizungumza kwamba SUMA JKT wanadai zaidi ya shilingi bilioni 40 katika taasisi mbalimbali, katika Mawizara. Hebu Taasisi na Wizara zilipe SUMA JKT hizi shilingi bilioni 40 ili mipango yao iweze kuendelea vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii katika taarifa yao, SUMA JKT wamekwama kuanzisha kiwanda cha kutengeneza madawa, kutengeneza vifaatiba pamoja na kutengeneza mbolea kwa sababu tu hawana fedha. Kama wangelipwa hizi shilingi bilioni 40, mimi nafikiri kiwanda hiki kingeanzishwa vilevile na vijana wetu wengi wangepata ajira katika hii taasisi yetu ya SUMA JKT.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli naomba niwasihi sana, Serikali pamoja na Wizara wajitahidi hata katika bajeti ya mwaka ujao, walipe hizi fedha ili SUMA JKT iweze kuwaajiri vijana wetu waweze kupata kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nichukue nafasi hii pia kulipongeza Jeshi letu la Zimamoto kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya. Kama unavyojua, Jeshi hili bado lina tatizo la vifaa, lakini juzi juzi, mnakumbuka Dar es Salaam umetokea moto, baada ya kupatikana gari refu la kuzima moto juu ya magorofa, Jeshi la Zimamoto limeweza kudhibiti moto ambao ungeweza kuharibu gorofa zima lile. Kwa hiyo, tunaomba vifaa hivi viweze kununuliwa kwa wingi ili jeshi letu liweze kufanya kazi zake kwa weledi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa taarifa, tunaambiwa kuna karibu vituo vya Zimamoto 157 nchini bado havina vifaa vya kutosha. Kwa hiyo tunaiomba Serikali iangalie kwa umakini, kutokana na vifaa hivi vya Jeshi la Zimamoto, wawape vifaa madhubuti ili waweze kuzima moto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza sana wanakamati wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama pamoja na Mwenyekiti kwa taarifa nzuri, na niwapongeze sana Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo, Biashara na Viwanda kwa taarifa yao nzuri. Kazi ni nzuri ambayo wanaifanya Wenyeviti wetu pamoja na Wajumbe wa hizi Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache, nakushukuru sana, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mkenge. Mheshimiwa Mohamed Said Issa, atafuatiwa na Mheshimiwa Samweli Xaday Hhayuma na Mheshimiwa Sophia Mwakagenda ajiandae.

**MHE. MOHAMED SAID ISSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uhai na uzima na kusimama kwenye Bunge lako Tuku hili. Pia nakushukuru wewe kwa kunipa nafasi ili nami niweze kutoa mchango wangu katika taarifa za Kamati hizi mbili ambazo zimewasilishwa leo asubuhi mapema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze mchango wangu kwenye Wizara ya Viwanda. Kwanza naipongeza kazi nzuri wanayofanya *TRA* katika ukusanyaji wa mapato. Tumeona kwamba kila wakati mapato yamekuwa yakiongezeka. Nampongeza sana Mkurugenzi Mkuu au *DG* wa *TRA* kwa mbinu ambazo anakuja nazo, ambazo siyo za kulazimisha, lakini kodi inaongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na yote hayo, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Viwanda, Biashara, Kilimo, Uvuvi na Mifugo na nilibahatika kutembea katika sehemu mbalimbali.

Tulitembelea kule Horohoro Tanga, tumekuta utendaji kazi siyo mzuri kutokana na kazi nyingi ambazo zinafanywa *manually*. Tuliona hamna *scanner* pale, na Horohoro ni mpaka mkubwa sana. Sasa tukaona kuna mambo mengi ambayo yanadumaza uchumi wetu pamoja na ukosefu wa mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili kwanza ni hatarishi kiusalama kwa sababu wale ambao wanakagua, hatujui kama ni waaminifu kiasi gani, lakini pili linatukosesha mapato kutokana na mambo ambayo yanaweza kufichwa pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo mipaka mikubwa 18, lakini mipaka ambayo ina *scanner* hizi kubwa ni mipaka mitano tu ambazo ni zile bandari zetu. Pia kuna *scanner* hizi ndogo ndogo ambazo wanapitia abiria, pia nazo ni tatizo. Sehemu kubwa ambazo zinahitaji *scanner* kubwa na ndogo, hamna nchini. Kwa hiyo, jambo hili lilitakiwa lipewe upeo wa hali ya juu kwa sababu linadumaza uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kutokuwepo kwa *scanner,* baadhi ya sehemu ni bugudha kwa wananchi. Nitoe mfano, siku moja niliuliza swali hapa kwa Wizara ya Uchukuzi kuhusu suala la ukaguzi wa mbwa kuwa ni wa kawaida pale bandarini Dar es Salaam; kutoka Dar es Salaam kwenda Zanzibar. Nilijibiwa vizuri tu na Mheshimiwa Waziri, na akatoa agizo kwamba ukaguzi ule unatumika pale ambapo utahitajika, lakini ukaguzi mwengine ndiyo unatakiwa kufanywa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kusikitisha, watendaji wa bandarini pale Dar es Salaam wamekuwa wakilazimisha kukagua kwa mbwa. Sasa Mheshimiwa Waziri nataka atoe pia tamko, kwa nini katika jambo hili, Bunge linadharauliwa? Kwa nini Maazimio ya Bunge yanadharauliwa? Mbwa wale wanaendelea kubughudhi watu, wananusa chakula, wananusa nguo za ibada na watu wanashindwa kufanya ibada siku nzima. Huo ulikuwa ni mchango wangu wa kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, niende kwenye upungufu wa sukari. Mwaka 2024 tulikuwa na upungufu wa sukari na tulipata shida kubwa sana, na ilisababisha kutungwa sheria hapa, ili kuwapa mamlaka *NFRA* kuweza ku-*control* upungufu wa sukari. Jambo hili mimi sitaki nilizungumze kwa ukubwa sana, lakini napenda kutoa angalizo kwa Waziri wa Kilimo kwamba jambo hili liliichafua nchi, ilifikia mahali wananchi wakanunua sukari kwa kilo moja shilingi 10,000/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mambo tuliyoyachukua, muda unakaribia huu, tunapofika mwezi Mei, Juni na Julai viwanda vitafungwa. Uzalishaji wa sukari kwenye viwanda vyetu bado hautoshelezi. Maana yake ni nini? Tutahitajika kuwa na sukari ya ziada. Kwa hiyo, tusije tukaona kwamba sukari tena imepungua, tujiandae mapema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na yote, Mheshimiwa Waziri wa Kilimo alisema kwamba kutakuwa na bei elekezi. Bei hizi elekezi wanazijua wafanyabiashara tu, wananchi hawazijui. Tunaomba Wizara hii iweke wazi ili wananchi wajue bei elekezi, kwamba anakwenda kununua sukari dukani kiasi hiki. Siyo muuzaji tu, kwa sababu wauzaji kule wanaweza wakauza na mwananchi akaona kuwa ni sawa. Hii iwe *public,* watu wote wafahamu kwamba bei elekezi ni hii, ndipo italeta tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee na suala la upungufu wa fedha za kigeni. Kumekuwa na upungufu mkubwa wa fedha za kigeni. Katika jambo hili ningependa hasa huyu Mheshimiwa Waziri wa Fedha ajibu ni kwa nini fedha za kigeni zilishuka kwa muda wa wiki moja na zikapanda kwa muda wa wiki moja? Ni uchumi wa aina gani huu? Maana jambo hili sijui hata lilitokeaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi katika maisha yangu sijawahi kuona, lakini sijui ni *terminology* gani tunaweza tukau-*term* huu uchumi wa namna hii, kwamba wiki moja ilishuka kutoka 2,800 mpaka 2,360, lakini wiki moja ikapanda mpaka 2,600. Jambo hili linakuwaje? Nini kilitokea? Vyombo vya ulinzi na usalama vinatakiwa kuchunguza jambo hili, kwani suala hili siyo la kawaida.

Hadi sasa hivi fedha za kigeni ukienda benki unakuta umeandikiwa bei za ununuzi na uuzaji, lakini hakuna. Kwa nini? Waziri wa Biashara hapo anaweza kutueleza ni kwa nini hakuna?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine nije kwenye suala la mifugo. Kwanza naipongeza Serikali kwa kuweka mkazo kwenye suala la chanjo. Jambo hili ni zuri na litatusaidia kupata fedha za kigeni kwa kuwa tutauza nyama yetu nje. Tunajua kwamba nyama haiuzwi nje. Wananchi huwa wanakataa kuchanjwa mifugo yao kwa sababu ya elimu, lakini siyo elimu tu, hata watendaji wetu wanaochanja kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa tukisikiliza wadau mbalimbali; mtu unakwenda kuchanja mfugo ambao tayari ulishaathirika na magonjwa. Maana yake ni kwamba unauongezea dozi na hivyo unakwenda kufa. Mwananchi hatakubali. Au mfugo ambao una mimba, ule hauwezi tena kuendelea. Matokeo yake wananchi wanaona kwamba chanjo hizi ni shida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi ombi langu kama Mjumbe wa Kamati ni kwamba Serikali iende hatua kwa hatua kwenye kutekeleza jambo hili, wasikurupuke tu kwamba yoyote tu achanjwe lende na elimu nzuri ya kuwasaidia wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni kuhusiana na uvuvi haramu. Tumezungumza kwenye Ripoti ya Kamati hapa. Suala la uvuvi haramu Serikali ijikite kuuzuia kwenye *deep sea.* Tumeelezea kwa upande wa Zanzibar, Serikali inashirikisha vyombo vya KMKM, Kikosi cha Kuzuia Magendo pamoja na *Navy* lakini pamoja na Uchumi wa Bluu. Hili ni jambo zuri kwa sababu Serikali ni moja, ni Serikali ya Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule kwetu Zanzibar hili jambo halikueleweka. Mimi jimboni kwangu asilimia kubwa ni wavuvi, ni bahari, lakini jambo la kushangaza ni kwamba, wananchi ambao miaka nenda miaka rudi wanavua katika uvuvi wa kawaida, wamezuiwa kuvua sasa hivi, na hivyo hawana kazi. Hatujui kazi

gani za kufanya. Halafu CCM wanatafuta kura kule, watazipata wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule kwetu hawawezi kupata kura kwa sababu huu uchumi ambao wanatuletea siyo rafiki. Wao wakiwa na nia ya kupata kura, labda waje watupige bakora, lakini kura kule kwetu Jimbo la Konde na Pemba yote CCM hawana kura kwa sababu hii.

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. MOHAMED SAID ISSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *otherwise,* waweze kujisahihisha. Acheni, tulieni, sisi tunaendelea.

**MWENYEKITI:** Taarifa, Mheshimiwa Asha.

**TAARIFA**

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba nimfahamishe msemaji kwamba kura tutapata, tena za kishindo. *(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mohamed Said Issa, unakubali na unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. MOHAMED SAID ISSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa yake siipokei, na huyu Mheshimiwa ni mama yangu, lakini huo ndiyo ukweli. Ni kwamba kule sera zao CCM ni mbovu. Kwa hiyo, hawatapata kura. Waniache niendelee, *otherwise,* wabadilishe sera. Wakibadilisha sera hizi za kuwashirikisha wananchi, kwa sababu tunajua kwamba kwenye huu uvuvi nyavu zinanunuliwa wapi na wapi; mishipi, na uvuvi ni ule ule wa kawaida.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. MOHAMED SAID ISSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naomba dakika moja nizungumze kuhusu vitambulisho vya *NIDA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vitambulisho vya *NIDA* vimekuwa ni shida, na vinasababisha watoto wetu ambao wanataka kupata mikopo ya elimu ya juu kushindwa kuvipata. Sasa jambo hili ni la kuwekewa mkazo. Hili ni tatizo lingine ambalo pia litasababisha matatizo kwenye uchaguzi wetu. Kwa sababu kule Zanzibar, hii Tume ya Uchaguzi inatumia vitambulisho hivi, lakini kwa kumpa Mamlaka Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar. Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar yenyewe haijitambui, inatoa vitambulisho. Kule Jimboni kwangu vitambulisho vya Tume ya Uchaguzi zaidi ya 380 havisomi kwenye mfumo. Sasa ni Tume ya Serikali hiyo au Tume tu ni kikundi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, jambo hili Serikali ya Muungano imekasimu…

**MHE. RASHID ABDALLA RASHID:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. MOHAMED SAID ISSA:** …madaraka yake kwa Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar inaharibu kabisa uchaguzi wetu wa Zanzibar.

**MHE. RASHID ABDALLA RASHID:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. MOHAMED SAID ISSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi *ACT* tumejipanga kushinda uchaguzi huu, lakini kwa ghiliba hii itakuwa na shida.

**MHE. RASHID ABDALLA RASHID:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa, Mheshimiwa Rashid.

**TAARIFA**

**MHE. RASHID ABDALLA RASHID:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa kwamba Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar ni

Tume inayojitambua, ina wafanyakazi weledi, watendaji weledi. Kwa hiyo, naomba achukue taarifa hiyo kwamba Tume inajitambua. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mohamed Said unakubaliana na taarifa?

**MHE. MOHAMED SAID ISSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sikubaliani na taarifa. Mimi nimetoa *data,* na akitaka twende nimkusanyie watu hao ambao vitambulisho vyao havijasoma kwenye mfumo. Kwa hiyo, ile Tume haiwezi kufanya kazi zake kwa weledi…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Muda wako umeisha. Nakushukuru sana kwa kuchangia. Ahsante sana, Mheshimiwa.

Sasa namwita Mheshimiwa Samweli Xaday Hhayuma, atafuatiwa na Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, na Mheshimiwa Francis Isack Mtinga, ajiande.

**MHE. SAMWELI X. HHAYUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia kwenye taarifa za Kamati zetu mbili. Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama na Kamati ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nianze kwa kupongeza Kamati zote mbili kwa jinsi ambavyo wanasimamia Wizara za kisekta na Wizara zinafanya kazi nzuri kwa sababu ya kazi nzuri ambayo Kamati zetu zinafanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni mara yangu ya kwanza ninasimama hapa Bungeni baada ya kuwa uteuzi umefanyika wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kuwa Mgombea wa nafasi ya Urais kupitia Chama cha Mapinduzi kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; na Mheshimiwa Dkt. Emmanuel Nchimbi

kuwa Mgombea Mwenza, pamoja lakini Mheshimiwa Dkt. Mwinyi kuwa mgombea kwa nafasi ya Urais wa Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza wote kwa sababu hili ni zao la kazi nzuri ambayo imekwishakufanyika. Tunaposema kazi iendelee, na kazi kweli inaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kutoa mfano, kwenye eneo la kilimo wakati Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan anashika nchi, bajeti ya kilimo ilikuwa shilingi bilioni 294. Tunapoongea sasa kwa bajeti tunayoitekeleza ni shilingi bilioni 1,248 na kuendelea. Hii ni kazi kubwa; na matokeo tunayaona kwenye ruzuku za mbolea na mbegu, ambako tunatarajia, kwa sababu mwaka huu tulianza kwenye upande wa mbegu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ilikuwepo kidogo, wakulima walikuwa wanalalamika, kwa maana ya upatikanaji na usajili wa wakulima na usajili wa wasambazaji. Ninaamini tunavyoenda kwenye 2025/2026, msimu huo maandalizi yatafanyika ya kina na watu watapata mbegu kwa wakati, watapata mbolea kwa wakati, na kazi hiyo itaenda vizuri na uzalishaji utaendelea kuongezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunavyosema sasa, kwamba uzalishaji wa mahindi umeongezeka kutoka tani milioni 6,000,000 mpaka milioni 11,000,000. Ninaamini baada ya muda tutahakikisha kwamba Afrika yote, sisi ndio tutakaokuwa wazalishaji wakubwa wa mazao yanayolisha wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi wananchi wa Hanang' ni wakulima wakubwa wa mahindi, na tumepata soko la uhakika pale *NFRA* Babati. Namshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, namshukuru Mheshimiwa Bashe, ametutengenezea mazingira angalau tunajidai. pale ambapo tunakwama, tunapata fedha za kutosha. Hii ni kazi nzuri ya uwekezaji kwenye sekta ya kilimo na ni mambo mazuri ambayo yanafanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo, nigusie kidogo kwenye Taarifa yetu ya Kamati. Kamati kwenye taarifa yake kwenye eneo la mtazamo na maoni ya jumla, waligusia eneo la chai, kwamba kuna wawekezaji wamechukua mashamba makubwa pamoja na viwanda, lakini utekelezaji na ufanisi wao ni mdogo. Jambo hili halipo kwenye chai pekee yake, lipo mpaka kwenye ngano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Hanang' tunao wawekezaji ambao wamewekeza kwenye mashamba makubwa. Tunao wawekezaji wawili pale. Mmoja *HLH,* anafanya kazi vizuri, na ufanisi wake ni takribani 85% na kuendelea. Pia tunao rafiki zetu wa *Ngano Limited,* ufanisi wao ni mdogo kupitiliza. Kwa sasa mashamba wameyaacha, wananchi wamelima. Wamelima kwa sababu hawakuwa na matumaini kama wao wanaweza kulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu hawa kwa miaka yote waliyokaa na hayo mashamba hawajawahi kutoa *cess* yoyote kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Hanang'. Wananchi wamelima. Ninachoomba, Serikali iwalinde hawa wananchi waliolima ili wavune mazao yao iwe sehemu ya *cess.* Nina hakika baada ya wananchi hao kuvuna, wakilima dengu Serikali itapata *cess* na tutajenga vituo vya afya, zahanati na madarasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mahindi vivyo hivyo, hawa wananchi wakalindwe ili kuhakikisha kwamba mwakani iwe ni changamoto kwa mwekezaji, ili aanze kulima kwa ufanisi. Akilima mashamba yake yote, Wanahanang' wala hawana shida naye, ni rafiki yao, wanampenda. Ila wakilaza, ni kawaida tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wewe kama nyumbani zipo familia mbili, moja watoto wanakula wanashiba, familia nyingine ina njaa; ule familia yenye njaa, ikiona chakula huku, lazima wataanza kuhemea. Wana-Hanang' wamehemea yale mashamba kwa sababu hao hawalimi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba wale Wana-Hanang' waliohemea yale mashamba walindwe. Uwekezaji walioufanya

ulindwe ili mwakani nao wawe makini, walime yale mashamba kwa ufanisi unaotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka kuongelea ni jambo la Stakabadhi Ghalani. Hili jambo nimeongea na Mheshimiwa Bashe mara nyingi sana. Siyo kwamba mimi ni mpinzani wa Stakabadhi Ghalani. Stakabadhi Ghalani mimi ni muumuni wake na nilitoa elimu kubwa sana kwa wananchi wangu. Mimi baada ya kumaliza Kidato cha Nne kazi niliyoifanya ni kilimo na biashara ya mazao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wanahanang wengi wanafanya biashara ya mazao na biashara ya mifugo. Hatupendi mnavyotuita sisi madalali. Sisi ni wafanyabiashara wa mazao, mtuite hivy, mtuheshimu hivyo. Hatupendi mtuite sisi madalali wa mifugo, kwa sababu mifugo tumekuwanayo, tumeishinayo. Mtuite wafanyabiashara wa mifugo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachotaka, kazi inayofanywa na Mamlaka ya Udhibiti wa Nafaka na Mazao Mchanganyiko wajengewe uwezo, wapewe rasilimali, wafanye kazi vizuri. Kazi inayofanywa na Bodi ya Stakabadhi, Ghalani wajengewe uwezo wafanye kazi zao vizuri. Kazi inayofanywa na soko la bidhaa Tanzania, wajengewe uwezo ili wafanye kazi zao vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninao mwongozo hapa, nimeshamwonyesha Mheshimiwa Waziri. Mimi na yeye tumeongea mara nyingi sana. Nampenda yeye kwa sababu ni muwazi, anaongea ukweli na anawapenda wakulima wa Tanzania, lakini nikianza kusoma kuanzia ukurasa wa saba hadi ukurasa wa 23, wakulima na wafanyabiashara wa kawaida wa mazao wamepigwa pembeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye ukurasa wa sita hapa wamesema wakusanyaji wa mazao *(aggregators),* wakulima wakubwa, baada ya hapo wanatuambia kwamba kuna kiambatisho namba moja. Yaani sisi wakulima wa Tanzania ni watu wa viambatisho kweli! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara nyingi Mheshimiwa Waziri wa Kilimo amesema kuwa sekta hii ya kilimo ni ya watu binafsi. Tunakwenda shambani, hatulazimishwi; tunakwenda kulima wenyewe mbaazi, tunakwenda kulima wenyewe choroko, tunakwenda kulima wenyewe dengu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakulima wa Hanang' wananiambia, kwa sasa tukalime dengu au tusilime? Tunatakiwa tuwahamasishe wakalime. Awape utaratibu wakulima wa Hanang' kwamba wakivuna, je, tutakuwa na kila geti kama ilivyokuwa mwaka 2024? Kwenye mchanganuo huu wa bei kuna gharama za usimamizi wa mkoa…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, muda wako umekwisha, tafadhali.

**MHE. SAMWELI X. HHAYUMA:** …gharama ya usimamizi wa Wilaya, kwenye kilimo, *control* zote za nini? Tunaenda kulima wenyewe kwa hiari.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa.

**MHE. SAMWELI X. HHAYUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba hili liangaliwe, liwekwe sawasawa ili angalau wakulima wakafanye kazi zao kwa ufanisi, tusifanye kazi kwa kulazimishwa, na mambo yaende na tupate mapato ya Serikali kama ilivyotakiwa. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Samweli Xaday Hhayuma. Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, atafuatiwa na Mheshimiwa Francis Isack Mtinga, Mheshimiwa Felista Njau ajiandae. *(Makofi)*

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Nitazungumzia kidogo tu mambo yanayohusu kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni ya Kamati kuhusiana na zao la chai ni maoni ambayo yapo *very clear,* yanaeleza jinsi gani wawekezaji wameweza kununua mashamba makubwa na kuyatelekeza bila kuyafanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri tabia hii siyo njema kwa sababu kama mwekezaji alifikiri anaweza akaifanya biashara, amefanya utafiti wa kina kwa ajili ya kufanya biashara ya chai. Anaposhindwa, ninaamini Mheshimiwa Bashe, kama wenzangu walivyomsifia, ni mtu makini, ni mtu anayesikiliza. Basi wangerudisha kwenye Wizara na kusema tumeshindwa kuendelea na zao la chai, tunaomba tupate mwekezaji mwingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 31 Mei, mwaka 2024 Mheshimiwa Bashe alituita wadau wa chai wote, akatoa angalizo na akatoa onyo kwamba kiwanda cha Chai cha *ROTCO* kilichopo Rungwe kisifungwe mpaka ambapo wananchi watakaa kwa muda na kuhakikisha wale watu wameandaliwa; maana chai zinachumwa kila siku, lakini mwekezaji huyu akaendelea kufunga kiwanda. Leo hii tunaongea mashamba yale yamefungwa, wafanyakazi zaidi ya 300 hawana kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninavyofahamu, ni kweli kwamba tunatakiwa kuwa na mazingira mazuri kwa wawekezaji, ni lazima tuwalinde wawekezaji, lakini mwisho wa siku lazima tuwalinde wananchi ambao chai hii wameilima tangu sisi tukiwa wadogo mpaka sasa tumekuwa wazee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba, Mheshimiwa Bashe ni mtu mwema sana na wamemsifia, na katika maeneo mengi amefanya kazi nzuri sana, lakini kwa suala la Rungwe naomba aje mwenyewe, asitume mtu. Aje yeye mwenyewe. Mimi kila siku nagombana naye, ninamshirikisha anatuma Tume, anatuma Bodi. Bodi inakwenda pale, sijui inakuwaje wanarudi na mambo bado yanakwama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafahamu kwamba anajua namna ya kuwalinda wawekezaji, kwa sababu ni ukweli kwamba tunaruhusu wawezaji waje na watusaidie. Basi kama ni hivyo, huu uwekezaji ameshindwa, tunaomba watuletee wawekezaji wengine ili wananchi wale waendelee kuuza chai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo mashamba ya chai yamekuwa na nyasi. Leo hii ukienda ile njia ya Bujela kuelekea Masukulu chai imekufa, viwanja vimekufa kabisa. Kulikuwa kuna nyumba pale, zimekwisha kabisa. Ina maana ajira ya Wana-Rungwe pale haipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Bodi ya Mheshimiwa Bashe iende. Naomba Naibu Waziri aende, wasitume mtu mwingine kufika pale zaidi ya wao watu wawili. Najua maeneo mengine amemaliza, lakini kwetu bado hajamaliza. Tunaomba suala la chai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala parachichi limekuwa ni kilio cha kila siku ambacho tunazungumza hapa. Mwenzangu wa Lupembe ametoka kuzungumza hapa. Tunaiita dhahabu ya kijani. Ni kweli tumetoka kwenye mafungo ya 100 zote sasa hivi tunakwenda angalau kwa shilingi 1,800/= hadi shilingi 2,000/= kwa kilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshauri asiziachie halmashauri zipange bei, kwa sababu halmashauri zikipanga bei Halmashauri ya Njombe inapanga bei ya chini, halmashauri nyingine inapanga bei nyingine. Naomba aunde Bodi ya zao hili, kwa sababu zao hili ni la kimkakati kwa sasa. Basi ahakikishe kwamba Wizara inatoa mapendekezo ya bei zinazofanana, labda itafanya madalali wanunue maparachichi kote na kutokununua sehemu nyingine na kukimbia kwingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii wananchi wanalalamika kwamba wanunuzi wachache ndio wanaoenda kununua wengine hawajanunua. Ni kweli amefanyia kazi siku mbili hizi, lakini wiki mbili za nyuma zilizopita parachichi zimeoza. Wanunuzi walikuwa hawaendi, ni KUZA peke yake alikuwa anaenda, naye

anafanya masharti. Anataka mkulima atoe parachichi shambani, ampelekee kiwandani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna kata 29, ni mkulima gani ana uwezo wa kubeba tani tano au sita kwenda kumpelekea kiwandani? Nashukuru hilo amelifanyia kazi siku mbili hizi, lakini kwa msimu unaokuja namwomba Mheshimiwa Waziri, kila mnunuzi afuate zao shambani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, wale ambao hawajaja kununua bila kutoa taarifa wachukuliwe hatua. Kama waliona parachichi zitakuwa bei, na wao haiwalipi, nafahamu kwamba nao ni wafanyabiashara, lakini kwa nini hawajatoa taarifa kwamba hatutanunua msimu huu ili Wizara iweze kutafuta *alternative* nyingine?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wanaumia. Naomba Mheshimiwa Waziri mwenyewe ndio aje. Ninaamini Waziri akija na akaongea na wakulima wote, akaweka kikao nao bila kupitia watu wa Katikati, atakuwa amewasaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala la madalali. Madalali wamekuwa ni watu wabaya sana wanaopita katikati. Tunaomba kabisa wale wawekezaji au wanunuzi waje wenyewe na wala sio madalali. Dalali anakuja shambani anasema, '*reject*'. Kwenye tani moja, nusu tani ni *reject,* kwa macho yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafahamu kuna Maafisa Ugani wanajitahidi, kwani juzi wameweza kukamata hata mizani ambayo siyo mizuri. Kwa hilo, nawapongeza, lakini naomba msimu ujao tujipange kama timu, tuhakikishe tunawasaidia wananchi hawa waweze kupatiwa kile wanachohitaji, kwa sababu mwisho wa siku mkulima analima na anapanda mwenyewe, basi apate kile kidogo anachokipata kwa haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina mengi ya kusema zaidi ya hayo, ninaamini Mheshimiwa Bashe atasimamia hilo na atafika sehemu husika ili kuweza kuwasaidia ndugu zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba alisimamie hili na ninaamini atalifanyia kazi, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Sophia Mwakagenda. Hayupo, namwita Mheshimiwa Francis Isack Mtinga, atafuatiwa na Mheshimiwa Felista Njau, na Mheshimiwa Vedastus Manyinyi Mathayo ajiandae.

**MHE. FRANCIS I. MTINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia katika Kamati yangu ya Kilimo, Biashara, Viwanda na Uvuvi. Unajua hii sekta inabeba kila kitu mpaka unashindwa hata uanzie wapi kwa sababu inabeba uchumi wa nchi na maisha ya wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze pia kwa kumpongeza sana Rais wangu kwa kuteuliwa tena na Chama hiki kuwa Rais atakayetuongoza tena katika miaka mitano. Ninaamini aliyoyafanya katika miaka mitano hii, basi nchi hii inaenda kuwa ya asali na maziwa katika miaka mitano mingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, nampongeza sana Dkt. Emmanuel Nchimbi kwa kuteuliwa kuwa mgombea kwa maana ya Makamu wa Rais wa nchi hii na pia Rais wa Zanzibar kuendelea tena kushika bendera ya kukiongoza chama chetu kwa Urais wa Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye kilimo, nitagusa jambo la watumishi. Umesikia Wabunge wengi hapa wanalalamika kuna vitu kama vituo vya kilimo vimebadilishiwa matumizi na mambo mengi hayaendi. Hii ni kwa sababu hatuna watumishi wa kutosha wa kilimo. Kama tungekuwa tuna watumishi wa kutosha, nina hakika hata hivi vituo vyetu visingechukuliwa kwa sababu wangekuwepo wafanyakazi wa kutosha ambao wangehakikisha kwamba hivi vituo vinafanya kazi. Serikali yetu inapambana sana na suala la watumishi. Kupanga ni kuchagua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba waalimu ni muhimu sana…

**MWENYEKITI:** Samahani Mheshimiwa Mtinga, subiri kidogo.

Waheshimiwa Wabunge, upande wangu wa kushoto kuna kelele sana. Samahani kidogo Mheshimiwa, endelea.

**MHE. FRANCIS I. MTINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kupanga ni kuchagua. Ajira katika nchi yetu bado ni tatizo sehemu nyingi, lakini tunaishukuru Serikali inajitahidi sana kwa walimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwenye kilimo, kwanza ndiyo mwajiri mkuu wa nchi, lakini pia kilimo ndiyo kinasababisha tuweze kuishi kwa sababu ya chakula. Ni kweli Serikali inaweza kuwa inahangaika sana kwenye shule moja ndani ya Kijiji, kuwe na waalimu angalau 10 au saba, lakini angalau kungekuwa kuna Afisa Kilimo mmoja tu kwenye kila kijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule zipo karibu kila kijiji. Tunahangaika, tunakuwa tuna waalimu 10 au saba, lakini tumesahau kuwa Afisa Kilimo angalau mmoja tu angekuwepo kwenye kila Kijiji, akatoa elimu ya kilimo chenye tija kwa wakulima wetu, tutabadilisha sana uchumi wa nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naiomba sana Serikali yangu, pamoja na kuwa bado tuna umuhimu sana na ajira nyingine, basi iangaliwe kwenye kilimo angalau Afisa Kilimo mmoja kwenye kila kijiji afundishe wale wakulima ambao wengi wao wakishamaliza, hata shule wanabaki pale pale kuwa wakulima. Kwa hiyo, tukiwa na Maafisa Kilimo kwenye kila kijiji ambao watafundisha wakulima wetu kulima kwa tija katika maeneo yao madogo, tutafanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii tumetangazwa kuwa wa pili Afrika kulisha mahindi, lakini kwa kilimo cha kawaida sana cha wananchi wetu wa kijijini ambao wanajihangaikia wenyewe, hawana hata Maafisa Ugani wa kutosha. Je, tukiwapata Maafisa Ugani kwenye kila kijiji wakawafundisha wakulima wetu kutumia

maeneo yao madogo ya ekari mbili, tatu au nne kwa tija, tutakuwa wapi? Tutalisha dunia nzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naiomba sana Serikali, najua ikama na mambo ya fedha, lakini hebu tuangalie suala la kuajiri Maafisa Ugani kwenye kila kijiji na wafanye kazi. *Resources* tayari tunazo kwenye kila kata, kama tunavyosema, ni nyingi, lakini wakiwepo hawa watu, na wakafuatiliwa kufundisha wakulima wetu, nina hakika tutafika mbali sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo mbinu za kufundisha wakulima wetu hata kuchanganya mazao. Ukienda kwenye jimbo langu utakuta kwenye shamba la ekari mbili la mkulima, kuna miti mingi ya kawaida tu. Ukimwuliza ya nini? Anakwambia ya kuni. Kama wangepata wataalamu wa kilimo, wakawaambia, basi badala ya kuni kwenye ekari mbili hizo, wangeweka hata miembe 200 tu badala ya kuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo miembe 200 inaweza kumpatia shilingi milioni 50 kila mwaka, lakini ni kwa sababu hajui, hajaelekezwa. Maana akipanda miembe, bado atalima mahindi yake kwenye shamba lile lile kwa sababu miembe 200 kwenye ekari mbili, ni upana karibu wa mita kumi kutoka mwembe hadi mwembe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wangekuwa wameelekezwa, akalima miembe badala ya kuacha miti ya kuni, angekuwa anapata *over 50 milions* kila mwaka kwa zao lile la embe, wakati bado analima mahindi yake ambayo amezoea kwenye shamba lake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hawa wataalamu kuwepo ili kubadilisha fikra za wakulima wetu ni jambo la msingi sana. Kwa hiyo, naiomba Serikali iangalie katika umuhimu wa ajira inazotoa kila mwaka. Suala la Maafisa Kilimo ni la msingi sana. Hii itakwenda, wakishaajiriwa hawa, wawe na mwangalizi wa karibu ambaye ni mamlaka ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo kwa halmashauri siyo kipaumbele kabisa, yaani halmashauri wanawajua wakulima wakati wa kudai ushuru tu. Wakati wa ushuru, mageti mengi, kila njia wakidai hela ambazo hawakushiriki hata kidogo katika kumsaidia mkulima kulima lile shamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hiki kilimo kikiwa na mamlaka yake ambayo itamjali huyu mkulima, basi hata hizo halmashauri zitaupata huo ushuru zaidi ambao zinaupenda sana wakati wa mavuno, lakini wakati wa kumsaidia mkulima hamna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri zetu zinahangaika sana na waalimu, zinahangaika na manesi, hujawahi kusikia zinahangaika na mkulima. Hata kama kuna Afisa Kilimo mmoja au wawili kwenye kata, wanapewa majukumu mengine; hukaimu Ofisi ya Kata au anakaimu Utawala. Kwa hiyo, wakulima wanakuwa wameachwa, kitu ambacho ndiyo uti wa mgongo hata wa hizo halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hili suala la mamlaka ya kilimo ni la muhimu sana. Sehemu zote ambazo tumeweka mamlaka tumefanikiwa. Tumeweka *TARURA* tumefanikiwa, tumeweka *RUWASA* tumefanikiwa na tumeweka *TANROADS* tumefanikiwa. Hebu sasa tugeukie kwenye kilimo tuweke mamlaka, hili jambo ambalo ndiyo uti wa mgongo wa nchi hii, nina hakika tutafanikiwa kiasi kikubwa na tutailisha dunia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili la mamlaka pia liende pia kwenye suala la uvuvi. Sekta za Uvuvi na Mifugo ni kubwa sana. Kwenye mifugo kuna sekta ndogo ya maziwa ambayo ni kubwa sana, kuna sekta ndogo ya nyama ambayo ni kubwa sana, na kuna sekta ndogo ya ngozi ambayo pia ni kubwa. Haya yote yangefanyiwa kazi yangebadilisha kabisa uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaimba tu kila siku kuwa tuna mifugo, wa pili Afrika, lakini hamna chochote ambacho tunafanya. Ni kwa sababu Sekta ni kubwa. Sasa njoo kwenye

uvuvi; kuna wa bahari kuu, kuna wa maji baridi, kuna ufugaji wa samaki unakuja kwa kasi. Hizi zote ni sekta kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namwomba sana Mheshimiwa Rais wangu, ikibidi hii Wizara ya Mifugo ibaki kuwa Wizara kamili na Uvuvi iwe Wizara kamili, kwa sababu hivi ni vitu vikubwa ambavyo vinaweza kubadilisha kabisa uchumi wa nchi hii. Ukienda huko halmashauri ndiyo kabisa. Eti unakuta Mkuu wa Idara ya Mifugo na Kilimo ni mmoja na wakati vitu vyenyewe hivi ni vipana kweli kweli, akiwa amesomea kilimo, habari ya mifugo anasahau; akiwa amesomea mifugo, habari ya kilimo anasahau.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba na TAMISEMI, kwanza mwongozo uende kabisa, hii Idara ya Kilimo na Mifugo zirudi kuwa Idara tofauti na Wakuu wa Idara yake tofauti, kwa sababu ni vitu vikubwa vinavyoshikilia uchumi wa nchi hii. Kwa hiyo, namwomba sana Rais wangu, atenganishe hii Wizara, pia halmashauri kule Idara ziwe tofauti na mamlaka ya Mifugo na Mamlaka ya Uvuvi, zianze kwa mara moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge, mtaona jinsi nchi hii itakavyobadilika kwa sababu ndiyo fursa ambayo imeshikilia uchumi wa nchi, imeshikilia maisha ya Watanzania na kila kitu ambacho kitaenda vizuri kabisa katika nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona umeshika hiyo mic yako, lakini yalikuwepo mengi ya kusema. Naomba haya ya mamlaka yafanyiwe kazi, kwani yatatusaidia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mtinga. Mheshimiwa Felista Njau, atafuatia Mheshimiwa Vedastus Manyinyi Mathayo na baada ya hapo Waheshimiwa Naibu Mawaziri na Mawaziri mtaanza kuchangia ambapo ataanza Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani, atafuatia Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji, Waziri wa Mifugo; Mheshimiwa Dkt. Selemani

Jaffo, Waziri wa Viwanda na Biashara; na michango itahitimishwa na Mheshimiwa Hussein Bashe, Waziri wa Kilimo; na baada ya hapo watoa hoja wajiandae.

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi jioni ya leo niweze kuchangia kwa uchache ripoti ya Kamati yetu ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema kwa kunipatia kibali saa hii. Pia, napongeza vyombo vyetu vya ulinzi na usalama ambavyo vinafanya kazi kwa uzalendo na weledi mkubwa vikiongozwa na Amiri Jeshi Mkuu, Mama yetu Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa kuliko yote, Mwenyekiti wetu wa Kamati ambaye kwa kweli amekuwa akituongoza kwa umakini mkubwa, Spika wetu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama ambaye kiukweli amesimama kidete, Bunge limekuwa imara, tunamwombea Mwenyezi Mungu ampe heri na miaka mingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nitajikita kwenye usafiri wa bodaboda na ulinzi na usalama wa Taifa letu. Tutakubaliana sote, kama sio sisi, ni watoto wetu, ni jamii, ni watu waliotuzunguka wanatumia bodaboda kama usafiri rahisi na kuwafikisha mahali haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bodaboda na bajaji ni 70% ya vyombo vyote vya usafiri nchini. Yaani ukichukua vyombo vyote ukajumlisha, 70% ni bodaboda na bajaji. Kwa hiyo, wigo huu ni mpana sana, lakini hakuna mchango unaopatikana kwenye bodaboda au bajaji. Mchango wake ni mdogo na tija kwa Taifa ni ndogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bodaboda ndiyo wanaoongoza kwa ajali nchini, ndiyo wanaoongoza kwa ulemavu nchini, ndiyo wanaoongoza kwa kukaa hospitali kwa muda mrefu na hivyo Serikali kutumia fedha nyingi sana kutibu watu hawa. Ni kwa

sababu hawajawekewa utaratibu mzuri. Bodaboda hawana maegesho maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema haya, na Kamati ililiona kwa sababu kuna watu wasio na nia njema wanatumia mlango ulio wazi wa bodaboda kufanya uhalifu. Niseme tu, vijana wetu wa bodaboda hawawezi kuwa wahalifu, lakini wapo watu wanaingia kwenye ule mwanya wa bodaboda, wanafanya uhalifu; wanapora, wanaiba, wanafanya vitu vigumu kabisa na kuhatarisha usalama wa watu na mali zao, lakini linaitwa jina la pamoja "bodaboda". *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutakuwa mashahidi, wengi wetu tumepanda bodaboda, wapo ma-*graduate* ambao ni bodaboda, *degree holders* bodaboda wapo hapa wanafanya biashara na wanaweza kujikimu. Unaweza kuona hii Sekta ni pana namna gani? Sekta hii haijawekewa mwongozo maalum ili uweze kukidhi mahitaji ya bodaboda wenyewe, lakini na jamii kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulishauri, tukasema Serikali isimame kidete, ishirikiane na *LATRA*, Mamlaka ya Miji, Wilaya, iweze kujenga mfumo wa kisasa wa kidijiti wa kuweza kufanya utambuzi wa bodaboda wote nchini. Huu mfumo uwe wa Kitaifa. Mfumo huu ukiwa wa Kitaifa unaweza kupunguza athari hasi…

**MHE. ABEID R. IGHONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Felista kuna taarifa, unaweza ukaketi. Mheshimiwa Ighondo.

**TAARIFA**

**MHE. ABEID R. IGHONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpa mzungumzaji taarifa kwamba, hayo anayoyazungumza, nchi ya Rwanda wamefanikiwa sana kudhibiti ajali za barabarani na mfumo usio wa kiholela wa bodaboda kwa kuzingatia kusimamia sheria na pia kutumia mfumo wa kidijiti. Kwa hiyo, nchi

yetu pia inaweza kwenda kujifunza kule ili hoja ya mzungumzaji ilete tija kwenye nchi yetu, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Ighondo. Mheshimiwa Felista unaipokea taarifa?

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea kwa heshima kubwa, ahsante. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiweka mifumo thabiti tutaiheshimisha sekta hii ambayo inaonekana ni ya kawaida. Hata hivyo, katika Taifa letu, ni zaidi ya vijana 800,000 kwa mwaka wanahitimu vyuo vikuu na sekondari, lakini hawana ajira. Katika hawa vijana, 54% kila mwaka wapo tu mtaani, hawafanyi chochote. Tukiirasimisha sekta hii, tukaweza kuiwekea mipangilio, tutakwenda kuzalisha kitu kikubwa, na Serikali itapata mapato, na vijana wetu watasimama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bodaboda sasa hivi ni kama maji, usipooga utakunywa, usipokunywa utapikia. Kila tunapopita tunakutana na bodaboda, watoto wetu wanapanda bodaboda, tuurasimishe mfumo huu ili tuweze kusaidia Serikali ipate mapato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nayazungumza haya ili tuone tija ya sekta hii. Katika Taifa letu, kidunia tumekuwa wa kumi ambapo vijana wetu wengi hawana ajira. Tukiirasimisha hii sekta, tunaweza tukapata ajira na vijana wetu wakakaa vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba hili lichukuliwe kwa u-*serious* wake, lakini kuna watu ambao sio waendesha bodaboda, ni wamiliki wa bodaboda. Hawa wamiliki nao warasimishwe ili wajulikane. Unapoenda kupanda bodaboda umtambue huyu ametoka wapi? *ID number* yake, anapaki kituo gani? Wilaya yake ni ipi? Hii ni kwa usalama wa Taifa letu na nchi yetu, ili kuweza kukinga watu wenye nia mbaya wa kwenda kulichafua Taifa kupitia mwanya huu wa bodaboda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hilo nasema, kama Taifa tukiazimia kufanya jambo, tukaliweka hapa, tutafanikiwa. Mheshimiwa Bashe amefanikiwa sana kwenye Sekta ya Kilimo. Tusipoongea sisi, mawe yataongea. Mheshimiwa Bashe amefanikiwa kwa sababu amekuwa *serious*, ameyachukua mambo kwa uzito wake, ameyatekeleza. Hili nalo lichukuliwe namna hiyo ili tuweze kwenda nalo kwa tija ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikitoka hapo nina msiba mkubwa wa JKT. Inawezekana wale wenzetu kwa sababu ni askari wazalendo, hawawezi kwenda *front* kudai haya madeni; shilingi bilioni 40 ni msiba, ni kilio. Tulisema tutasaida wakandarasi wetu wa ndani. SUMA JKT ni wakandarasi wa ndani wanaopambana, wa viwango vinavyotosha, lakini mitaji yao ni duni, imekaa kwa watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta za Kiserikali na sekta binafsi hawalipi pesa zao. Wamedai mpaka wamekuja kwenye Kamati. Tunapandisha sauti kwamba yeyote anayedaiwa na JKT, walipe fedha hizi, na wazilipe haraka kwa kuwa wale hawawezi kuandamana, hawawezi kunung'unika, wale ni wazalendo, sauti yao ni sisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba hili lichukuliwe kwa u-*serious* mkubwa. Katika hili, tumeshindwa kufanya mambo makubwa. Tulienda Misri, tuliona namna gani majeshi yanavyochangia pato la Taifa zaidi ya 45%. Tukiwezesha vyombo vyetu vya ulinzi na usalama kwa uzalendo wanaouonyesha, kwa tija wanayoionyesha, Taifa hili litakwenda *next level.* Niwaambie, tusichukulie *blah blah* kwa sababu ni wenzetu, tulipe madeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Felista Njau. Sasa namwita Mheshimiwa Vedastus Manyinyi Mathayo.

**MHE. VEDASTUS M. MATHAYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwanza kwa kunipa nafasi hii ili niweze kutoa

mchango wangu kidogo. Mchango wangu utajikita kwenye huu upande wa ulinzi na usalama, na vile vile kwenye suala zima la uvuvi haramu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea kuishukuru Serikali kwa juhudi kubwa ambazo inafanya hasa katika kuzuia huu uvuvi haramu. Kule Musoma kusema ukweli suala la ziwa, hasa Ziwa Victoria limekuwa likitusaidia sana katika kipindi cha zamani, kwa sababu ndiyo lilikuwa msingi wa uchumi wa miji yetu yote iliyoko pembezoni mwa Ziwa Victoria. Kwa bahati mbaya samaki tuliokuwa tunawategemea hawapo, viwanda vyote vimekufa na hii ni kwa sababu ya uvuvi haramu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana Serikali inajaribu kufanya juhudi kwa kadri iwezavyo ili kuona kama inaweza ikasaidia kuokoa. Kusema ukweli, pamoja na juhudi ambazo Serikali inafanya ya kupeleka vyombo vya ulinzi kule ziwani, lakini bado hawawezi kumaliza uvuvi haramu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawawezi kumaliza uvuvi haramu, kwa namna ambavyo sasa watu wamekuwa na *technics* nyingi zinazohusiana na huu uvuvi. Kwa hiyo, wakati mwingine unakuta wanaenda kule, kwa bahati mbaya, kabla hawajafika, taarifa zimeshafika. Hivyo, unakuta wale wavuvi haramu hawapo, tayari wamesha-*escape*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ushauri wangu ni kwamba, lazima Serikali ijiongeze, ione namna ya kufanya kuhakikisha kwamba lile ziwa linaendelea kuwepo na kuwasaidia watu wetu. Kwa maoni yangu, kama tunataka kupunguza uvuvi haramu, ziko njia mbili tu ambazo nadhani zikifuatwa zinaweza zikatusaidia. Njia ya kwanza ya kuweza kupunguza uvuvi haramu, ni kukubali kuwa na Mamlaka ya Uhifadhi wa Maziwa pamoja na Bahari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jirani yangu Mheshimiwa Francis amezungumzia suala la mamlaka, ni ukweli usiopingika, kila mahali ambapo mamlaka imewekwa, ufanisi umeonekana. Sasa

unapozungumza suala la ziwa na uhifadhi wake wote ule, kwamba liwe chini ya Wizara, kusema ukweli hii tutatwanga maji kwenye kinu. Ndiyo maana nasema kwamba, hili halina mbadala, ni lazima tuwe na mamlaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri suala hili nililichangia kwenye lile Bunge, na Waziri aliahidi kwamba hivi karibuni wangeleta hiyo sheria ya kuunda mamlaka. Kwa hiyo, leo nafurahi kumwona Mheshimiwa Waziri Dkt. Kijaji yuko hapa. Naomba basi, aifuatilie hiyo sheria na tuikamilishe ili tuwe na mamlaka ili iweze kutusaidia, kuhakikisha kwamba haya maziwa yetu na yenyewe walau yanaweza kuwa na tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliona mfano kwa wenzetu wa pale Kigoma, kwa muda mfupi tu lile Ziwa Tanganyika lilipolindwa, tuliweza kusikia mafanikio na kuyaona. Sasa leo ukizungumza, Musoma, viwanda kama vitano vyote vimekufa. Bahati nzuri Mheshimiwa Waziri amekuja Musoma na alivyohudumu tu kwenye hiyo Wizara, alikuja Musoma na alijionea, na akapata taarifa zao kwamba pale sasa hakuna kiwanda hata kimoja kinachofanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati nzuri aliahidi kwamba atakuja, akiwa hapo aliniambia kwamba akipata nafasi tukimaliza Bunge atakuja kwa ajili ya kukaa na wafanyabiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa angalia, kwa sababu ya umuhimu wa lile ziwa, mpaka wafanyabiashara au wale wavuvi wenyewe wamehiari kutoa michango yao kwa ajili ya kuchangia katika zile gharama za kuzuia uvuvi haramu. Kwa hiyo, nadhani hili ni suala la mamlaka na njia ambayo itatusaidia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni la kuwashirikisha wale wananchi na wavuvi wenyewe. Unajua pamoja na juhudi ambazo Serikali inatumia, lakini bado uvuvi haramu upo wa namna nyingi. Yaani unakuta hata pale ufukweni tu mtu ana kile kimtumbwi kidogo anafanya uvuvi haramu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati nzuri, kwa sababu hawa wavuvi haramu ni watu ambao tunakaa nao, ni rahisi zaidi kuwatambua hasa tukiwashirikisha wananchi wakatusaidia hata kuwatambua, na kutambua hata nyavu na zana zao wanazotumia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mwingine kwa kutokufahamu, tunadhani kwamba viwanda vinavyotengeneza nyavu vikizuiwa, uvuvi haramu utapungua. La hasha, kwa sababu leo watu wanashonea nyavu majumbani. Leo zile nyavu unakuta zinaunganishwa, badala ya kuwa na ule unene unaotakiwa au urefu unaotakiwa, wanaunganisha, zinakuwa ndefu zaidi. Hivyo basi, kutokana na hali hii, kwa namna yoyote ile suala la uvuvi haramu litaendelea kwa muda mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaamini kwamba kama haya mambo mawili yakifuatwa, kama tukawa na mamlaka na vilevile tukawa na ushirikishwaji wa wananchi, ambao ndio wanaoishi na hawa watu itakuwa rahisi kudhibiti uvuvi haramu kila unapojitokeza. Hii haitaokea kwa sababu nyingine, bali kwa sababu wananchi wenyewe watakuwa wamechoshwa na hali hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unakuta mtu anaenda na mtumbwi ziwani, anarudi na kilo tano au kilo kumi. Hivyo, hata gharama alizotumia kwa mafuta ya kwenda na kurudi, hazirejeshwi. bado haziwezi kurudi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa sababu wanaona kwamba wanajikuta katika hali ngumu, ndiyo maana wameamua kwa hiari kutoa ushirikiano kwa Serikali ili tatizo liweze kutatuliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru Serikali, hasa Mheshimiwa Mama Samia, kwa kuleta hizi *cage* kwa maana ya ufugaji wa vizimba. Hivyo, nasema, endapo hatutazuia uvuvi haramu, hata hivi vizimba navyo havitakuwa na maana kabisa, kwa sababu uvuvi haramu wa sumu utaua samaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sumu hiyo haiishii tu kuua samaki wa nje, itaingia pia kwenye vizimba. Hii inamaanisha kwamba mtu atakuwa amewekeza fedha nyingi kwenye vizimba akiwa na matumaini ya kupata samaki, lakini kesho yake anakuta samaki wote wamekufa. Hali hiyo imetokea na kila leo tunaiona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, njia pekee ya kuhakikisha ufanisi, ni kutumia vizuri rasilimali ziwa, na tutakapokuwa na njia mbili, ambazo ni imani yangu kwamba zitatusaidia na maisha ya watu wetu yataboreka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Vedastus. Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Daniel Baran Sillo.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia hoja iliyoko mbele yetu kuhusu hoja ya Kamati yetu ya Ulinzi na Usalama pamoja na Kamati ya Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naungana na waliotangulia kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa anayofanya, sambamba na Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa kazi kubwa anayofanya kwa upande wa Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na utendaji kazi uliotukuka wa viongozi hawa wakuu, ndiyo ulisababisha Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa CCM Taifa, kwa kauli moja kumpitisha Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kuwa Mgombea Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi kuwa Mgombea wa Urais kwa upande wa Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hayo, pia nampongeza Balozi Dkt. Emmanuel Nchimbi, kwa kuteuliwa kuwa Mgombea mwenza na hatimaye kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii kuipongeza Kamati yetu ya Kudumu ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kwa kazi kubwa wanayofanya chini ya uongozi mahiri wa Mheshimiwa Vita Kawawa, Mwenyekiti wetu; Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Vincent Mbogo pamoja na Wajumbe wa Kamati hii, ambao kwa kweli wamekuwa na ushirikiano Mkubwa sana kwetu. Ushauri wao, mapendekezo na maelekezo yao yamekuwa chachu kubwa katika utendaji kazi ndani ya Wizara yetu ya Mambo ya Ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, nampongeza Mheshimiwa Mwenyekiti kwa taarifa nzuri iliyojaa mambo mazuri kabisa ya kujenga taasisi zetu hizi. Naungana na waliotangulia, kupongeza vyombo vya ulinzi na usalama vilivyo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi pamoja na vilivyo chini ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa kazi kubwa wanayofanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi imeendelea kuwa tulivu na kuwa salama kwa sababu watu hawa wanafanya kazi kubwa sana. Usalama wa nchi uko mikononi mwa jamii nzima, Serikali pamoja na vyombo vya ulinzi na usalama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia kwa upande wa Jeshi la Polisi. Imezungumzwa habari ya ajali za barabarani. Ni kweli ajali za barabarani zimekuwa ni changamoto kubwa inayopunguza nguvu kazi ya Taifa. Hivyo, kama Wizara kupitia Jeshi la Polisi, tuna mikakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkakati wa kwanza ni marekebisho ya Sheria ya Usalama Barabarani Sura 168, sheria ambayo ni ya mwaka 1973 na ilifanyiwa marejeo mwaka 2002. Ni sheria iliyopitwa na wakati, kwa hiyo, tuko hatua za mwisho kupata maoni ya wadau mbalimbali ili kuhakikisha tunatunga sheria

inayoendana na wakati na kuzingatia matakwa ya wakati huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni usimikaji wa kamera za kisasa 6,500 ambazo kwa kuanzia, tutazisimika katika Jiji la Dar es Salaam, Arusha, Mwanza na Dodoma na baadaye nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkakati wa tatu ni ukaguzi wa lazima wa magari *(Mandatory Vehicle Inspection)*. Miradi hii karibia inaanza na katika hili tutakagua magari yote yanayoingia nchini pamoja na yanayotumika nchini ili kuhakikisha kwamba magari yanafaa kutembea katika barabara zetu na kuepusha ajari ambazo siyo za lazima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la nne ambalo tunaendelea kulifanya kazi, ni kuendelea kutoa elimu kwa umma; shuleni, makanisani, misikitini, masokoni pamoja na maeneo mbalimbali kuhakikisha kwamba wadau wote wanashirikishwa katika suala zima la kuepuka ajali za barabarani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande wa vitendea kazi kwa Jeshi la Polisi, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais ametoa fedha. Hivi ninavyozungumza, tumeshaleta magari kwa ajili ya *highway patrols* na tumeshatoa magari 50 kwa ajili ya ma-*OCD* nchi nzima. Mwisho wa mwezi huu wa Pili, tunapokea magari 122 kwa ajili ya ma-*OCD* waliobaki nchi nzima ili kuhakikisha kwamba tunaendelea kulinda raia na mali zao katika maeneo mbalimbali hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Waheshimiwa Wabunge wengi wamechangia, hasa Wajumbe wa Kamati, kwamba kuna upungufu wa vitendea kazi na vituo katika mikoa mbalimbali. Katika hili, Mheshimiwa Rais ametupatia fedha dola milioni 100 kutoka Taasisi ya *Adex* iliyoko katika Falme za Kiarabu kupitia Kampuni ya *NAFFCO FZCO,* ambayo iko Dubai, tumenunua vifaa vya zimamoto pamoja na magari kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, tunanunua boti 23 za kuzima moto, *helicopter* moja, magari ya kuzima moto 150 ambazo tutayasambaza katika mikoa mbalimbali na wilaya zote hapa nchini, mtambo mmoja wa kunyanyua vitu vizito, magari 40 ya kubebea majeruhi na wagonjwa, magari matatu ya kukabiriana na kemikali hatarishi na milipuko, magari matatu ya ngazi, magari 30 ya mawasiliano na amri na karakana sita zinazotembea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hili, pia tuna ujenzi wa vituo saba katika Mikoa ya Songwe, Kagera, Njombe, Manyara, Geita, Katavi na Simiyu. Pia, kwa upande wa rasilimali watu tayari mwaka 2024 wamehitimu askari 221, na katika mwaka huu wa fedha tayari tumeshapata kibali cha kuajiri askari 425. Hii yote ni katika kuboresha utendaji kazi wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya magari 12 ya kisasa yameshapokelewa, yameenda Mkoa wa Arusha, Mkoa wa Mwanza, Kilimanjaro na Dar es Salaam kwa maana ya Ilala, Temeke pamoja na Kinondoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Jeshi la Magereza, ziko changamoto ambazo zimesemwa na Waheshimiwa Wabunge hasa kuhusu uchakavu wa magereza ya zamani. Katika hili Mheshimiwa Rais ametoa fedha, tumepewa shilingi bilioni 6.5 kwa ajili ya ukarabati wa magereza ya zamani. Kwa mfano, Gereza la Lilungu ambalo liko Mtwara, Gereza la Ukonga, Segerea pamoja na Keko ambayo yako Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha zimetengwa kwenye mwaka huu wa fedha wa 2024/2025. Ni imani yangu kwamba baada ya ukarabati huu, basi magereza haya yataendelea kutoa huduma na pia tutaendelea kukarabati magereza mbalimbali awamu kwa awamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hili, Jeshi pia limeendelea kujenga magereza katika maeneo ambayo hayana

magereza hasa kwenye wilaya ambazo hazina magereza na katika hili tumetenga shilingi bilioni nne kwa ajili ya ukamilishaji wa magereza katika Gereza la Karatu ambalo liko katika Mkoa wa Arusha na Gereza la Kilosa ambalo liko katika Mkoa wa Morogoro. Haya yakikamilika, basi nadhani tutakuwa tumepunguza changamoto kubwa ya uhifadhi wa wafungwa na mahabusu katika magereza yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, hivi leo tunavyozungumza wafungwa walioko magerezani pamoja na mahabusu ni 27,154. Hivyo, uwezo wa magereza yote 129 tuliyonayo nchini, tunaweza kuhifadhi wafungwa na mahabusu 29,902. Kwa ushirikiano wa taasisi za mnyororo mzima wa hakijinai, msongamano umepungua kwenye magereza mbalimbali hapa nchini. Hii ni hatua kubwa ya kuipongeza Serikali kwa kazi hii kubwa inayofanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo moja la upande deni la Jeshi la Suma JKT limezungumzwa. Kwa sababu nipo hapa kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani na kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Kujenga Taifa, hili jambo tumelipokea kwa uzito mkubwa na kama Serikali tumelichukua, tutalifanyia kazi kwa kushirikiana na taasisi mbalimbali za umma, na binafsi ili sasa madeni haya yalipwe, ili wenzetu wa Suma JKT waendelee na kazi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, nilihakikishie Bunge lako Tukufu, maazimio tisa yaliyoelekezwa kwenye Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na maazimio mawili yaliyoelekezwa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, tumeyachukua tayari kwa ajili ya utekelezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nashukuru kwa fursa hii, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri, Daniel Sillo. Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji, Waziri wa Mifugo na Uvuvi.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kuwapongeza sana wenyeviti wote wawili kwa mawasilisho mazuri waliyoyaweka Mezani na kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza zaidi Mheshimiwa Deodatus Mwanyika, Mwenyekiti wetu wa Kamati ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo, pamoja na Wajumbe wote wa Kamati kwa kazi nzuri wanayoendelea kuifanya ya kuishauri Serikali na kutusimamia. Kazi yao ni nzuri sana, na ninaomba niseme kwamba sisi kama Wizara ya Mifugo na Uvuvi tutaendelea kupokea, kusikia na kutekeleza yale ambayo wanatuelekeza na kutusimamia kama Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, naomba niseme tumepokea maazimio na maoni ya Kamati, na tutakwenda kuyatekeleza kama yalivyowasilishwa, kama ambavyo tumetangulia kutekeleza maazimio mengine ya Kamati yetu hii ndani ya mwaka huu ambao tuko kwenye utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya shukrani hizo, naomba nichangie machache sana. Naanza kwa kuunga mkono hoja hii, na kama nilivyosema, tunakwenda kwenye utekelezaji, hivyo nitasema machache sana mbele ya Bunge lako siku hii ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza kabisa, naomba nianze na hili la uvuvi haramu. Kwenye uvuvi haramu, tunakiri na tunatambua Bunge lako lilituelekeza kuanzishwa kwa mamlaka ili tuwe na ufanisi kwenye eneo hili. Nasi tulianza utekelezaji na tayari iko kwenye ngazi mbalimbali ndani ya Serikali yetu. Tutakapokamilisha, basi kama Waheshimiwa Wabunge walivyosema na Kamati yetu ilivyotuelekeza, tutaileta sheria hiyo hapa Bungeni ili tuweze kutekeleza kwa 100% maelekezo ya Bunge letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wamesema na naomba nianze kwa ndugu yangu Mheshimiwa Mohamed Said Issa, Mbunge wa Jimbo la Konde kuhusu

kinachoendelea kule Pemba. Naomba tu nimwambie kwamba, uvuvi wa maji ya ndani, au maji ya Kitaifa unasimamiwa na Mkurugenzi wa Uvuvi kwa Serikali ya Zanzibar, na kwa upande wa Bara pia inasimamiwa na Mkurugenzi wa Uvuvi ndani ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumjulisha Mheshimiwa Mohamed kwamba, hatujazuia wavuvi wetu kuendelea kuvua, lakini yeye mwenyewe kama alivyotangulia kusema kwamba tunashughulika na wavuvi haramu, na kwenye hili hatuna simile. Tunahakikisha tunalinda rasilimali zetu zote za maji ili tuweze kunufaika kama Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mohamed kwamba tutaendelea kusimamia rasilimali hizi na wala hatuna hofu ya ushindi kwa Chama cha Mapinduzi. Kwa Timu ambayo imetambulishwa jana kwa Watanzania, sisi Chama cha Mapinduzi hatuna mashaka na kura zetu. Ni timu imara na makini. Tunakwenda kushinda, na Pemba yote tunakwenda kuichukua. Kwa hiyo usiwe na mashaka kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, timu yetu iko imara sana na kwenye hili ni kwa sababu tu tumesimamisha timu makini na tunafanya yale ambayo wananchi wa Tanzania wamekituma Chama cha Mapinduzi kufanya na sisi Serikali yao tunaendelea kuyatekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme jambo la pili, nalo ni kuhusu chanjo ya mifugo. Kwa hili naomba sana Waheshimiwa Wabunge, moja, tumpongeze Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa mapenzi yake mema kwa Taifa hili na kwa usimamizi wake makini wa rasilimali za Taifa hasa sekta zetu hizi za uzalishaji ikiwemo sekta hii ya mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema tumpongeze Mheshimiwa Rais wetu kwa sababu ameendelea kuandika historia ya kipekee

tangu akabidhiwe mamlaka ya nchi hii kama Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo hili ndani ya bajeti yetu tunayoitekeleza mwaka huu, ametupatia shilingi bilioni 28.1 kwa ajili ya chanjo ya mifugo. Haijawahi kutokea ndani ya miaka 60 ya Uhuru wa Taifa letu, aliifanya Baba wa Taifa na sasa anaifanya Jemedari makini Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan. Tayari tumeshazindua kampeni ya chanjo na kampeni ya uhamasishaji, ninaomba niwashukuru na kuwapongeza wafugaji wa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chama chetu cha wafugaji ndani ya Taifa letu wamekubaliana na jambo hili na tayari mikataba ya wazabuni tumeshasaini tunakwenda kuifanya kazi hii kwa umakini wa hali ya juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wamesema tuangalie na twende kwa umakini na tulishapokea kutoka kwenye Kamati yetu. Nawashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati yetu. Tunakwenda kwa umakini wa hali ya juu na Mheshimiwa Rais wetu akasema kumekuwa na malalamiko ya chanjo ambazo hazifanyi kazi sawasawa. Ni chanjo bandia, ni chanjo ya aina gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais akasema Hapana, amefungua mipaka ya nchi hii. Tuna wawekezaji wamewekeza kwenye viwanda vya chanjo ndani ya Taifa letu na wataalamu wetu wanasimamia. Mheshimiwa Rais katuelekeza chanjo tunayoipeleka kwenye mifugo ya wafugaji wetu kwamba rasilimali ya Taifa letu zitatoka kwenye viwanda vyetu vya ndani. Kwa hiyo, tunaifahamu tangu hatua ya kwanza mpaka hatua ya mwisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunakwenda kuifanya kazi hii kwa umakini mkubwa. Wataalamu wetu wa mifugo wanakwenda kusimamia zoezi hili pamoja na wataalamu wetu. Tunajua ni wachache, hawatoshi kwenye kata zote tulizonazo,

Mheshimiwa Rais akatoa ruhusa tuwatumie watalaamu wetu waliofundishwa ndani ya nchi yetu kuhusu mifugo ambao hawajaajiriwa na Serikali yetu, tuwachukue 3,500. Moja, tutakuwa tumetengeneza ajira za vijana wetu ambao wamefundishwa na watakwenda kutekeleza zoezi hili kwa umakini mkubwa.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba dakika moja ili nimalizie. Nawaomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu, sisi ni Madiwani na viongozi kwenye halmashauri zetu, jambo hili tulibebe, tulipeleke kwenye halmashauri zetu ili tunapoenda kuanza zoezi hili, wananchi wetu wote wawe tayari na watoe mifugo yao ili tuweze kuchanja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais ametoa shilingi 500/= kwa kila ng'ombe na mfugaji atatoa shilingi 500/= kwa kila ng'ombe. Mheshimiwa Rais ametoa shilingi 300/= kwa kila mbuzi na kondoo, na mfugaji atatoa shilingi 300/= kwa kila mbuzi na kondoo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua mifugo aina ya kuku kwamba wanaohusika ni akina mama, Mheshimiwa Rais kwa mapenzi makubwa ya wanawake wa nchi hii amesema kuku wetu wote tunapoenda kuwachanja ni bure kabisa bila kuchangia chochote. Hayo ndiyo mapenzi ya Mheshimiwa Rais wetu. Nawaomba sana Waheshimiwa Wabunge tufikishe elimu hii ili mifugo yetu yote iweze kuchanjwa. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Selemani Jafo, Waziri wa Viwanda na Biashara.

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu ambapo kwa mara nyingine ametupa kibali, tumefika salama katika Bunge hili na tunaendelea na mchakato huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kumpongeza sana kwa jambo kubwa lililotokea hivi karibuni baada ya Wajumbe wa Mkutano Mkuu Taifa wa Chama cha Mapinduzi kumpendekeza yeye kuwa mgombea wetu katika uchaguzi unaokuja mwaka huu, na lakini halikadhalika kule Zanzibar pamoja na kupata mgombea mwenza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchukua fursa hii kuwashukuru sana Wenyeviti wetu wa Kamati wote wawili: ndugu yangu, Mheshimiwa Mwanyika na Mheshimiwa Vita Kawawa pamoja na Mheshimiwa Makamu Wenyeviti. Naomba nimpongeze dada yangu, Mheshimiwa Mariam Ditopile Mzuzuri kwa kazi kubwa anayoendelea kuifanya.

Mheshimiwa Mwenyeiti, vilevile, naomba nawapongeza Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati. Kamati yetu hii ya Viwanda, Biashara, Kilimo, Mifugo imekuwa tofauti kidogo. Mara nyingi sana imekuwa ni Kamati ya kutoa maelekezo yale yanayoleta tija katika Taifa letu hili. Nawashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania tuna kila sababu kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu katika muda wa sasa ametupatia Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Hii ni bahati kubwa sana. Wakati nikichangia hoja hizi za Kamati mbili, nchi yetu inaweka historia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ya Kamati imezungumzia baadhi ya miradi, lakini nataka ku-*cite* miradi michache sana. Mradi wa kwanza, ni wa Mchuchuma na Liganga ambao toka mimi ninaingia mwaka 2010 katika Bunge hili, mradi huu umeendelea kuzungumziwa; lakini chini ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, ameonyesha mwelekeo tofauti kabisa katika mradi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mara ya kwanza, kule Njombe, zaidi ya shilingi bilioni 15.4 zimetolewa kwa wananchi. Huu ni

mfano wa kuigwa kutoka kwa Mheshimiwa Rais, mwenye *commitment* ya kutekeleza matatizo ya wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu unaenda vizuri na muda siyo mrefu, ndani ya mwaka huu wa fedha tunaondoka nao. Imani yetu ni kwamba kwa mara ya kwanza inawezekana tukaona sasa Tanzania tunaenda kuhakikisha kwamba tunaenda kuzalisha chuma ambayo ni malighafi muhimu sana katika maendeleo ya viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine la pili ni la Mradi wa Maganga Matitu ambapo mradi ule umesainiwa kwa mara ya kwanza vilevile unaenda kuzalisha chuma na upo Ludewa. Hii ni kazi kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile hivi karibuni kuna mradi ambao ni wa kihistoria; toka mwaka 2004, tafiti ya kwanza ilivyofanyika katika ya Taasisi yetu ya *NDC* na *TATA Chemical Limited,* mradi ule ukashindwa kutekelezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa chini ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa mara ya kwanza mradi ule ambao uwekezaji wake utakuwa zaidi ya shilingi trilioni moja ambapo fidia yake ni zaidi ya shilingi bilioni 14.84, imetolewa fedha yote ya fidia. Katika eneo hili tuna kila sababu ya kumpongeza na kumshukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii watu wa Engaruka, mpaka hivi sasa tumefikia takribani 64%, watu 404 wamelipwa kati ya watu 599. Ni imani yetu kabla ya tarehe 15 ulipaji wa fidia utakuwa umekamilika. Siyo hivyo tu, mradi huu umeshatangazwa tangu tarehe 27 Desemba, sasa hivi *tender* zinapokelewa. Imani yetu ni kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mara ya kwanza tutaona nchi yetu imejielekeza katika upande wa uzalishaji wa magadisoda ambayo ni malighafi muhimu katika ujenzi wa viwanda vya vioo,

na pia ni malighafi muhimu katika viwanda vya *detergent* zote na maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili naomba niipongeze Kamati kwa sababu toka nilivyopewa Wizara hii na Mheshimiwa Rais, Kamati hii imekuwa ni kielelezo ili tuweze kufanya utekelezaji wa miradi hii. Naomba kwa fursa ya Bunge hili, niipongeze Kamati hii, imefanya kazi kubwa ambayo inaendelea hivi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wajumbe wameeleza hoja mbalimbali hapa nami kazi yangu ni ya kuchangia, mimi sio mtoa hoja. Jambo la kwanza ni suala zima la kibajeti, hili tumelipokea na ninaomba nimhakikishie Mwenyekiti wetu wa Kamati, jambo hili Wizara tumelipokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la hoja mbalimbali na hasa upande wa bajeti, ufinyu wa bajeti katika taasisi zetu kama *TEMDO, CAMARTEC* na nyingine zote, jambo hili tutaenda kulihangaikia ili kuhakikisha kwamba Serikali kupitia Wizara ya Fedha na kwa sababu tathmini ya kina imeshafanyika kuona kwamba kila taasisi inahitaji fedha kiasi gani, ni imani yetu kubwa tutaenda vizuri katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande wa pili ni suala zima la biashara, kwamba taasisi zetu wakati mwingine zinatengeneza vifaa. Kwa upande huo, naomba nilipongeze Jeshi la Wananchi, kwa mara ya kwanza vifaa vilizalishwa kule *TEMDO,* tumeona yale mafriji ya kisasa sana yamechukuliwa, yamewekwa katika *cell.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi la Wananchi Tanzania wameonesha mfano wa hali ya juu sana, mafriji yale ukienda kuyaangalia ni *durable* sana na *value for money* ipo, yanatengenezwa na Tanzania. Jeshi la Wananchi ni Taasisi ya kwanza kufanya hayo manunuzi, tunalipongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni imani yetu na taasisi nyingine zitaenda kuhakikisha kwamba zinatumia vifaa vinavyozaliswa

nchini kwetu. Naomba nikuhakikishie kwamba tutaendelea kutoa elimu kwa baadhi ya taasisi zetu kuhusu nini kinapatikana katika maeneo yetu. Kwa hiyo, lengo kubwa ni kwamba nchi yetu isonge mbele na kuhakikisha taasisi hizi zinafanya vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala zima la changamoto ya mitaji, kama tulivyosema mwanzo kwamba ni kweli maoni haya yamepokelewa na Serikali sasa hivi inaendelea kuhakikisha kwamba jinsi ya kufanya tupate fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati walishauri mbinu mbalimbali za kufanya, hata kutumia *Agriculture Development Bank* kuona kwamba tunapataje fursa ili mradi taasisi zetu zifanye vizuri. Maeneo hayo tunayachukua yote nasi kama Wizara tunaendelea kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni suala zima la Stakabadhi Ghalani. Kwenye hili naomba nimshukuru sana ndugu yangu Mheshimiwa Bashe. Taasisi ya Stakabadhi Ghalani ipo Wizara ya Viwanda na Biashara, lakini tumeendelea kufanya kazi vizuri sana na ndugu yangu Mheshimiwa Bashe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mara ya kwanza, katika mwaka huo 2024/2025 mazao zaidi ya tani 810,000 yameuzwa katika utaratibu huo. Zaidi ya shilingi trilioni 2.6 zimeenda kwa wananchi, na zaidi ya shilingi bilioni 87 zimeenda katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwaambie ndugu zangu, halmashauri zile takribani 62 ambazo zinatumia utaratibu mzuri wa Stakabadhi Ghalani zimeonyesha *outstanding performance* hivi sasa. Leo hii ukienda Halmashauri ya Mtwara, Halmashauri ya Newala na Halmashauri ya Nachingwea, hawawezi kukubali hata siku moja. Kwa mfano, mnakumbuka watu wa Manyara bei ya mbaazi ilikuwa mpaka shilingi 200, leo hii imefika kati ya shilingi 1,600 mpaka 2,000 kwa ajili ya Stakabadhi Ghalani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo hili mimi na ndugu yangu Mheshimiwa Bashe tutaendelea kulitolea elimu ya kutosha, kuona kwamba halmashauri nyingine zitumie utaratibu huu mzuri, lakini mwisho wa siku inaleta thamani katika halmashauri zetu kwa kupata fedha nyingi bila kutoa jasho la aina yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni imani yetu kubwa kwamba jambo hili tutaenda kulifanyia kazi na kuhakikisha kwamba tunatoa elimu kwa maeneo mbalimbali. Kwa mfano, Mheshimiwa Hhayuma alizungumza hapa kwamba wale ambao hatu-*integrate* tuweze ku-*integrate* vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri Bodi yetu ya Stakabadhi Ghalani sasa hivi wamefunga utaratibu wa kamera, juzi nimezindua hapo, lakini wameweka namna ya kuandaa utaratibu wa kuwahusisha wafanyabiashara wale wengine ambao wanaonekana wanaachwa nje ya mfumo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni imani yetu kubwa wale wadau wengine wa Kitanzania kwa maboresho yanayofanywa, kila mtu atashirikishwa vizuri, tukiwa na lengo kubwa kwamba nchi yetu isonge mbele. Ni imani yangu kubwa kwamba tukishirikiana vizuri katika hili, tutapata mafanikio makubwa sana katika upande wa uwekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande mwingine ni suala zima la Kiwanda chetu cha Viuadudu pale Kibaha. Naishukuru Wizara ya Afya, kwa mara ya kwanza wamenunua dawa ya shilingi bilioni 3.5, hongereni sana Wizara ya Afya. Hata hivyo, suala la kimkataba tunaendelea kulifanyia kazi. Tunamshukuru sana *AG* ameshafanya kazi yake ya msingi, tunaenda ku-*finalize*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka ya Serikali za Mitaa tunajipanga vizuri tukiwa na lengo la kuhakikisha kiwanda kile kinafanya vizuri. Ni kweli kiwanda ni kikubwa, kina thamani kubwa lakini kazi yetu kubwa sasa, tunaendelea kuboresha maeneo haya. Ni imani yangu kubwa tutafanya vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande wa *scanner,* tumeshirikiana na wenzetu wa *TRA,* sasa hivi kuna mchakato wa ununuzi wa *scanner* sita. Ni kweli Kamati ilienda Horohoro, maeneo mengine *scanner* hakuna. Ni imani yetu kubwa kwamba mchakato huo wa manunuzi kwa kushirikiana na *TRA* utakamilika, na mwisho wa siku tutapata mafanikio makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, na pia nawashukuru sana Wajumbe wa Kamati zote mbili, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Selemani Jafo, Waziri wa Viwanda na Biashara. Sasa namwita Mheshimiwa Hussein Bashe, Waziri wa Kilimo.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie nafasi hii kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya na kufika wakati huu. Pili, nianze kwa kuunga mkono hoja iliyoletwa Mezani na Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo, Uvuvi na Biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, nitumie nafasi hii kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote na niwahakikishie maoni na mapendekeo yote ambayo wamekuwa wakitushauri kama Serikali tutaendelea kuyafanyia kazi na tutayaweka katika mipango ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa kabisa, nitumie nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa dhati. Kama Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana ya Kilimo, haikuwa rahisi kuhangaika na changamoto za wakulima wetu, ambao wengi ni wakulima wadogo ambao ndio wameshikilia uchumi na usalama wa nchi hii, lakini amekuwa tayari kutoa fedha kwa ajili ya kuwa-*support*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawahakikishia Waheshimiwa Wabunge kuwa wakulima wadogo wa nchi hii wataendelea kuwa kipaumbele cha Taifa hili na mipango ya Serikali mpaka pale tutakapofika eneo lingine ambalo tunatarajia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, namshukuru sana Mheshimiwa Deo na Kamati nzima. Pia, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge kwani hapa leo wamekuwa wakitoa pongezi. Pongezi hizi mbele ya Mwenyezi Mungu wanaostahili ni Mheshimiwa Rais wa nchi hii na Bunge hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunazungumzia mafanikio ya sekta ya kilimo ambayo ukuaji wake umefika 4.2%, tunakimbilia asilimia tano kutoka 2.7%. Ni *reform* na mapendekezo ya Bunge hili. Leo tunazungumzia *export value* imefika zaidi ya dola bilioni 3.5 kutoka dola bilioni 1.2, ni Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tumezungumzia ukuaji, kwamba sisi ni nchi ya pili leo Afrika kwenye uzalishaji wa zao la mahindi. Kama siyo Bunge hili na Mheshimiwa Rais kuridhia kuanza *schemes* za kutoa ruzuku kwenye mazao ya chakula, leo tusingekuwa hapa. Wakati tunaanza kutoa ruzuku ya mbolea kwa mara ya kwanza, kelele zilikuwa nyingi na changamoto zilikuwa nyingi, lakini Bunge hili liliendelea kusimama imara kwa maslahi ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2021, mbolea yote iliyokuwa inatumika katika nchi hii ilikuwa ni tani 360,000; *per capital consumption*. Kwa hekta, ilikuwa ni kilogramu 15. Kwa msimu huu uliyokwisha juzi tumetumia jumla ya tani 840,000, *per capital consumption,* imefika kwa hekta kilogramu 24.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo letu ni kufika kilogramu 50 ambayo ndiyo *standard* ya nchi za *SADC*. Hii ni kazi ya miaka mitatu. *Productivity per hectare* ya mahindi imefika tani mbili, lengo tulilojiwekea ni kufika tani tatu msimu ujao wa kilimo. Hizi ni hatua, na Bunge hili limekuwa sehemu ya *reform* hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge wameongelea *issues* za mazao kama mpunga (mchele), tumetoka uzalishaji wa tani milioni 1.6 kwenye zao la mpunga, leo kama nchi, tumefika zaidi ya tani milioni tatu. Tanzania ni nchi ya nne Afrika kwenye uzalishaji. Kwa hiyo, tupo kwenye mwelekeo

sahihi, ni mwelekeo ambao unahitaji *commitment* ya muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeanza kuwekeza kwenye umwagiliaji. Serikali ya Awamu ya Sita Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan wakati anahutubia Bunge hili hapa, tulikuwa na mtandao usiozidi hekta 500,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ilani ya Uchaguzi na ninashukuru aliyekuwa Katibu Mkuu wa Chama, mimi nikiwa Naibu Waziri tunapojadili juu ya mtandao wa *irrigation* aliniagiza kuandika *paper* maalumu ya kuomba maeneo ya *priority,* yule pale Mheshimiwa Dkt. Bashiru akasema kama hatutawekeza kwenye eneo la umwagiliaji, hatutafanikiwa. Leo sisi kama nchi ilani inatupa *target* ya hekta milioni 1.2.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Awamu ya Sita, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan alipomaliza kusoma hotuba hapa, tulikuwa na hekta zisizozidi 500,000. Hivi sasa tunatekeleza miradi 780 ambayo tukiikamilisha yote, tutafikia hekta milioni 1.2 msimu wa 2025/2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatekeleza jumla ya mabwawa 100. Maji haya yanayosambaa kati ya mabwawa 100 ambayo tunaendelea kuyafanyia *feasibility study* mabwawa 14, tayari yana wakandarasi, na kati ya hayo 14, mabwawa matatu yapo zaidi ya 90%. Hizi ni hatua, na ni safari, hatuwezi kumaliza kwa siku moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaomba Waheshimiwa Wabunge, matamanio yetu ni makubwa, na matarajio ni makubwa. Tunatakiwa kupiga hatua, lakini ni lazima tuendelee kuwekeza. Leo kwenye kahawa tumetoka tani 55,000, leo tupo tani 85,000 kwa mwaka huu. Serikali inatoa ruzuku ya miche bure, kwa mwaka, zaidi ya miche milioni 20 tunaigawa kama Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu korosho, Waheshimiwa Wabunge wote mnafahamu, Mfumo huu wa Stakabadhi ya

Ghala, Mfumo huu wa Ushirika ambao tumekuwa tukiuhoji, umetufikisha mahali kwa miaka mitatu Serikali imekuwa ikigawa pembejeo na miche bure kwa wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaenda kuvunja rekodi ya korosho kwenye nchi hii, tunaenda kufikia tani laki tano. Minada ilimekwisha hivi karibuni katika mikoa minne tu, bado mingine inaendelea. Nimwambie Mheshimiwa Dkt. Chaya kwamba tumepokea mapendekezo yake ya kuwa na minada zaidi ya mara mbili, mara tatu. Tuta-*reform* mfumo wa Manyoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo wakulima wa Lindi, Mtwara, Ruvuma na Pwani wamepokea zaidi ya shilingi trilioni 1.5 kwenye mifuko yao, na huu ni mfumo wa ushirika. Kwa hiyo, nilitaka niwaambie tu wakulima wa chai, hili ni fundisho kwa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikimjibu ndugu yangu Mbunge wa Hanang', tulifanya maamuzi kama Taifa, kufanya kitu ambacho mimi naita, *Blind Privatization.* Tumejifunza, tumeona, tumewapa watu mashamba wameyaacha mapori, wamekopea fedha benki. Tumewapa watu mashamba hawayatumii na viwanda wameua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inafanya nini? Namshukuru Waziri wa Ardhi kwamba timu yetu ya uthamini imemaliza kazi yake, wametuletea *draft* ya kwanza. Hawa wawekezaji wanayo *commitment* ya mikataba ambapo kama hawatatekeleza, tumefanya tathmini ya *value* ya yale mashamba na hali ya viwanda walivyovitelekeza, tumeangalia thamani yake, tutayachukua kwa mujibu wa sheria na kuwagawia wakulima wadogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni suala la muda, nawaomba tuwe na *patient,* tusije tukaonekana ni Taifa ambalo haliheshimu sheria. Tutafuata utaratibu wa sheria kuweza ku-*reclaim* zao la chai. Kwenye parachichi tunaenda vizuri. Dada yangu nimekuelewa, tatizo lililopo Rungwe tunalifahamu wote, tutalichukulia hatua.

Tumeshaanza kutatua na tunaamini kama Serikali, tutaendelea kutatua matatizo yaliyopo kwenye parachichi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, nataka niseme jambo moja. Taifa hili huwezi kuongelea kilimo kama hutamwongelea Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. Huwezi kuongelea kilimo kama hutaongelea Azimio la Iringa. Ndiyo msingi wa *reform* ya kilimo. Anachokifanya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan leo, ataandikwa katika rekodi ya nchi hii, Mwenyezi Mungu akijalia, kwani Hatua anazochukua ni *investment* kwenye *basic. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo 71% ya mbegu zinazotumika nchi hii zinazalishwa ndani ya nchi hii. Tumepunguza *importation by 50%.* Kwa hiyo, nawaomba Waheshimiwa Wabunge tuendelee kuwa na hii *root* kama Taifa, tusitoke kwenye mwelekeo huu tulionao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *irrigation is a direction; research and development are directions; seed multiplication* ndiyo uelekeo; siyo uwekezaji wa muda mfupi, ni wa muda mrefu na sekta hii itabebwa na wakulima wadogo. Ndiyo *transformation* itakapotokea, na hatutaondoka katika mwelekeo huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Hussein Bashe, Waziri wa Kilimo. Sasa namwita Mheshimiwa Deodatus Mwanyika, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo aje kuhitimisha hoja yake.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA, KILIMO NA MIFUGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kunipa nafasi ili niweze kuhitimisha hoja ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo. Awali ya yote tumepokea michango mingi sana kutoka kwa Wabunge 15. Kati ya hao, Wabunge watatu ni Mawaziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kutoka rohoni kwamba, nashukuru sana kwa michango hiyo. Tunathamini sana michango ambayo Waheshimiwa Wabunge wameitoa, michango ambayo imetoa msisitizo, imetambulisha zaidi na imetoa maelezo ambayo inaonesha wazi hoja ya Kamati katika Bunge lako, imeeleweka vizuri kwa Wajumbe walio wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, waongeaji walikuwa ni wengi, mambo ni mengi na muda wetu hautaturuhusu kuyaongea yote, lakini nitaongea machache waliyoongea Waheshimiwa Wabunge. Wengi wameongelea suala zima la uvuvi haramu na haja ya kuhakikisha kwamba, Serikali inachukua hatua madhubuti katika kushughulika na uvuvi haramu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili ni kubwa, na kama lilivyojitokeza katika maelezo hapa, limeonesha wazi kabisa inatakiwa kuwe na hatua madhubuti na za uhakika. Sasa Kamati nayo imelisema na kwa kweli tukubaliane kwamba, kwenye suala la uvuvi haramu inaonekana watu wengi wana maslahi, na kwa hiyo, usimamizi wake umekuwa hafifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, baada ya Kamati kulitafakari kwa dhati, imeona moja ya mambo au *solution* au suluhisho kwenye suala la uvuvi haramu, pamoja na kwamba ni jambo gumu, ni ipatikane mamlaka maalum ambayo itapewa jukumu madhubuti la kushughulika na suala la uvuvi kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hoja ya mamlaka bado inabaki kuwa ni hoja ya msingi kwa Kamati yetu. Tumeisema na Wabunge wengi wamechangia kutaka mamlaka. Nimemsikia Mheshimiwa Vedastus Manyinyi, ameliongelea hilo, Mheshimiwa Dkt. Pius Chaya ameliongelea hilo na Waheshimiwa Wabunge, wanakamati, wengi wameliongelea hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ili tuweze kuthibiti, kwa kweli iko haja ya kuacha utaratibu wa sasa ambapo Wizara yenyewe ndiyo inakuwa msimamizi wa hii sekta ya uvuvi. Ndugu zangu tuvuke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukumbuke kwamba, uvuvi ni biashara, mifugo ni biashara na Serikali siyo taasisi ambayo inaweza kuwa nyepesi au nzuri zaidi kufanya biashara au kusimamia biashara au kudhibiti moja kwa moja. Kwa hiyo, ni vizuri tukawa na mamlaka ambayo itakuwa *accountable* na bado Waziri atakuwa na *role* kubwa kwenye shughuli hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto nyingine ambazo zimejitokeza kwa Wajumbe ni pamoja na ile ambayo Mheshimiwa Mwijage ameiongelea kuhusu magugu katika maeneo ya uvuvi. Tuseme wazi kwamba halikujitokeza sana kwenye Kamati yetu, lakini tunalichukua kama moja ya changamoto na kama Kamati tungependa kutembelea hayo maeneo ili tuweze kujifunza vizuri zaidi ni mambo gani tunaweza kuyafanya ili kuondokananayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo mengine ambayo Waheshimiwa Wabunge, na hasa Wanakamati; Mheshimiwa Kunti, Mheshimiwa Janejelly, Mheshimiwa Khadija Aboud, Mheshimiwa Francis Mtinga, Mheshimiwa Mohamed, wameyaongelea kwa undani na wameyakazia katika kufafanua hoja ya Kamati yetu, ni mambo ambayo yamejitokeza kwenye changamoto mbalimbali za kampuni ambazo ziko chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara. Namshukuru Mheshimiwa Waziri, ametoa maelezo hapa kujaribu kuelezea Kampuni kama *CAMARTEC* na *TEMDO*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi ni kampuni ambazo zilianzishwa kimkakati miaka mingi toka wakati wa Mwalimu Nyerere. Kampuni hizi zilikuwa zifanye utafiti na uzalishaji wa zana za bei nafuu kwa ajili ya wakulima, lakini kampuni hizi zimeendelea na zimefanya makubwa zaidi, zimeingia kwenye utafiti na zimekwenda mpaka kuanza kutengeneza mitambo mbalimbali ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama Kamati tunasema kwa kweli, iko haja taasisi hizi ziongezewe fedha ili ziweze kufanya kazi ambazo zilikusudiwa. Kwa kusema hili, tumetembelea *CAMARTEC, TEMDO, KMTC;* tuseme wazi, Serikali yetu inahitaji kuhakikisha kwamba kampuni hizi siyo tu inazipa ruzuku, siyo tu zinaomba

fedha, lakini inaziwezesha zifanye biashara kwa sababu ni kampuni za kibiashara na hilo linawezekana, na baadhi ya Wajumbe wamesema hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, *TEMDO* wamekuwa na uwezo mkubwa wa kutengeneza majokofu, nasi tumeyaona na tukajaribu kulieleza kwenye Wizara ya Viwanda na Biashara. Tunashukuru kwamba hata kama TAMISEMI bado hawajaweza kuingia na kuanza kuchukua majokofu hayo kwa ajili ya vituo vya afya na zahanati zetu, lakini angalau Jeshi la Wananchi limeonesha mfano. Hospitali nyingi za Jeshi la Wananchi zinatumia majokofu yaliyotengenezwa na *TEMDO* na yanafanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tutoe wazo au wito kwa Serikali kuhakikisha kwamba, kupitia TAMISEMI kwa kweli, ina sababu ya kujipanga, ili TAMISEMI iweze kuwa ni moja ya wabia wakubwa wa kuzifanya kampuni hizi zifanye kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala zima ambalo limeongelewa na Wajumbe wengi kuhusu uhaba wa *scanner.* Hili ni jambo la muhimu sana. Kwanza, tuhakikishe kodi inalipwa; na pili, tuwe na uhakika tunapata mizigo ambayo ina usalama kwa nchi yetu. Ni vizuri tukaifahamu mizigo na njia pekee, rahisi na ya kisayansi ni kuwa na *scanners.* Sasa kwa jambo hili tunamshukuru Mheshimiwa Waziri, amelielezea hapa kwamba wameliingiza kwenye bajeti. Kwa kweli, tunaomba bajeti hii itekelezwe ili tuweze kupata hizo *scanners.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la Kiwanda cha Dawa pale Kibaha na chenyewe ni cha kimkakati. Nchi hii, moja ya maadui wake wakubwa ni maradhi, kwa maana ya Malaria. Nchi hii inahitaji kiwanda hiki kifanye kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kumekuwa na *competing interest* kwamba, labda ukiwa na vyandarua vingi unaweza ukashughulika na Malaria. Sisi, kama Kamati, bado tunaona kwamba ni vizuri kiwanda hiki kikapewa nguvu; kikapewa

biashara, kikapewa mtaji, ili kiwe ni *source* kubwa ya ku-*eliminate* Malaria katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuseme wazi kwamba tunamshukuru Mheshimiwa Waziri kwamba, sasa wameanza, na ni kweli. Nami taarifa zangu zinaonesha wazi kwamba, wameanza, na mwaka uliopita wamenunua lita 374,999 kwa shilingi bilioni 3.5. Ni fedha nyingi, lakini utaratibu wa manunuzi bado ni ule wa Wizara ya Afya inachukua inapeleka TAMISEMI, ili wazigawanye kwenye Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunadhani ni vizuri kukawa na mikataba. Kwa mfano, mwaka 2025/2026 kwa mujibu wa *National Malaria Strategic Plan* itahitajika dawa lita milioni 1.6; mwaka 2026/2027 kutahitajika lita milioni 2.4. Ni lita nyingi na ni fedha nyingi zinatakiwa ziingie katika mfumo wa bajeti, ili jambo hili lifanyike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukumbuke vyandarua vingi vilikuwa vinatolewa na wafadhili, na ndugu zangu wengi tunajua kwamba, baadhi ya wafadhili sasa wameamua kujitoa. Kwa hiyo, turudi kwenye kiwanda chetu tukiimarishe, kizalishe, tukipe bajeti, ili kiweze kufanya biashara iwaokoe Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala zima la viwanda limeongelewa kwa kirefu sana hapa, na ni vile ambavyo tunasema kwamba tuvilinde na tuhakikishe vinafanya kazi. Kuna wachangiaji wameongelea viwanda vya sukari, dawa, viuatilifu na mchangiaji mwingine ameongelea suala la viwanda vya maziwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kamati, katika maazimio mbalimbali tumeongelea haja ya Serikali kuendelea kutoa vivutio, kuendelea kutengeneza mazingira mazuri ya kuvutia uwekezaji wa viwanda mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa tuseme, kwenye sukari tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais na Waziri wa Kilimo,

walichukua maamuzi ya haraka na madhubuti ya kuwaokoa Watanzania kwenye janga la sukari, lakini tunachosema ni kwamba, tuendelee kuongeza uwekezaji kwenye eneo la viwanda vya sukari, ili viweze kutusaidia tuweze kuondoa uagizaji wa sukari na kuokoa fedha ambazo tunatumia katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo ni uti wa mgongo. Nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Bashe, wengi wamemwelezea hapa. Sisi kama Kamati tumeona ambavyo Wabunge wengi wamemwongelea, ni Waziri mahiri ambaye ameonyesha wazi kabisa anataka na anafanikiwa ku-*transform* na kutoa uongozi katika Wizara ya Kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengi tunajua na tunasikia hakuna Wizara ngumu kuiendesha kama ya Kilimo, lakini Mheshimiwa Bashe ameweza, tunampongeza sana. Mheshimiwa Bashe ametuambia hapa siri yake, kwamba aliyemwezesha kufika alipofika ni Mheshimiwa Rais, Jemedari Mkuu, Dkt. Samia Suluhu Hassan. Tunamshukuru sana na kumpongeza Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo mengi sana kwenye kilimo yamefanyika. Kweli, kilimo kimeshughulikiwa kama vile ni uti wa mgongo wa nchi yetu. Pembejeo za kilimo, tumesikia hususan ruzuku; tumesikia uwekezaji kwenye ugani kwa ukubwa; tumesikia vitendea kazi kwa wingi; maslahi ya wafanyakazi yameboreshwa; na tumesikia magari yamenunuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni mambo mengi yamefanyika, nasi, kama Kamati, tunasema tutafanya kazi kwa ukaribu na Wizara hii kuhakikisha yale yote ambayo wamejipangia kama vipaumbele tunawasimamia ili yaweze kutekelezwa, lakini kuna machache ambayo, Mheshimiwa Waziri Bashe, ameyaongea katika kuchangia kwake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la umwagiliaji ni kweli, ndiyo maana sisi tumetoa mapendekezo kwamba, fedha za umwagiliaji zitolewe kwa wakati. Jambo hili ni la muhimu na nisingependa

kuliongelea zaidi kwa vile Mheshimiwa Waziri ameliongelea, na ni kwa nini tumekwenda polepole? Kuna mambo mengi yamefanyika ambayo nayo yalihitaji fedha. Kuanzisha ofisi 136 za umwagiliaji nchi nzima na kununua mitambo, vitu hivi vyote vinakwenda pamoja na ku-*invest* kwenye umwagiliaji wenyewe na mabwawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kumekuwa na uwekezaji mkubwa hata ku-*set up* hiyo *institution*. Kwa hiyo, kama Kamati, tunapenda waongezewe fedha, lakini tunasema tutaendelea kuwa *patient* wakati Serikali inaendelea kujipanga zaidi kwenye suala la umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni Stakabadhi Ghalani. Waheshimiwa Wabunge wengi wameongea hapa kwamba ni mfumo mzuri wenye faida na ambao tunadhani unahitaji elimu zaidi, lakini ni mfumo ambao kwenye mapendekezo yetu tumesema unahitaji miundombinu zaidi iweze kuwekwa kwenye maeneo ambayo kuna mazao. Tunaiomba Serikali iweze kutenga fedha zaidi ili jambo hili liweze kufanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna changamoto ambayo imeendelea kujitokeza, Mheshimiwa Hhayuma na Wanakamati wenzangu wameielezea. Bado kunahitajika kuwa na uwazi zaidi kwenye eneo la utendaji wa Stakabadhi Ghalani. Kuna maeneo ambayo tungependa watu wapate imani zaidi na mfumo huu, lakini inaonesha kwenye utendaji kuna gharama nyingine ambazo zinakwenda kwa wananchi nao wanaamini pengine inaweza isiwe kweli. Ni vizuri kukawa na elimu na uwazi, ili stakabadhi ghalani kama mfumo ufanikiwe kwa sababu, umekuwa mkombozi wa wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zao la chai limekuwa ni kizungumkuti. Namshukuru sana Mheshimiwa Bashe alikuja kutueleza sisi Kamati, na tulilichukua jambo hili kwa uzito mkubwa sana. Ni zao ambalo linatakiwa lifanyiwe maamuzi magumu. Namshukuru Mheshimiwa Bashe kwa aliyoyasema hapa, na kwa vile tunajua Serikali inachofikiria, sisi kama Kamati, tumeomba

muda ili tuweze kutembelea maeneo yote na siyo chai peke yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mashamba yaliyoachwa na wawekezaji, yako kwenye chai, yako kwenye mkonge, yako kwenye ngano. Kote huko ni maeneo ambayo yanatakiwa yaangaliwe kwa umakini. Nafurahi kwamba, Mheshimiwa Bashe na Wizara wako katika mpango kazi wa kujaribu kuona namna gani watafanya, lakini na sisi tungependa twende kuona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la vituo rasilimali vya kata ambavyo katika mapendekezo yetu tumeomba…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tafadhali. Unaweza ukahitimisha hoja.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA, KILIMO NA MIFUGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nahitimisha hoja yangu, nizungumzie moja tu la mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Mifugo inaonekana inaweza ikatufikisha mbali sana kiuchumi, lakini bado hatujaitumia vizuri. Kwenye sekta hii ya mifugo na uvuvi pendekezo letu kubwa ni moja kwamba, inahitaji usimamizi wa karibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mambo yote makubwa yaliyofanyika, pamoja na uwekezaji mkubwa uliyofanyika, sekta hii ili iweze kutoa mchango kuweza kubadilisha maisha ya Watanzania, inahitaji usimamizi wa karibu sana. Pendekezo letu ni kwamba, hata huko kunahitaji kuwa na mamlaka ambayo itasimamia moja kwa moja suala la mifugo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nihitimishe hoja yangu jioni ya leo kwa kusema kwamba, Bunge sasa lipokee na liikubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge, Viwanda,

Biashara, Kilimo na Mifugo pamoja na Mapendekezo yaliyomo katika taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. MOHAMED S. ISSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imetolewa na imeungwa mkono. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Mapendekezo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge, Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo yalipitishwa na Bunge kuwa Maazimio ya Bunge kwa Serikali)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni ya 34(5), ya Kanuni za Kudumu za Bunge, naongeza muda ili kukamilisha shughuli zilizopo mbele yetu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama. Mheshimiwa Vita Rashid Mfaume Kawawa aje kuhitimisha hoja ya Kamati.

**MHE. VITA R. KAWAWA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba nishukuru kwa kunipa fursa hii kuja kuhitimisha hoja ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, waliochangia hoja ya Kamati katika eneo langu wapo tisa, na kati yao Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Daniel Sillo, akiwa mmojawapo. Pia, yupo Mheshimiwa Zahor, Mheshimiwa Kunti Majala, Mheshimiwa Mkundi, Mheshimiwa Balozi Mulamula, Mheshimiwa Vicent Mbogo, Mheshimiwa Grace Tendega, Mheshimiwa *Advocate* Swalle, Mheshimiwa Mkenge, Mheshimiwa Njau,

Mheshimiwa Mathayo Manyinyi na Mheshimiwa Daniel Sillo, kama nilivyosema hapo awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiujumla wachangiaji wamesisitiza mlemle, maeneo yote ambayo Kamati tuliyotolea taarifa. Kwa hiyo, naamini Serikali imesikia msisitizo wa Waheshimiwa Wabunge na pia, imesikia ushauri wa Kamati. Vilevile, naomba niseme kwamba, kama Kamati, tumepokea ushauri uliotolewa na Wabunge na tutasisitiza kwa Serikali waifanyie kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiujumla maoni yetu ya Kamati na Mapendekezo ya Maazimio kwa Bunge yamesheheni yote ambayo Waheshimiwa Wabunge wameshauri leo hapa. Hivyo, tunawaomba mtuunge mkono kupitisha maazimio haya ili Serikali ikayafanyie kazi na kuongeza ufanisi katika kuleta tija kwa maeneo ambayo Kamati yetu ya Ulinzi na Usalama tunasimamia kwa niaba ya Bunge letu Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo naomba kutoa hoja ili Bunge lako Tukufu liweze kukubali mapendekezo yawe maazimio. Naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MHE. ZAHOR MOHAMED HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Hoja imetolewa na imeungwa mkono. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Mapendekeo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, yalipitishwa na Bunge kuwa Maazimio ya Bunge kwa Serikali)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, hoja za kamati zetu mbili; Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo pamoja na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya

Nje, Ulinzi na Usalama, taarifa zote hizi mbili, zimepitishwa na Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, nitumie fursa hii kuzishukuru sana Kamati zote mbili kwa kazi nzuri waliyoifanya kwenye Kamati ya kuishauri na kuisimamia Serikali. Pia, tulipata fursa ya kuisikia Serikali nayo ikichangia hoja mbalimbali, kuzipokea na kuahidi kwenda kuzifanyia kazi. Kwa hiyo, ni matumaini yetu kwamba, Serikali sasa itakwenda kuyatekeleza yale ambayo Bunge limeyaazimia leo kupitia kikao hiki cha jioni.

Baada ya kuwashukuru naomba sasa niahirishe Kikao cha Bunge hadi kesho, Siku ya Ijumaa, tarehe 7 Februari, 2025 saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 1.43 Usiku, Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Ijumaa, Tarehe 7 Februari, 2025, Saa Tatu Asubuhi)*